JAMHURI YA KENYA

BUNGE

Bunge la Taifa

# KANUNI ZA KUDUMU

(Toleo la Saba)

Kama zilivyoridhiwa na Bunge la Taifa tarehe 9 Januari 2013 katika Kipindi cha Nne cha Bunge la Kumi na kurekebishwa mnamo tarehe 15 Juni 2017 katika Kipindi cha Tano cha Bunge la Kumi na Moja; mnamo tarehe 7 Desemba 2017 katika Kipindi cha Kwanza cha Bunge la Kumi na Mbili; mnamo tarehe 23 Agosti 2018 katika Kipindi cha Pili cha Bunge la Kumi na Mbili; mnamo tarehe 7 Juni 2022 katika Kipindi cha Sita cha Bunge la Kumi na Mbili; na mnamo tarehe 9 Machi 2023 katika Kipindi cha Pili cha Bunge la Kumi na Tatu.

# Bunge la Taifa

–

# KANUNI ZA KUDUMU

**(Toleo la Saba)**

## KANUNI ZA KUDUMU ZA BUNGE LA TAIFA

*Katika utekelezaji wa mamlaka yanayotolewa na Ibara ya 124 ya Katiba ya Jamhuri ya Kenya, Bunge la Taifa, kutokana na uamuzi uliopitishwa mnamo tarehe 9 Januari 2013, liliridhia kanuni hizi pamoja na Masharti ya Vikao vya Pamoja vya Bunge.*

***Iwapo kutakuwa na mkinzano kati ya matoleo ya lugha tofauti ya Kanuni hizi, toleo la Kiingereza ndilo litakalofuatwa***

## MAREKEBISHO

Toleo hili la 7 la Kanuni za Kudumu linajumuisha marekebisho yaliyofanywa na Bunge la Taifa tarehe zifuatazo–

(a) 25 Aprili 2013;

(b) 6 Mei 2013;

(c) 4 Desemba 2013;

(d) 11 Juni 2014;

(e) 28 Agosti 2014;

(f) 15 Juni 2017;

(g) 7 Desemba 2017;

(h) 23 Agosti 2018;

(i) 20 Mei 2020;

(j) 7 Juni 2022; na

(k) 9 Machi 2023.

# YALIYOMO

## SEHEMU YA I - UTANGULIZI


**1.** Katika hali ambazo jambo lolote halijaelezwa waziwazi, Spika ataamua ........ 1

**2.** Ufafanuzi ........ 1

**2A.** Siwa ........ 5

**2B.** Katibu kupata Mikataba ya Miungano ........ 5


## SEHEMU YA II — KUAPISHWA KWA WABUNGE NA UCHAGUZI WA SPIKA


**3.** Shughuli kwenye kikao cha kwanza cha Bunge jipya la Taifa ........ 5

**4.** Kumchagua Spika baada ya Uchaguzi Mkuu ........ 7

**5.** Uteuzi wa wagombeaji ........ 7

**6.** Kura ya siri ........ 8

**7.** Viwango vya upeo wa kuchaguliwa ........ 9

**8.** Kujiondoa kwa Mgombeaji ........ 10

**9.** Idadi sawa ya kura ........ 10

**10.** Uhifadhi wa karatasi za kura ........ 10

**11.** Mgombeaji mmoja anapoteuliwa kikamilifu ........ 10

**12.** Kuapishwa kwa Spika ........ 11


## SEHEMU YA IIA— KUJIONDOA AU KUONDOLEWA KATIKA OFISI YA SPIKA NA NAIBU SPIKA


**12A.** Kujiuzulu ........ 11

**12B.** Kuondolewa mamlakani ........ 11

**12C.** Kuondoka mamlakani kwa mujibu wa Ibara ya 103 ya Katiba ........ 13


## SEHEMU YA III—NAIBU SPIKA NA MWENYEKITI WA KAMATI


**13.** Uchaguzi wa Naibu Spika ........ 14

**14.** Arifa ya ufunguzi wa Bunge ........ 14

**15.** Mwenyekiti wa Kamati za Bunge la Taifa ........ 14

**16.** Jopo la Mwenyekiti ........ 15

**17.** Kumwondoa Mjumbe kwenye Jopo la Mwenyekiti ........................ 15
**18.** Kuongoza Kikao cha Bunge la Taifa ................................................ 16

**SEHEMU YA IV — KIONGOZI WA CHAMA CHA WALIO WENGI NA KIONGOZI WA CHAMA CHA WALIO WACHACHE**

**19.** Viongozi wa Vyama na itifaki ........................................................ 16
**19A.** Kuchaguliwa na Kuondolewa mamlakani kwa Kiongozi wa Chama cha walio Wengi na Naibu Kiongozi wa Chama cha walio Wengi . 17
**20.** Kuchaguliwa na Kuondolewa kwa Kiongozi wa Chama cha walio Wachache na Naibu Kiongozi wa Chama cha walio Wachache .... 19
**20A.** Kutambuliwa kwa Vyama Bunge na Kuteuliwa kwa Viongozi na Waratibu ........................................................................................ 21

**SEHEMU YA V—HOTUBA YA RAIS, MGENI MASHUHURI AU WAGENI WENGINE**

**21.** Hotuba ya Rais wakati wa ufunguzi rasmi wa Bunge jipya............. 22
**22.** Hotuba ya Rais wakati wa vikao maalum........................................ 22
**23.** Rais anapoingia au anapoondoka katika Ukumbi ........................... 23
**24.** Hotuba ya Rais kwa Bunge ............................................................ 23
**25.** Mgeni mashuhuri ........................................................................... 23
**25A.** Kutenga sehemu maalum katika Ukumbi kwa ajili ya Mawaziri na watu wengine ........................................................................... 24

**SEHEMU YA VI — KALENDA, VIKAO NA MAAHIRISHO YA BUNGE LA TAIFA**

**26.** Mahali pa kikao cha kwanza cha Bunge jipya ............................... 24
**27.** Vipindi vya kawaida vya Bunge la Taifa ......................................... 24
**28.** Kalenda ya Bunge la Taifa.............................................................. 25
**29.** Vikao maalum vya Bunge la Taifa .................................................. 25
**30.** Saa za vikao .................................................................................. 26
**31.** Kuahirisha Kikao............................................................................. 28
**32.** *(Imefutwa)*
**33.** Kuahirisha shughuli ili kujadili suala mahususi, la dharura na muhimu kwa taifa........................................................................................ 28

## SEHEMU YA VII—AKIDI YA BUNGE LA TAIFA

**34.** Akidi wakati wa kuanza kikao .......... 29
**35.** Akidi wakati wa shughuli za Kikao .......... 29
**36.** Akidi wakati wa kupiga kura .......... 30
**37.** Staha akidi inapokosekana .......... 30

## SEHEMU YA VIII — MPANGILIO WA SHUGHULI

**38.** Ratiba ya Shughuli kutayarishwa na kusambazwa .......... 30
**39.** Mipango ya kila wiki ya Bunge la Taifa .......... 30
**40.** Mtiririko wa shughuli .......... 31

## SEHEMU YA IX — JUMBE

**41.** Jumbe za kwenda na kutoka Seneti .......... 32
**42.** Jumbe kutoka kwa Rais .......... 32

## SEHEMU YA IXA – MASWALI

**42A.** Arifa ya Swali .......... 33
**42B.** Masharti ya jumla kuhusu Maswali .......... 34
**42C.** Namna ya kushughulikia Maswali .......... 36
**42D.** Maswali yanayohitaji majibu kwa maandishi .......... 37
**42E.** Muda wa kujibu .......... 37
**42F.** Ripoti kuhusu Maswali .......... 37
**42G.** Maswali kwa Tume na Ofisi Huru .......... 38

## SEHEMU YA X — KAULI

**43.** Kauli za jumla za Wajumbe .......... 38
**44.** Saa ya Kauli .......... 38

## SEHEMU YA XI—KUIDHINISHA UTEUZI WA MAOFISA WA UMMA

**45.** Kukabidhiwa kwa Kamati .......... 39

## SEHEMU YA XII—HOJA


**46.** Matumizi ........ 40
**47.** Arifa za Hoja ........ 40
**48.** Marekebisho ya Arifa ya Hoja ........ 42
**49.** Hoja ambazo haziruhusiwi kutolewa ........ 42
**50.** Wakati wa kutoa Hoja ........ 42
**51.** Hoja iliyoondolewa inaweza kuwasilishwa tena ........ 43
**52.** Hoja zinazoweza kutolewa bila Arifa ........ 43
**53.** Utaratibu wa kujadili hoja ........ 44
**54.** Marekebisho ya Hoja ........ 44
**55.** Marekebisho kuwa kwa maandishi ........ 46
**56.** Marekebisho yawiane na Hoja ........ 46
**57.** Hoja kupendekezwa baada ya kuafikiwa ........ 46
**58.** Hoja inayomilikiwa na Bunge la Taifa ........ 47
**59.** Kutoa Hoja iliyorekebishwa iamuliwe ........ 47
**60.** Rekebisho lililopendekezwa lisipofaulu ........ 47


## SEHEMU YA XIII — HOJA MAALUM


**61.** Maana ya Hoja Maalum ........ 47
**62.** Katiba inapohitaji wingi wa idadi mahususi ........ 49


## SEHEMU YA XIV—UTARATIBU WA KUMWONDOA OFISA WA SERIKALI MAMLAKANI


**63.** Utaratibu wa kumwondoa Rais mamlakani kwa kushindwa kutekeleza majukumu ........ 49
**64.** Utaratibu wa kumwondoa Rais mamlakani kwa mashtaka ........ 51
**65.** Utaratibu wa kumwondoa Naibu Rais mamlakani ........ 53
**66.** Utaratibu wa kumwondoa Waziri mamlakani ........ 53
**67.** Haki ya kusikilizwa ........ 55
**68.** Hoja kupewa kipaumbele ........ 55


## SEHEMU YA XV – UPIGAJI KURA NA KURA YA MGAWANYIKO


**69.** Utaratibu wa kupiga kura katika Bunge la Taifa ........ 55

**70.** Kura ya kielektroniki ........ 56
**71.** Hitilafu ya mitambo, mkanganyiko au kasoro inapotokea ........ 56
**72.** Kura ya kuita majina inapodaiwa ........ 57
**73.** Kura ya kuita majina ........ 57
**74.** Mkanganyiko au kasoro inapotokea ........ 58
**75.** Kurekebisha kasoro ........ 58
**76.** Staha wakati wa kura ya mgawanyiko ........ 58

## SEHEMU YA XVI- MASHARTI YA MJADALA

**77.** Shughuli kuendeshwa kwa Kiswahili, Kiingereza au Lugha Ishara ya Kenya ........ 59
**78.** Wabunge kuelekeza ombi kwa Spika ........ 59
**79.** Wabunge wawili au zaidi wanapoomba kuchangia ........ 59
**80.** Kutosoma Michango ........ 59
**81.** Mbunge kutozungumza baada ya Hoja kutolewa iamuliwe ........ 60
**82.** Kuchangia Hoja mara mbili ........ 60
**82A.** Mbunge aliyechangia Hoja anaweza kuchangia rekebisho ........ 60
**82B.** Mjadala wa rekebisho kujikita kwenye rekebisho ........ 60
**82C.** Kuhifadhi haki ya kuchangia ........ 61
**83.** *(Imefutwa)*
**84.** Hoja ya Nidhamu ........ 61
**85.** Kuwahi mjadala ........ 62
**86.** Kutorejelea shughuli za Kamati ........ 62
**87.** Maudhui ya michango ........ 62
**88.** Kuondoa machukizo na kuomba radhi ........ 63
**89.** Masuala yanayosubiri uamuzi wa Mahakama au masuala ya siri ... 63
**90.** Kutangaza maslahi ya kibinafsi ........ 64
**91.** Kuwajibikia madai ........ 65
**92.** *(Imefutwa)*
**93.** *(Imefutwa)*
**94.** *(Imefutwa)*
**95.** Kuhitimisha mjadala ........ 65
**95A.** Kuendeleza shughuli iliyositishwa ........ 66
**96.** Kuahirisha mjadala ........ 66

## SEHEMU YA XVII—KUDHIBITI MJADALA

**97.** Kudhibiti mjadala .......................................................................... 67

## SEHEMU YA XVIII - UTULIVU KATIKA UKUMBI NA KWENYE KAMATI YA BUNGE ZIMA

**98.** Kudumisha utulivu.......................................................................... 68
**99.** Ukaguzi wa kiusalama...................................................................... 68
**100.** Bunduki na silaha nyingine hatari.................................................. 68
**101.** Mikoba ya Wabunge wa kike.......................................................... 68
**102.** Wabunge kuwa kimya Spika anaposimama .................................. 68
**103.** Wabunge na Kiongozi wa Kikao.................................................... 69
**104.** Wabunge kuketi ............................................................................. 69
**105.** Wabunge kusalia mahali pao hadi Spika atakapoondoka katika Ukumbi .69
**106.** Kutoka nje ya mada au kurudiarudia ........................................... 69
**107.** Utovu wa nidhamu.......................................................................... 69
**107A.** Utovu mkubwa wa nidhamu ...................................................... 70
**108.** Mbunge anaweza kusimamishwa kwa muda baada ya kutajwa jina 72
**109.** Mbunge aliyesimamishwa kuhudhuria vikao vya Bunge kwa muda ataondoka katika maeneo ya Bunge............................................. 72
**110.** Muda wa Mbunge kusimamishwa kwa muda ................................ 72
**110A.** Athari za kusimamishwa kwa muda ............................................ 73
**110B.** Rufaa dhidi ya kusimamishwa kwa muda .................................... 73
**111.** Hatua itakayochukuliwa kwa kukaidi amri ya kuondoka ............... 74
**112.** Utovu wa nidhamu uliokithiri katika Bunge la Taifa ...................... 75
**112A.** Maana ya siku .............................................................................. 75

## SEHEMU YA XIX—MISWADA YA UMMA

**113.** Matumizi na udhibiti ...................................................................... 75
**114.** Uwasilishaji wa Miswada ............................................................... 75
**114A.** Spika kuruhusu baadhi ya mapendekezo ya miswada ................... 79
**115.** Kupiga chapa vifungu vinavyorekebisha sheria .............................. 80
**116.** Kauli tekelezi .................................................................................. 80
**117.** Maelezo ya Madhumuni na Sababu ............................................... 80

**118.** Vifungu kuhusu ukasimishaji wa mamlaka .................................. 80
**119.** Udhibiti wa haki na uhuru wa kimsingi ......................................... 81
**120.** Uchapishaji na Uwasilishaji wa Miswada ..................................... 81
**121.** Miswada inayohusu serikali za kaunti ........................................... 82
**122.** *(Imefutwa)*
**123.** *(Imefutwa)*
**124.** Mswada hautashughulikiwa kwa hatua zaidi ya moja katika kikao kimoja ..................................................................................... 83
**125.** Kusomwa kwa Miswada ........................................................... 83
**126.** Kusomwa Mara ya Kwanza ......................................................... 83
**127.** Kamati kukabidhiwa Miswada na ushirikishwaji wa umma........... 83
**128.** Kusomwa Mara ya Pili ............................................................... 85
**129.** Kusomwa Mara ya Pili kwa Mswada wa kurekebisha Katiba .......... 85
**130.** Kukabidhi Miswada kwa Kamati ya Bunge Zima............................ 86
**130A.** Mipaka ya mamlaka ya Kamati.................................................. 86
**130B.** Kamati ya Bunge Zima kutojiahirisha ......................................... 86
**130C.** Ripoti......................................................................................... 86
**130D.** Hoja ya Ripoti kutojadiliwa ...................................................... 86
**130E.** Matumizi ya jumla ya masharti kwenye Kamati ............................ 87
**131.** Mapendekezo ya marekebisho kukabidhiwa Kamati...................... 87
**132.** Mtiririko utakaozingatiwa Mswada ukiwa kwenye Kamati ............. 87
**133.** Utaratibu wa kushughulikia Mswada katika Kamati ya Bunge Zima 88
**134.** Ripoti ya hatua iliyofikiwa ....................................................... 90
**135.** Mswada kuripotiwa ................................................................... 90
**136.** Utaratibu kwa Miswada inayoripotiwa kutoka kwa Kamati ya Bunge Zima......................................................................................... 91
**136A.** Utaratibu wa Urejeshaji ............................................................ 91
**137.** Utaratibu kwa Miswada inayoripotiwa kutoka kwa Kamati ........... 91
**138.** Utaratibu utakaotumika Mswada ukirejeshwa kwenye Kamati ....... 92
**139.** Kusomwa Mara ya Tatu ............................................................. 92
**140.** Kuondolewa kwa Miswada ......................................................... 93
**141.** Kutanguka na kuwasilishwa tena kwa Miswada ............................ 93
**142.** Maafikiano na Seneti ................................................................ 94
**143.** Utaratibu wa kushughulikia Miswada inayoanzia Seneti ............... 95

**144.** Utaratibu wa kushughulikia Miswada ya Seneti baada ya Kusomwa Mara ya Tatu katika Bunge la Taifa ................................................ 95

**145.** Marekebisho ya Seneti kwa Miswada iliyoanzia katika Bunge la Taifa 96

**146.** Kushughulikia marekebisho ya Seneti kwa Miswada iliyoanzia katika Bunge la Taifa ........................................................................ 96

**147.** Utaratibu wa kushughulikia marekebisho ya Seneti kwa Miswada iliyoanzia katika Bunge la Taifa ................................................... 96

**148.** Kuhitimisha kushughulikia marekebisho ya Seneti kwa Miswada iliyoanzia katika Bunge la Taifa ................................................... 96

**149.** Kamati ya Upatanisho................................................................... 97

**150.** Kushughulikia Ripoti ya Kamati ya Upatanisho ............................. 98

**151.** Mswada Maalum unaohusu serikali ya kaunti................................ 99

**152.** Uhifadhi wa Miswada.................................................................... 99

**153.** Kuwasilisha Miswada ipate kibali ............................................... 100

**154.** Miswada iliyorejeshwa na Rais .................................................. 100

**155.** *(Imefutwa)*

**SEHEMU YA XX- MISWADA BINAFSI**

**156.** Utaratibu wa Mswada wa umma kutumika ................................ 102

**157.** Kifungu cha uhifadhi ................................................................. 102

**158.** Mswada Binafsi unaoathiri haki binafsi....................................... 102

**159.** Ardhilhali ya Idhini..................................................................... 103

**160.** Dhamana ya gharama za uchapishaji ......................................... 103

**161.** Miswada inayoidhinisha kazi za ujenzi....................................... 104

**162.** Kusomwa Mara ya Kwanza ....................................................... 104

**163.** Haki ya kusikilizwa na Kamati kuhusu Mswada unaopingwa....... 104

**164.** Namna Miswada inavyoweza kupingwa .................................. 105

**165.** Gharama za kupiga chapa.......................................................... 105

**166.** *(Imefutwa)*

**167.** *(Imefutwa)*

**168.** *(Imefutwa)*

**169.** *(Imefutwa)*

**170.** *(Imefutwa)*

**SEHEMU YA XXI— KURIDHIA MIKATABA**

**170A.** Kuridhia Mikataba........................................................................ 105

**SEHEMU YA XXII— KAMATI**

**171.** Kamati ya Kuratibu Shughuli za Bunge la Taifa............................ 107
**172.** Kamati ya Kuteua Wajumbe wa Kamati ...................................... 108
**173.** Uteuzi wa Wajumbe wa Kamati .................................................. 109
**173A.** Uanachama wa Kamati ............................................................ 109
**174.** Vigezo vya uteuzi ....................................................................... 110
**175.** Kuidhinisha uteuzi....................................................................... 111
**176.** Kuondolewa kwa Mjumbe kwenye Kamati ................................. 111
**177.** Idadi ya wajumbe wa kamati ...................................................... 112
**177A.** Uteuzi wa Kamati inayosimamia haki na mwenendo wa Wabunge..... 112
**178.** Uongozi na akidi ya Kamati ........................................................ 113
**179.** Utaratibu wa uchaguzi ................................................................ 114
**180.** Majukumu ya Mwenyekiti wa Kamati......................................... 116
**181.** Arifa za mikutano ....................................................................... 116
**182.** Vikao vya Kamati......................................................................... 116
**183.** Kamati ndogo .............................................................................. 116
**184.** Mbunge aliyetuhumiwa hatahudhuria mikutano.......................... 117
**185.** Ahirisho kutokana na akidi kutotimia ......................................... 117
**186.** Idadi ya mikutano........................................................................ 117
**187.** Kutohudhuria mikutano .............................................................. 117
**188.** Kutokuwepo kwa Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti .............. 118
**189.** Orodha ya mahudhurio ............................................................... 118
**190.** Kumbukumbu za kamati ............................................................. 118
**191.** Mamlaka na haki za kamati......................................................... 118
**191A.** Utaratibu shahidi asipohudhuria .............................................. 121
**192.** Mjumbe asipohudhuria kwa muda ............................................. 121
**193.** Kura ya kutokuwa na imani na Mwenyekiti au Makamu Mwenyekiti .. 121
**194.** Kura asilia ................................................................................... 122

**195.** Kuhudhuria mikutano ya kamati kwa Wabunge wasio wajumbe wa kamati ........ 122
**196.** Utaratibu katika Kamati ........ 123
**197.** Udhibiti wa wajibu ........ 124
**198.** Mikutano ya Kamati kuwa wazi kwa umma ........ 124
**199.** Ripoti za Kamati ........ 124
**200.** Ripoti za utendakazi wa kamati ........ 125
**200A.** Ripoti za mwisho wa muhula ........ 126
**201.** Ripoti za maamuzi ya Bunge la Taifa ........ 126
**202.** Mikutano ya Pamoja ya kamati za Bunge la Taifa ........ 126
**202A.** Ruhusa ya mikutano ya pamoja na Kamati ya Seneti ........ 127
**203.** Kushirikisha wataalamu ........ 127
**204.** Kamati ya Uteuzi ........ 127
**205.** Kamati ya Hesabu za Umma ........ 128
**205A.** Kamati ya Hesabu za Hazina Maalum ........ 128
**205B.** Kamati ya Hesabu za Hazina Tengwa ........ 129
**206.** Kamati ya Uwekezaji wa Umma kuhusu Utawala na Elimu ........ 130
**206A.** Kamati ya Uwekezaji wa Umma kuhusu Masuala ya Kibiashara na Kawi ........ 132
**206B.** Kamati ya Uwekezaji wa Umma kuhusu Huduma kwa Jamii, Usimamizi na Kilimo ........ 133
**207.** Kamati ya Bajeti na Uidhinishaji wa Matumizi ........ 134
**207A.** Kamati ya Deni la Umma na Ubinafsishaji ........ 135
**208.** Kamati ya Utaratibu na Kanuni za Bunge la Taifa ........ 138
**208A.** Kamati ya Ardhilhali za Umma ........ 139
**208B.** Kamati ya Masuala ya Ughaibuni na Wafanyakazi Wahamiaji ........ 139
**209.** Kamati ya Utekelezaji ........ 140
**210.** Kamati ya Sheria Ndogo ........ 141
**211.** Kuafiki uamuzi wa Seneti kuhusu sheria ndogo ........ 144
**212.** Kamati ya Utangamano wa Kikanda ........ 145
**212A.** Utaratibu wa kuwasilisha ripoti za Bunge la Afrika Mashariki na Bunge la Afrika ........ 146
**212B.** Kamati ya Huduma na Vifaa kwa Wabunge ........ 147
**212C.** Kamati ya Mshikamano wa Kitaifa na Fursa Sawa ........ 147
**212D.** Kamati ya Utangazaji wa Shughuli za Bunge na Maktaba ........ 148

**213.** Uteuzi wa Kamati za Pamoja ........................................................ 149
**214.** *(Imefutwa)*
**215.** *(Imefutwa)*
**216.** Uteuzi na wajibu wa Kamati za Kiidara ........................................ 150
**217.** Kamati ya Kuratibu Shughuli za Kamati ......................................... 152
**218.** Kamati kujikita katika Wajibu ....................................................... 153

**SEHEMU YA XXIII- ARDHILHALI ZA UMMA**

**219.** Maana ya Ardhilhali ....................................................................... 153
**220.** Kuwasilishwa kwa Ardhilhali ........................................................ 153
**221.** Ardhilhali ya Mswada Binafsi ....................................................... 154
**222.** Arifa ya nia ya kuwasilisha Ardhilhali ........................................... 154
**223.** *(Imefutwa)*
**224.** Muundo wa Ardhilhali .................................................................... 154
**225.** Uwasilishaji wa Ardhilhali ............................................................. 156
**226.** Maoni kuhusu Ardhilhali ............................................................... 157
**227.** Ardhilhali kukabidhiwa Kamati...................................................... 157
**228.** Nakala za majibu ........................................................................... 157
**229.** Sajili ya Ardhilhali ......................................................................... 157

**SEHEMU YA XXIIIA — ARDHILHALI YA KUMWONDOA MJUMBE WA TUME AU OFISI HURU**

**230.** Ardhilhali ya kumwondoa Mamlakani Mjumbe wa Tume au ofisa wa Ofisi Huru ......................................................................................... 158

**SEHEMU YA XXIV – UTARATIBU WA MASUALA YA FEDHA**

**231.** Udhibiti wa masuala mahususi ya kifedha .................................... 159
**232.** Kuwasilishwa kwa Taarifa ya Sera ya Bajeti .................................. 160
**232A.** Kuwasilishwa kwa Mkakati wa Kudhibiti Deni ............................ 162
**233.** Kushughulikia Mswada wa Kugawa Mapato ................................. 164
**234.** Kushughulikia Mswada wa Kutenga Mapato kwa Kaunti ............. 165
**235.** Uwasilishaji wa Makadirio ya Bajeti na Kukabidhiwa Kamati ..... 165
**236.** Kamati ya Ugavi wa Fedha ........................................................... 166
**237.** Fasili ya siku ................................................................................. 166

**238.** *(Imefutwa)*

**239.** Kuingia katika hatua ya Kamati ya Ugavi wa Fedha...................... 166

**240.** Kushughulikia Makadirio kwenye Kamati ya Ugavi wa Fedha..... 167

**240A.** Kushughulikia Maamuzi ya Ugavi wa Fedha................................ 169

**240B.** Mswada wa Kuidhinisha Matumizi ya Fedha na Mswada wa Kuidhinisha Matumizi ya Fedha ya Hazina ya Usawazishaji........ 170

**241.** *(Imefutwa)*

**242.** Idhini ya kutoa Fedha ................................................................. 171

**243.** Utaratibu wa Makadirio ya Ziada ................................................ 171

**244.** *(Imefutwa)*

**244A.** Kuidhinisha matumizi yanayozidi asilimia kumi ......................... 173

**244B.** Mswada wa Kuidhinisha Matumizi ya Ziada ya Fedha................. 173

**244C.** Kutangazwa kwa vidokezo vya Bajeti na mikakati ya Ukusanyaji mapato ....................................................................................... 174

**245.** Kushughulikia Mswada wa Fedha ................................................ 175

**245A.** Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Bajeti............................................ 176

**SEHEMU YA XXV–MAJARIDA, REKODI NA UPEPERUSHAJI WA MATANGAZO YA VIKAO**

**246.** Majarida ya Bunge la Taifa......................................................... 177

**247.** Hifadhi ya Majarida na Rekodi za Bunge la Taifa........................ 177

**248.** Taarifa Rasmi ............................................................................. 178

**249.** Masuala ya siri au ya kibinafsi .................................................... 178

**250.** Upeperushaji wa matangazo ya shughuli za Bunge la Taifa ......... 178

**251.** *(Imefutwa)*

**SEHEMU YA XXVII - BUNGE LA TAIFA NA KAMATI ZAKE KUWA WAZI KWA UMMA**

**252.** Masharti ya jumla ya kuingia kwenye Bunge la Taifa.................... 179

**253.** Udhibiti wa kuingia katika Ukumbi ............................................ 179

**254.** Kuondolewa bungeni au kwenye Kamati .................................... 180

**255.** Wanahabari wanapokiuka Kanuni hizi au Kanuni za Spika ......... 180

## SEHEMU YA XXVIII — JUMLA


**256.** Kutengua Kanuni ........................................................................ 181
**256A.** Kuongeza muda uliotengewa shughuli ........................................ 181
**256B.** Hati ya Wito ............................................................................ 182
**257.** Kufika mbele ya Seneti ........................................................... 183
**257A.** Ruhusa ya kutohudhuria vikao.................................................. 183
**258.** Kutohudhuria vikao .................................................................. 184
**259.** Utaratibu wa kuketi katika Ukumbi ........................................... 185
**259A.** Kutambuliwa kwa Kikundi cha Wabunge.................................. 185
**259B.** Kikundi cha Wabunge Huru ...................................................... 186
**259C.** Kamati za Muda ....................................................................... 186
**259D.** Risala za Bunge la Taifa .......................................................... 187
**259E.** Bunge la Taifa kupendekeza au kuteua maafisa kwa Ofisi za Umma.... .................................................................................................. 187
**259F.** Wasifu na Sajili ya Wabunge ................................................... 188
**259G.** Utambuzi wa Wabunge wenye Hadhi ....................................... 188
**260.** Wabunge wanaosafiri nje ya Kenya .......................................... 189
**261.** Gharama za mashahidi.............................................................. 189


## SEHEMU YA XXIX — MAREKEBISHO YA KANUNI


**262.** Mapendekezo ya kurekebisha Kanuni kutoka kwenye Kamati ya Utaratibu na Kanuni za Bunge la Taifa ........................................ 189
**263.** Rekebisho linalotokana na Mbunge........................................... 190
**264.** Udurusu wa mara kwa mara wa Kanuni za Kudumu .................. 191
**265.** Kushughulikia ripoti za Kamati ya Utaratibu na Kanuni za Bunge la Taifa ....................................................................................... 191


## SEHEMU YA XXIXA— UENDESHAJI VIKAO KATIKA HALI ZA KIPEKEE


**265A.** Matumizi.................................................................................. 191
**265B.** Mipangilio mbadala ya Vikao ................................................... 192
**265C.** Mipango mingine ..................................................................... 193
**265D.** Matumizi ya teknolojia............................................................. 194

## SEHEMU YA XXX—MASHARTI YA MPITO

**266.** Uamuzi wa Bunge la Taifa kuhusu Kanuni za Kudumu ................ 194
**267.** Kubatilisha Kanuni za Kudumu za awali ..................................... 195
**267A.** Kuanza kutumika ................................................................... 195

**NYONGEZA YA KWANZA**

Masharti ya Upeperushaji wa Matangazo ya Shughuli za Bunge............ 196

**NYONGEZA YA PILI**

Kamati za Kiidara ........................................................................... 200

**NYONGEZA YA TATU**

Muundo wa Jumla wa Ardhilhali ......................................................... 204

**NYONGEZA YA NNE**

Masharti ya Vikao vya Pamoja............................................................. 206

**NYONGEZA YA TANO**

Muundo wa Hati ya Uteuzi ................................................................ 210

**NYONGEZA YA SITA**

Muundo wa Kiapo/Kukiri Kuwajibika kwa Shahidi Aliyefika Mbele ya Kamati ya Bunge la Taifa ........................................................................... 212

**NYONGEZA YA SABA**

Wito kwa Mashahidi ........................................................................ 213

**NYONGEZA YA NANE**

Hati ya Kiapo ya Kupokeza Hati ya Wito ............................................ 214

**NYONGEZA YA TISA**

Muundo wa Hati ya Uteuzi ........................................................ 215

**NYONGEZA YA KUMI**

Fomu ya Wasifu ........................................................................ 218

## MAOMBI

Ewe Mwenyezi Mungu, ambaye kwa hekima na wema wako umeteua nyadhifa za viongozi na mabunge kwa ustawi wa jamii na utawala wa haki wa wanadamu, twakusihi ututazame kwa neema nyingi sisi watumishi wako, ambao umeridhika kutuita ili tutekeleze shughuli muhimu za Jamhuri hii yetu.

Twakuomba ututeremshie baraka zako sisi tuliokutanika hapa, na utujalie tuyatende na kufikiria mambo yote yatakayofikishwa mbele yetu kwa njia ya haki na uaminifu ili utukufu na sifa zako ziendelezwe, na ili kustawisha amani, ufanisi na heri ya nchi hii yetu na wale ambao haja zao umezikabidhi mikononi mwetu.

**AMINA**

# SEHEMU YA I - UTANGULIZI

**Katika hali ambazo jambo lolote halijaelezwa waziwazi, Spika ataamua**

**1.** (1) Katika hali ambazo jambo lolote halijaelezwa waziwazi katika Kanuni hizi au kwa Amri nyingine za Bunge la Taifa, basi Spika ataamua utaratibu wa kufuatwa.

(2) Uamuzi utakaofanywa kwa mujibu wa aya ya (1) utazingatia Katiba ya Kenya, sheria za nchi na mazoea, mitindo, uamuzi wa awali, desturi, taratibu, mila na mienendo ya Bunge la Kenya na mabunge mengine, ilimradi matumizi yao yanakubalika Kenya.

**Ufafanuzi**

**2.** (1) Katika Kanuni hizi—

(a) isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo—

"Siku Tengwa" ina maana ya muda uliotengwa kujadili Hotuba ya Rais kwa Bunge kwa mujibu wa Sehemu ya V ya Kanuni za Kudumu au kushughulikia, katika Kamati ya Ugavi, mapendekezo kuhusu Makadirio ya Mwaka na Makadirio ya Ziada kulingana na Sehemu ya XXIV ya Kanuni hizi;

"Utangazaji" unajumuisha upeperushaji wa moja kwa moja wa matukio ya Bunge la Taifa kupitia redio, runinga au matangazo ya mtandaoni;

"Waziri" ina maana ya mtu aliyeteuliwa kuwa Waziri chini ya Ibara ya 152(2) ya Katiba;

"Katibu" ina maana ya Katibu wa Bunge la Taifa au mtu yeyote anayetekeleza majukumu ya Katibu iwapo Katibu hayupo au nafasi yake inapokuwa wazi;

"Orodha ya Wabunge" ina maana ya orodha inayoandaliwa na Katibu ikiwa na majina ya Wabunge kialfabeti kulingana na—

(i) maeneo bunge yao; na

(i) maslahi maalum yanayowakilishwa na Wabunge walioteuliwa kwa mujibu wa Ibara ya 97(1)(c) ya Katiba;

"Kiongozi wa Chama cha walio Wengi" ina maana ya Mbunge ambaye ni kiongozi katika Bunge la Taifa wa chama au muungano wa vyama wenye idadi kubwa ya Wabunge kwa mujibu wa Kanuni ya 19A *(Kuchaguliwa na Kuondolewa kwa Kiongozi wa Chama cha walio Wengi na Naibu Kiongozi wa Chama cha walio Wengi);*

"Kiongozi wa Chama cha walio Wachache" ina maana ya Mbunge ambaye ni kiongozi katika Bunge la Taifa wa chama au muungano wa vyama wenye idadi ya pili kwa wingi wa Wabunge kwa mujibu wa Kanuni ya 20 *(Kuchaguliwa na Kuondolewa kwa Kiongozi wa Chama cha walio Wachache na Naibu Kiongozi wa Chama cha walio Wachache);*

"Idhini ya Bunge la Taifa" ina maana ya kutokuwepo kwa pingamizi kutoka kwa Mbunge yeyote na ikiwa pingamizi ipo, itahitajika kupata ridhaa ya Spika ama Mbunge anayepinga apate uungwaji mkono na Wabunge wasiopungua watano.

"Chama cha walio Wengi" ina maana ya chama chenye idadi kubwa ya Wabunge au muungano wa vyama wenye idadi kubwa ya Wabunge katika Bunge la Taifa;

"Mratibu wa Chama cha walio Wengi" ina maana ya Mbunge aliyeteuliwa na Kiongozi wa Chama cha walio Wengi kuwa Mratibu wa Chama cha walio Wengi;

"Mbunge" ina maana ya Mbunge wa Bunge la Taifa;

“Chama cha walio Wachache” ina maana ya chama au muungano wa vyama wenye idadi inayofuatia kwa wingi wa Wabunge katika Bunge la Taifa;

“Mratibu wa Chama cha walio Wachache” ina maana ya Mbunge aliyeteuliwa na Chama cha walio Wachache kuwa Mratibu wake;

“Arifa ya Shughuli” ina maana ya mpangilio rasmi wa shughuli zinazokusudiwa kutekelezwa na Bunge la Taifa kwa wiki na zinazochapishwa na kusambazwa na Katibu kwa amri ya Kamati ya Kuratibu Shughuli za Bunge la Taifa kwa mujibu wa Kanuni ya 38 *(Ratiba ya Shughuli kutayarishwa na kusambazwa);*

“Ratiba ya Shughuli” ina maana ya waraka utakaochapishwa na kusambazwa na Katibu kwa mujibu wa Kanuni ya 38 *(Ratiba ya Shughuli kutayarishwa na kusambazwa)* ikionyesha shughuli zitakazowasilishwa Bungeni au kushughulikiwa na Bunge la Taifa katika siku inayohusika;

“Waraka” ina maana ya ujumbe uliochapishwa au wa kielektroniki au wa namna nyingine yoyote itakayoamuliwa na Spika uliowasilishwa juu ya Meza ya Bunge au kwenye kamati ya Bunge kwa mujibu wa sheria yoyote au Kanuni hizi;

“Chama Bunge” ina maana ya chama kilichotambuliwa na Spika kuwa chama bunge kwa mujibu wa Kanuni ya 20A *(Kutambuliwa kwa Vyama Bunge na Kuteuliwa kwa Viongozi na Waratibu);*

“Mratibu wa Chama” ina maana ya Mbunge aliyeteuliwa na chama bunge kuwa Mratibu wake kwa minajili ya kutekeleza shughuli bungeni na inajumuisha Mratibu wa Chama cha walio Wengi na Mratibu wa Chama cha walio Wachache;

“Maeneo ya Bunge” inajumuisha Ukumbi wa Bunge la Taifa na ule wa Seneti, sehemu zote za majengo zilipo Kumbi, ofisi za Bunge, sehemu za ndani ya Ukumbi zilizotengewa wageni, sehemu zinazotumiwa na Wabunge, umma na wanahabari na nyuga, ua, bustani, eneo wazi linalomilikiwa au kutengwa kwa matumizi ya Bunge;

“Rais” ina maana ya Rais wa Jamhuri ya Kenya na inajumuisha Naibu wa Rais anapokaimu nafasi ya Rais na mtu yeyote anayetekeleza majukumu ya Rais kwa mujibu wa Ibara ya 146(2) ya Katiba;

“Mswada Binafsi” ina maana ya Mswada wowote unaokusudia kuathiri au kunufaisha mtu fulani, kikundi au shirika;

“Mswada Umma” ina maana ya Mswada wowote unaokusudia kuathiri umma kwa jumla au sehemu ya umma;

“Likizo” ina maana ya muda ambao Bunge la Taifa limeahirishwa hadi siku nyingine ambayo sio ile siku inayofuata siku ya kawaida ya kikao;

“Kipindi” ina maana ya Vikao vya Bunge la Taifa kuanzia linapokutana kwa mara ya kwanza baada ya uchaguzi mkuu au siku inayorejelewa na Kanuni ya 27 *(Vipindi vya Kawaida vya Bunge la Taifa)* na kukamilika Bunge linapoahirishwa mwishoni mwa mwaka au mwishoni mwa muhula wa Bunge;

“Kikao” ina maana ya muda ambao Bunge la Taifa linaendesha vikao vyake mfululizo bila ahirisho na inajumuisha muda wowote Bunge linapofanya vikao vyake katika Kamati;

“Siku ya Kikao” ina maana ya siku yoyote ambayo Bunge la Taifa linaketi;

(a) Mwenyekiti wa Kamati inajumuisha Spika anapoongoza Kamati ya Bunge zima au Mbunge yeyote anayeongoza kikao;

(b) Spika inajumuisha Naibu Spika au Mbunge yeyote anapoongoza kikao cha Bunge kwa mujibu wa Ibara ya 107 ya Katiba.

(2) Katika Kanuni hizi, kila mara waraka unapotakiwa kutolewa au kuwafikia Wabunge, waraka huo utachukuliwa kuwa umetolewa na kuwafikia Wabunge iwapo umewekwa katika visanduku vya barua vya Wabunge au afisi za Bunge; kielektroniki kupitia anwani rasmi za mawasiliano za Wabunge au nambari zao rasmi za simu au atakavyoelekeza Spika.

**Siwa**

**2A.** Siwa ya Bunge la Taifa ni kielelezo cha mamlaka ya Spika na Bunge la Taifa na itahifadhiwa kwa usalama na Mpambe wa Bunge la Taifa.

**Katibu kupata Mikataba ya Miungano**

**2B.** Katibu atapokea nakala iliyoidhinishwa ya mkataba wowote wa muungano baina ya vyama viwili au zaidi vilivyo ndani ya Bunge la Taifa kutoka kwa Msajili wa Vyama vya Kisiasa kwa minajili ya kuhakikisha wingi wao katika Bunge la Taifa ili kuwezesha utekelezaji wa shughuli za Bunge la Taifa.

## SEHEMU YA II — KUAPISHWA KWA WABUNGE NA UCHAGUZI WA SPIKA

**Shughuli kwenye kikao cha kwanza cha Bunge jipya la Taifa**

**3.** (1) Katika Kikao cha kwanza cha Bunge jipya kufuatia arifa ya Rais kwa mujibu wa Ibara 126(2) ya Katiba, Katibu—

(a) atasoma arifa ya Rais ilivyochapishwa katika *Gazeti Rasmi la Serikali*;

(b) atawasilisha orodha ya majina ya waliochaguliwa kuwa Wabunge juu ya Meza ya Bunge la Taifa; na

(c) atasimamia kiapo au kukiri kuwajibika katika mamlaka ya ubunge kwa Wabunge wote waliomo katika Ukumbi kwa mujibu wa Nyongeza ya Tatu ya Katiba kwa utaratibu ulioorodheshwa katika aya ya (3).

(2) Kwa mujibu wa Ibara ya 74 ya Katiba, hakuna mtu atakayechukua au kutekeleza majukumu ya ofisi ya Mbunge kabla ya kula kiapo au kukiri kuwajibikia mamlaka ya ubunge kulingana na aya ya (1).

(3) Katibu atasimamia kiapo au kukiri kuwajibika katika mamlaka ya ubunge kwa Wabunge waliochaguliwa kwa kufuata mpangilio wa kialfabeti kulingana na utaratibu ufuatao—

(a) Mbunge aliyechaguliwa na aliyewahi kuhudumu katika Bunge la Taifa au Seneti kama—

(i) Spika;

(ii) Kiongozi wa Chama cha walio Wengi;

(iii) Kiongozi wa Chama cha walio Wachache; au

(iv) Naibu Spika;

(b) Wabunge waliochaguliwa na ambao wamehudumu kwa jumla ya muda mrefu zaidi katika Bunge la Taifa;

(c) Wabunge waliochaguliwa na ambao wamehudumu kwa muda mrefu zaidi kwa jumla katika Bunge la Taifa, Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki na Seneti;

(d) Wabunge waliochaguliwa na ambao wamehudumu kwa jumla ya muda mrefu zaidi katika Seneti;

(e) Wabunge waliochaguliwa na ambao wamehudumu kwa jumla ya muda mrefu zaidi katika Bunge la Afrika Mashariki;

(f) Wabunge wengine wote waliochaguliwa.

(4) Katibu anaposimamia kiapo au kukiri kuwajibikia mamlaka ya ubunge kwa Wabunge waliochaguliwa na kabla hajasimamia kiapo cha Spika au kukiri kuwajibikia mamlaka ya Spika, suala lolote litakaloibuka wakati huo litaamuliwa na Katibu ambaye atakuwa na mamlaka ya Spika.

(5) Wakati mwingine wowote ule, Spika atasimamia kiapo cha Wabunge au kukiri kuwajibikia mamlaka ya ubunge mara tu baada ya maombi.

(6) Pindi Mbunge aliyechaguliwa anapohudhuria kikao kwa mara ya kwanza kufuatia uchaguzi mdogo na kabla hajachukua nafasi yake, Mbunge huyo atasindikizwa na Wabunge wawili hadi kwenye Meza na kutambulishwa kwa Spika ambaye atasimamia kiapo au kukiri kuwajibikia mamlaka ya ubunge.

(7) Bila kuzingatia masharti ya Kanuni ya 30 (*Saa za Vikao*), siku ambayo uchaguzi wa Spika umepangwa kufanyika baada ya uchaguzi mkuu, kikao cha Bunge kitaanza saa 3.00 asubuhi hadi mwisho wa shughuli katika Orodha ya Shughuli.

**Kumchagua Spika baada ya Uchaguzi Mkuu**

**4.** Spika atachaguliwa katika kikao cha kwanza cha Bunge la Taifa baada ya Uchaguzi Mkuu na kabla ya Bunge la Taifa kutekeleza shughuli yoyote nyingine, isipokuwa tu shughuli ya kiapo au kukiri kuwajibikia mamlaka ya ubunge kwa Wabunge wachaguliwa waliopo.

**Uteuzi wa wagombeaji**

**5.** (1) Baada ya Rais kutoa arifa ya mahali na tarehe ya kikao cha kwanza cha Bunge jipya kwa mujibu wa Ibara ya 126 (2) ya Katiba, Katibu, kupitia arifa katika *Gazeti Rasmi la Serikali*—

(a) atatoa taarifa ya nafasi ya Spika kuwa wazi na kuwaalika watu wenye nia ya kugombea nafasi hiyo wawasilishe hati zao za uteuzi kwa ajili ya kuchaguliwa kuwa Spika; na

(b) atachagua siku ya uteuzi na kutenga mahali na muda wa kupokea hati za uteuzi.

(2) Majina ya wagombeaji wa ofisi ya Spika yatanakiliwa kwenye hati za uteuzi zitakazochukuliwa kutoka kwa Katibu na kurudishwa kwake angalau saa arobaini na nane kabla ya wakati uliotengwa kwa Bunge kukutana ili kumchagua Spika.

(3) Hati za uteuzi za mgombeaji zitaambatisha majina na saini za Wabunge ishirini wanaomuunga mkono na kuthibitisha kuwa mgombeaji huyo amehitimu kuchaguliwa kama Mbunge kwa mujibu wa Ibara ya 99 ya Katiba na ameridhia kuhudumu kama Spika wa Bunge la Taifa.

(3A) Hati ya uteuzi ya mgombeaji kwa mujibu wa aya (3) itakuwa kwa muundo unaoelekezwa katika Nyongeza ya Tisa.

(4) Katibu atahifadhi sajili ikionyesha tarehe na wakati hati za uteuzi za kila mgombeaji zilipopokewa na atathibitisha iwapo kila mgombeaji katika uchaguzi wa ofisi ya Spika anahitimu kuchaguliwa kama Spika kwa mujibu wa Ibara ya 106 ya Katiba.

(5) Mara tu muda wa uteuzi kwa mujibu wa aya ya (2) utakapokamilika, Katibu—

(a) atatangaza na kuwapa Wabunge wote orodha ya wagombeaji waliohitimu; na

(b) atawapa Wabunge wote nakala za wasifukazi za wagombeaji waliohitimu.

(6) Katibu atatayarisha karatasi za kura zinazoonyesha majina ya wagombeaji wote walioteuliwa ipasavyo angalau saa mbili kabla ya Kikao cha Bunge la Taifa kwa mujibu wa aya ya (5) ya Kanuni hii.

**Kura ya siri**

**6.** (1) Uchaguzi wa Spika utafanyika kwa kura ya siri.

(2) Mwanzoni mwa kila shughuli ya kupiga kura, Katibu ataelekeza sanduku tupu lililo wazi lionyeshwe katika Ukumbi kisha atalifunga na kuliweka hadharani kwenye Ukumbi hadi shughuli ya uchaguzi itakapokamilika.

(3) Katibu atampa kila Mbunge atakayekuja kwenye Meza karatasi moja pekee ya kura na kila atakayetaka kupiga kura ataelekea kwenye eneo lililotengwa na Katibu kwa ajili hiyo na Mbunge huyo ataweka alama kwenye nafasi mkabala na jina la Mgombeaji anayemtaka awe Spika kisha ataikunja na kuitumbukiza karatasi hiyo katika sanduku la kura.

(4) Mbunge ambaye kabla ya shughuli ya upigaji kura kumalizika atakosea katika kuweka alama kwenye karatasi ya kura ataruhusiwa kumrudishia Katibu karatasi hiyo, na papo hapo Katibu ataibatilisha na kumpa Mbunge huyo karatasi nyingine.

(5) Katibu ataweka mipangilio itakayomwezesha Mbunge yeyote mwenye ulemavu kupiga kura.

(6) Baada ya Katibu kubaini kwamba Wabunge wote walio katika Ukumbi na wanaotaka kupiga kura wamepiga kura na kutumbukiza karatasi za kura kwenye sanduku la kura, Katibu atalifungua sanduku na kukagua karatasi za kura, na akishazikagua, ataziondoa zile zisizo na alama au zilizoharibika kisha atatangaza matokeo ya kura; na hakuna Mbunge atakayeruhusiwa kupiga kura baada ya sanduku kufunguliwa.

(7) Karatasi ya kura itakuwa imeharibika iwapo, kwa maoni ya Katibu, karatasi hiyo haibainishi mgombeaji aliyepigiwa kura.

**Viwango vya upeo wa kuchaguliwa**

**7.** (1) Mgombeaji atachaguliwa kuwa Spika iwapo atapata thuluthi mbili ya kura za Wabunge wote.

(2) Iwapo hakuna mgombeaji aliyepata thuluthi mbili ya kura za Wabunge wote, mgombeaji au wagombeaji waliopata idadi ya juu zaidi ya kura kwa mujibu wa aya ya (1)

(3) na mgombeaji au wagombeaji waliopata idadi ya pili kwa wingi wa kura ndio hao tu watapigiwa kura katika awamu ya pili na mgombeaji atakayepata kura nyingi zaidi katika awamu ya pili atakuwa amechaguliwa kuwa Spika.

**Kujiondoa kwa Mgombeaji**

**8.** Mgombeaji anaweza kujiondoa kwenye uchaguzi kwa kumuarifu Katibu kwa maandishi kabla ya shughuli ya uchaguzi kuanza na kujiondoa huko kunapotokea, Katibu atafuta jina la mgombeaji huyo kwenye karatasi za kura zilizopigwa chapa kwa ajili ya uchaguzi huo au za kura yoyote itakayofuata.

**Idadi sawa ya kura**

**9.** Iwapo katika awamu nyingine ya kura kwa mujibu wa Kanuni ya 7 (*Viwango vya upeo wa kuchaguliwa*) zaidi ya mgombeaji mmoja atapata kura nyingi, awamu nyingine ya kura itafanywa na iwapo zaidi ya mgombeaji mmoja atapata idadi sawa ya kura, upigaji kura utarudiwa hadi mgombeaji mmoja atakapopata kura nyingi kuliko mwingine au wengine.

**Uhifadhi wa karatasi za kura**

**10.** Mara tu baada ya matokeo kutangazwa, karatasi zote za kura zilizotumiwa katika uchaguzi wa Spika na karatasi zozote za kura zilizoharibika zitakusanywa na kufungwa mbele ya kikao cha Bunge la Taifa, kuhifadhiwa na Katibu kwa muda wa miezi sita na baadaye kuharibiwa.

**Mgombeaji mmoja anapoteuliwa kikamilifu**

**11.** Licha ya masharti ya Sehemu hii, iwapo mgombeaji mmoja tu ameteuliwa kwa uchaguzi wa Spika kipindi cha uteuzi kinapomalizika, mgombeaji huyo atatangazwa mara moja kama aliyechaguliwa kuwa Spika bila uchaguzi au kura yoyote kuhitajika.

**Kuapishwa kwa Spika**

**12.** Mara tu baada ya uchaguzi wa Spika, Katibu atamlisha kiapo cha Spika au kiapo cha kukiri kuwajibikia mamlaka ya Spika mbele ya Wabunge walio katika Ukumbi.

## SEHEMU YA IIA— KUJIONDOA AU KUONDOLEWA KATIKA OFISI YA SPIKA NA NAIBU SPIKA

**Kujiuzulu**

**12A.** (1) Ofisi ya Spika au Naibu Spika itakuwa wazi iwapo anayeshikilia ofisi hiyo amejiuzulu kupitia barua kwa Bunge kwa mujibu wa Ibara ya 106(2)(d) ya Katiba.

(1A) Barua kwa mujibu wa aya ya (1) itawasilishwa kwa Katibu.

(2) Mara tu baada ya kupokea barua ya kujiuzulu, Katibu, bila kuchelewa—

(a) atamjulisha Naibu Spika, iwapo anayejiuzulu ni Spika; au

(b) atamjulisha Spika, iwapo anayejiuzulu ni Naibu Spika.

(3) Bunge la Taifa litajulishwa kuhusu kujiuzulu kwa mujibu wa Kanuni hii katika muda usiozidi siku saba.

**Kuondolewa mamlakani**

**12B.** (1) Iwapo Mbunge ataungwa mkono na angalau thuluthi moja ya Wabunge wote, Mbunge huyo anaweza kupendekeza hoja ya kumwondoa Spika au Naibu Spika kutokana na—

(a) ukiukaji mkubwa wa masharti ya Katiba au sheria nyingine ikijumuisha ukiukaji wa Sura ya Sita ya Katiba;

(b) utovu mkubwa wa nidhamu katika utekelezaji wa majukumu ya Spika au Naibu Spika au vinginevyo;

(c) kutokuwa na uwezo wa kimwili au kiakili wa kutekeleza majukumu ya ofisi;

(d) kushindwa kutekeleza majukumu ya ofisi; au

(e) kufilisika.

(2) Kabla ya kutoa arifa ya Hoja kwa mujibu wa aya ya (1), Mbunge atamwasilishia Katibu, kwa maandishi, nakala ya Hoja anayopendekeza—

(a) ikitaja misingi na maelezo ya Hoja anayopendekeza;

(b) iliyotiwa saini na Mbunge huyo;

(c) yenye saini za uungwaji mkono za angalau thuluthi moja ya Wabunge wote.

(3) Mbunge hataruhusiwa kuondoa saini yake ya kuunga mkono hoja mara baada ya Hoja hiyo kupokelewa na Katibu.

(4) Mbunge atatoa arifa ya siku tatu ya hoja iliyotolewa kwa mujibu wa aya ya (1) kwa muda usiopita siku tatu baada ya hoja kuidhinishwa.

(5) Katibu ataorodhesha Hoja kwenye Ratiba ya Shughuli ikibainisha —

(a) misingi na maelezo ya Hoja iliyopendekezwa;

(b) jina la Mbunge anayedhamini Hoja; na

(c) majina ya Wabunge wanaounga mkono Hoja hiyo.

(6) Iwapo Hoja hiyo itapitishwa—

(a) Bunge la Taifa litateua kamati ya Wabunge kumi na mmoja kuchunguza suala hilo; na

(b) Kamati itachunguza suala hilo kwa muda usiopita siku saba na kulijulisha Bunge la Taifa ikiwa tuhuma dhidi ya Spika au Naibu Spika zinathibitika.

(7) Spika au Naibu Spika ana haki ya kufika na kuwakilishwa mbele ya kamati wakati wa uchunguzi huo.

(8) Iwapo kamati itaripoti kwamba imebaini kuwa tuhuma —

(a) hazithibitiki, hakuna hatua zaidi zitakazochukuliwa; au

(b) zinathibitika, Bunge la Taifa—

(i) litampa Spika au Naibu Spika ripoti ya Kamati pamoja na ushahidi mwingine wowote uliotolewa na nyaraka zilizowasilishwa kwenye kamati angalau siku tatu kabla ya siku aliyotengewa kufika mbele ya Bunge la Taifa;

(ii) litatoa nafasi kwa Spika au Naibu Spika ili kusikilizwa;

(iii) litashughulikia Ripoti ya Kamati; na

(iv) litapiga kura iwapo litaidhinisha uamuzi wa kumwondoa Spika au Naibu Spika mamlakani.

(9) Iwapo uamuzi wa kumwondoa Spika au Naibu Spika mamlakani utaungwa mkono na angalau thuluthi mbili ya Wabunge, Spika au Naibu Spika ataondoka mamlakani.

**Kuondoka mamlakani kwa mujibu wa Ibara ya 103 ya Katiba**

**12C.** (1) Ofisi ya Spika au Naibu Spika itakuwa wazi iwapo anayeshikilia ofisi hiyo ameondoka mamlakani kwa mujibu wa Ibara ya 103 ya Katiba.

(2) Iwapo nafasi ya Spika itakuwa wazi wakati wowote kabla ya mwisho wa muhula wa Bunge, hakuna shughuli ya Bunge itakayoendeshwa hadi Spika mwingine atakapochaguliwa.

(3) Naibu Spika ataongoza uchaguzi kwa mujibu wa aya ya (1) lakini iwapo Naibu Spika ni mgombeaji, Mbunge atakayechaguliwa na Bunge la Taifa kwa mujibu wa Ibara ya 107 ya Katiba ataongoza uchaguzi huo.

## SEHEMU YA III—NAIBU SPIKA NA MWENYEKITI WA KAMATI

**Uchaguzi wa Naibu Spika**

**13.** (1) Baada ya Uchaguzi Mkuu na haraka iwezekanavyo baada ya uchaguzi wa Spika, uchaguzi wa Naibu Spika utafanyika.

(2) Iwapo nafasi ya Naibu Spika itakuwa wazi wakati wowote kabla ya muhula wa Bunge kumalizika, haraka iwezekanavyo, Bunge la Taifa litamchagua Mbunge yeyote kwenye wadhifa huo.

(3) Utaratibu wa kumchagua Naibu Spika utakuwa sawa na ule uliowekwa kumchagua Spika, ukifanyiwa mabadiliko kadri itakavyohitajika.

**Arifa ya ufunguzi wa Bunge**

**14.** (1) Baada ya kula kiapo au kukiri kuwajibikia mamlaka ya Spika kwa mujibu wa Kanuni ya 12 (*Kuapishwa kwa Spika*), Spika atawaarifu Wabunge mahali, tarehe na saa ya ufunguzi rasmi wa Bunge, ambayo haitakuwa zaidi ya siku thelathini baada ya kikao cha kwanza cha Bunge la Taifa.

(2) Kufuatia arifa ya Spika iliyotolewa kwa mujibu wa aya ya (1), kikao cha Bunge la Taifa kitaahirishwa hadi tarehe na saa ya ufunguzi rasmi wa Bunge.

**Mwenyekiti wa Kamati za Bunge la Taifa**

**15.** (1) Naibu Spika atakuwa Mwenyekiti wa Kamati za Bunge la Taifa na ataongoza vikao vya Kamati za Bunge Zima.

(2) Iwapo Naibu Spika hayupo au ameamua kushiriki mjadala wowote kwenye Kamati ya Bunge Zima kama Mbunge wa kawaida, Spika ataongoza kikao kinachohusika.

## Jopo la Mwenyekiti

**16.** (1) Kutakuwa na jopo litakalojulikana kama Jopo la Mwenyekiti litakalokuwa na Wajumbe sita watakaotambulika kama Mwenyekiti wa Kwanza, wa Pili, wa Tatu, wa Nne, wa Tano na wa Sita mtawalia na watatekeleza mamlaka yote ya Mwenyekiti wa Kamati.

(2) Kufuatia uchaguzi Mkuu na mara itakapowezekana baada ya uchaguzi wa Naibu Spika, Spika akishauriana na viongozi wa vyama bunge, atawasilisha orodha ya majina ya Wabunge sita kwa Kamati ya Kuratibu Shughuli za Bunge la Taifa kwa ajili ya kujadiliwa.

(3) Kamati ya Kuratibu Shughuli za Bunge itawasilisha majina ya walioteuliwa Bungeni na kutoa arifa ya Hoja ya kuwaidhinisha kwa muda usiopita siku saba baada ya kuyapokea.

(4) Kila mara Hoja ya kuidhinisha Wanajopo kwa mujibu wa aya ya (3) inapotolewa Bungeni, hakutaruhusiwa pingamizi dhidi ya Mwanajopo mmoja na iwapo pingamizi litakuwapo, litachukuliwa kuwa dhidi ya wanajopo wote.

(5) Katika kuwateua wajumbe wa Jopo la Mwenyekiti, Spika na Kamati ya Kuratibu Shughuli za Bunge watazingatia wingi wa Wabunge katika vyama Bunge na kwa kadri itakavyowezekana, angalau mwanajopo mmoja awe wa jinsia tofauti.

## Kumwondoa Mjumbe kwenye Jopo la Mwenyekiti

**17.** (1) Spika ataiarifu, kwa maandishi, Kamati ya Kuratibu Shughuli za Bunge la Taifa kuhusu kuondolewa kwa Mjumbe kwenye Jopo la Mwenyekiti.

(2) Kamati ya Kuratibu Shughuli za Bunge la Taifa itashughulikia arifa hiyo na kutoa Arifa ya Hoja ya kumbadilisha mjumbe huyo kwa muda usiozidi siku saba baada ya kupokea arifa kwa mujibu wa aya ya (1).

**Kuongoza Kikao cha Bunge la Taifa**

**18.** (1) Spika ataongoza kikao chochote cha Bunge la Taifa na asipokuwepo, kikao kitaongozwa na Naibu Spika na iwapo Spika na Naibu Spika hawapo, Mbunge aliyechaguliwa kwa lengo hilo kuambatana na Ibara ya 107 ya Katiba ataongoza kikao.

(2) Kuidhinishwa kwa Mwenyekiti wa Kwanza, wa Pili, wa Tatu na wa Nne kwa mujibu wa Kanuni ya 16 (*Jopo la Mwenyekiti*) kutachukuliwa kuwa uchaguzi kulingana na aya ya (1) na yeyote kati yao anaweza kuongoza vikao vya Bunge la Taifa iwapo Spika na Naibu Spika hawapo.

## SEHEMU YA IV — KIONGOZI WA CHAMA CHA WALIO WENGI NA KIONGOZI WA CHAMA CHA WALIO WACHACHE

**Viongozi wa Vyama na itifaki**

**19.** (1) Kwa mujibu wa Ibara ya 108 ya Katiba, kutakuwepo Kiongozi wa Chama cha walio Wengi na Kiongozi wa Chama cha walio Wachache.

(2) Kiongozi wa Chama cha walio Wengi atakuwa Mbunge aliye kiongozi katika Bunge la Taifa wa chama au muungano wa vyama unaoongoza kwa idadi ya Wabunge.

(3) Kiongozi wa Chama cha walio Wachache atakuwa Mbunge aliye kiongozi katika Bunge la Taifa wa chama au muungano wa vyama wenye idadi inayofuatia kwa wingi wa Wabunge.

(4) Itifaki ifuatayo itazingatiwa katika Bunge la Taifa—

(a) Spika wa Bunge la Taifa;

(b) Kiongozi wa Chama cha walio Wengi; na

(c) Kiongozi wa Chama cha walio Wachache.

(5) Spika atawezesha Kiongozi wa Chama cha walio Wengi na Kiongozi wa Chama cha walio Wachache kutekeleza shughuli za Bunge la Taifa kwa niaba ya vyama au miungano yao katika Bunge la Taifa.

**Kuchaguliwa na Kuondolewa mamlakani kwa Kiongozi wa Chama cha walio Wengi na Naibu Kiongozi wa Chama cha walio Wengi**

**19A.** (1) Chama kilicho na idadi kubwa zaidi ya Wabunge au muungano wa vyama ulio na idadi kubwa zaidi ya Wabunge katika Bunge la Taifa utamchagua—

(a) Mbunge wa Bunge la Taifa kutoka chama hicho au muungano huo wa vyama awe Kiongozi wa Chama cha walio Wengi; na

(b) Mbunge wa Bunge la Taifa kutoka chama hicho au muungano huo wa vyama awe Naibu Kiongozi wa Chama cha walio Wengi;

(2) Katika kuchagua Wabunge kwa mujibu wa aya ya (1), chama kilicho na idadi kubwa zaidi ya Wabunge au muungano wa vyama ulio na idadi kubwa zaidi ya Wabunge katika Bunge la Taifa utazingatia—

(a) mkataba wowote uliopo wa muungano ulioafikiwa kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Kisiasa; na

(b) umuhimu wa kuwepo kwa usawa wa kijinsia.

(3) Mratibu wa Chama cha walio Wengi atamwasilishia Spika kwa maandishi majina ya Wabunge waliochaguliwa kwa mujibu wa aya ya (1) kwa niaba ya Chama cha walio Wengi.

(4) Mara itakapowezakana, Spika atawasilisha majina aliyopokea kwa mujibu wa aya ya (3) kwenye kikao cha Bunge au kuwaarifu Wabunge iwapo Bunge haliko kwenye vikao.

(5) Mbunge wa chama kilicho na idadi kubwa zaidi ya Wabunge au muungano wa vyama ulio na idadi kubwa zaidi

ya Wabunge anaweza kupendekeza kuondolewa kwa Mbunge aliyechaguliwa kwa mujibu wa aya ya (1) kwa kuwasilisha hoja izingatiwe na chama kilicho na idadi kubwa zaidi ya Wabunge au muungano wa vyama ulio na idadi kubwa zaidi ya Wabunge pamoja na majina na saini za angalau robo ya Wabunge wote wa chama kilicho na idadi kubwa zaidi ya Wabunge au muungano wa vyama ulio na idadi kubwa zaidi ya Wabunge wanaomuunga mkono.

(6) Mbunge aliyechaguliwa kwa mujibu wa aya ya (1) anaweza kuondolewa kwa wingi wa kura za Wabunge wa chama kilicho na idadi kubwa zaidi ya Wabunge au muungano wa vyama ulio na idadi kubwa zaidi ya Wabunge katika Bunge la Taifa.

(7) Mratibu wa Chama cha walio Wengi, kufuatia uamuzi wa chama kilicho na idadi kubwa zaidi ya Wabunge au muungano wa vyama ulio na idadi kubwa zaidi ya Wabunge, atamwarifu Spika kwa maandishi kuhusu uamuzi wa chama kilicho na idadi kubwa zaidi ya Wabunge au muungano wa vyama ulio na idadi kubwa zaidi ya Wabunge kumwondoa Mbunge aliyechaguliwa kwa mujibu wa aya ya (1) na kuwasilisha—

(a) kumbukumbu za mkutano wa chama kilicho na idadi kubwa zaidi ya Wabunge au za muungano wa vyama ulio na idadi kubwa zaidi ya Wabunge uliofanya uamuzi huo; na

(b) majina na saini za Wabunge waliokutana na kuamua kumwondoa Mbunge huyo.

(8) Baada ya kupokea arifa na nyaraka kwa mujibu wa aya ya (7) na kuthibitisha kuwa kiwango cha kumwondoa Mbunge kimefikiwa, Spika ataliarifu Bunge kuhusu uamuzi huo wa chama kilicho na idadi kubwa zaidi ya Wabunge au za muungano wa vyama ulio na idadi kubwa zaidi ya Wabunge na wadhifa wa Mbunge aliyechaguliwa kwa mujibu wa aya ya (1) utakuwa wazi.

**Kuchaguliwa na Kuondolewa kwa Kiongozi wa Chama cha walio Wachache na Naibu Kiongozi wa Chama cha walio Wachache**

**20.** (1) Chama kilicho na idadi ya pili kwa wingi wa Wabunge au muungano wa vyama ulio na idadi ya pili kwa wingi wa Wabunge katika Bunge la Taifa utamchagua—

(a) Mbunge wa Bunge la Taifa aliye mwanachama wa chama kilicho na idadi ya pili kwa wingi wa Wabunge au muungano wa vyama ulio na idadi ya pili kwa wingi wa Wabunge kuwa Kiongozi wa Chama cha walio Wachache; na

(b) Mbunge wa Bunge la Taifa aliye mwanachama wa chama kilicho na idadi ya pili kwa wingi wa Wabunge au muungano wa vyama ulio na idadi ya pili kwa wingi wa Wabunge kuwa Naibu Kiongozi wa Chama cha walio Wachache.

(2) Katika kuwachagua wabunge kwa mujibu wa aya ya (1), chama kilicho na idadi ya pili kwa wingi wa Wabunge au muungano wa vyama ulio na idadi ya pili kwa wingi wa Wabunge katika Bunge la Taifa utazingatia—

(a) mkataba wowote uliopo wa muungano ulioafikiwa kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Kisiasa; na

(b) umuhimu wa kuwepo kwa usawa wa kijinsia.

(3) Mratibu wa Chama cha walio Wachache atamwasilishia Spika kwa maandishi majina ya Wabunge waliochaguliwa kwa mujibu wa aya ya (1) kwa niaba ya Chama cha walio Wengi.

(4) Mara itakapowezekana, Spika atawasilisha majina aliyopokea kwa mujibu wa aya ya (3) kwenye kikao cha Bunge au kuwaarifu Wabunge iwapo Bunge haliko kwenye vikao.

(5) Mbunge wa chama kilicho na idadi ya pili kwa wingi wa Wabunge au muungano wa vyama ulio na idadi ya pili kwa wingi wa Wabunge anaweza kupendekeza kuondolewa

kwa Mbunge aliyechaguliwa kwa mujibu wa aya ya (1) kwa kuwasilisha hoja izingatiwe na chama kilicho na idadi ya pili kwa wingi wa Wabunge au muungano wa vyama ulio na idadi ya pili kwa wingi wa Wabunge pamoja na majina na saini za angalau robo ya Wabunge wote wa chama kilicho na idadi ya pili kwa wingi wa Wabunge au muungano wa vyama ulio na idadi ya pili kwa wingi wa Wabunge wanaomuunga mkono.

(6) Mbunge aliyechaguliwa kwa mujibu wa aya ya (1) anaweza kuondolewa kwa wingi wa kura za Wabunge wa chama kilicho na idadi ya pili kwa wingi wa Wabunge au muungano wa vyama ulio na idadi ya pili kwa wingi wa Wabunge katika Bunge la Taifa.

(7) Mratibu wa Chama cha walio Wachache, mara kufuatia uamuzi wa chama kilicho na idadi ya pili kwa wingi wa Wabunge au muungano wa vyama ulio na idadi ya pili kwa wingi wa Wabunge, atamwarifu Spika kwa maandishi kuhusu uamuzi wa chama kilicho na idadi ya pili kwa wingi wa Wabunge au muungano wa vyama ulio na idadi ya pili kwa wingi wa Wabunge, kumwondoa Mbunge aliyechaguliwa kwa mujibu wa aya ya (1) na kuwasilisha—

- (a) kumbukumbu za mkutano wa chama kilicho na idadi ya pili kwa wingi wa Wabunge au za muungano wa vyama ulio na idadi ya pili kwa wingi wa Wabunge uliofanya uamuzi huo; na
- (b) majina na saini za Wabunge waliokutana na kuamua kumwondoa Mbunge huyo.

(8) Baada ya kupokea arifa na nyaraka kwa mujibu wa aya ya (7) na kuthibitisha kuwa kiwango cha kumwondoa Mbunge kimefikiwa, Spika ataliarifu Bunge kuhusu uamuzi huo wa chama kilicho na idadi ya pili kwa wingi wa Wabunge au za muungano wa vyama ulio na idadi ya pili kwa wingi wa Wabunge na wadhifa wa Mbunge aliyechaguliwa kwa mujibu wa aya ya (1) utakuwa wazi.

**Kutambuliwa kwa Vyama Bunge na Kuteuliwa kwa Viongozi na Waratibu**

**20A.** (1) Spika atatambua chama au muungano wa vyama ulio na angalau asilimia tano ya Wabunge wote wa Bunge la Taifa kuwa Chama Bunge.

(2) Kwa kuzingatia Kanuni ya 19A (*Kuchaguliwa na Kuondolewa mamlakani kwa Kiongozi wa Chama cha walio Wengi na Naibu Kiongozi wa Chama cha walio Wengi*) na Kanuni ya 20 (*Kuchaguliwa na Kuondolewa kwa Kiongozi wa Chama cha walio Wachache na Naibu Kiongozi wa Chama cha walio Wachache*) Chama Bunge kitateua kutoka miongoni mwa Wabunge wake—

(a) kiongozi wake katika Bunge la Taifa na kumwarifu Spika jina la Mbunge aliyeteuliwa kwa maandishi; na

(b) Mratibu na Naibu Mratibu wa Chama kwa minajili ya kutekeleza shughuli za Bunge.

(3) Majina ya Wabunge walioteuliwa kuwa waratibu wa vyama yatawasilishwa kwa Spika kwa maandishi na—

(a) Kiongozi wa Chama cha walio Wengi kwa niaba ya Chama cha walio Wengi;

(b) Kiongozi wa Chama cha walio Wachache kwa niaba ya Chama cha walio Wachache; au

(c) Kiongozi wa Chama Bunge katika Bunge la Taifa iwapo Chama Bunge hicho sio sehemu ya muungano unaounda Chama cha walio Wengi au Chama cha walio Wachache.

(4) Uamuzi wa Chama Bunge kubadilisha mratibu au naibu mratibu wake utawasilishwa kwa Spika kwa maandishi na—

(a) Kiongozi wa Chama cha walio Wengi kwa niaba ya Chama cha walio Wengi;

(b) Kiongozi wa Chama cha walio Wachache kwa niaba ya Chama cha walio Wachache; au

(c) Kiongozi wa Chama Bunge katika Bunge la Taifa iwapo Chama Bunge hicho sio sehemu ya muungano unaounda Chama cha walio Wengi au Chama cha walio Wachache.

(5) Mara itakapowezekana, baada ya kupokea majina kwa mujibu wa aya ya (2) na ya (3) au uamuzi kwa mujibu wa aya ya (4) Spika atawasilisha taarifa hiyo kwenye kikao cha Bunge au kuwaarifu Wabunge iwapo Bunge haliko kwenye vikao.

## SEHEMU YA V—HOTUBA YA RAIS, MGENI MASHUHURI AU WAGENI WENGINE

**Hotuba ya Rais wakati wa ufunguzi rasmi wa Bunge jipya**

**21.** (1) Rais atahutubia Bunge wakati wa ufunguzi rasmi wa kila Bunge jipya.

(2) Rais atakapokamilisha hotuba yake, Spika atasitisha au kuahirisha kikao hadi wakati au siku atakayoitaja.

**Hotuba ya Rais wakati wa vikao maalum**

**22.** (1) Rais atahutubia kikao maalum cha Bunge mara moja kila mwaka na anaweza kuhutubia Bunge wakati mwingine wowote.

(2) Kwa mujibu wa aya ya (1), Spika atawaarifu Wabunge kuhusu mahali, tarehe na wakati wa kikao.

(3) Spika anapoarifiwa kwamba Rais atahutubia kikao maalum cha Bunge siku na saa iliyotajwa, siku hiyo hakutakuwa na Hoja ya kuahirisha Bunge kabla ya wakati ambao Rais amepangiwa kuwasili.

**Rais anapoingia au anapoondoka katika Ukumbi**

**23.** Rais anapoingia au anapoondoka katika Ukumbi, Wabunge watahitajika kuwa watulivu na kusimama kimya.

**Hotuba ya Rais kwa Bunge**

**24.** (1) Rais anaweza kuandamana na Mpambe wake wa kijeshi katika Ukumbi.

(2) Rais anapohutubia Bunge, Spika wa Bunge la Taifa ataketi upande wa kulia wa Rais na Spika wa Seneti ataketi upande wa kushoto wa Rais.

(3) Kikao chochote kitakachofanyika kwa mujibu wa Kanuni hii kitaongozwa na Spika wa Bunge la Taifa akisaidiwa na Spika wa Seneti.

(4) Rais anapohutubia Bunge, Wabunge watahitajika kuwa kimya wakimsikiliza na atakapokamilisha hotuba, hakutakuwa na maoni au swali lolote.

(5) Kila mara baada ya hotuba ya Rais, Mbunge yeyote anaweza kuwasilisha nakala ya hotuba ya Rais kwenye Meza ya Bunge la Taifa haraka iwezekanavyo.

(6) Mbunge anaweza kutoa arifa ya Hoja ***"Kwamba shukrani za Bunge la Taifa zinakiliwe kwa ajili ya ufafanuzi wa sera ya umma kwenye Hotuba ya Rais iliyotolewa mnamo…;"*** lakini mjadala kuhusu hoja hiyo hautazidi vikao vinne vya Bunge la Taifa.

**Mgeni mashuhuri**

**25.** (1) Spika, kwa kushauriana na Kiongozi wa Chama cha Walio Wengi na Kiongozi wa Chama cha Walio Wachache, anaweza kuruhusu Rais wa taifa lingine au mgeni yeyote mashuhuri kuhutubia Bunge la Taifa na anaweza kushauriana na Spika wa Seneti kupanga kikao cha pamoja cha Bunge kwa ajili ya Rais au mgeni huyo mashuhuri kuhutubia Bunge.

(2) Kanuni ya 23 (*Rais anapoingia au anapoondoka katika Ukumbi*) na aya ya (1), (3) na (4) ya Kanuni ya 24 (*Hotuba ya Rais kwa Bunge*), kadri inavyowezekana, zitatumika wakati Wakuu wa Nchi nyingine na mgeni yeyote mashuhuri anapohutubia Bunge.

**Kutenga sehemu maalum katika Ukumbi kwa ajili ya Mawaziri na watu wengine**

**25A.** Spika anaweza kutenga sehemu maalum katika Ukumbi au kwenye Kizuio maalum cha Ukumbi ili —

(a) Waziri anayehusika na masuala ya fedha atangaze vidokezo vya sera ya bajeti na mikakati ya ukusanyaji wa mapato ya serikali ya taifa kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma;

(b) Waziri afafanue sera ya serikali, ajibu Maswali na awasilishe ripoti kuhusu masuala yaliyo chini ya usimamizi wake;

(c) watu wengine watoe mawasilisho yao katika Ukumbi.

## SEHEMU YA VI — KALENDA, VIKAO NA MAAHIRISHO YA BUNGE LA TAIFA

**Mahali pa kikao cha kwanza cha Bunge jipya**

**26.** Kila baada ya Bunge jipya kuchaguliwa, Rais atatoa arifa katika *Gazeti Rasmi la Serikali* akitaja mahali na tarehe ya kikao cha kwanza cha Bunge jipya ambayo haitakuwa zaidi ya siku thelathini baada ya uchaguzi.

**Vipindi vya kawaida vya Bunge la Taifa**

**27.** (1) Vipindi vya kawaida vya Bunge vitaanza Jumanne ya pili ya Februari na kuhitimishwa mnamo Alhamisi ya kwanza ya Desemba isipokuwa Kipindi cha kwanza baada ya Uchaguzi Mkuu.

(2) Licha ya aya ya (1), Bunge la Taifa linaweza kufanya uamuzi kubadilisha tarehe iliyotajwa katika aya ya (1) kuhusiana na Kipindi mahususi.

(3) Kwa kuzingatia masharti ya aya ya (1), Bunge la Taifa litaendelea na vikao na linaweza kuahirisha vikao hivyo kwa siku kadhaa kama litakavyoamua katika kalenda yake.

(4) Licha ya aya (1), (2) na (3), Bunge la Taifa halitakuwa na mapumziko yanayozidi miezi mitatu kutoka kikao cha mwisho cha Kipindi na kikao cha kwanza cha Kipindi kinachofuata.

**Kalenda ya Bunge la Taifa**

**28.** (1) Kamati ya kuratibu shughuli za Bunge la Taifa itapanga Kalenda itakayoidhinishwa na Bunge la Taifa.

(2) Baada ya kuidhinishwa, Kalenda ya Bunge la Taifa itachapishwa kwenye *Gazeti Rasmi la Serikali*, wavuti wa Bunge na angalau kwenye magazeti mawili yanayosambazwa nchini kote.

(3) Siku ambayo imepangwa Bunge la Taifa kuahirishwa hadi siku isiyokuwa ya kawaida ya kikao inayofuata kwa mujibu wa Kalenda ya Bunge la Taifa, Spika atawaarifu Wabunge, na ifikapo wakati wa kuahirisha kikao, Bunge la Taifa litaahirishwa bila kutoa Hoja iamuliwe.

(4) Licha ya aya (2), Bunge la Taifa linaweza kufanya uamuzi wa kubadilisha Kalenda yake au siku ya kuahirishwa kwake.

**Vikao maalum vya Bunge la Taifa**

**29.** (1) Wakati wowote katika Kipindi Bunge la Taifa linapokuwa limeahirishwa, iwe siku ya kikao kinachofuata imetajwa au la, Spika anaweza kuamua siku ya kikao maalum cha Bunge la Taifa baada ya kupokea ombi la Kiongozi wa Chama cha walio Wengi au Kiongozi wa Chama cha walio Wachache.

(2) Spika anaweza kuruhusu ombi lililotolewa kwa mujibu wa aya ya (1) ikiwa ataridhika kuwa shughuli inayopendekezwa inahusiana na masuala yaliyotajwa katika Kanuni ya 61 (*Maana ya Hoja Maalum*) au shughuli nyingine yoyote ya dharura na ya kipekee kadri Spika atakavyoamua.

(3) Spika atawaarifu Wabunge kupitia tangazo katika *Gazeti Rasmi la Serikali* kuhusu mahali, tarehe na wakati ambao kikao maalum cha Bunge la Taifa kimepangwa kufanyika.

(4) Licha ya aya ya (1), iwapo shughuli ya Bunge la Taifa inayopendekezwa inahitaji Seneti kuchukua hatua, Spika wa Bunge la Taifa atamwarifu Spika wa Seneti kwa maandishi kuhusu tarehe ambayo kikao maalum kimepangwa kufanyika.

(5) Wakati wowote Bunge la Taifa linapokutana kwa kikao maalum kwa mujibu wa aya ya (1), Spika atabainisha shughuli zilizopangwa kushughulikiwa siku hiyo au siku hizo na shughuli hizo pekee ndizo zitakazoshughulikiwa katika kikao hicho na baadaye kikao kitaahirishwa hadi siku iliyotajwa katika kalenda ya Bunge la Taifa.

(6) Bunge linapoandaa kikao maalum siku yoyote kati ya vipindi vyake viwili, kikao hicho kitachukuliwa kama kilichoandaliwa ndani ya kipindi kinachotangulia kikao hicho.

**Saa za vikao**

**30.** (1) Bunge la Taifa litakutana Jumatano saa 3.30 asubuhi na saa 8.30 mchana siku ya Jumanne, Jumatano na Alhamisi isipokuwa kama Spika ataelekeza vinginevyo kwa kuzingatia unafuu wa Bunge la Taifa ingawa kikao zaidi ya kimoja kinaweza kufanyika siku iyo hiyo.

(2) Isipokuwa kama Spika au Mwenyekiti wa Kamati ataelekeza kusitishwa kwa shughuli kabla au baada ya saa iliyoratibiwa kwa ajili ya unafuu wa Bunge la Taifa, Spika au Mwenyekiti wa Kamati atasitisha shughuli itakayokuwa ikiendelea na iwapo Bunge la Taifa liko katika Kamati ya Bunge Zima, Mwenyekiti ataondoka kwenye Kiti na kutoa

taarifa ya hatua iliyofikiwa na kuomba idhini ya kufanya kikao tena—

(a) saa 7.00 mchana kama ni kikao cha asubuhi;

(b) saa 1.00 usiku kama ni kikao cha Jumanne na Alhamisi mchana;

(c) saa 3.00 usiku kama ni kikao cha Jumatano mchana; au

(d) iwapo ni Siku Tengwa—

(i) saa 1.30 usiku kama ni kikao cha Jumanne na Alhamisi mchana;

(ii) saa 3.30 usiku kama ni kikao cha Jumatano mchana.

(3) Bila kuzingatia aya ya (1) na ya (2), Bunge la Taifa linaweza kuamua—

(a) kuongeza muda wa kikao; au

(b) kukutana saa nyingine yoyote siku ya kikao; au

(c) kukutana siku nyingine yoyote ili kutekeleza shughuli.

(4) Hoja kwa mujibu wa aya ya (3)(a) itatolewa angalau dakika thelathini kabla ya wakati uliopangwa kuahirisha kikao.

(5) Iwapo wakati uliopangwa kusitisha shughuli umefika na kura ya mgawanyiko inaendelea au hoja imetolewa na Kiongozi wa Kikao ili iamuliwe na kura ya mgawanyiko ikaibuka papo hapo, kikao hakitasitishwa hadi hesabu ya kura na matokeo ya kura ya mgawanyiko kutangazwa.

(6) Spika ataahirisha kikao bila kuhoji Bunge la Taifa pindi shughuli zote zilizopangwa kwenye Ratiba ya shughuli kwa mujibu wa aya ya (2), (3) au (4) ya Kanuni hii zitakapokamilika mapema au kuahirishwa.

**Kuahirisha Kikao**

**31.** (1) Wakati wowote Mbunge anaweza kuomba kutoa hoja ***"Kwamba, kikao cha Bunge la Taifa kiahirishwe sasa"*** na kutoa sababu.

(2) Iwapo kwa maoni ya Spika Hoja hiyo ya kuahirisha kikao haina maana, inakera au inahujumu shughuli za Bunge la Taifa, Spika anaweza kulihoji Bunge la Taifa kuamua Hoja wakati huo huo au kukataa kuipendekeza.

(3) Mjadala kuhusu Hoja kwa mujibu wa Kanuni hii utajikita katika masuala yaliyo kwenye Hoja husika.

**32.** *(imefutwa)*.

**Kuahirisha shughuli ili kujadili suala mahususi, la dharura na muhimu kwa taifa**

**33.** (1) Mbunge yeyote anaweza kusimama mahali pake wakati wowote na kuomba kutoa Hoja ya kuahirisha shughuli za Bunge ili kujadili suala mahususi, la dharura na muhimu kwa taifa.

(2) Mbunge anayekusudia kutoa hoja ya kuahirisha shughuli za Bunge la Taifa atawasilisha kwa Spika arifa iliyoandikwa ikibainisha suala husika angalau saa mbili kabla kikao kuanza, hata hivyo, Spika hataruhusu Hoja hiyo iwapo hajaridhika kuwa suala hilo ni mahususi, la dharura na muhimu kwa taifa na linafaa kutolewa kupitia Hoja ya kuahirisha shughuli za Bunge la Taifa.

(3) Iwapo Spika ameridhika kwa mujibu wa aya ya (2) na Wabunge wasiopungua ishirini wamesimama kuunga mkono hoja hiyo, Spika atataja wakati wa kutoa hoja siku iyo hiyo.

(4) Mbunge anayezungumzia suala kwa mujibu wa Kanuni hii hataongea kwa zaidi ya dakika tano bila idhini ya Bunge la Taifa, isipokuwa Mtoahoja anaweza kuongea kwa dakika kumi.

## SEHEMU YA VII—AKIDI YA BUNGE LA TAIFA

**Akidi wakati wa kuanza kikao**

**34.** (1) Akidi ya Bunge la Taifa au Kamati ya Bunge Zima itakuwa ni Wabunge hamsini.

(2) Iwapo akidi haijatimia wakati wa kuanza kikao cha Bunge pindi tu baada ya maombi, Spika ataamuru kengele kukirizwa kwa dakika kumi na, iwapo akidi haitatimia baada ya dakika kumi, Spika anaweza kuamuru kengele kukirizwa kwa dakika tano zaidi na iwapo akidi bado haijatimia, Spika ataahirisha kikao papo hapo hadi kikao kijacho.

**Akidi wakati wa shughuli za Kikao**

**35.** (1) Iwapo Mbunge yeyote atadai kuwa akidi haijatimia katika kikao wakati wowote kikao cha Bunge la Taifa au Kamati kinapoendelea, Spika au Mwenyekiti atahesabu Wabunge walio katika Ukumbi au Kamati.

(2) Iwapo akidi haitatimia baada ya hesabu kwa mujibu wa aya ya (1), Spika au Mwenyekiti ataamuru kengele ikirizwe kama inavyofanyika wakati wa kura ya mgawanyiko na iwapo akidi haitatimia baada ya dakika kumi kumalizika —

(a) kama Spika anaongoza kikao, ataahirisha kikao hadi kikao kinachofuata bila kuhoji Bunge;

(b) kama Bunge lipo kwenye Kamati, Mwenyekiti ataondoka kwenye Kiti na kuripoti kwa Spika kuhusu tukio hilo na Spika ataahirisha kikao hadi kikao kinachofuata bila kuhoji Bunge.

(3) Wakati wowote Spika au Mwenyekiti anapohesabu Wabunge walio katika Bunge la Taifa au kwenye Kamati, milango itasalia wazi lakini hakuna Mbunge atakayeruhusiwa kutoka katika Ukumbi isipokuwa Mratibu wa chama ambaye anaweza kuruhusiwa kutoka katika Ukumbi kwa ajili ya kutafuta Wabunge ili kutimiza akidi.

**Akidi wakati wa kupiga kura**

**36.** Iwapo wakati wa kupiga kura ya kielektroniki au kura ya mgawanyiko kwa kuita majina inadhihirika kuwa idadi ya Wabunge wanaoshiriki kupiga kura haikidhi akidi, kura hiyo itakuwa batili na shughuli iliyokuwa ikiendelea itaahirishwa hadi kikao kinachofuata na Spika atachukua hatua kama kwamba amearifiwa kuwa akidi haijatimia, ila ikiwa akidi itatimia baada ya kuchukua hatua hizo, shughuli inayofuata itaendelea.

**Staha akidi inapokosekana**

**37.** Kengele ya Akidi inapokirizwa Wabunge watahitajika kudumisha utulivu katika Ukumbi.

## SEHEMU YA VIII — MPANGILIO WA SHUGHULI

**Ratiba ya Shughuli kutayarishwa na kusambazwa**

**38.** (1) Katibu atatayarisha Ratiba ya Shughuli inayoonyesha mpangilio wa shughuli ambazo zimependekezwa au zimepangwa kushughulikiwa na Bunge la Taifa, ikijumuisha Arifa ya Shughuli inayoonyesha shughuli zinazokusudiwa kutekelezwa kwa kila kikao katika wiki, pamoja na taarifa yoyote ambayo Spika anaweza kuelekeza kadri itakavyohitajika.

(2) Ratiba ya Shughuli itawekwa kwenye wavuti wa Bunge na kusambazwa kwa Wabunge angalau saa kumi na mbili kabla ya kikao kuanza, isipokuwa kama kutakuwa na Ratiba ya Shughuli ya Nyongeza itakayosambazwa angalau saa moja kabla ya kikao kuanza.

**Mipango ya kila wiki ya Bunge la Taifa**

**39.** Katibu atatayarisha na kuchapisha kwenye wavuti wa Bunge mpango wa kila wiki ukionyesha shughuli za Bunge la Taifa, orodha ya muda ya mawaziri walioratibiwa kujibu Maswali au kuwasilisha ripoti kwa Bunge la Taifa na mpangilio wa vikao vya Kamati za Bunge la Taifa na kusambaza mipango hiyo kwa

Wabunge, Idara za Serikali na vyombo vya habari ilimradi isiwe baada ya Ijumaa ya wiki inayotangulia shughuli hizo.

**Mtiririko wa shughuli**

**40.** (1) Kila siku baada ya maombi na mara baada ya kikao kuanza, shughuSli za Bunge zitaendeshwa kwa mtiririko ufuatao –

(a) Kiapo;

(b) Taarifa ya Spika;

(c) Jumbe;

(d) Ardhilhali;

(e) Nyaraka;

(f) Arifa za Hoja;

(g) Maswali na Kauli;

(h) Hoja na Miswada.

(2) Shughuli zitatekelezwa kwa kufuata mtiririko jinsi ulivyo katika Ratiba ya Shughuli au kwa kufuata mtiririko mwingine utakaoelekezwa na Spika kwa kuzingatia unafuu wa Bunge la Taifa.

(3) Jumatano asubuhi, Mswada au Hoja isiyodhaminiwa na Chama cha walio Wengi au na Chama cha walio Wachache au na Kamati itapewa kipaumbele ikilinganishwa na shughuli nyingine zote kwa mtiririko utakaoamuliwa na Kamati ya Kuratibu Shughuli za Bunge.

(3A) Siku ya Jumatano alasiri, kwa muda usiozidi saa tatu, majibu kwa Maswali na ripoti za mawaziri zitapewa kipaumbele ikilinganishwa na shughuli nyingine zote.

(4) Spika atamwelekeza Katibu kusoma Shughuli za Siku ya kikao bila kuhoji Bunge la Taifa.

## SEHEMU YA IX — JUMBE

### Jumbe za kwenda na kutoka Seneti

**41.** (1) Ujumbe kutoka Bunge la Taifa kwenda Seneti utakuwa kwa maandishi na utatiwa saini na Spika.

(2) Katibu wa Bunge la Taifa atatuma kwa Katibu wa Seneti ujumbe kutoka kwa Bunge la Taifa na atapokea jumbe kutoka kwa Seneti.

(3) Katibu atawasilisha kwa Spika ujumbe atakaopokea kutoka kwa Seneti kwa mujibu wa aya ya (2) pindi fursa inapopatikana na kwa vyovyote vile, bora isipite siku inayofuata ilimradi siku hiyo isiwe Jumamosi, Jumapili au sikukuu ya umma.

(4) Iwapo ujumbe kutoka kwa Seneti utapokelewa wakati Bunge la Taifa linaendelea na vikao vyake, Spika atawasilisha ujumbe huo Bungeni pindi itakapowezekana baada ya kuupokea na kwa vyovyote vile, isipite siku ya kikao inayofuata.

(5) Iwapo ujumbe kutoka kwa Seneti utapokelewa wakati Bunge la Taifa likiwa likizoni, Spika ataagiza, bila kukawia, ujumbe huo utumwe kwa kila Mbunge na atauwasilisha Bungeni katika kikao kinachofuata.

(6) Spika anapowasilisha ujumbe kutoka kwa Seneti kwa mujibu wa aya ya (4) au ya (5), ujumbe huo utachukuliwa kuwa umewasilishwa mbele ya Bunge la Taifa, na Spika anaweza—

(a) kuelekeza ujumbe ushughulikiwe mara moja; au

(b) kutenga siku ya ujumbe huo kushughulikiwa; au

(c) kukabidhi ujumbe huo kwa Kamati husika ili ushughulikiwe.

### Jumbe kutoka kwa Rais

**42.** (1) Spika atasoma Bungeni ujumbe wowote aliopokea kutoka kwa Rais kwa minajili ya kulijulisha Bunge la Taifa.

(2) Iwapo ujumbe kutoka kwa Rais utapokelewa wakati Bunge la Taifa likiwa likizoni, Spika ataagiza, bila kukawia, ujumbe huo utumwe kwa kila Mbunge na atauwasilisha Bungeni katika kikao kinachofuata.

(3) Ujumbe wa Rais unaposomwa Bungeni utachukuliwa kuwa umewasilishwa mbele ya Bunge na Spika anaweza—

(a) kuelekeza ujumbe ushughulikiwe mara moja; au

(b) kutenga siku ya ujumbe huo kushughulikiwa; au

(c) kukabidhi ujumbe huo kwa Kamati husika ili ushughulikiwe.

(4) Aya ya (1), ya (2) na ya (3) zikifanyiwa mabadiliko kadri itakavyohitajika zitatumika kushughulikia ujumbe utakaopelekwa na Waziri kwa Spika ili kuwasilishwa katika Bunge la Taifa kwa mujibu wa sheria yoyote inayoweka masharti ya kupeleka jumbe kutoka kwa Baraza la Mawaziri hadi Bunge la Taifa.

## SEHEMU YA IXA – MASWALI

**Arifa ya Swali**

**42A.** (1) Mbunge anayekusudia kuuliza Swali katika Bunge la Taifa atatoa arifa kwa Katibu.

(2) Mbunge huyo atampa Katibu nakala ya swali analopendekeza iliyotiwa saini ili iwasilishwe kwa Spika kwa ajili ya kuidhinishwa.

(3) Spika akiidhinisha Swali na kubainisha Waziri anayehusika na Swali hilo, Katibu, katika wakati unaofaa, ataliweka Swali hilo kwenye Ratiba ya Shughuli.

(4) Katika kuorodhesha Swali katika Ratiba ya Shughuli, Katibu atazingatia dharura ya Swali kama ilivyoamuliwa na Spika.

(5) Kiongozi wa Chama cha walio Wengi ataliarifu Bunge la Taifa kuhusu tarehe, saa na mpangilio wa jinsi Mawaziri watafika mbele ya Bunge la Taifa na kamati zake ili kujibu Maswali na kuwasilisha ripoti kwa kuzingatia aya ya (6).

(5A) Mbunge atauliza Swali lake siku ambayo limeorodheshwa katika Ratiba ya Shughuli.

(6) Katika kuamua siku na wakati ambao Waziri atahitajika kujibu Swali, Kiongozi wa Chama cha walio Wengi atazingatia dharura ya Swali kama ilivyoamuliwa na Spika.

(6A) Spika anaweza kubadilisha mpangilio utakaofuatwa kushughulikia Maswali au kuahirisha Swali lililoorodheshwa kujibiwa.

(6B) Waziri atahudhuria na kujibu Swali lolote linalohusu masuala yaliyo chini ya usimamizi wa Waziri huyo.

(7) Endapo Chama cha walio Wachache ndicho kinachounda serikali ya taifa, majukumu kwa mujibu wa aya ya (5) na (6) yatatekelezwa na Kiongozi wa Chama cha walio Wachache.

**Masharti ya jumla kuhusu Maswali**

**42B.** (1) Masharti haya yatatumika kwa Maswali yanayoulizwa katika Bunge la Taifa na kujibiwa katika Bunge la Taifa au Kamati.

(2) Isipokuwa kwa ruhusa ya Spika, Mbunge hafai kuuliza Swali ambalo—

(a) ni hotuba;

(b) ni refu;

(c) linatoa habari tu;

(d) limetungwa kwa namna ambayo inadokeza jibu lake au kutambulisha mtazamo fulani.

(e) linajumuisha dondoo za magazeti au nukuu za hotuba;

(f) lina mtazamo unaozua mjadala, makisio, maoni, shutuma, kejeli au matusi;

(g) linakusudia kuibua maoni;

(h) linarudia maudhui ya suala ambalo tayari limeshughulikiwa na Kamati ya Bunge la Taifa au kupitia kwa mjadala katika Bunge la Taifa katika Kipindi hicho;

(i) linahusu zaidi ya suala moja;

(j) linamtaja mtu yeyote kwa jina au kutoa maelezo ila tu kama ni lazima kulifanya Swali hilo lieleweke;

(k) lina madai ambayo Mbunge hawezi au hayuko tayari kuthibitisha;

(l) linadokeza tuhuma dhidi ya tabia au mwenendo wa mtu yeyote ambaye mwenendo wake unaweza tu kujadiliwa kwa Hoja mahususi au kuhusu mwenendo wa mtu mwingine yeyote isipokuwa kwa wadhifa wake rasmi.

(m) linahusu suala ambalo linasubiri uamuzi wa Mahakama au ni la siri kulingana na sheria yoyote kwa mujibu wa Kanuni ya 89 (*Masuala yanayosubiri uamuzi wa Mahakama au masuala ya siri*).

(n) linahusu masuala ambayo ni majukumu na mamlaka ya serikali za kaunti kwa mujibu wa Sehemu ya II ya Nyongeza ya Nne ya Katiba.

(o) linahitaji jibu ambalo tayari linapatikana kwenye matini ya kawaida au machapisho rasmi;

(p) linadhalilisha nchi rafiki, Mkuu wa Nchi au Serikali au mwakilishi wa nchi rafiki nchini Kenya; au

(q) linazungumzia jambo linaloshughulikiwa na Bunge la Taifa au Kamati.

(3) Mbunge atawajibikia usahihi wa maudhui ya Swali lake.

(4) Kwa idhini ya Spika, Mbunge yeyote anaweza kuuliza swali la ziada kwa Swali ambalo limeulizwa katika Bunge kabla ya Swali hilo kukabidhiwa Kamati ili lijibiwe.

(5) Iwapo Mbunge aliyepangiwa kuuliza Swali hayupo katika Bunge bila ruhusa ya Spika, Swali lake litaondolewa na halitashughulikiwa tena katika Kipindi hicho.

(5A) Mbunge aliyeratibiwa kuuliza Swali katika Bunge la Taifa anaweza—

(a) kumuomba Spika kuahirisha Swali hadi wakati mwingine au siku nyingine;

(b) kuondoa Swali iwapo limepitwa na wakati; au

(c) kumteua Mbunge mwingine kuuliza swali hilo kwa niaba yake kama hatakuwepo kwa kumwarifu Spika kwa maandishi angalau saa mbili kabla ya kikao.

(6) Spika anaweza kuahirisha Swali kutoka wakati au siku iliyoratibiwa hadi wakati au siku nyingine.

(7) Swali linaweza kujumuisha ombi la ripoti kutoka kwa Waziri kuhusu masuala yaliyo chini ya usimamizi wa Waziri huyo.

**Namna ya kushughulikia Maswali**

**42C.** (1) Waziri atawasilisha nakala zilizochapishwa na za kieletroniki angalau siku moja kabla ya kufika mbele ya Bunge la Taifa.

(2) Kwa kuzingatia Kanuni ya 42A (*Arifa ya Swali*), Bunge la Taifa litashughulikia Swali kwa kufuata mtiririko wa Orodha ya Maswali au atakavyoelekeza Spika.

(3) Spika anaweza—

(a) kumruhusu Mbunge aliyeuliza Swali kuuliza Maswali ya ziada yasiyozidi mawili ambayo yanahusiana na Swali asilia;

(b) kumruhusu Mbunge mwingine kuuliza Swali la ziada ambalo linahusiana na Swali asilia;

(c) kumwelekeza Waziri kutoa taarifa zaidi au jibu la ziada kwa Swali au Maswali ya ziada katika kamati husika ya Bunge la Taifa; au

(d) kuahirisha Swali hadi wakati au siku nyingine kutoka wakati au siku Swali hilo liliratibiwa kuulizwa.

(4) Waziri atajibu Swali siku ambayo Swali hilo limeratibiwa kujibiwa hata kama Mbunge aliyeuliza Swali hilo hayupo.

**Maswali yanayohitaji majibu kwa maandishi**

**42D.** Endapo Mbunge anapendelea Swali lake lijibiwe kwa maandishi —

(a) Spika ataelekeza Swali hilo lijibiwe kwa maandishi; na

(b) Katibu atawasilisha Swali hilo kwa Waziri husika ambaye baada ya kulipokea atatoa jibu kwa maandishi kwa Mbunge huyo.

**Muda wa kujibu**

**42E.** (1) Waziri atajibu Swali katika muda usiozidi siku kumi na nne baada ya Swali hilo kuwasilishwa kwake.

(2) Licha ya masharti ya aya ya (1), iwapo Spika ataamua kuwa Swali ni la dharura, Waziri atajibu Swali hilo katika muda usiozidi saa arubaini na nane baada ya Swali hilo kuwasilishwa kwake.

**Ripoti kuhusu Maswali**

**42F.** Mwenyekiti wa Kamati atawasilisha ripoti kwa Bunge la Taifa kupitia njia ya Kauli kuhusu Maswali—

(a) yaliyokabidhiwa Kamati;

(b) yaliyojibiwa;

(c) ambayo Kamati imemwelekeza Waziri kutoa habari zaidi au jibu la ziada; na

(d) ambayo bado yanashughulikiwa na Kamati.

**Maswali kwa Tume na Ofisi Huru**

**42G.** (1) Utaratibu wa kushughulikia Maswali kwa Mawaziri, ukifanyiwa marekebisho kama itakavyohitajika, utatumika kwa Maswali yanaloelekezwa kwa Tume au Ofisi Huru.

(2) Tume au Ofisi Huru iliyoelekezewa Swali italijibu katika Kamati husika ya Bunge la Taifa.

## SEHEMU YA X — KAULI

**Kauli za jumla za Wajumbe**

**43.** (1) Bila kuzingatia Kanuni ya 30 (*Saa za Vikao*), Spika atasitisha shughuli za Bunge kila Jumanne saa 12.30 jioni ili kuwawezesha Wabunge kutoa kauli za jumla kuhusu masuala ibuka.

(2) Mbunge anayekusudia kuomba idhini ya kutoa kauli kwa mujibu wa Kanuni hii atawasilisha arifa iliyoandikwa kwa Spika kabla ya saa 9.00 alasiri ya siku anayotaka kutoa kauli hiyo, hata hivyo, Spika hataidhinisha ombi hilo iwapo hajaridhika kuwa suala hilo linaweza kujadiliwa katika Bunge.

(3) Mbunge anayetoa kauli kwa mujibu wa Kanuni hii hataongea kwa zaidi ya dakika tatu isipokuwa kwa ruhusa ya Spika.

**Saa ya Kauli**

**44.** (1) Bila kuzingatia Kanuni ya 40 *(Mtiririko wa Shughuli)*, kutatengwa muda utakaoitwa Saa ya Kauli utakaoanza sio baada ya saa 9.00 alasiri.

(2) Wakati wa Saa ya Kauli —

(a) kila Alhamisi au katika siku ya mwisho ya vikao, kwa muda usiozidi dakika kumi, Mjumbe aliyeteuliwa na Kamati ya Kuratibu Shughuli za Bunge la Taifa atatoa na kuwasilisha kwenye Meza kauli inayoarifu Bunge la Taifa kuhusu shughuli itakayoletwa katika Bunge wiki inayofuata;

(b) Kiongozi wa Chama cha walio Wengi, Kiongozi wa Chama cha walio Wachache, Mwenyekiti wa Kamati au wawakilishi wao wanaweza kutoa Kauli inayohusu majukumu yao katika Bunge la Taifa au shughuli za Kamati;

(c) Mbunge anaweza kuomba Kauli kutoka kwa Mwenyekiti wa Kamati kuhusu masuala yanayohusu wajibu wa kamati hiyo na ripoti itatolewa katika muda usiozidi siku ishirini na moja au muda mfupi zaidi kama atakavyoagiza Spika.

(d) Kwa idhini ya Spika, Mwenyekiti wa Kamati anaweza kutoa Kauli inayohusu wajibu wa Kamati hiyo;

(e) Kwa idhini ya Bunge, Mbunge anaweza kueleza masuala ya kibinafsi hata kama hakuna hoja katika Bunge kuhusu masuala hayo, ila masuala hayo hayatajadiliwa.

(3) Ombi la Kauli au jibu kwa ombi la Kauli kwa mujibu wa aya ya (2)(c) halitaruhusiwa isipokuwa kama arifa imeidhinishwa na Spika angalau siku moja kabla ya kikao husika na imetajwa katika Orodha ya Shughuli.

## SEHEMU YA XI—KUIDHINISHA UTEUZI WA MAOFISA WA UMMA

**Kukabidhiwa kwa Kamati**

**45.** (1) Baada ya kupokea taarifa ya uteuzi kwa Ofisi ya Serikali au ofisi nyingine yoyote kwa mujibu wa Katiba au sheria nyingine unaotaka kuidhinishwa na Bunge, uteuzi huo utakabidhiwa Kamati ya Kiidara inayohusika ili ushughulikiwe.

(2) Licha ya aya ya (1) —

(a) uteuzi uliotajwa katika Ibara ya 152(2) ya Katiba utakabidhiwa Kamati ya Uteuzi; na

(b) Spika, katika hali za kipekee, anaweza kuagiza uteuzi mahususi ukabidhiwe Kamati atakayoamua.

(3) Kabla ya kikao cha kuidhinisha uteuzi, Kamati iliyokabidhiwa uteuzi unaopendekezwa itamuarifu mteuliwa na umma, angalau siku saba kabla ya kikao hicho, kuhusu wakati na mahali ambapo kikao cha kumuidhinisha kitafanyika.

(4) Kamati itafanya kikao kwa ajili ya kushughulikia uteuzi uliopendekezwa na isipokuwa kama imeelezwa vinginevyo katika sheria, itawasilisha ripoti yake kwa Bunge la Taifa katika muda usiozidi siku ishirini na moja baada ya kukabidhiwa taarifa ya uteuzi kwa mujibu wa aya ya (1).

## SEHEMU YA XII—HOJA

**Matumizi**

**46.** Sehemu hii itatumika kwa Hoja zote, zikiwemo Hoja Maalum.

**Arifa za Hoja**

**47.** (1) Isipokuwa kama Kanuni hizi zitahitaji vinginevyo, Mbunge yeyote anayekusudia kutoa Hoja atatoa Arifa ya Hoja.

(2) Kabla ya kutoa Arifa ya Hoja, Mbunge atampa Katibu nakala ya Hoja anayopendekeza kwa maandishi ikiwa imetiwa saini na Mbunge huyo na Katibu ataiwasilisha Hoja hiyo kwa Spika.

(3) Iwapo Spika ana maoni kwamba Hoja yoyote inayopendekezwa—

(a) inakiuka au mjadala wake huenda ukakiuka Kanuni hizi;

(b) ni kinyume na Katiba au Sheria yoyote, bila kueleza wazi marekebisho yanayofaa kufanyiwa Katiba au Sheria;

(c) ni ndefu sana;

(d) imetungwa kwa namna ambayo haiwiani na hadhi ya Bunge;

(e) ina tuhuma au inadokeza tuhuma ambazo Spika hajaridhika kwamba Mtoahoja anaweza kuthibitisha; au

(f) itasababisha matumizi ya pesa za umma ambazo hazimo katika Makadirio ya Mwaka yaliyoidhinishwa na Bunge la Taifa,

Spika anaweza kuelekeza kwamba Hoja hiyo haikubaliki, au arifa ya Hoja hiyo haiwezi kutolewa bila kuifanyia marekebisho atakayoelekeza Spika, au kuelekeza kwamba Hoja hiyo ipelekwe kwenye Kamati inayohusika kwa mujibu wa Ibara ya 114(2) ya Katiba.

(4) Mbunge anayetoa arifa ya Hoja iliyoidhinishwa na Spika atasoma matini ya arifa hiyo katika Bunge na kueleza iwapo nakala asilia ya arifa ya Hoja iliyopokelewa na Katibu imeidhinishwa na kiongozi wa chama au mratibu wa chama ili kudhaminiwa na chama cha Mbunge huyo.

(4A) Arifa ya Hoja kwa mujibu wa Sehemu ya XIV *(Utaratibu wa kuwaondoa Maofisa wa Serikali Mamlakani)* itatolewa katika Bunge kwa muda usiozidi siku tatu za vikao baada ya kuidhinishwa na Spika la sivyo, Hoja hiyo itachukuliwa kama iliyoondolewa na haitawasilishwa tena ikiwa na maudhui yale yale katika Kipindi hicho, ila kwa idhini ya Spika.

(5) Isipokuwa kama Bunge la Taifa litaamua vinginevyo—

(a) Hoja ambayo imedhaminiwa na chama itapewa kipaumbele ikilinganishwa na Hoja nyingine zote katika siku ambayo Kamati ya Kuratibu Shughuli za Bunge inaweza kuamua kwa kushauriana na Spika,

lakini iwapo chama kimedhamini Hoja mbili au zaidi, chama hicho kitaamua Hoja ipi ipewe kipaumbele.

(b) Arifa ya Hoja iliyoidhinishwa isipokuwa Hoja zilizotajwa katika aya ndogo ya (a) inaweza kutolewa kwa Wabunge kupitia orodha iliyochapishwa kwa namna itakayoamuliwa na Spika angalau siku moja kabla ya Hoja hiyo kuorodheshwa kwenye Ratiba ya Shughuli na Mbunge anayetoa arifa atasoma matini ya arifa hiyo katika Bunge wakati Hoja hiyo itapewa kipaumbele kwa mujibu wa Kanuni ya 50 (*Wakati wa kutoa Hoja*).

**Marekebisho ya Arifa ya Hoja**

**48.** Spika anaweza kumruhusu Mbunge kutoa Hoja iliyorekebishwa na ambayo arifa yake ilishawasilishwa iwapo Spika ataridhika kwamba marekebisho yaliyofanywa hayabadilishi msingi wa Hoja hiyo.

**Hoja ambazo haziruhusiwi kutolewa**

**49.** (1) Hoja ambayo ina maudhui yanayofanana na suala ambalo lilishaamuliwa (kwa kukubaliwa au kukataliwa) haitaruhusiwa kutolewa ndani ya miezi sita katika Kipindi hicho.

(2) Licha ya masharti ya aya ya (1)—

(a) Hoja ya kutengua uamuzi wa suala lolote inaweza kutolewa kwa ruhusa ya Spika;

(b) Hoja ya kutengua uamuzi wa suala lililoamuliwa kwa Hoja Maalum haitaruhusiwa.

**Wakati wa kutoa Hoja**

**50.** (1) Kamati ya kuratibu Shughuli za Bunge la Taifa itaamua wakati na mtiririko wa kuweka Hoja zilizoidhinishwa na Spika kwenye Ratiba ya Shughuli.

(2) Mbunge mwenye Hoja anaweza kumruhusu Mbunge mwingine, kwa maandishi, kutoa Hoja kwa niaba yake isipokuwa kama ni Hoja Maalum.

(3) Iwapo hakuna Mbunge atakayetoa Hoja katika muda uliotengwa au kulingana na Kanuni hizi, Hoja hiyo haitawekwa tena kwenye Ratiba ya Shughuli katika Kipindi hicho cha Bunge isipokuwa kwa idhini ya Spika.

**Hoja iliyoondolewa inaweza kuwasilishwa tena**

**51.** (1) Arifa ya Hoja inaweza kuondolewa na Mbunge aliyeitoa lakini arifa ya Hoja hiyo inaweza kuwasilishwa tena na Mbunge huyo au na Mbunge mwingine yeyote.

(2) Licha ya aya ya (1), arifa ya Hoja Maalum haiwezi kuondolewa ila kwa idhini ya Bunge la Taifa.

**Hoja zinazoweza kutolewa bila Arifa**

**52.** Hoja zifuatazo zinaweza kutolewa bila arifa—

(a) Hoja ya kurekebisha hoja ambayo imependekezwa na Kiongozi wa kikao ili ijadiliwe;

(b) Hoja ya kuahirisha kikao cha Bunge au mjadala;

(c) Hoja kwamba Bunge lijigeuze kuwa Kamati ya Bunge Zima;

(d) Hoja inayotolewa wakati Bunge liko katika Kamati;

(e) Hoja ya kumsimamisha Mbunge kuhudhuria vikao kwa muda;

(f) Hoja inayotolewa kwa mujibu wa Kanuni zinazoongoza utaratibu wa Miswada;

(g) Hoja ya Bunge kuridhia uamuzi ulioripotiwa na Kamati ya Bunge Zima, au kuirejesha Hoja kwenye Kamati ya Bunge Zima au kuiahirisha Hoja ili ishughulikiwe zaidi;

(h) Hoja inayohusu suala la haki za Wabunge;

(i) Hoja ya amri za Bunge kwa mujibu wa Kanuni hizi;

(j) Hoja kwa mujibu wa Kanuni ya 256 *(Kutengua Kanuni);*

(k) Hoja ya kudhibiti mjadala kwa mujibu wa Kanuni ya 97 (*Kudhibiti mjadala*);

(ka) Hoja ya kipekee ya risala za Bunge la Taifa kwa mujibu wa Kanuni ya 259D (*Risala za Bunge*).

(l) Hoja ya kuahirisha au kuondoa au kuipa kipaumbele shughuli fulani ya siku; na

(m) Hoja ya kuongeza muda wa kikao.

**Utaratibu wa kujadili hoja**

**53.** (1) Hoja ikishatolewa na ikiwa inahitaji kuafikiwa iafikiwe, Spika atapendekeza Hoja hiyo ijadiliwe jinsi ilivyo na kisha mjadala unaweza kuanza.

(2) Baada ya mjadala kuhitimishwa, Spika atatoa Hoja ili iamuliwe.

(3) Licha ya aya ya (2), kufuatia ombi la Mbunge la kutaka uamuzi wa Hoja uahirishwe, Spika anaweza kuahirisha uamuzi wa Hoja hadi siku itakayofuata na atataja wakati ambapo Hoja hiyo itaamuliwa.

**Marekebisho ya Hoja**

**54.** (1) Isipokuwa kama imeelekezwa vinginevyo katika Kanuni hizi, rekebisho lolote la Hoja ambalo Mbunge anakusudia kupendekeza linaweza kutolewa na kuafikiwa, ikiwa linahitaji kuafikiwa, wakati wowote baada ya Hoja kutolewa na kabla ya kuamuliwa.

(2) Baada ya kila rekebisho kuhitimishwa kwa mujibu wa aya ya (1), Spika atapendekeza tena Hoja ijadiliwe au atapendekeza

Hoja iliyorekebishwa ijadiliwe kama inavyohitajika na baada ya kuruhusu Hoja hiyo kujadiliwa, atatoa Hoja iamuliwe.

(3) Iwapo rekebisho ni la kuondoa maneno katika Hoja, Hoja itapendekezwa ijadiliwe kwa maneno yafuatayo ***"Kwamba, maneno yaliyopendekezwa kuondolewa yaondolewe".***

(4) Iwapo rekebisho ni la kuchopeka au kuongeza maneno mwishoni mwa Hoja, Hoja itapendekezwa ili ijadiliwe kwa maneno ***"Kwamba, maneno [ya marekebisho] yachopekwe" (au "yaongezwe").***

(5) Iwapo rekebisho ni la kuondoa maneno na kuchopeka au kuongeza maneno mengine badala yake, Hoja itapendekezwa ili ijadiliwe kwa maneno ***"Kwamba, maneno yaliyopendekezwa kuondolewa yaondolewe kwenye Hoja",*** na iwapo Hoja hiyo itakubaliwa, Hoja itapendekezwa ili ijadiliwe kwa maneno ***"Kwamba, maneno [ya marekebisho] yachopekwe" (au "yaongezwe"),*** lakini iwapo Hoja ya kwanza itakataliwa, hakuna rekebisho la nyongeza litakaloruhusiwa kupendekezwa kwa maneno ambayo imeamuliwa yasiondolewe.

(6) Marekebisho mawili au zaidi yanapopendekezwa kwa Hoja, Spika atawaita Wabunge wenye marekebisho akizingatia jinsi marekebisho hayo yanavyoathiri matini ya Hoja hiyo, au kukiwepo na tashwishi, kwa mpangilio utakaoamuliwa na Spika.

(7) Rekebisho la kuondoa maneno na kuweka maneno mengine litapewa kipaumbele ikilinganishwa na rekebisho la kuondoa maneno bila ya kupendekeza maneno mengine.

(8) Hakuna rekebisho ambalo litatolewa kuhusu maneno yoyote ambayo imeamuliwa yasiondolewe kwenye Hoja.

(9) Rekebisho la rekebisho lingine linaweza kutolewa, na kuafikiwa ikiwa linahitaji kuafikiwa, wakati wowote baada ya rekebisho la awali kupendekezwa lijadiliwe na kabla ya uamuzi kufanyika.

(10) Aya ya (3), (4), (5), (6), (7), (8) na (9) za Kanuni hii zitatumika katika mjadala wa marekebisho ya marekebisho mengine na maneno "rekebisho la awali" yakibadilishwa na "hoja" popote patakapohitajika.

(11) Baada ya kila rekebisho la rekebisho lingine kuamuliwa, Spika atapendekeza tena rekebisho la awali ili lijadiliwe au atapendekeza hoja kuhusu rekebisho la awali lilivyorekebishwa ili lijadiliwe kadri itakavyohitajika.

**Marekebisho kuwa kwa maandishi**

**55.** (1) Mbunge anayependekeza rekebisho la Hoja, kabla ya kutoa hoja ya rekebisho, atampa Katibu pendekezo hilo kwa maandishi likiwa limetiwa saini na Mbunge huyo, angalau saa mbili kabla ya shughuli hiyo kusomwa.

(2) Licha ya aya ya (1) na katika hali za kipekee, Spika anaweza kumruhusu Mbunge kutoa hoja ya rekebisho la Hoja katika Bunge wakati wowote Bunge linaposhughulikia Hoja hiyo.

**Marekebisho yawiane na Hoja**

**56.** (1) Kila rekebisho sharti liwiane na Hoja ambayo linapendekeza kurekebisha na halipaswi kuibua suala lolote ambalo, kwa maoni ya Spika, linafaa kuwasilishwa kwa Hoja mahususi baada ya arifa kutolewa.

(2) Spika hataruhusu rekebisho ambalo, kwa maoni yake, linakinzana na hoja iliyopendekezwa.

**Hoja kupendekezwa baada ya kuafikiwa**

**57.** (1) Hoja haitapendekezwa kujadiliwa ikiwa haijaafikiwa na Hoja yoyote ambayo haijaafikiwa itachukuliwa kuwa imeondolewa na haitatolewa tena katika Kipindi hicho.

(2) Licha ya aya ya (1), Hoja itakayotolewa wakati wa Kamati ya Bunge Zima haitahitaji kuafikiwa.

**Hoja inayomilikiwa na Bunge la Taifa**

**58.** Baada ya Hoja kupendekezwa ili ijadiliwe, Hoja itachukuliwa kuwa inamilikiwa na Bunge na Hoja hiyo haitaondolewa bila ya idhini ya Bunge la Taifa.

**Kutoa Hoja iliyorekebishwa iamuliwe**

**59.** Endapo Hoja imerekebishwa, itakapotolewa ili iamuliwe, itatolewa jinsi ilivyorekebishwa.

**Rekebisho lililopendekezwa lisipofaulu**

**60.** Endapo rekebisho lolote limependekezwa lakini halijafaulu, Hoja itakapotolewa ili iamuliwe, itatolewa jinsi ilivyopendekezwa awali.

## SEHEMU YA XIII — HOJA MAALUM

**Maana ya Hoja Maalum**

**61.** (1) Kwa minajili ya Sehemu hii, Hoja Maalum ni ile—

(a) inayohitaji uamuzi wa Bunge kuidhinisha uteuzi au uteuzi wa mara ya pili kwa mujibu wa Sehemu ya XI (*Kuidhinisha Uteuzi wa Maofisa wa Umma) ya Kanuni hizi)*; au

(b) inayotolewa kwa mujibu wa Ibara zifuatazo za Katiba—

(i) Ibara ya 58 (*kuongeza muda wa* tangazo *la hali ya hatari*);

(ii) Ibara ya 102 (*kuongeza muhula wa Bunge Kenya ikiwa vitani*);

(iii) Ibara ya 111 (*kurekebisha au kubatilisha Mswada Maalum uliopitishwa na Seneti*);

(iiia) Ibara ya 106 (*uamuzi wa kumwondoa Spika au Naibu Spika mamlakani*);

(iv) Ibara ya 132 (*tangazo la vita*);

(v) Ibara ya 144 (*kuondolewa kwa Rais kwa misingi ya kushindwa kutekeleza majukumu*);

(vi) Ibara ya 145 (*kuondolewa kwa Rais kupitia mashtaka*);

(vii) Ibara ya 149 (*wadhifa wa Naibu Rais unapokuwa wazi*);

(viii) Ibara ya 150 (*kuondolewa kwa Naibu Rais*);

(ix) Ibara ya 152 (*kumwachisha kazi waziri*);

(x) Ibara ya 188 (*kubadilishwa kwa mipaka ya kaunti*);

(xi) Ibara ya 211 (*ukopaji wa serikali ya taifa*);

(xii) Ibara ya 217 (*mgao wa mapato*);

(xiii) Ibara ya 225 (*idhini ya uamuzi wa kusimamisha uhamishaji wa fedha kwa kitengo fulani cha serikali au shirika lolote la serikali*);

(xiv) Ibara ya 240 (*kutuma majeshi ya usalama ya taifa nje ya Kenya na kuruhusu jeshi la kigeni nchini Kenya*);

(xv) Ibara ya 241 (*kutuma Majeshi ya Ulinzi ndani ya nchi ya Kenya*);

(xvi) Ibara ya 251 (*ardhilhali ya kumwondoa Mjumbe wa Tume au ofisa wa ofisi huru*);

(xvii) Ibara ya 261 (*utungaji wa sheria zinazotokana na mabadiliko ya Katiba*);

(2) Isipokuwa kama Katiba, sheria nyingine au Kanuni hizi zimetaja muda mfupi au zaidi, Hoja Maalum—

(a) itashughulikiwa na Spika kwa mujibu wa Kanuni ya 53 (*Utaratibu wa kujadili Hoja*) katika muda usiozidi siku saba baada ya kupokea arifa ya Mbunge kwa mujibu wa aya ya (2); na

(b) itashughulikiwa na Bunge kwa muda usiozidi siku kumi na nne za kalenda baada ya arifa kutolewa kwa mujibu swa Kanuni ya 47 (*Arifa za Hoja*), vinginevyo, Hoja hiyo itachukuliwa kuwa imeondolewa na haitawasilishwa tena katika Kipindi hicho ila kwa kibali cha Spika.

**Katiba inapohitaji wingi wa idadi mahususi**

**62.** (1) Katika kila hali ambapo Katiba inataja kwamba idadi mahususi ya Wabunge inahitajika kuunga mkono kutolewa au kuamuliwa kwa Hoja, hoja ya rekebisho lolote la Hoja asilia haitapitishwa isipokuwa kama imeungwa mkono na idadi mahususi inayohitajika kupitisha Hoja asilia.

(2) Bila kuzingatia aya ya (1), kila mara Mswada au Hoja Maalum ambayo kupitishwa kwake kunahitaji kuungwa mkono na idadi mahususi ya Wabunge katika Bunge la Taifa itakosa idadi hiyo na kuwe na wingi wa kura za waliopiga kura ya "Ndiyo" lakini idadi ya waliopiga kura ya "La" haijafikia angalau thuluthi moja ya Wabunge wote, Spika anaweza kuelekeza awamu nyingine ya kura ili kuamua hoja hiyo katika muda usiozidi siku tano za vikao baada ya kura ya kwanza au wakati mwingine atakaoamua Spika.

(3) Iwapo Spika hataagiza awamu nyingine ya kura au ikiwa baada ya awamu nyingine ya kura idadi hiyo mahususi haijatimia, Spika atatangaza kuwa Hoja hiyo imeanguka.

## SEHEMU YA XIV—UTARATIBU WA KUMWONDOA OFISA WA SERIKALI MAMLAKANI

**Utaratibu wa kumwondoa Rais mamlakani kwa kushindwa kutekeleza majukumu**

**63.** (1) Kabla ya kutoa arifa ya Hoja kwa mujibu wa Ibara ya 144(1) ya Katiba, Mbunge atawasilisha kwa Katibu, kwa maandishi, nakala ya Hoja anayopendekeza—

(a) ikitaja misingi na maelezo ya Hoja anayopendekeza;

(b) iliyotiwa saini na Mbunge huyo; na

(c) yenye saini za uungwaji mkono za angalau robo ya Wabunge wote.

(1A) Hoja kwa mujibu wa Kanuni hii itaonyesha mada yake katika kila ukurasa.

(2) Hoja kwa mujibu wa aya ya (1) itashughulikiwa na—

(a) Spika kwa muda usiozidi siku tatu baada ya kupokea arifa kutoka kwa Mbunge kwa mujibu wa aya ya (1); na

(b) Bunge la Taifa kwa muda usiozidi siku saba baada ya Mbunge kutoa arifa kwa mujibu wa Kanuni ya 47 (*Arifa za Hoja*), vinginevyo, Hoja hiyo itachukuliwa kuwa imeondolewa na haitatolewa tena katika Kipindi hicho isipokuwa kwa idhini ya Spika.

(3) Iwapo Bunge la Taifa lipo likizoni, Spika ataagiza kufanyika kwa kikao maalum cha Bunge la Taifa ili kushughulikia Hoja hiyo.

(4) Ratiba ya Shughuli ambamo Hoja hiyo imeorodheshwa kwa mujibu wa aya ya (1) itaeleza—

(a) misingi na maelezo ya Hoja inayopendekezwa;

(b) jina la Mbunge anayedhamini Hoja; na

(c) majina ya Wabunge wanaounga mkono Hoja hiyo.

(5) Pindi Katibu anapopokea Hoja, saini yoyote iliyowekwa kwenye orodha ya Wabunge wanaounga mkono kwa mujibu wa aya ya (4) haitaondolewa.

(6) Wakati Hoja hiyo imepitishwa na wingi wa Wabunge wote wa Bunge la Taifa, Spika atamjulisha Jaji Mkuu kuhusu uamuzi huo katika muda usiozidi siku mbili.

(7) Pindi Spika anapopokea ripoti ya baraza kwa mujibu wa Ibara ya 144 (6) ya Katiba, ataelekeza ripoti hiyo iwasilishwe katika Bunge la Taifa katika muda usiozidi siku saba baada ya kuipokea na—

(a) iwapo baraza litaripoti kuwa Rais ana uwezo wa kutekeleza majukumu ya ofisi, Spika wa Bunge la Taifa atatoa tangazo hilo katika Bunge na shughuli zote kuhusu jambo hilo zitasitishwa;

(b) iwapo baraza litaripoti kuwa Rais hana uwezo wa kutekeleza majukumu ya ofisi na baada ya Bunge la Taifa kupokea Hoja ya Mbunge aliyependekeza Hoja ya kumchunguza Rais na Bunge la Taifa kuridhia Hoja hiyo kwa wingi wa kura za Wabunge wote, Rais ataondoka mamlakani.

**Utaratibu wa kumwondoa Rais mamlakani kwa mashtaka**

**64.** (1) Kabla ya kutoa arifa ya Hoja kwa mujibu wa Ibara ya 145(1) ya Katiba, Mbunge atawasilisha kwa Katibu, kwa maandishi, nakala ya Hoja anayopendekeza—

(a) ikitaja misingi na maelezo, kwa mujibu wa Ibara ya 145(1) ya Katiba, ya Hoja anayopendekeza;

(b) iliyotiwa saini na Mbunge huyo; na

(c) iliyotiwa saini za uungwaji mkono na angalau thuluthi moja ya Wabunge wote.

(1A) Misingi inayotajwa katika Hoja kwa mujibu wa Kanuni hii itakubalika ikiwa—

(a) imetungwa kwa uwazi ili kubainisha na kufichua ukiukaji mkubwa wa Katiba au sheria yoyote pale ambapo ukiukaji mkubwa wa Katiba au sheria yoyote umetajwa kama msingi wa kutaka kumwondoa;

(b) inataja kwa usahihi vipengele vya Katiba au sheria yoyote ambayo inadaiwa kukiukwa kwa kiasi kikubwa pale ambapo ukiukaji mkubwa wa Katiba

au sheria yoyote umetajwa kama msingi wa kutaka kumwondoa; na

(c) imeambatisha ushahidi unaofaa, ukijumuisha viambatisho au ushahidi uliotolewa kwa kiapo kuhusiana na tuhuma hizo.

(2) Hoja kwa mujibu wa aya ya (1) itashughulikiwa na—

(a) Spika kwa mujibu wa Kanuni ya 47 (*Arifa za Hoja*) katika muda usiozidi siku tatu baada ya kupokea arifa kutoka kwa Mbunge kwa mujibu wa aya ya (1); na

(b) Bunge katika muda usiozidi siku saba baada ya Mbunge kutoa arifa kwa mujibu wa Kanuni ya 47 (*Arifa za Hoja*), vinginevyo, Hoja hiyo itachukuliwa kuwa imeondolewa na haitatolewa tena katika Kipindi hicho isipokuwa kwa idhini ya Spika.

(3) Iwapo Bunge la Taifa lipo likizoni, Spika ataagiza kufanyika kwa kikao maalum cha Bunge la Taifa ili kushughulikia Hoja hiyo.

(4) Ratiba ya Shughuli ambamo Hoja hiyo imeorodheshwa kwa mujibu wa aya ya (1) itaeleza—

(a) misingi na maelezo ya Hoja inayopendekezwa;

(b) jina la Mbunge anayedhamini Hoja; na

(c) majina ya Wabunge wanaounga mkono Hoja hiyo.

(5) Pindi Katibu anapopokea Hoja, saini yoyote iliyowekwa kwenye orodha ya Wabunge wanaounga mkono kwa mujibu wa aya ya (4) haitaondolewa.

(6) Hoja hiyo ikipitishwa na angalau thuluthi mbili ya Wabunge wote, Spika atamjulisha Spika wa Seneti kuhusu uamuzi huo katika muda usiozidi siku mbili kwa mujibu wa Ibara ya 145(2)(a) ya Katiba.

**Utaratibu wa kumwondoa Naibu Rais mamlakani**

**65.** (1) Mbunge anapopendekeza kumwondoa Naibu Rais mamlakani kwa misingi ya kukosa uwezo wa kimwili au wa kiakili kwa mujibu wa Ibara ya 150 (1)(a) ya Katiba, Kanuni ya 63 (*Utaratibu wa kumwondoa Rais mamlakani kwa kushindwa kutekeleza majukumu*) itatumika kadri iwezekanavyo.

(2) Mbunge anapopendekeza Hoja ya kumshtaki Naibu Rais kwa mujibu wa Ibara ya 150(1)(b) ya Katiba, Kanuni ya 64 (*Utaratibu wa kumwondoa Rais kwa mashtaka*) itatumika kadri iwezekanavyo.

**Utaratibu wa kumwondoa Waziri mamlakani**

**66.** (1) Kabla ya kutoa Arifa ya Hoja kwa mujibu wa Ibara ya 152(6) ya Katiba, Mbunge atawasilisha kwa Katibu, kwa maandishi, nakala ya Hoja anayopendekeza—

(a) ikitaja misingi na maelezo, kwa mujibu wa Ibara ya 152(6) ya Katiba, ya Hoja anayopendekeza;

(b) iliyotiwa saini na Mbunge huyo; na

(c) iliyotiwa saini za uungwaji mkono na angalau robo ya Wabunge wote.

(2) Masharti ya Kanuni ya 64 *(Utaratibu wa kumwondoa Rais kwa mashtaka)* yatatumika kwa Hoja kwa mujibu wa aya ya (1).

(3) Ratiba ya Shughuli ambamo Hoja hiyo imeorodheshwa kwa mujibu wa aya ya (1) itaeleza—

(a) misingi na maelezo ya Hoja inayopendekezwa;

(b) jina la Mbunge anayedhamini Hoja; na

(c) majina ya Wabunge wanaounga mkono Hoja hiyo.

(4) Pindi Katibu anapopokea Hoja, saini yoyote iliyowekwa kwenye orodha ya Wabunge wanaounga mkono kwa mujibu wa aya ya (3) haitaondolewa.

(5) Iwapo Hoja inaungwa mkono na angalau thuluthi moja ya Wabunge wote wa Bunge la Taifa—

(a) Bunge la Taifa, katika muda usiozidi siku saba, litateua kamati ya Wabunge kumi na mmoja kuchunguza suala hilo; na

(b) Kamati, katika muda usiozidi siku kumi, itaripoti katika Bunge la Taifa iwapo imebaini kuwa tuhuma dhidi ya Waziri zinathibitika.

(6) Waziri ana haki ya kufika na kuwakilishwa mbele ya kamati wakati wa uchunguzi huo.

(7) Iwapo kamati itaripoti kuwa imebaini ya kwamba tuhuma —

(a) hazithibitiki, hakuna hatua zaidi zitakazochukuliwa; au

(b) zinathibitika, Bunge la Taifa—

(i) litampa Waziri ripoti ya Kamati pamoja na ushahidi mwingine wowote uliotolewa na nyaraka zilizowasilishwa kwenye kamati angalau siku tatu kabla ya siku aliyotengewa kufika mbele ya Bunge la Taifa;

(ii) litatoa nafasi kwa Waziri ili kusikilizwa; na

(iii) litashughulikia Ripoti ya Kamati na kupiga kura kuamua iwapo litaidhinisha uamuzi wa kumwondoa Waziri mamlakani.

(8) Iwapo uamuzi wa kumtaka Rais amwondoe Waziri mamlakani utaungwa mkono na wingi wa Wabunge wa Bunge la Taifa, Spika atawasilisha uamuzi huo kwa Rais mara moja.

**Haki ya kusikilizwa**

**67.** Kila mara Katiba, sheria yoyote au Kanuni hizi—

(a) zinalihitaji Bunge la Taifa kushughulikia ardhilhali au pendekezo la kumwondoa mtu mamlakani, mtu huyo ana haki ya kufika mbele ya Kamati ya Bunge la Taifa inayoshughulikia suala hilo na atakuwa na haki ya kuwakilishwa kisheria;

(b) zinalihitaji Bunge la Taifa kumsikiliza mtu kuhusu sababu za kumwondoa mamlakani, au katika hali sawa na hiyo, Bunge la Taifa litamsikiliza mtu huyo—

(i) siku na wakati utakaoamuliwa na Spika;

(ii) kwa muda usiozidi saa mbili, au kwa muda zaidi ya huo, kama Spika atakavyoamua kwa kutegemea kila hali; na

(iii) kwa namna na mpangilio mwingine wowote kama Spika atakavyoamua kwa kutegemea kila hali.

**Hoja kupewa kipaumbele**

**68.** Hoja ya kumwondoa mtu mamlakani kwa mujibu wa Sehemu hii itapewa kipaumbele ikilinganishwa na shughuli nyingine zote kwenye Ratiba ya Shughuli ya siku hiyo.

## SEHEMU YA XV – UPIGAJI KURA NA KURA YA MGAWANYIKO

**Utaratibu wa kupiga kura katika Bunge la Taifa**

**69.** (1) Isipokuwa kama Katiba imeelekeza vinginevyo, hoja inayoibuka katika Bunge la Taifa itaamuliwa na wingi wa Wabunge watakaokuwa katika Ukumbi na kupiga kura.

(2) Katika kuthibitisha matokeo ya Hoja kwa mujibu wa aya ya (1), Spika atakadiria sauti za kura ya “Ndiyo” na ya “La” mara ya kwanza na kutangaza matokeo ipasavyo.

(3) Spika hana kura kwa Hoja inayopendekezwa kuamuliwa na Bunge la Taifa.

(4) Katika kuamua idadi ya Wabunge kwa minajili ya kupiga kura, Spika hatahesabiwa kama Mbunge.

**Kura ya kielektroniki**

**70.** (1) Isipokuwa kama Spika ataelekeza vinginevyo kwa unafuu wa shughuli za Bunge la Taifa, upigaji wa kura ya mgawanyiko utafanyika kielektroniki.

(2) Spika anapoelekeza kura ya kielektroniki itumike, Kengele ya Kura ya Mgawanyiko itakirizwa kwa muda usiozidi dakika kumi na Bunge la Taifa litapiga kura baada ya muda huo au katika muda mwingine zaidi ambao Spika anaweza kuelekeza kwa unafuu wa shughuli za Bunge la Taifa.

(3) Katika kura ya kielektroniki, Wabunge watapiga kura kwa kubofya kitufe cha "Ndiyo", "La" au "Mzio".

(4) Dakika tano zitakapotimia au pindi matokeo ya kura yatakapoonekana kwenye kiwambo, Spika au Mwenyekiti atatangaza matokeo ya kura ya mgawanyiko mara moja.

(5) Mbunge ambaye hakuweza kupiga kura kutokana na sababu ambazo Spika ataridhika nazo anaweza, kabla ya matokeo ya kura ya mgawanyiko kutangazwa, kupiga kura yake kwa kutamka kura ya kuunga au kupinga Hoja hiyo baada ya kupata ruhusa ya Spika.

(6) Iwapo Kiongozi wa kikao ana kura asilia, atapiga kura yake akiwa kwenye Kiti.

**Hitilafu ya mitambo, mkanganyiko au kasoro inapotokea**

**71.** Pale ambapo hitilafu ya mitambo, mkanganyiko au kasoro itatokea wakati wa kupiga kura na kwa maoni ya Spika tatizo lililotokea haliwezi kurekebishwa, Spika anaweza kuelekeza

awamu nyingine ya kura ya kielektroniki ifanyike au kuamuru kura ya kuita majina ifanyike.

**Kura ya kuita majina inapodaiwa**

**72.** (1) Spika ataelekeza kura ya kuita majina itumike iwapo Mbunge atadai kura ya mgawanyiko na—

(a) Spika ameshawishika kuwa kuna tashwishi kuhusu matokeo ya kura inayohusika; au

(b) iwapo, kwa Hoja isipokuwa Hoja ya utaratibu, na Wabunge thelathini au zaidi wasimame mahali pao kumuunga mkono Mbunge anayedai kura ya kuita majina.

(2) Spika ataelekeza kura ya mgawanyiko itumike katika kila hali ambapo Katiba inahitaji wingi wa idadi mahususi ya Wabunge itumike kuamua suala lolote.

**Kura ya kuita majina**

**73.** (1) Spika anapoelekeza kura ya kuita majina itumike, Kengele ya Mgawanyiko itakirizwa kwa dakika kumi.

(2) Majina ya mawakala, mmoja wa upande wa "Ndiyo" na mwingine wa upande wa "La", yatawasilishwa kwa Spika ambaye ataelekeza mawakala hao kuketi katika sehemu iliyotengwa.

(3) Dakika kumi zitakapoisha, Spika ataagiza milango ya Ukumbi ifungwe na Kizuio kifungwe na baada ya hapo hakuna Mbunge yeyote atakayeingia au kutoka katika Ukumbi hadi kura ya kuita majina itakapokamilika.

(4) Mara baada ya milango ya Ukumbi kufungwa na Kizuio kufungwa na majina ya mawakala kutangazwa, Spika atatoa tena Hoja iamuliwe na atamwelekeza Katibu kuita majina ya Wabunge kwa kufuata mpangilio wa kialfabeti mbele ya mawakala.

(5) Kila Mbunge atakayeitwa atasimama mahali pake na kutamka kuridhia au kutoridhia Hoja inayohusika kwa namna ifuatayo: "Ninapiga Kura ya Ndiyo"; au, "Ninapiga Kura ya La"; au, "Nazia" au atumie ishara zifaazo za Lugha ya Ishara ya Kenya kupiga kura.

(6) Baada ya Katibu kusoma jina la mwisho kwenye Orodha ya Wabunge wote, mawakala watawasilisha matokeo ya kura ya kuita majina kwa Spika ambaye atatangaza matokeo hayo kwa Bunge mara hiyo.

**Mkanganyiko au kasoro inapotokea**

**74.** Iwapo wakati wa kura ya kuita majina kutatokea mkanganyiko au kasoro isiyoweza kurekebishwa kuhusiana na idadi au majina ya Wabunge waliorekodiwa, Spika ataelekeza kura ya kuita majina irudiwe.

**Kurekebisha kasoro**

**75.** Iwapo baada ya kura ya kuita majina kukamilika itagunduliwa kwamba idadi iliyoripotiwa si sahihi au kasoro imetokea kwenye Orodha ya Wabunge wote, Bunge la Taifa litajulishwa na Spika ataelekeza marekebisho yafaayo yafanywe.

**Staha wakati wa kura ya mgawanyiko**

**76.** (1) Hakuna Mbunge atakayeshurutishwa kupiga kura wakati wa kura ya mgawanyiko, lakini waliopo na hawapigi kura watahitajika ama—

(a) kubofya kitufe cha **"Mzio"** iwapo ni kura ya kielektroniki; au

(b) kuandikisha kura yake ya kuzia kwa Katibu iwapo ni kura ya kuita majina.

(2) Itakuwa ni utovu wa nidhamu kwa Mbunge kutoandikisha kura yake ya kuzia katika kura ya mgawanyiko.

(3) Mbunge hatapiga kura kwa hoja yoyote ambamo ana maslahi ya kifedha.

(4) Wakati wa kura ya mgawanyiko, Wabunge watadumisha utulivu katika Ukumbi na sharti wasalie vitini mwao hadi matokeo ya kura yatangazwe.

## SEHEMU YA XVI- MASHARTI YA MJADALA

### Shughuli kuendeshwa kwa Kiswahili, Kiingereza au Lugha Ishara ya Kenya

**77.** (1) Shughuli zote za Bunge la Taifa zitaendeshwa kwa Kiswahili, Kiingereza au Lugha Ishara ya Kenya.

(2) Mbunge anapoanza kutoa mchango wake katika lugha yoyote kati ya zile zilizotajwa katika aya ya (1) ataendelea kwa lugha hiyo hadi mwisho wa mchango wake.

### Wabunge kuelekeza ombi kwa Spika

**78.** Kila Mbunge anayetaka kuzungumza ataelekeza ombi lake kwa Spika.

### Wabunge wawili au zaidi wanapoomba kuchangia

**79.** Iwapo Wabunge wawili au zaidi wataomba kuchangia kwa wakati mmoja, Mbunge atakayeteuliwa na Spika ndiye atakayechangia.

### Kutosoma Michango

**80.** (1) Mbunge hatasoma mchango lakini anaweza kusoma dondoo fupi kwenye nyaraka na machapisho ili kuthibitisha hoja zake na anaweza kujikumbusha kwa kurejelea vidokezo alivyoandika.

(2) Spika anaweza kumruhusu Mbunge kusoma mchango wake ikiwa Spika ameridhika kwamba kufanya hivyo ni muhimu katika kufafanua usahihi na udhahiri wa maelezo yake.

**Mbunge kutozungumza baada ya Hoja kutolewa iamuliwe**

**81.** Mbunge hatazungumzia hoja yoyote baada ya Spika kutoa Hoja iamuliwe.

**Kuchangia Hoja mara mbili**

**82.** (1) Mbunge hatachangia Hoja zaidi ya mara moja ila tu katika Kamati ya Bunge Zima.

(2) Licha ya aya ya (1)—

(a) Mbunge ambaye amechangia Hoja anaweza kuruhusiwa kuongea tena ili kufafanua sehemu ya mchango wake ambao haukueleweka vizuri ilimradi asiibue suala jipya;

(b) Mbunge aliyewasilisha Hoja mahususi atapewa haki ya kuhitimisha Hoja lakini Mbunge aliyewasilisha marekebisho hana haki hiyo.

(3) Mbunge mwenye Hoja mahususi anaweza kuacha haki yake yote ya kuhitimisha Hoja au sehemu ya haki hiyo kwa Mbunge mwingine au wengine atakaowateua na ambao hawajachangia Hoja hiyo.

**Mbunge aliyechangia Hoja anaweza kuchangia rekebisho**

**82A.** Rekebisho linapopendekezwa na kuafikiwa, ikiwa lafaa kuafikiwa, Mbunge ambaye amechangia Hoja anaweza kuchangia rekebisho na Mbunge yeyote ambaye hajachangia Hoja lakini amechangia rekebisho hatapoteza haki yake ya kuchangia Hoja.

**Mjadala wa rekebisho kujikita kwenye rekebisho**

**82B.** (1) Rekebisho la Hoja likishatolewa, na kuafikiwa ikiwa lafaa kuafikiwa, mjadala wake utajikita kwenye rekebisho hilo.

(2) Licha ya aya ya (1), Spika anaweza kuelekeza kuwa mjadala kuhusu rekebisho unaweza kujumuisha masuala yanayohusiana na Hoja iwapo, kwa maoni yake, sio rahisi

kutenganisha masuala yanayoibuka kwenye rekebisho kutokana na maudhui ya hoja.

(3) Spika anapotoa maelekezo kwa mujibu wa aya ya (2), Mbunge ambaye amechangia rekebisho atapoteza haki ya kuchangia Hoja baada ya rekebisho hilo kuamuliwa na iwapo Mbunge yeyote aliyechangia Hoja atachangia rekebisho, atazungumzia tu suala jipya litakaloibuka.

**Kuhifadhi haki ya kuchangia**

**82C.** Hoja ikishatolewa, isipokuwa Hoja ya rekebisho iliyopendekezwa na Spika, Mbunge anaweza kusimama mahali pake na kuinamisha kichwa kuashiria kuafiki Hoja bila kuzungumza na kwa kufanya hivyo atakuwa amehifadhi haki ya kuchangia kana kwamba Hoja hiyo imeafikiwa na Mbunge mwingine.

**Hoja ya Nidhamu**

**83.** (1) Mbunge yeyote anaweza kuibua hoja ya nidhamu wakati wowote Mbunge mwingine anapochangia kwa kueleza kwamba anasimama kwa hoja ya nidhamu na atahitajika kuitaja Kanuni inayokiukwa.

(2) Mbunge anapoibua hoja ya nidhamu wakati wa mchango wa Mbunge mwingine, Mbunge aliyekuwa akichangia ataketi na Mbunge anayeibua hoja ya nidhamu pia atafanya vivyo hivyo atakapomaliza kuiwasilisha, hakuna Mbunge mwingine yeyote atakayechangia hoja hiyo ya nidhamu ila tu kwa idhini ya Spika.

(3) Spika atatoa uamuzi kuhusu hoja ya nidhamu papo hapo au atatangaza kuwa uamuzi utatolewa baada ya kuitathmini na Mbunge aliyekuwa akichangia kabla ya hoja ya nidhamu kutolewa anaweza kuendelea kuchangia.

(4) Spika au Mwenyekiti atamuamuru Mbunge yeyote ambaye anaendelea kuvuruga shughuli bila sababu za msingi au kushauriana kwa sauti ya juu, aondoke katika Ukumbi na

masharti ya Kanuni ya 107 (*Utovu wa Nidhamu*) yatatumika kwa Mbunge mwingine yeyote kama huyo.

**84.** (*imefutwa).*

**Kuwahi mjadala**

**85.** (1) Ni marufuku kuwahi mjadala wa Mswada ambao tayari umechapishwa kwenye *Gazeti Rasmi la Serikali* kupitia kwa Hoja mahususi au kwa rekebisho, au kuibua maudhui ya Mswada huo kupitia Hoja ya kuahirisha shughuli za Bunge la Taifa.

(2) Ni marufuku kuwahi mjadala wa Hoja ambayo arifa yake imeshatolewa katika Bunge kwa kujadili Hoja mahususi au rekebisho, au kuibua maudhui yanayofanana na Hoja hiyo kupitia kwa Hoja ya kuahirisha shughuli za Bunge la Taifa.

(3) Katika kuamua iwapo mjadala umekiuka utaratibu kwa misingi ya kuuwahi, uamuzi utazingatia uwezekano wa jambo hilo kuwasilishwa katika Bunge la Taifa kwa muda ufaao.

**Kutorejelea shughuli za Kamati**

**86.** Mbunge yeyote hatarejelea au kujadili kiini cha mambo yanayoshughulikiwa na Kamati kabla Kamati hiyo haijawasilisha ripoti yake katika Bunge la Taifa.

**Maudhui ya michango**

**87.** (1) Hairuhusiwi kudhalilisha mwenendo binafsi wa Rais, Spika, Jaji, mtu yeyote anayetekeleza majukumu ya kimahakama, mwenendo wa Mkuu wa Nchi au Serikali, mwakilishi wa nchi yoyote rafiki nchini Kenya au mwenendo wa ofisa yeyote ambaye kuondolewa kwake mamlakani kunahitaji uamuzi wa Bunge la Taifa, isipokuwa kupitia kwa Hoja mahususi ambayo arifa yake imetolewa angalau siku tatu kabla ya Hoja hiyo kujadiliwa.

(2) Ni marufuku kuibua mjadala kuhusu suala ambalo limeamuliwa na Bunge la Taifa katika Kipindi hicho, isipokuwa kupitia Hoja ya kutengua uamuzi huo ambayo itatolewa kwa ruhusa ya Spika.

(3) Ni marufuku kutumia lugha ya kuudhi au ya matusi kwa Wabunge au watu wengine.

(4) Mbunge hatatoa tuhuma zisizo na msingi kuhusu Mbunge mwingine yeyote au Seneta isipokuwa kwa Hoja mahususi ambayo arifa yake imetolewa angalau siku tatu kabla ya Hoja ya kujadili mwenendo wa Mbunge au Seneta huyo.

(5) Ni marufuku kwa Mbunge kushutumu au kukosoa shughuli za Seneti au Uamuzi Maalum wa Spika wa Seneti ingawa mjadala unaweza kuruhusiwa kuhusu muundo na majukumu ya Seneti au Bunge.

(6) Isipokuwa Spika aruhusu vinginevyo, itakuwa marufuku kwa Mbunge kurejelea dondoo kutoka katika magazeti au vyombo vya habari vya kielektroniki kama rejeleo rasmi katika hotuba yake.

**Kuondoa machukizo na kuomba radhi**

**88.** Mbunge ambaye ametumia maneno yanayochukiza na kukataa kutoa maelezo na kuondoa maneno hayo au kuomba radhi inayomridhisha Spika atachukuliwa kuwa mtovu wa nidhamu na ataadhibiwa kwa mujibu wa masharti yanayohusu utovu wa nidhamu.

**Masuala yanayosubiri uamuzi wa Mahakama au masuala ya siri**

**89.** (1) Kwa kuzingatia aya ya (5), Mbunge hataruhusiwa kuzungumzia suala lolote ambalo linasubiri uamuzi wa Mahakama au ni la siri kwa mujibu wa sheria yoyote.

(2) Suala litachukuliwa kuwa linasubiri uamuzi wa Mahakama ikiwa linarejelea kesi ya jinai au daawa inayoendelea na mjadala kuhusu suala hilo unaweza kuathiri uamuzi wa haki.

(3) Katika kuamua iwapo kesi ya jinai au daawa inaendelea, yafuatayo yatazingatiwa—

(a) kesi ya jinai itachukuliwa kuwa inaendelea ikiwa mashtaka yamesomwa mahakamani au hati ya wito wa mahakama imetolewa;

(b) kesi ya jinai itachukuliwa kuwa imekwisha iwapo itahitimishwa baada ya uamuzi na hukumu kutolewa au baada ya kesi kukomeshwa;

(c) kesi ya daawa itachukuliwa kuwa inaendelea iwapo taratibu za kusikiliza kesi hiyo, kama vile kupanga kesi kwa ajili ya kusikilizwa, zimefanywa, hadi kesi itakapohitimishwa baada ya hukumu kutolewa au kesi kukomeshwa;

(d) Rufaa ya kesi ya jinai au ya daawa itachukuliwa kuwa inaendelea kuanzia wakati ambapo rufaa imeanzishwa kupitia kwa ombi la idhini au notisi ya kukata rufaa inapotolewa hadi rufaa itakapohitimishwa baada ya hukumu kutolewa au kesi kukomeshwa.

(4) Mbunge anayedai kuwa suala linasubiri uamuzi wa Mahakama atahitajika kutoa ithibati inayoonyesha kwamba aya ya (2) na ya (3) zinatumika.

(5) Licha ya Kanuni hii, Spika anaweza kuruhusu kurejelewa kwa jambo lolote lililo katika Bunge la Taifa au kwenye Kamati.

### Kutangaza maslahi ya kibinafsi

**90.** (1) Mbunge anayetaka kuzungumzia jambo lolote ambalo ana maslahi ya kibinafsi nalo, atataja maslahi hayo kabla ya kulizungumzia jambo hilo.

(2) Maslahi ya kibinafsi yanajumuisha maslahi ya kifedha, maslahi ya umiliki wa mali, mahusiano ya kibinafsi na ya kibiashara.

(3) Spika anaweza kumruhusu Mbunge kuchangia suala linalojadiliwa baada ya kutathmini hali, upeo na athari za maslahi aliyotangaza Mbunge huyo.

(4) Tangazo lolote la maslahi litakalotolewa kwa mujibu wa kanuni hii litahifadhiwa katika Majarida ya Bunge la Taifa.

**Kuwajibikia madai**

**91.** (1) Mbunge atawajibikia usahihi wa jambo lolote analodai kuwa ni la kweli na anaweza kutakiwa kuthibitisha madai hayo papo hapo.

(2) Iwapo Mbunge ana sababu ya kumridhisha Spika kwamba Mbunge anayechangia hawezi kuthibitisha madai yake papo hapo, Spika atamhitaji Mbunge anayechangia kuthibitisha madai yake isiwe baada ya kikao kinachofuata, vinginevyo, atachukuliwa kuwa amekiuka masharti kwa mujibu wa Kanuni ya 107 (*Utovu wa Nidhamu*) isipokuwa kama Mbunge huyo ataondoa madai hayo na kuomba radhi ifaayo, iwapo Spika atamhitaji kufanya hivyo.

**92.** *(imefutwa).*

**93.** *(imefutwa).*

**94.** *(imefutwa).*

**Kuhitimisha mjadala**

**95.** (1) Baada ya Hoja ambayo Mtoahoja ana haki ya kuhitimisha imependekezwa ijadiliwe, Mbunge anaweza kusimama mahali pake na kutoa Hoja ***"Kwamba, Mtoahoja sasa aitwe kuhitimisha,"*** na, isipokuwa kama Spika ana maoni kwamba Hoja hiyo inahujumu shughuli za Bunge la Taifa au inakiuka haki za Wabunge, Hoja ***"Kwamba, Mtoahoja sasa aitwe kuhitimisha,"*** itatolewa mara moja ili iamuliwe na itaamuliwa bila rekebisho au mjadala na ikipitishwa, Mtoahoja anaweza kuhitimisha papo hapo na, punde baada ya Mtoahoja kuhitimisha, au kama hataki kuhitimisha, Spika atalihoji

Bunge la Taifa kuamua Hoja hiyo mara moja kwa mujibu wa aya ya 3 ya Kanuni ya 53 (*Utaratibu wa kujadili Hoja*).

(2) Baada ya Hoja ambayo Mtoahoja hana haki ya kuhitimisha imependekezwa ijadiliwe, Mbunge anaweza kusimama mahali pake na kutoa Hoja ***"Kwamba, Hoja sasa itolewe ili iamuliwe"*** na, isipokuwa kama Spika ana maoni kwamba Hoja hiyo inahujumu shughuli za Bunge la Taifa au inakiuka haki za Wabunge, Hoja ***"Kwamba, Hoja sasa itolewe ili iamuliwe,"*** itatolewa mara moja ili iamuliwe na itaamuliwa bila rekebisho au mjadala na ikipitishwa, Spika atalihoji Bunge la Taifa kuamua Hoja hiyo mara moja kwa mujibu wa aya ya 3 ya Kanuni ya 53 (*Utaratibu wa kujadili Hoja*).

(3) Masharti ya Kanuni hii hayatatumika kwa Mswada wa kurekebisha Katiba.

**Kuendeleza shughuli iliyositishwa**

**95A.** Mjadala wowote uliositishwa kwa mujibu wa Sehemu hii utakaporejewa katika Bunge la Taifa au kwenye Kamati, utaendelezwa mahali ulipokuwa umefikia na Mbunge yeyote ambaye mchango wake ulisitishwa atakuwa na haki ya kuchangia kwa muda wake uliosalia vinginevyo Mbunge huyo asipojitokeza kutumia haki yake, itachukuliwa kwamba alikuwa amekamilisha mchango wake.

**Kuahirisha mjadala**

**96.** (1) Mbunge anayekusudia kuahirisha mjadala wa Hoja iliyopendekezwa na Spika au Mwenyekiti ili ijadiliwe wakati mwingine anaweza kuomba kuwasilisha Hoja ***"Kwamba, sasa mjadala uahirishwe,"*** au, iwapo Bunge la Taifa lipo kwenye Kamati ya Bunge Zima ***"Kwamba, Mwenyekiti aripoti hatua iliyofikiwa."***

(2) Mjadala wa Hoja ya Mkawilisho utajikita kwenye suala la Hoja hiyo.

(3) Iwapo Spika ana maoni kwamba Hoja ya Mkawilisho inahujumu shughuli za Bunge la Taifa, anaweza kukataa kuipendekeza ijadiliwe.

(4) Mbunge ambaye ametoa au ameafiki Hoja ya Mkawilisho na kukataliwa hataruhusiwa kutoa au kuafiki Hoja nyingine kama hiyo katika mjadala huo kwenye Kamati ya Bunge Zima au katika Bunge la Taifa.

## SEHEMU YA XVII—KUDHIBITI MJADALA

**Kudhibiti mjadala**

**97.** (1) Bunge la Taifa linaweza kudhibiti mjadala kuhusu Hoja au Mswada kwa kutenga muda wa mjadala huo au kwa kudhibiti muda ambao Wabunge wanaweza kuchangia mjadala huo au kwa kuweka vidhibiti vinginevyo, kufuatia Hoja iliyotolewa na Mbunge yeyote kwa mujibu wa Kanuni hii.

(2) Hoja ya kudhibiti mjadala kwa mujibu wa Kanuni hii inaweza kutolewa bila arifa.

(3) Hoja kwa mujibu wa aya ya (2) haitatolewa iwapo inadhibiti mjadala unaoendelea isipokuwa kama Hoja hiyo imetolewa baada ya kuahirishwa kwa mjadala huo na kabla ya mjadala huo kuendelezwa.

(4) Mbunge yeyote hataruhusiwa kuchangia Miswada, Sera za Serikali, Hoja au Ripoti za Kamati kwa zaidi ya dakika ishirini bila idhini ya Spika isipokuwa Kiongozi wa Chama cha walio Wengi na Kiongozi wa Chama cha Walio wachache ambao wanaweza kuchangia kwa muda usiozidi dakika sitini kila mmoja.

(5) Masharti ya Kanuni hii hayatatumika kwa Mswada wa kurekebisha Katiba.

## SEHEMU YA XVIII - UTULIVU KATIKA UKUMBI NA KWENYE KAMATI YA BUNGE ZIMA

**Kudumisha utulivu**

**98.** Spika atakuwa na wajibu wa kudumisha utulivu katika Bunge la Taifa na Mwenyekiti atadumisha utulivu katika Kamati ya Bunge Zima lakini kukosekana kwa utulivu wakati wa Kamati ya Bunge Zima kutakaripiwa na Bunge la Taifa baada ya kupokea ripoti.

**Ukaguzi wa kiusalama**

**99.** (1) Mbunge atakaguliwa kwa ajili ya kuhakikisha usalama kabla ya kuingia katika Ukumbi.

(2) Ukaguzi wa kiusalama kwa mujibu wa aya ya (1) utahusisha ukaguzi wa mkoba au kifaa kingine ambacho Mbunge anakusudia kuingia nacho katika Ukumbi.

**Bunduki na silaha nyingine hatari**

**100.** Mbunge hataruhusiwa kuingia katika Ukumbi na bunduki au silaha nyingine yoyote hatari na atahitajika kumkabidhi Mpambe wa Bunge la Taifa bunduki au silaha hiyo kabla ya kuingia katika Ukumbi na atarejeshewa akitoka katika Ukumbi.

**Mikoba ya Wabunge wa kike**

**101.** Mbunge wa kike anaweza kuruhusiwa kuingia katika Ukumbi na mkoba wa ukubwa wa wastani.

**Wabunge kuwa kimya Spika anaposimama**

**102.** Kila wakati Spika au Mwenyekiti wa Kamati anaposimama, Mbunge yeyote anayechangia au anayetaka kuchangia ataketi kwenye kiti chake na Bunge la Taifa au Kamati litakuwa kimya ili Spika au Mwenyekiti wa Kamati asikilizwe bila kukatizwa.

**Wabunge na Kiongozi wa Kikao**

**103.** (1) Kila Mbunge anapopita kutoka au kuelekea kwenye kiti chake au anapovuka Sakafu ya Ukumbi, atainamisha kichwa kwa staha kuelekea kwa Kiongozi wa Kikao au kuonyesha heshima kwa Kiongozi wa Kikao kwa namna nyingine yoyote kulingana na imani yake na hadhi ya Bunge.

(2) Hakuna Mbunge atakayepita kati ya Kiongozi wa Kikao na Mbunge anayechangia au kati ya Kiongozi wa Kikao na Meza isipokuwa pale itakapohitajika wakati wa kiapo au kukiri kuwajibikia mamlaka ya ubunge.

**Wabunge kuketi**

**104.** Kila Mbunge atasalia ameketi akiwa katika Ukumbi na hataruhusiwa kusimama kwenye vijia baina ya viti isipokuwa wakati anaondoka au kurejea kwenye kiti chake au anapochangia.

**Wabunge kusalia mahali pao hadi Spika atakapoondoka katika Ukumbi**

**105.** Kikao cha Bunge la Taifa kinapoahirishwa, Wabunge watasimama mahali pao hadi Spika atakapoondoka katika Ukumbi.

**Kutoka nje ya mada au kurudiarudia**

**106.** Spika au Mwenyekiti wa Kamati akishamjulisha Mbunge kuhusu mwenendo wake wa kuendelea kutoka nje ya mada au kurudiarudia maneno au mchango wake au michango ya Wabunge wengine katika mjadala, anaweza kumwamuru Mbunge huyo akomeshe mchango wake baada ya kumpa onyo.

**Utovu wa nidhamu**

**107.** (1) Mbunge atakuwa ametenda kosa la utovu wa nidhamu ikiwa—

(a) atasababisha vurugu;

(b) ataibua hoja ya nidhamu isiyo ya ukweli kimakusudi;

(c) atachachawiza shughuli za Bunge la Taifa bila msingi au kushauriana kwa namna inayovuruga shughuli;

(d) atakosa kuandikisha kura yake ya mzio katika kura ya mgawanyiko;

(e) hatatangaza maslahi ya kibinafsi katika jambo linaloshughulikiwa na Bunge la Taifa au Kamati kwa mujibu wa Kanuni ya 90 (*Kutangaza maslahi ya kibinafsi*);

(f) atatoa habari zisizo za ukweli katika Bunge la Taifa kimakusudi;

(g) atatoa tuhuma ambazo, kwa maoni ya Spika, hazina ushahidi wa kutosha;

(h) atatishia kutumia nguvu dhidi ya Mbunge au mtu mwingine katika Bunge la Taifa au kwenye Kamati;

(i) atapiga kura zaidi ya mara moja kinyume na Kanuni hizi;

(j) atakiuka Kanuni hizi kwa namna nyingine yoyote ambayo, kwa maoni ya Spika, ni utovu wa nidhamu.

(2) Spika anaweza kumtaka Mbunge ambaye ametenda kosa la utovu wa nidhamu kujirekebisha, na—

(a) kumwonya Mbunge huyo; au

(b) kumuamuru Mbunge huyo kuondoka maeneo ya Bunge kwa muda usiozidi siku nne.

**Utovu mkubwa wa nidhamu**

**107A.** (1) Mbunge atakuwa ametenda kosa la utovu mkubwa wa nidhamu ikiwa—

(a) atapuuza uamuzi au maelekezo ya Spika au Mwenyekiti wa Kamati;

(b) atakataa kufafanua au kuondoa maneno yasiyo ya kibunge au atakataa kuomba radhi licha ya Spika kumtaka kufanya hivyo;

(c) atadhihirisha au kutoa matamshi ya ubishi dhidi ya uamuzi wa kumsimamisha Mbunge kutohudhuria vikao kwa muda;

(d) atajaribu kutenda au atatenda kosa la utovu wa nidhamu wa namna yoyote wakati wa hotuba ya mgeni mashuhuri;

(e) atatumia nguvu dhidi ya Mbunge au mtu mwingine katika Bunge la Taifa au kwenye Kamati;

(f) atajaribu kuvuruga au atavuruga Msafara wa Spika unapoingia au unapotoka katika Ukumbi;

(g) atajaribu kuondoa au ataondoa siwa kutoka mahali pake katika Ukumbi;

(h) atatenda kwa namna nyingine yoyote ambayo itashusha hadhi ya Bunge la Taifa kwa kiasi kikubwa au kuvuruga utaratibu wa Bunge la Taifa;

(i) atakiuka Kanuni hizi kwa namna nyingine yoyote ambayo, kwa maoni ya Spika, ni utovu mkubwa wa nidhamu.

(2) Katika Kanuni hii, "matamshi yasiyo ya kibunge" ina maana ya kutumia maneno ambayo, kwa maoni ya kiongozi wa kikao, yanaashiria ujeuri, kukosa adabu, matusi au kutozingatia utaratibu au desturi za Bunge.

(3) Spika anaweza kumtaka Mbunge ambaye ametenda kosa la utovu mkubwa wa nidhamu kujirekebisha, na kumuamuru Mbunge huyo kuondoka maeneo ya Bunge mara moja kwa muda usiopungua siku tano na usiozidi siku ishirini na nane, ikiwemo siku aliyosimamishwa kuhudhuria vikao kwa muda.

**Mbunge anaweza kusimamishwa kwa muda baada ya kutajwa jina**

**108.** (1) Mbunge yeyote wakati wowote ule, kupitia hoja ya nidhamu, anaweza kumuomba Spika au Mwenyekiti wa Kamati kumtaja Mbunge jina kwa utovu mkubwa wa nidhamu lakini uamuzi wa kufanya hivyo ni wa Spika au Mwenyekiti.

(2) Wakati wowote Mbunge atakapotajwa kwa jina na Spika au Mwenyekiti, basi

(a) iwapo ukiukaji umefanywa na Mbunge katika Ukumbi, Hoja itawasilishwa na Mbunge yeyote ***"Kwamba, Mbunge huyo (jina la Mbunge) asimamishwe kuhudhuria vikao kwa muda,"*** na Spika atatoa Hoja ili iamuliwe mara moja bila marekebisho, ahirisho au mjadala;

(b) iwapo ukiukaji huo umefanywa kwenye Kamati ya Bunge Zima, Mwenyekiti ataondoka kwenye Kiti mara moja na kuripoti suala hilo kwa Bunge la Taifa; na Spika, kufuatia Hoja iliyotolewa, atatoa Hoja ili iamuliwe mara moja bila marekebisho, ahirisho au mjadala, kama kwamba kosa hilo lilifanyika wakati Bunge la Taifa likiendelea.

**Mbunge aliyesimamishwa kuhudhuria vikao vya Bunge kwa muda ataondoka katika maeneo ya Bunge**

**109.** Mbunge anapotajwa jina kwa mujibu wa Kanuni ya 108 (*Mbunge anaweza kusimamishwa kwa muda baada ya kutajwa jina*), Spika atamwamuru Mbunge huyo kutoka katika Ukumbi na katika maeneo ya Bunge.

**Muda wa Mbunge kusimamishwa kwa muda**

**110.** Iwapo Mbunge atasimamishwa kwa muda kwa mujibu wa Kanuni ya 108 (*Mbunge anaweza kusimamishwa kwa muda baada ya kutajwa jina*), ikiwa ni mara ya kwanza kusimamishwa, atasimamishwa kwa siku nne ikijumuisha siku ya kusimamishwa; ikiwa ni mara ya pili katika Kipindi

hicho, atasimamishwa kwa siku nane ikijumuisha siku ya kusimamishwa; na ikiwa ni mara ya tatu au zaidi katika Kipindi hicho, atasimamishwa kwa siku ishirini na nane ikijumuisha siku ya kusimamishwa.

**Athari za kusimamishwa kwa muda**

**110A.** (1) Mbunge anayeamriwa kuondoka katika maeneo ya Bunge kwa mujibu wa Kanuni ya 108 (*Mbunge anaweza kusimamishwa kwa muda baada ya kutajwa jina*) na Kanuni ya 111 (*Hatua itakayochukuliwa kwa kukaidi amri ya kuondoka*) katika kipindi ambacho atakuwa amesimamishwa kwa muda atapoteza—

(a) haki ya kuingia katika maeneo ya Bunge; na

(b) mshahara na marupurupu yote ambayo angelipwa katika kipindi hicho.

(2) Mbunge aliyesimamishwa kwa muda hatazuiwa kuhudhuria kikao cha Kamati kinachoshughulikia Mswada anaoudhamini.

**Rufaa dhidi ya kusimamishwa kwa muda**

**110B.** (1) Isipokuwa kama ilivyoelekezwa katika Kanuni hii, hakutakuwa na mjadala kuhusu kusimamishwa kwa Mbunge kwa muda au pale ambapo Kanuni hii itatumika.

(2) Mbunge aliyesimamishwa kwa muda kwa mujibu wa Sehemu hii, anaweza kukata rufaa kwa maandishi kwa Kamati ya Haki za Bunge katika muda usiozidi siku tatu baada ya kusimamishwa kwa muda.

(3) Licha ya aya ya (2), Kamati hiyo kwa idhini ya Bunge la Taifa, inaweza kukubali rufaa iliyopokelewa baada ya siku tatu kupita.

(4) Baada ya kupokea rufaa ya Mbunge, Kamati, katika muda usiozidi siku saba —

(a) itamuarifu Mbunge kwa maandishi kuhusu siku iliyotengwa ili kusikiliza rufaa hiyo;

(b) itamuarifu Spika, ambaye atamruhusu Mbunge huyo kuingia maeneo ya Bunge siku iliyotengwa ili kusikiliza rufaa; na

(c) itashughulikia rufaa na baada ya kumpa Mbunge huyo haki ya kusikilizwa, itawasilisha ripoti katika Bunge la Taifa—

(i) ikikubaliana na adhabu ya kusimamishwa kwa muda; au

(ii) kupunguza muda wa kusimamishwa; au

(iii) kumruhusu Mbunge huyo kurudi bungeni.

(5) Uamuzi wa Kamati hiyo kuhusu kusimamishwa kwa muda utakuwa wa mwisho.

(6) Mbunge aliyeongoza kikao cha Bunge la Taifa au Kamati ya Bunge Zima wakati wa kumsimamisha kwa muda Mbunge aliyekata rufaa hatashiriki katika vikao vya Kamati inaposhughulikia rufaa hiyo, isipokuwa kama atahitajika kutoa ushahidi.

(7) Mbunge aliyeteuliwa na Kamati atalijulisha Bunge la Taifa uamuzi wa Kamati kuhusu usimamishwaji huo na Spika atatekeleza uamuzi huo mara moja.

(8) Katika hali za kipekee zitakazoruhusiwa na Spika, Bunge la Taifa linaweza kujadili ripoti ya Kamati hiyo bila rekebisho au uamuzi wowote kufanywa.

**Hatua itakayochukuliwa kwa kukaidi amri ya kuondoka**

**111.** Iwapo Mbunge yeyote atakataa kuondoka kama alivyoamriwa kwa mujibu wa Kanuni hizi, Spika au Mwenyekiti wa Kamati, baada ya kulifahamisha Bunge la Taifa au Kamati kwamba kuna haja ya nguvu kutumika kumwondoa Mbunge huyo, ataamuru Mbunge aondolewe na Mbunge husika

atasimamishwa kuhudhuria vikao vya Bunge la Taifa kwa muda usiopungua siku ishirini na moja na usiozidi siku tisini bila ya kulihoji Bunge la Taifa na katika kipindi hicho, Mbunge huyo atapoteza haki ya kuingia maeneo ya Bunge na Mpambe wa Bunge la Taifa atachukua hatua itakayohitajika kutekeleza amri hiyo.

**Utovu wa nidhamu uliokithiri katika Bunge la Taifa**

**112.** (1) Iwapo patatokea utovu wa nidhamu uliokithiri katika Bunge, Spika anaweza kuahirisha kikao cha Bunge la Taifa mara moja au kusimamisha kikao chochote kwa muda atakaoamua.

(2) Iwapo patatokea utovu wa nidhamu uliokithiri katika Kamati ya Bunge Zima, Spika atarejea kwenye Kiti mara moja.

**Maana ya siku**

**112A.** Kwa mujibu wa Sehemu hii, "siku" ina maana ya siku ya kalenda.

## SEHEMU YA XIX—MISWADA YA UMMA

**Matumizi na udhibiti**

**113.** Sehemu hii itatumika kwa miswada yote ya umma.

**Uwasilishaji wa Miswada**

**114.** (1) Pendekezo la mswada linaweza kutolewa kwa Spika na Mbunge mmoja au zaidi au Kamati ili kuwasilishwa katika Bunge la Taifa likiwa na maelezo ya madhumuni na masuala yaliyotajwa katika Kanuni ya 117 *(Maelezo ya Madhumuni na Sababu).*

(1A) Wabunge wanapotoa pendekezo kwa pamoja kwa mujibu wa aya ya (1) wataonyesha—

(a) jina la mdhamini mkuu wa pendekezo hilo ambaye ni Mbunge atakayelisimamia katika Bunge la Taifa; na

(b) majina ya wadhamini wenza wa pendekezo hilo kwa kufuata mpangilio wa kialfabeti.

(2) Spika atamkabidhi Katibu pendekezo la mswada pamoja na maelezo ya madhumuni na sababu, na Katibu atashughulikia pendekezo hilo na kuliandika katika muundo unaofaa kisha ataliwasilisha kwa Spika likiwa na maoni kuhusu—

(a) ikiwa pendekezo hilo la mswada linaathiri au haliathiri kaunti, na kama linaathiri kaunti, kueleza iwapo ni Mswada maalum au wa kawaida;

(b) ikiwa pendekezo hilo la mswada linahusu masuala ya fedha kwa mujibu wa Ibara ya 114 ya Katiba; na

(c) ikiwa pendekezo la mswada halikiuki masharti ya Katiba na sheria na liko sawa katika muundo na mtindo kuambatana na Kanuni hizi.

(3) Baada ya kupokea pendekezo la mswada kutoka kwa Katibu kwa mujibu wa aya ya (2), Spika—

(a) akiwa na maoni kuwa pendekezo la mswada halihusu masuala ya fedha kwa mujibu wa Ibara ya 114 ya Katiba—

(i) ataelekeza pendekezo likabidhiwe kamati husika ya kiidara ili lichanganuliwe kabla ya kuchapishwa iwapo pendekezo la mswada halijadhaminiwa na Kamati; au

(ii) ataelekeza pendekezo hilo lichapishwe kuwa mswada, iwapo limedhaminiwa na Kamati; au

(b) akiwa na maoni kwamba pendekezo la mswada linahusu masuala ya fedha kwa mujibu wa Ibara ya 114 ya Katiba, ataelekeza pendekezo hilo likabidhiwe Kamati ya Bajeti na Uidhinishaji wa Matumizi na

pendekezo hilo litashughulikiwa tu kulingana na mapendekezo ya Kamati ya Bajeti na Uidhinishaji wa Matumizi baada ya kuzingatia maoni ya Waziri anayehusika na masuala ya fedha.

(4) Kamati ya Bajeti na Uidhinishaji wa Matumizi itashughulikia tu masuala ya fedha au vipengele vyenye masuala ya kifedha vilivyomo kwenye pendekezo na kutoa ripoti kwa Spika katika muda usiozidi siku thelathini baada ya kupokelewa kwa pendekezo hilo.

(5) Ripoti itakayotolewa kwa mujibu wa aya ya (4) itakuwa na—

(a) maoni ya Waziri anayehusika na masuala ya fedha, ikiwa yapo;

(b) uchunguzi wa kina wa namna pendekezo hilo linavyoathiri bajeti iliyopo na bajeti za baadaye na inaweza kujumuisha maelezo ya athari kwa mikakati ya utozaji kodi;

(c) maoni iwapo pendekezo la mswada lishughulikiwe au lisishughulikiwe;

(d) maoni mengine yoyote mwafaka yanayohusiana na vipengele vya masuala ya fedha vilivyomo kwenye pendekezo.

(6) Baada ya kupokea maoni ya Kamati ya Bajeti na Uidhinishaji wa Matumizi, Spika anaweza kuelekeza kwamba—

(a) pendekezo la mswada lifanyiwe uchanganuzi kabla ya kuchapishwa na kamati husika ya kiidara ikiwa pendekezo hilo halijadhaminiwa na Kamati; au

(b) pendekezo hilo lichapishwe ili kuwa mswada, ikiwa pendekezo hilo limedhaminiwa na Kamati; au

(c) pendekezo hilo la mswada lisishughulikiwe.

(7) Kamati ya Kiidara ambayo imekabidhiwa pendekezo la mswada ili kulichanganua kabla ya kuchapishwa kwa mujibu wa aya ya (3)(a)(i) na (6)(a) itashughulikia pendekezo hilo la mswada na kutoa ripoti kwa Spika katika muda usiozidi siku thelathini ikitoa maoni iwapo pendekezo hilo lichapishwe au la.

(7A) Kwa mujibu wa pendekezo la Mswada wa kurekebisha Katiba—

- (a) pendekezo litaambatanishwa na saini za angalau Wabunge wasiopungua hamsini wanaoiunga mkono, isipokuwa kama imedhaminiwa na Chama cha walio Wengi au Chama cha walio Wachache;
- (b) pale ambapo Spika anaidhinisha uchanganuzi kabla ya kuchapishwa kwa pendekezo, Spika ataliarifu Bunge la Taifa kuhusu idhinisho hilo na anaweza—
    - (i) kumruhusu mdhamini atoe kauli ya madhumuni na sababu za pendekezo;
    - (ii) kuruhusu maoni yatolewe kuhusiana na kauli iliyotolewa na Mbunge;
    - (iii) kuwezesha kujumuishwa kwa maoni ya wabunge katika baraza faafu; na
    - (iv) kuwaalika Wabunge walio na mapendekezo yanayofanana au yanayohusiana kutoa mawasilisho yao mbele ya Kamati inayokabidhiwa pendekezo;
- (c) baraza au kamati inayokabidhiwa pendekezo la Mswada kwa mujibu wa aya ndogo ya (b)—
    - (i) itaalika na kushughulikia mawasilisho ya Mwanasheria Mkuu; tume na ofisi huru zilizoundwa kwa mujibu wa Sura ya kumi na tano ya Katiba na asasi yoyote ya kikatiba au kisheria iliyo na wajibu wa kurekebisha sheria; na

(ii) kwa kushauriana na mdhamini, itajitahidi kuandaa na kupendekeza nakala patanifu ya pendekezo kutokana na mawasilisho yaliyopokewa.

(8) Kufuatia maoni ya Kamati ya Kiidara inayohusika, Spika ataelekeza pendekezo hilo la mswada lichapishwe au lisichapishwe kuwa mswada.

**Spika kuruhusu baadhi ya mapendekezo ya miswada**

**114A.** (1) Spika anaweza kuruhusu pendekezo la mswada lisifuate masharti ya Kanuni ya 114 *(Uwasilishaji wa Miswada)* ikiwa—

(a) linatoka kwa—

(i) Chama kinachounda serikali ya taifa; au

(ii) Tume ya kikatiba au Ofisi Huru na linahusiana na wajibu wa Tume au Ofisi Huru;

(b) linakusudia kutekeleza uamuzi wa Bunge au pendekezo la Kamati ya Ardhilhali za Umma, kutekeleza, kurekebisha au kufuta sheria yoyote; au

(c) linafanana na Mswada uliopitishwa na Bunge la Taifa lakini ukatanguka mwishoni mwa muhula wa Bunge lililotangulia; au

(d) liliwasilishwa na Mbunge yuyo huyo na likasomwa kwa mara ya pili lakini likatanguka mwisho wa muhula wa Bunge lililotangulia.

(2) Ruhusa kwa mujibu wa aya ya (1) haitatolewa isipokuwa kama pendekezo la mswada limeambatishwa na—

(a) nakala ya idhini ya Baraza la Mawaziri, ikiwa pendekezo la mswada limetolewa na Chama kinachounda serikali ya taifa; au

(b) sera iliyo msingi wa pendekezo la mswada na ushahidi wa mashauriano ya wadau, ikiwa pendekezo limetolewa na Tume au Ofisi Huru.

(3) Chama kinachounda serikali ya taifa kitataja jina la Mbunge atakayewasilisha pendekezo la mswada ili lichapishwe.

(4) Baada ya ruhusa kutolewa, Spika ataamuru pendekezo hilo la mswada lichapishwe kuwa mswada.

**Kupiga chapa vifungu vinavyorekebisha sheria**

**115.** Mswada unapokusudia kurekebisha kifungu chochote cha Sheria iliyopo, sehemu inayohusika itapigwa chapa na kusambazwa kwa Wabunge kama sehemu ya mswada huo, isipokuwa kama kwa maoni ya Spika, rekebisho hilo ni dogo au linaeleweka kwa urahisi.

**Kauli tekelezi**

**116.** Kila Mswada utakuwa na kauli tekelezi kwamba *"Imepitishwa na Bunge la Kenya."*

**Maelezo ya Madhumuni na Sababu**

**117.** Kila Mswada utaambatisha maelezo yatakayoonyesha—

(a) kauli ya madhumuni na sababu za Mswada;

(b) kauli ya kukasimisha mamlaka ya kutunga sheria na udhibiti wa haki na uhuru wa kimsingi, ikiwa upo;

(c) ikiwa mswada unahusu serikali za kaunti; na

(d) kauli ya athari za kifedha na iwapo fedha za umma zitatumika ikiwa Mswada huo utapitishwa na ikiwezekana, kutaja makadirio ya matumizi hayo.

**Vifungu kuhusu ukasimishaji wa mamlaka**

**118.** Kila Mswada ambao unakasimisha mamlaka kwa chombo chochote cha serikali, ofisa wa serikali au mtu yeyote, mamlaka ya kutunga masharti yenye nguvu ya kisheria nchini Kenya kwa mujibu wa Ibara ya 94(6) ya Katiba utakuwa na

sehemu maalum katika mswada yenye kichwa "Vifungu kuhusu ukasimishaji wa mamlaka" ambayo itataja—

(a) madhumuni na malengo ya kukasimisha mamlaka hayo;

(b) mipaka ya mamlaka;

(c) aina na upeo wa sheria itakayotungwa; na

(d) misingi na viwango vitakavyotumika kwa sheria itakayotungwa na mamlaka inayohusika.

**Udhibiti wa haki na uhuru wa kimsingi**

**119.** Kila Mswada ulio na kifungu kinachodhibiti haki au uhuru wa kimsingi kwa mujibu wa Ibara ya 24(2) ya Katiba utakuwa na vifungu tofauti na mahususi—

(a) vinavyoelezea haki na uhuru wa msingi unaodhibitiwa; na

(b) vinavyoonyesha aina na upeo wa mipaka hiyo.

**Uchapishaji na Uwasilishaji wa Miswada**

**120.** (1) Mswada hautawasilishwa katika Bunge la Taifa isipokuwa kama—

(a) umetiwa saini na Mbunge au Kamati husika;

(b) una majina ya wadhamini wenza wowote, ikiwa umedhaminiwa kwa pamoja; na

(c) Mswada huo pamoja na maelezo yanayotajwa katika Kanuni ya 117 (*Maelezo ya Madhumuni na Sababu*) umechapishwa katika *Gazeti Rasmi la Serikali* (kama Mswada utakaoanzia katika Bunge la Taifa) na muda wa siku saba umepita tangu uchapishwe ikiwa ni Mswada wa Kugawa Mapato, Mswada wa Kutenga Mapato kwa Kaunti, Mswada wa Kuidhinisha Matumizi ya Fedha au Mswada wa Kuidhinisha Matumizi ya Ziada ya Fedha, Mswada wa Fedha, Mswada wa Kutenga Mapato ya Ziada kwa Kaunti,

na Mswada wa Hazina ya Usawazishaji, na muda wa siku kumi na nne umepita tangu uchapishwe ikiwa ni mswada mwingine wowote, au muda wowote mfupi utakaoamuliwa na Bunge la Taifa kuhusiana na Mswada husika.

(2) Mswada wa Kamati unaweza kutiwa saini na kuwasilishwa na Mwenyekiti wa Kamati au mjumbe aliyeteuliwa na Kamati kwa ajili hiyo.

(3) Baada ya Mswada kuchapishwa katika *Gazeti Rasmi la Serikali*, Katibu atahakikisha kuna nakala za kutosha za Mswada huo kwa kila Mbunge.

**Miswada inayohusu serikali za kaunti**

**121.** (1) Mswada unaohusu serikali za kaunti ni—

(a) mswada maalum ambao utashughulikiwa kwa mujibu wa Ibara ya 111 ya Katiba iwapo—

(i) unahusiana na uchaguzi wa wawakilishi katika bunge la kaunti au gavana na naibu wake; au

(ii) ni Mswada wa kila mwaka wa Kutenga Mapato kwa Kaunti unaotajwa katika Ibara ya 218 ya Katiba; au

(b) mswada wa kawaida ambao utashughulikiwa kwa mujibu wa Ibara ya 112 ya Katiba au kwa utaratibu mwingine wowote.

(2) Kwa mujibu wa Ibara ya 110(3) ya Katiba, kabla ya Bunge la Taifa au Seneti kushughulikia Mswada, Spika wa Bunge la Taifa na Spika wa Seneti wataamua kwa pamoja iwapo ni Mswada unaohusu kaunti, na ikiwa ni hivyo, kama ni Mswada maalum au Mswada wa kawaida.

(3) *(imefutwa)*.

**122.** *(imefutwa)*.

**123.** *(imefutwa)*.

**Mswada hautashughulikiwa kwa hatua zaidi ya moja katika kikao kimoja**

**124.** (1) Mswada hautashughulikiwa kwa hatua zaidi ya moja katika kikao kimoja isipokuwa kwa idhini ya Bunge la Taifa.

(2) Aya ya (1) haitatumika kwa au kuhusiana na—

(a) Mswada wa Kuidhinisha Matumizi ya Fedha, Mswada wa Hazina Kuu, Mswada wa Kutenga Mapato kwa Kaunti, Mswada wa Kugawa Mapato na Mswada wa Hazina ya Usawazishaji; au

(b) Mswada wa kurekebisha Katiba unaposomwa Mara ya Pili na ya Tatu.

**Kusomwa kwa Miswada**

**125.** Mswada utachukuliwa kuwa umesomwa pindi Katibu atakaposoma jina la Mswada katika Bunge la Taifa.

**Kusomwa Mara ya Kwanza**

**126.** Kila Mswada utasomwa Mara ya Kwanza bila kuhitaji Hoja kutolewa au Hoja kutolewa iamuliwe.

**Kamati kukabidhiwa Miswada na ushirikishwaji wa umma**

**127.** (1) Mswada ukishasomwa Mara ya Kwanza, utakabidhiwa Kamati husika ya kiidara bila Hoja kutolewa iamuliwe.

(1A) Isipokuwa Mswada wa Fedha, Spika anaweza kuelekeza vipengele vya Mswada vinavyopendekeza kurekebisha zaidi ya sheria moja katika masharti yake ya kimsingi kwa kamati husika za kiidara kwa kuzingatia wajibu wa kamati hizo.

(2) Bila kuzingatia aya ya (1), Bunge la Taifa linaweza kuamua kukabidhi Mswada kwa kamati iliyoundwa kwa ajili hiyo.

(3) Kamati ya Kiidara ambayo imekabidhiwa Mswada itashirikisha umma katika Mswada huo kwa utaratibu mwafaka, ikijumuisha—

(a) kualika uwasilishwaji wa maoni;

(b) kufanya vikao vya kusikiliza maoni ya umma;

(c) kuwashirikisha wadau wa sekta inayohusika; na

(d) kuwashirikisha wataalamu katika masuala ya kitaaluma.

(3A) Kamati ya Kiidara itazingatia mitazamo na maoni ya umma kwa mujibu wa aya ya (3) katika ripoti yake kwa Bunge la Taifa.

(4) Kwa kuzingatia Kanuni ya 129 *(Kusomwa Mara ya Pili kwa Mswada wa kurekebisha Katiba),* Mwenyekiti wa Kamati ya Kiidara ambayo imekabidhiwa Mswada au mjumbe wa Kamati aliyeteuliwa kwa ajili hiyo atawasilisha ripoti ya Kamati katika Bunge la Taifa kwa muda usiozidi siku thelathini za kalenda baada ya kukabidhiwa Mswada ili kuboresha mjadala, au iwapo ripoti ya Kamati haitawasilishwa ndani ya muda huo, itaamriwa kwamba Mswada usomwe Mara ya Pili katika siku ambayo Kamati ya Kuratibu Shughuli za Bunge la Taifa itateua kwa kushauriana na mdhamini wa Mswada au Kamati husika.

(4A) Spika anaweza kuongeza muda wa ushirikishwaji wa umma kwa mujibu wa aya ya (4) pale ambapo vipengele mbalimbali vya Mswada vinavyopendekeza kurekebisha zaidi ya sheria moja katika masharti yake ya kimsingi vimekabidhiwa kamati tofauti za kiidara kwa mujibu wa aya ya (1A).

(4B) Aya ya (4) haitatumika kwa au kuhusiana na—

(a) Mswada wa Kuidhinisha Matumizi ya Fedha, Mswada wa Kuidhinisha Matumizi ya Ziada ya Fedha, Mswada wa Fedha, Mswada wa Hazina Kuu, Mswada wa Kutenga Mapato kwa Kaunti, Mswada wa Kugawa

Mapato, Mswada wa Hazina ya Usawazishaji na Mswada wa kutenga Mapato ya Ziada kwa Kaunti; au

(b) Mswada wa kurekebisha Katiba unaposomwa kwa Mara ya Pili na ya Tatu.

(5) Iwapo kwa sababu yoyote ile ripoti ya Kamati haitakuwa imewasilishwa mwanzoni mwa Mswada Kusomwa Mara ya Pili, Kamati husika itaripoti katika Bunge la Taifa kuhusu hatua iliyofikia katika kushughulikia Mswada na kushindwa kuwasilisha ripoti hiyo kutazingatiwa na Kamati ya Mahusiano ya Kamati kwa ajili ya kuchukua hatua mwafaka.

(6) Licha ya aya ya (1)—

(a) Spika anaweza kuagiza kwamba Mswada mahususi ukabidhiwe kamati atakayoamua.

(b) Mswada wa Hazina Kuu, Mswada wa Kuidhinisha Matumizi ya Fedha au Mswada wa Kuidhinisha Matumizi ya Ziada ya Fedha utakabidhiwa Kamati ya Bajeti na Uidhinishaji wa Matumizi.

**Kusomwa Mara ya Pili**

**128.** (1) Shughuli ya Siku itakaposomwa kwamba Mswada usomwe Mara ya Pili, Hoja itatolewa, ***"Kwamba, Mswada ... sasa usomwe Mara ya Pili."***

(2) Hakuna rekebisho litatolewa kwa Hoja ***"Kwamba, Mswada ... sasa usomwe Mara ya Pili",*** isipokuwa kama ni rekebisho la kuondoa neno "sasa" na kuongeza maneno "baada ya….(taja muda)" mwishoni mwa Hoja.

**Kusomwa Mara ya Pili kwa Mswada wa kurekebisha Katiba**

**129.** Mswada wa kurekebisha Katiba hautawasilishwa ili usomwe Mara ya Pili katika Bunge la Taifa katika muda usiozidi siku tisini baada ya Mswada huo kusomwa Mara ya Kwanza katika Bunge la Taifa.

**Kukabidhi Miswada kwa Kamati ya Bunge Zima**

**130.** (1) Mswada utakuwa umekabidhiwa kwa Kamati ya Bunge Zima ukishasomwa Mara ya Pili.

(2) Pindi shughuli ya siku inaposomwa kwamba Bunge la Taifa liingie katika Kamati ya Bunge Zima kushughulikia Mswada, Spika ataondoka kwenye Kiti bila kulihoji Bunge la Taifa.

**Mipaka ya mamlaka ya Kamati**

**130A.** Kamati haitashughulikia suala lolote isipokuwa suala ambalo imekabidhiwa au ambalo linahitaji kushughulikiwa na Kamati kwa mujibu wa Kanuni hizi.

**Kamati ya Bunge Zima kutojiahirisha**

**130B.** Kamati haitaahirisha kikao chake au kuahirisha kushughulikia suala lolote hadi kikao kingine lakini, kupitia Hoja, Mwenyekiti anaweza kuagizwa atoe ripoti kuhusu hatua iliyofikiwa katika kushughulikia masuala ambayo Kamati ilikabidhiwa licha ya kwamba haijakamilisha kushughulikia masuala hayo na kuomba idhini ya kufanya kikao kingine.

**Ripoti**

**130C.** Pale ambapo Kamati ya Bunge Zima imekamilisha kushughulikia masuala yote iliyokabidhiwa, Mwenyekiti ataagizwa, kupitia Hoja, atoe ripoti katika Bunge la Taifa.

**Hoja ya Ripoti kutojadiliwa**

**130D.** (1) Hoja inapotolewa kwamba Kamati itoe ripoti au itoe ripoti ya hatua iliyofikiwa na kuomba idhini ya kufanya kikao kingine, Hoja itatolewa ili iamuliwe bila kukawia na bila marekebisho au mjadala na ikikubaliwa, Mwenyekiti ataondoka kwenye Kiti bila kukawia.

(2) Isipokuwa kama Kanuni hizi zimeeleza vinginevyo, kila ripoti itakayotolewa kwa mujibu wa aya ya (1) itatolewa bila

kulihoji Bunge la Taifa na inaweza, kupitia Hoja, kukubaliwa au kukataliwa, au kurejeshwa kwa Kamati, au kuahirishwa ili kushughulikiwa zaidi.

**Matumizi ya jumla ya masharti kwenye Kamati**

**130E.** Isipokuwa kama Kanuni hizi zimeeleza vinginevyo, masharti yale yale ya utaratibu na ya mjadala yanayotumika kuendesha shughuli kwenye vikao vya Bunge yatatumika kwenye Kamati.

**Mapendekezo ya marekebisho kukabidhiwa Kamati**

**131.** Baada ya Mswada kusomwa Mara ya Pili na marekebisho kupendekezwa, marekebisho ambayo kwa maoni ya Spika yanahitaji kuoanishwa kabla ya hatua ya Kamati ya Bunge Zima kuanza, Spika anaweza kumwelekeza Mbunge yeyote anayependekeza marekebisho kwa Mswada huo kuhudhuria kikao cha Kamati husika ya kiidara inayoshughulikia Mswada huo ili awasilishe mapendekezo ya marekebisho yake na Kamati itatoa ripoti kwa Bunge la Taifa kuhusu matokeo ya shughuli hiyo kabla ya hatua ya Kamati ya Bunge Zima.

**Mtiririko utakaozingatiwa Mswada ukiwa kwenye Kamati**

**132.** Katika kushughulikia Mswada kwenye Kamati, sehemu tofauti za Mswada zitashughulikiwa kwa mtiririko ufuatao—

(a) vifungu kama vilivyopigwa chapa, bila ya kujumuisha vifungu vinavyotaja anwani fupi ya Mswada, mwanzo wa kutumika, iwapo vipo, na ufafanuzi;

(b) vifungu vipya;

(c) nyongeza;

(d) nyongeza mpya;

(e) ufafanuzi;

(f) dibaji, ikiwa ipo;

(g) anwani ndefu;

(h) vifungu vinavyotaja anwani fupi ya Mswada na mwanzo wa kutumika.

**Utaratibu wa kushughulikia Mswada katika Kamati ya Bunge Zima**

**133.** (1) Katibu atasoma kila sehemu ya Mswada kufuata mtiririko ulioelezwa katika Kanuni ya 132 (*Mtiririko utakaozingatiwa Mswada ukiwa kwenye Kamati*) na ikiwa hakuna marekebisho yanayopendekezwa au iwapo mapendekezo yote ya marekebisho yatakuwa yameamuliwa, Mwenyekiti atapendekeza Hoja ***"Kwamba, … (kama ilivyorekebishwa) yajumuishwe kwenye Mswada"*** na, baada ya Wabunge wanaokusudia kuchangia kutoa michango yao, Mwenyekiti atatoa Hoja kwa Kamati ili iamuliwe.

(1A) Mjadala kuhusu pendekezo la rekebisho utajikita katika maudhui ya rekebisho.

(2) Hakuna rekebisho lolote litakalototolewa katika sehemu yoyote ya Mswada na Mbunge yeyote isipokuwa Mdhamini wa Mswada, ila tu kama arifa ya rekebisho itakuwa imewasilishwa kwa Katibu kimaandishi saa ishirini na nne kabla ya kuanza kwa kikao ambacho sehemu hiyo ya Mswada imepangwa kushughulikiwa na Kamati ya Bunge Zima.

(3) Licha ya aya ya (2), endapo rekebisho limetolewa katika sehemu yoyote ya Mswada kulingana na aya hii, Mbunge yeyote anaweza kutoa hoja ya rekebisho kwa rekebisho hilo baada ya kumkabidhi Mwenyekiti rekebisho lake kimaandishi.

(4) Mbunge anayetoa hoja ya rekebisho au rekebisho la ziada katika sehemu yoyote ya Mswada kwa mujibu wa aya ya (2) na (3) atafafanua maana, kusudi na athari za rekebisho au rekebisho la ziada linalopendekezwa.

(5) Hakuna rekebisho litakaloruhusiwa kutolewa ikiwa rekebisho hilo linahusu mada tofauti au linapendekeza kupanua maudhui ya Mswada bila sababu au isivyostahili, au halifai au haliko katika mtiririko unaolingana na maudhui ya Mswada.

(6) Rekebisho ambalo haliwiani na sehemu yoyote ya Mswada ambayo imekubaliwa au imeamuliwa na Kamati halitatolewa, na wakati wowote mjadala wa pendekezo la rekebisho unapoendelea, Mwenyekiti anaweza kuliondoa pendekezo hilo lisishughulikiwe na Kamati iwapo kwa maoni yake, mjadala umeonyesha kwamba rekebisho hilo linakiuka aya hii.

(7) Pale ambapo Mswada wa Hazina Kuu, Mswada wa Hazina ya Usawazishaji, Mswada wa Kugawa Mapato, Mswada wa Kutenga Mapato kwa Kaunti au Mswada wa Kuidhinisha Matumizi ya Fedha unashughulikiwa, rekebisho ambalo athari yake ni kutoza au kuongeza gharama ya matumizi ya fedha zaidi ya kiwango kilichoamuliwa na Bunge la Taifa au na Kamati ya Ugavi wa Fedha halitatolewa isipokuwa kama Bunge la Taifa litaamua kuruhusu Hoja hiyo.

(8) Mwenyekiti anaweza kukataa kupendekeza Hoja ya rekebisho ambalo kwa maoni yake halina maana au litasababisha kifungu au nyongeza ya Mswada unaokusudiwa kurekebishwa kutoeleweka au kuwa na makosa ya kisarufi.

(9) Aya ya (4) ya Kanuni ya 54 (*Marekebisho ya Hoja*), kadri itakavyowezekana, itatumika kurekebisha Mswada katika Kamati.

(10) Kushughulikia sehemu yoyote au kifungu cha Mswada katika Kamati kunaweza kuahirishwa hadi hatua nyingine katika kamati inayoshughulikia Mswada huo, kulingana na uamuzi wa Kamati.

(11) Hoja yoyote ya kuongeza kifungu kipya inapotolewa, kifungu hicho kitachukuliwa kama kilichosomwa Mara ya Kwanza na Hoja itapendekezwa ***"Kwamba, kifungu kipya kisomwe Mara ya Pili"*** na iwapo itakubaliwa, marekebisho yanaweza kupendekezwa kwa kifungu hicho kipya na Hoja ya mwisho itakayopendekezwa itakuwa ***"Kwamba, kifungu (jinsi kilivyorekebishwa) kiongezwe kwenye Mswada".***

(12) Nyongeza mpya zitashughulikiwa kwa utaratibu ule ule unaotumika kushughulikia vifungu vipya.

(13) Hoja itakayotolewa ili iamuliwe kuhusu dibaji (iwapo ipo) itakuwa ***"Kwamba, dibaji (jinsi ilivyorekebishwa) iwe dibaji ya Mswada."***

(14) Hoja itakayotolewa ili iamuliwe kwa anwani ndefu ya Mswada itakuwa ***"Kwamba, anwani ndefu (jinsi ilivyorekebishwa) iwe anwani ya Mswada".***

(15) Hakuna Hoja kuhusu kauli tekelezi itatolewa ili iamuliwe.

(16) Mwishoni mwa shughuli za Kamati kuhusu Mswada, au, ikiwa ni zaidi ya Mswada mmoja, kwa Miswada yote kama hiyo, Mdhamini wa Mswada atatoa Hoja ***"Kwamba, Mswada au Miswada (jinsi ilivyorekebishwa) iripotiwe katika Bunge la Taifa,"*** na Hoja hiyo itaamuliwa bila rekebisho au mjadala.

**Ripoti ya hatua iliyofikiwa**

**134.** Iwapo Mbunge yeyote atatoa Hoja kwamba Kamati iripoti hatua iliyofikiwa kabla ya shughuli kuhusu Mswada katika Kamati ya Bunge Zima kuhitimishwa na Hoja hiyo ipitishwe, Mwenyekiti ataondoka kwenye Kiti cha Kamati na Mwenyekiti huyo, au kama Mwenyekiti huyo amechukua Kiti cha Spika, Mdhamini wa Mswada, ataripoti hatua zilizofikiwa na Kamati katika Bunge la Taifa na kuomba idhini ya kufanyika kwa kikao kingine cha Kamati, na siku ya kurejelea shughuli itapangwa na Kamati ya Kuratibu Shughuli za Bunge la Taifa ikishauriana na Mdhamini wa Mswada.

**Mswada kuripotiwa**

**135.** Kamati ya Bunge Zima inapokubaliana kwamba Mswada au Miswada kadhaa iripotiwe, Mwenyekiti ataondoka kwenye Kiti cha Kamati mara moja na Bunge la Taifa litarejea na Mwenyekiti huyo, au kama Mwenyekiti huyo amechukua Kiti cha Spika, Mdhamini wa Mswada, ataripoti Mswada katika

Bunge la Taifa, na kila Mswada utaripotiwa mmoja baada ya mwingine endapo itakuwa zaidi ya mmoja.

**Utaratibu kwa Miswada inayoripotiwa kutoka kwa Kamati ya Bunge Zima**

**136.** (1) Mswada unaporipotiwa kutoka kwa Kamati ya Bunge Zima, Bunge la Taifa litashughulikia Mswada huo kama ulivyoripotiwa kupitia Hoja ***"Kwamba Bunge la Taifa likubaliane na Kamati kuhusu ripoti hiyo".***

(2) Hoja kwa mujibu wa aya ya (1) itatolewa ili iamuliwe mara moja bila kuruhusu rekebisho, ahirisho au mjadala, isipokuwa kama Mbunge yeyote atakusudia kufuta au kurekebisha kifungu chochote kwenye Mswada, au kuingiza kifungu kipya kwenye Mswada.

**Utaratibu wa Urejeshaji**

**136A.** (1) Mbunge anayekusudia kurekebisha au kufuta kifungu cha Mswada ulioripotiwa kutoka kwa Kamati ya Bunge Zima au kuingiza kifungu kipya kwenye Mswada, anaweza kupendekeza rekebisho mwishoni mwa Hoja ya kukubaliana na Kamati ya Bunge Zima kwa kuongeza maneno *"kwa sharti kwamba Mswada (kuhusiana na kifungu fulani, sehemu au kifungu kipya kinachopendekezwa au nyongeza mpya) urejeshwe tena kwenye Kamati ya Bunge Zima"*.

(2) Iwapo rekebisho la Hoja ya kukubaliana na Kamati ya Bunge Zima litakubalika, Mswada utachukuliwa kuwa umerejeshwa tena na Bunge la Taifa litarejea kwenye Kamati ya Bunge Zima mara moja au kufanya hivyo siku ambayo itatajwa na Kamati ya Kuratibu Shughuli za Bunge la Taifa kwa kushauriana na Mdhamini wa Mswada, kwa ajili ya kushughulikia suala ambalo limerejeshwa.

**Utaratibu kwa Miswada inayoripotiwa kutoka kwa Kamati**

**137.** (1) Ripoti ya Kamati kuhusu Mswada itawasilishwa kwenye Meza ya Bunge la Taifa na Mwenyekiti au Naibu Mwenyekiti

wa Kamati hiyo au na mjumbe mwingine aliyeteuliwa na Kamati kwa niaba ya Kamati.

(2) Bunge la Taifa litashughulikia Mswada kama ulivyoripotiwa kutoka kwa Kamati kupitia Hoja ***"Kwamba ripoti ya Kamati iliyoundwa kwa mujibu wa Kanuni ya 127(2) kushughulikia Mswada … iidhinishwe."***

(3) Kanuni ya 136 (*Utaratibu kwa Miswada inayoripotiwa kutoka kwa Kamati ya Bunge Zima*) itatumika kwa hoja yoyote ya kuidhinisha ripoti ya Kamati iliyoundwa kushughulikia Mswada.

**Utaratibu utakaotumika Mswada ukirejeshwa kwenye Kamati**

**138.** (1) Mswada utakaporejeshwa kwenye Kamati ya Bunge Zima, Kamati itashughulikia tu masuala yaliyorejeshwa na suala lolote ambalo linaathiriwa moja kwa moja na masuala yaliyorejeshwa.

(2) Isipokuwa kama ilivyoelezwa katika aya ya (1), utaratibu katika Kamati ya Bunge Zima kuhusu Mswada ambao Kamati ilikabidhiwa kwa mara ya kwanza, kadri itakavyowezekana, utatumika kwa Mswada uliorejeshwa kwenye Kamati ya Bunge Zima.

(3) Pale ambapo Mswada umeripotiwa na Kamati ya Bunge Zima baada ya kurejeshwa, Kanuni ya 136 (*Utaratibu kwa Miswada inayoripotiwa kutoka kwa Kamati ya Bunge Zima*) itatumika.

**Kusomwa Mara ya Tatu**

**139.** (1) Baada ya ripoti ya Mswada kukubaliwa, Spika anaweza kuidhinisha Mswada usomwe Mara ya Tatu papo hapo na kama hautasomwa papo hapo, itaamriwa Mswada usomwe Mara ya Tatu siku ambayo itatajwa na Kamati ya Kuratibu Shughuli za Bunge la Taifa kwa kushauriana na Mdhamini wa Mswada.

(2) Katika hatua ya Mswada kusomwa Mara ya Tatu, Hoja itatolewa ***"Kwamba, Mswada … sasa usomwe Mara ya Tatu"*** na marekebisho yanaweza kupendekezwa kama inavyofanyika wakati wa Mswada Kusomwa Mara ya Pili.

**Kuondolewa kwa Miswada**

**140.** (1) Kabla ya shughuli kuanza au wakati wa kusoma shughuli hiyo kwenye Ratiba ya Shughuli katika hatua yoyote kwa Mswada kusomwa, Mdhamini wa Mswada anaweza kuomba kuondoa Mswada bila kutoa arifa.

(2) Iwapo kwa maoni ya Spika ombi linalotolewa halihujumu shughuli za Bunge la Taifa, ataelekeza Mswada uondolewe.

(2A) Mswada kwa mujibu wa Kanuni ya 114A(1)(b) unaweza kuondolewa tu kwa idhini ya Spika.

(3) Mswada ambao umeondolewa unaweza kuchapishwa tena na kuwasilishwa kwa kuzingatia Kanuni ya 114 (*Uwasilishaji wa Miswada*).

(4) Iwapo Mdhamini wa Mswada anakusudia kuondoa Mswada kabla ya kuuwasilisha katika Bunge la Taifa, Mbunge huyo atamjulisha Spika kwa maandishi akibainisha sababu za kuondoa Mswada wake, na aya ya (3) itatumika kwa Mswada kama huo.

**Kutanguka na kuwasilishwa tena kwa Miswada**

**141.** (1) Mswada ambao kusomwa kwake Mara ya Pili au ya Tatu kumekataliwa unaweza kuwasilishwa tena katika Kipindi kinachofuata au baada ya miezi sita katika Kipindi hicho ilimradi uchapishwe upya kwa mujibu wa Kanuni ya 114 (*Uwasilishwaji wa Miswada*).

(2) Mswada ambao umechapishwa, ukasomwa Mara ya Kwanza au ambao hatua ya kusomwa kwake Mara ya Pili haijakamilika—

(a) Mswada huo hautatanguka mwishoni mwa Kipindi ambamo ulichapishwa bali utaendelezwa katika

Kipindi kinachofuata cha Bunge hilo kuanzia hatua ambayo ulikatizwa;

(b) Mswada huo utatanguka ifikapo mwisho wa Kipindi cha pili cha Vipindi viwili vinavyofuatana katika Bunge lilo hilo na unaweza kuchapishwa upya ukiwa na maudhui yale yale au tofauti kwa kuzingatia Kanuni ya 114 (*Uwasilishwaji wa Miswada*).

(3) Kwa kuzingatia aya ya (2), Mswada ambao hatua ya kusomwa kwake Mara ya Pili ilikamilika mwishoni mwa Kipindi utaendelezwa katika Kipindi kinachofuata cha Bunge lilo hilo kuanzia hatua iliyofikiwa wakati ulipokatizwa.

(3A) Aya ya (1), (2), na (3) za Kanuni hii hazitatumika kwa Mswada wa kurekebisha Katiba, Mswada wa Kugawa Mapato, Mswada wa Kutenga Mapato kwa Kaunti au Mswada unaoanzia Seneti.

(4) Mswada ambao kushughulikiwa kwake hakutakuwa kumekamilika mwishoni mwa muhula wa Bunge utatanguka.

**Maafikiano na Seneti**

**142.** Pale ambapo Mswada, isipokuwa Mswada ambao kwa mujibu wa Ibara ya 109(3) ya Katiba unastahili kushughulikiwa na Bunge la Taifa pekee, umepitishwa—

(a) Mdhamini wa Mswada huo, katika muda usiozidi siku saba, atamjulisha Spika kwa maandishi jina au majina ya Mbunge au Wabunge wowote wa Seneti ambao amewateua kuwa wadhamini wenza wa Mswada huo katika Seneti; na

(b) Katibu wa Bunge la Taifa atawasilisha kwa Katibu wa Seneti nakala ya Mswada iliyothibitishwa, kwa kutiwa saini na Katibu na kuidhinishwa na Spika, ikiambatana na Ujumbe—

(i) wa kuomba maafikiano ya Seneti; na

(ii) ukiiarifu Seneti jina la Mbunge au Wabunge wa Seneti walioteuliwa kuwa wadhamini wenza wa Mswada huo.

**Utaratibu wa kushughulikia Miswada inayoanzia Seneti**

**143.** (1) Kila mara Spika anapopokea Mswada unaoanzia Seneti—

(a) atalifahamisha Bunge la Taifa kupitia Ujumbe;

(b) atalifahamisha Bunge la Taifa jina la Mbunge au Wabunge walioteuliwa na Mdhamini wa Mswada kuwa wadhamini wenza wa Mswada huo katika Bunge la Taifa; na

(c) ataelekeza Mswada huo usomwe Mara ya Kwanza.

(2) Baada ya kusomwa Mara ya Kwanza, Mswada utakabidhiwa Kamati husika na Mswada huo utashughulikiwa kwa namna ileile kama Mswada unaoanzia katika Bunge la Taifa.

**Utaratibu wa kushughulikia Miswada ya Seneti baada ya Kusomwa Mara ya Tatu katika Bunge la Taifa**

**144.** Pale ambapo Mswada unaoanzia katika Seneti umesomwa Mara ya Tatu katika Bunge la Taifa, Katibu—

(a) atarejesha Mswada huo kwa Seneti ukiwa na Ujumbe ***"Kwamba Bunge la Taifa limeukubali Mswada wa……………………bila marekebisho";***

(b) atarejesha Mswada huo kwa Seneti ukiwa na Ujumbe ***"Kwamba Bunge la Taifa limeukataa Mswada wa………………… na Mswada huo umekabidhiwa Kamati ya Upatanisho"***; au

(c) ataelekeza rekebisho au marekebisho yoyote ambayo yamefanywa katika Mswada huo katika Bunge la Taifa kujumuishwa kwenye Mswada uliopokelewa kutoka Seneti na nakala ya Mswada iliyorekebishwa na orodha ya marekebisho, iliyotiwa saini na Katibu

na kuidhinishwa na Spika, itarejeshwa kwa Seneti ikiambatisha Ujumbe wa kutaka maafikiano na Seneti kuhusu rekebisho au marekebisho ya Bunge la Taifa.

**Marekebisho ya Seneti kwa Miswada iliyoanzia katika Bunge la Taifa**

**145.** Marekebisho ya Seneti kwa Mswada ulioanzia katika Bunge la Taifa yatasambazwa kwa Wabunge katika muda wa siku saba baada ya kupokea marekebisho hayo kutoka Seneti na yatashughulikiwa na Kamati ya Bunge Zima siku itakayopangwa na Kamati ya Kuratibu Shughuli za Bunge la Taifa.

**Kushughulikia marekebisho ya Seneti kwa Miswada iliyoanzia katika Bunge la Taifa**

**146.** Hoja ***"Kwamba marekebisho ya Seneti kwa Mswada wa …………. sasa yashughulikiwe"*** inapotolewa ijadiliwe, hakuna rekebisho litakalotolewa kwa Hoja hiyo isipokuwa kama ni rekebisho la kuondoa neno "sasa" na kuongeza maneno "baada ya…. (taja muda)" mwishoni mwa Hoja na, iwapo rekebisho hilo litapitishwa, Katibu atatuma Ujumbe kwa Seneti ***"Kwamba Bunge la Taifa limeahirisha kushughulikia marekebisho ya Seneti kwa Mswada wa ……… hadi ……….. (taja muda)."***

**Utaratibu wa kushughulikia marekebisho ya Seneti kwa Miswada iliyoanzia katika Bunge la Taifa**

**147.** Pale ambapo Bunge la Taifa litaamua kushughulikia marekebisho ya Seneti kwa Mswada ulioanzia katika Bunge la Taifa, kila rekebisho litasomwa na Katibu na linaweza kukubaliwa au kukataliwa kwa mujibu wa Ibara ya 112(2) ya Katiba.

**Kuhitimisha kushughulikia marekebisho ya Seneti kwa Miswada iliyoanzia katika Bunge la Taifa**

**148.** Bunge la Taifa linapomaliza kushughulikia marekebisho ya Seneti kwa Mswada ulioanzia katika Bunge la Taifa na—

(a) lipitishe Mswada kama ulivyorekebishwa, Spika atauwasilisha Mswada huo kwa Rais katika muda usiozidi siku saba ili upate kibali cha Rais; au

(b) likatae Mswada kama ulivyorekebishwa, Spika ataukabidhi kwa Kamati ya Upatanisho kwa mujibu wa Ibara ya 113 ya Katiba.

**Kamati ya Upatanisho**

**149.** (1) Mswada utakabidhiwa Kamati ya upatanisho kila mara Bunge la Taifa—

(a) linapokataa marekebisho yote au rekebisho lolote lililofanywa na Seneti kwa Mswada unaohusu serikali za kaunti ambao ulianzia Bunge la Taifa;

(b) linapokataa Hoja kwamba Mswada ulioanzia Seneti usomwe Mara ya Pili au ya Tatu; au

(c) linapokubaliana na ripoti ya Kamati ya Bunge Zima inayopendekeza kufuta vifungu vyote vya Mswada unaoanzia Seneti.

(2) Spika wa Bunge la Taifa na Spika wa Seneti watateua Kamati ya upatanisho itakayokuwa na idadi sawa ya Wabunge kutoka Bunge la Taifa na Seneti ili ijaribu kuandaa Mswada Kubalifu ambao utapitishwa na Bunge la Taifa na Seneti.

(3) Akidi ya Wabunge wa Bunge la Taifa itakayohitajika kuwepo katika kikao cha Kamati ya upatanisho ni thuluthi moja ya wajumbe hao na kikao cha kamati hiyo hakitakuwa halali kama kitakosa akidi sawa ya Maseneta.

(4) Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya upatanisho watateuliwa na wingi wa wajumbe wa Kamati hiyo watakaohudhuria kikao cha kwanza.

(5) Iwapo Mwenyekiti wa Kamati ya upatanisho ni wa Bunge la Taifa, Makamu Mwenyekiti atakuwa wa Seneti na kinyume chake.

(6) ikiwa Kamati ya upatanisho haitakubaliana kuhusu Mswada kubalifu katika siku zisizozidi thelathini, au ikiwa Mswada kubalifu uliopendekezwa na kamati itakataliwa na Bunge la Taifa na Seneti, Mswada utaanguka.

(7) Katibu atatuma Ujumbe kwa Seneti kuhusu uamuzi wa Bunge la Taifa kwa mujibu wa Kanuni hii.

**Kushughulikia Ripoti ya Kamati ya Upatanisho**

**150.** (1) Ripoti ya Kamati ya upatanisho kwa Mswada iliyoandaliwa kwa mujibu wa Ibara ya 113 ya Katiba itawasilishwa Mezani na Mjumbe aliyeteuliwa na Kamati kwa niaba ya Kamati.

(2) Pale ambapo Kamati ya Upatanisho itaripoti kuwa haijakubaliana kuhusu Mswada itakaouwasilisha au, iwapo Kamati hiyo haijakubaliana kuhusu Mswada Kubalifu itakaouwasilisha katika siku zisizozidi thelathini kuanzia tarehe ambayo Kamati ilikabidhiwa Mswada, Mswada huo utachukuliwa kuwa umeanguka kwa mujibu wa Ibara ya 113(4) ya Katiba.

(3) Pale ambapo ripoti ya Kamati ya upatanisho imejumuisha Mswada uliokubaliwa kwa mujibu wa Ibara ya 113(2) ya Katiba, Bunge la Taifa litashughulikia ripoti ya Kamati hiyo kupitia Hoja ***"Kwamba ripoti ya Kamati ya upatanisho iidhinishwe"*** na Bunge la Taifa litapiga kura kukubali au kukataa Hoja hiyo.

(4) Iwapo Hoja kwa mujibu wa aya ya (3)—

(a) itakataliwa, Katibu ataitumia Seneti Ujumbe akieleza uamuzi huo, na Mswada huo utachukuliwa umeanguka; au

(b) imekubaliwa, Katibu ataitumia Seneti Ujumbe akieleza uamuzi huo, na Katibu atakapopokea Ujumbe kama huo kutoka Seneti, Mswada utachukuliwa kuwa umepitishwa na Bunge la Taifa na Seneti kama ulivyokubaliwa na Kamati ya upatanisho

na Spika wa Bunge la Taifa atauwasilisha kwa Rais ili upate kibali katika muda usiozidi siku saba kwa mujibu wa Ibara ya 113(3) ya Katiba.

**Mswada Maalum unaohusu serikali ya kaunti**

**151.** (1) Bunge la Taifa linaweza kurekebisha au kubatilisha Mswada Maalum uliopitishwa na Seneti kupitia tu uamuzi unaoungwa mkono na angalau thuluthi mbili ya Wabunge.

(2) Iwapo uamuzi wa Bunge la Taifa wa kurekebisha au kubatilisha Mswada Maalum hautapitishwa, Spika, katika muda usiozidi siku saba, atauwasilisha Mswada huo kwa Rais kama ulivyopitishwa na Seneti ili upate kibali cha Rais.

(3) Mswada utakapowasilishwa kwa Rais, Spika wa Bunge la Taifa atamwarifu Spika wa Seneti kuhusu uwasilishwaji huo.

**Uhifadhi wa Miswada**

**152.** (1) Kila Mswada usiohitaji maafikiano ya Seneti na ambao umepitishwa na Bunge la Taifa, ikijumuisha Mswada ulioshughulikiwa na Kamati ya upatanisho, utathibitishwa na kuhifadhiwa na Katibu.

(2) Kila Mswada unaoanzia Bunge la Taifa ambao unahitaji maafikiano ya Seneti na ambao umepitishwa na Bunge la Taifa na Seneti utahifadhiwa na Katibu wa Bunge la Taifa na kuthibitishwa na Katibu wa Bunge la Taifa na Katibu wa Seneti.

(3) Wakati wowote kabla ya Mswada kuthibitishwa, Spika anaweza kurekebisha makosa au kasoro ndogo kwenye Mswada bila kubadilisha maudhui ya Mswada huo na kisha atauwasilisha kwa Rais ili upate kibali.

(4) Kanuni hii itatumika kwa Mswada Maalum unaoshughulikiwa kwa mujibu wa Ibara ya 111(3) ya Katiba na Mswada ulioidhinishwa kwa mujibu wa Ibara ya 113(3) ya Katiba.

**Kuwasilisha Miswada ipate kibali**

**153.** Spika atatia saini Mswada uliothibitishwa kwa mujibu wa Kanuni ya 148 (*Kuhitimisha kushughulikia marekebisho ya Seneti kwa Miswada iliyoanzia katika Bunge la Taifa*) na ya 150 (*Kushughulikia Ripoti ya Kamati ya Upatanisho*) na atauwasilisha kwa Rais ili upate kibali katika muda usiozidi siku saba baada ya kupitishwa na Bunge la Taifa.

**Miswada iliyorejeshwa na Rais**

**154.** (1) Spika atakapopokea sababu za Rais kutoidhinisha mswada kwa mujibu wa Ibara ya 115 ya Katiba—

(a) atawasilisha Ujumbe kwa Bunge la Taifa katika muda usiozidi siku tatu baada ya kupokea sababu za Rais kutoidhinisha mswada ikiwa mswada huo haukushughulikiwa na Seneti;

(b) atawasilisha Ujumbe kwa Bunge la Taifa na kisha kuwasilisha sababu za Rais kutoidhinisha Mswada kwa Seneti katika muda usiozidi siku saba baada ya kuupokea ikiwa mswada huo ulishughulikiwa na Seneti.

(2) Bunge la Taifa, kwa mujibu wa Ibara ya 115 ya Katiba, litashughulikia sababu za Rais kutoidhinisha Mswada ambao umewasilishwa kwa mujibu wa aya ya (1) (a), katika muda usiozidi siku ishirini na moja pindi Bunge la Taifa litakaporejea kwenye vikao.

(3) Katika kushughulikia Mswada mara ya pili, Bunge la Taifa linaweza kupendekeza marekebisho yanayozingatia sababu za Rais za kutoidhinisha Mswada, ama kwa kuzikubali kikamilifu au kutozikubali kikamilifu sababu za Rais kutoidhinisha Mswada.

(4) Spika ataamua ikiwa rekebisho lolote linalopendekezwa kwenye Mswada uliorejeshwa na Rais linakubaliana kikamilifu au halikubaliani kikamilifu na sababu za Rais kutoidhinisha Mswada kwa mujibu wa Ibara ya 115 ya Katiba.

(5) Bunge la Taifa litapiga kura kuhusu marekebisho yaliyopendekezwa na linaweza kupitisha mswada—

(a) kwa kura ya thuluthi mbili ya Wabunge wote pale ambapo marekebisho hayakubaliani kikamilifu na sababu za Rais kutoidhinisha Mswada;

(b) kwa kufuata utaratibu uliowekwa katika Ibara ya 122(1) ya Katiba pale ambapo marekebisho yanakubaliana kikamilifu na sababu za Rais kutoidhinisha Mswada.

(6) Kwa ajili ya kushughulikia sababu za Rais kutoidhinisha Mswada uliowasilishwa kwa mujibu wa aya ya (1) (b), Bunge la Taifa na Seneti litaunda Kamati ya Pamoja katika muda usiozidi siku mbili baada ya Seneti kupokea sababu za Rais kutoidhinisha Mswada.

(7) Kamati ya Pamoja itashughulikia sababu za Rais kutoidhinisha Mswada katika muda usiozidi siku kumi na nne na kuwasilisha Ripoti katika Bunge la Taifa na Seneti.

(8) Katika kushughulikia Mswada kwa mara ya pili kwa mujibu ya Ibara ya 115 ya Katiba, Bunge la Taifa linaweza, na Seneti inaweza, kupendekeza marekebisho kwenye Mswada kwa kukubali sababu za Rais kutoidhinisha Mswada ama—

(a) kwa kukubali kikamilifu sababu za Rais kutoidhinisha Mswada; au,

(b) kwa kutokubali kikamilifu sababu za Rais kutoidhinisha Mswada.

(9) Spika wa Bunge la Taifa na Spika wa Seneti wataamua kwa pamoja ikiwa rekebisho lololote lililopendekezwa kwenye Mswada uliowasilishwa kwa mujibu wa aya ya (1)(b), linakubaliana au halikubaliani kikamilifu na sababu za Rais kutoidhinisha Mswada kwa mujibu wa Ibara ya 115 ya Katiba.

(10) Ikiwa Spika wa Bunge la Taifa na Spika wa Seneti hawatakubaliana kwa mujibu wa aya ya (9), rekebisho

litachukuliwa kuwa lisilokubaliana kikamilifu na sababu za Rais kutoidhinisha Mswada.

(11) Ikiwa Kamati ya Pamoja haitawasilisha ripoti baada ya kukamilika kwa muda uliotajwa katika aya ya (7) au ikiwa ripoti ya Kamati ya Pamoja inabainisha kwamba Kamati haijakubaliana kuhusu marekebisho yoyote, Bunge la Taifa litashughulikia, na Seneti itashughulikia, Mswada kwa mara ya pili na aya ya (8) itatumika.

**155.** *(imefutwa)*.

## SEHEMU YA XX- MISWADA BINAFSI

### Utaratibu wa Mswada wa umma kutumika

**156.** Isipokuwa kama imeelekezwa vinginevyo katika sehemu hii, kanuni zinazohusu miswada ya umma zitatumika kwa Miswada Binafsi.

### Kifungu cha uhifadhi

**157.** Kila Mswada Binafsi utakuwa na kifungu cha kuhifadhi haki za Rais, za serikali ya taifa na serikali za kaunti, za asasi au mashirika mbalimbali, na nyinginezo, isipokuwa zile zilizotajwa kwenye Mswada na wale wanaodai kuhusika katika mswada.

### Mswada Binafsi unaoathiri haki binafsi

**158.** (1) Hakuna Mswada Binafsi ambao moja kwa moja unaathiri haki binafsi au mali ya mtu yeyote, utaanzia katika Bunge la Taifa isipokuwa kama Kanuni hii kuhusu uwasilishaji wa arifa imezingatiwa.

(2) Arifa itachapishwa katika matoleo yasiyopungua matatu ya *Gazeti Rasmi la Serikali*, ikitaja maudhui ya jumla na madhumuni ya Mswada na chapisho la mwisho litachapishwa katika muda usiopungua siku kumi na nne kabla ya kuwasilisha

Ardhilhali iliyotajwa katika Kanuni ya 159 (*Ardhilhali ya Idhini*).

**Ardhilhali ya Idhini**

**159.** (1) Hakuna Mswada Binafsi utakaowasilishwa isipokuwa kama Ardhilhali, ambayo itakuwa na anwani fupi ya Mswada na kutiwa saini na wahusika wote au baadhi yao ambao ni wadhamini wa Mswada, itakuwa imewasilishwa katika Bunge la Taifa mbeleni ikiambatisha nakala ya Mswada.

(2) Katibu atahakiki ardhilhali zilizowasilishwa katika Bunge la Taifa na endapo hataridhika kuwa masharti ya Sehemu hii yamezingatiwa, Katibu ataripoti hali hiyo kwa Spika.

(3) Wadhamini wa Mswada watawasilisha kwa Katibu nakala za kutosha za Ardhilhali zikiwa zimeambatisha Mswada kwa ajili ya kusambazwa kwa Wabunge na baada ya kupokea nakala hizo, Katibu atazigawa kwa kila Mbunge bila kukawia.

(4) Ardhihali itasomwa katika kikao cha kwanza cha Bunge la Taifa baada ya kuwasilishwa na Hoja ***"Kwamba, wadhamini wapewe idhini ya kuendelea"*** itatolewa bila kukawia na kuamuliwa bila marekebisho au mjadala.

**Dhamana ya gharama za uchapishaji**

**160.** (1) Pale ambapo idhini itatolewa kwamba Mswada Binafsi uwasilishwe, Katibu atatoa makadirio ya gharama ya kuchapisha Mswada na wadhamini wa Mswada watagharimia uchapishaji.

(2) Wadhamini watawasilisha kwa Katibu angalau asilimia ishirini na tano ya jumla ya makadirio ya gharama ya kupiga chapa Mswada kama dhamana ya gharama za uchapishaji.

**Miswada inayoidhinisha kazi za ujenzi**

**161.** (1) Pale ambapo ni Mswada Binafsi unaoidhinisha kazi za ujenzi, kabla ya Mswada huo kusomwa Mara ya Kwanza, wadhamini—

(a) watamkabidhi Katibu makadirio ya gharama za shughuli hiyo, iliyotiwa saini na mtu aliyefanya makadirio hayo na kuidhinishwa na Katibu; na

(b) watamkabidhi Katibu angalau asilimia nne ya fedha ya makadirio yaliyowasilishwa kwa mujibu wa aya ya (1)

(2) Kila Mswada wa aina hii utakuwa na kifungu kwamba iwapo kazi za ujenzi zilizoidhinishwa hazitakamilishwa katika muda uliotajwa kwenye Mswada dhamana ya kifedha iliyokabidhiwa Katibu itatwaliwa na Hazina Kuu.

**Kusomwa Mara ya Kwanza**

**162.** Pale ambapo masharti ya sehemu hii yatakuwa yamezingatiwa, Katibu ataelekeza Mswada huo upigwe chapa, usambaziwe Wabunge na uchapishwe kwenye *Gazeti Rasmi la Serikali* na katika kikao cha kwanza cha Bunge la Taifa kitakachofanyika angalau siku kumi na nne baada ya kuchapishwa, Mswada huo utasomwa Mara ya Kwanza.

**Haki ya kusikilizwa na Kamati kuhusu Mswada unaopingwa**

**163.** (1) Kwa kuzingatia Kanuni hizi ardhilhali zote za kupinga Mswada Binafsi wenye ombi kuwa wawasilishaji wa ardhilhali wasikilizwe wenyewe au kupitia kwa mawakili wao, zitakabidhiwa Kamati ambayo itawasikiliza wenye ardhilhali au mawakili wao.

(2) Wadhamini wa Mswada Binafsi unaopingwa watakuwa na haki ya kusikilizwa na Kamati inayoshughulikia Mswada au kupitia mawakili wao, kwa ajili ya kuutetea Mswada na kupinga ardhilhali zinazopinga Mswada.

**Namna Miswada inavyoweza kupingwa**

**164.** Hakuna mtu yeyote, isipokuwa Mbunge, atakayesikilizwa yeye mwenyewe au wakili wake, katika kupinga Mswada Binafsi isipokuwa kama mtu huyo alishawasilisha kwa Katibu ardhilhali ikionyesha asili ya pingamizi zake kwa Mswada huo na kama pingamizi hizo zinahusu Mswada mzima au sehemu ya Mswada na kuomba asikilizwe mwenyewe au kupitia kwa wakili kwa kadri itakavyokuwa.

**Gharama za kupiga chapa**

**165.** Mara baada ya Mswada Binafsi kupitishwa, kukataliwa au kutelekezwa, Katibu ataandaa hesabu ya gharama zilizotumika katika kupiga chapa na iwapo gharama hizo ni chini ya kiasi cha dhamana iliyotolewa, atarejesha salio, na kama imezidi, atamtaka mdhamini kulipa kiasi kilichozidi.

**166.** *(imefutwa)*.

**167.** *(imefutwa)*.

**168.** *(imefutwa)*.

**169.** *(imefutwa)*.

**170.** (*imefutwa)*.

## SEHEMU YA XXI— KURIDHIA MIKATABA

**Kuridhia Mikataba**

**170A.** (1) Mkataba uliowasilishwa katika Bunge la Taifa ili uridhiwe utawasilishwa katika Meza ya Bunge na kukabidhiwa kamati husika ili ushughulikiwe.

(2) Kamati husika itashirikisha umma kabla ya kutoa ripoti yake katika Bunge la Taifa.

(3) Pamoja na taarifa inayohitajika kutolewa katika Bunge la Taifa kwa mujibu wa sheria, Kamati inaweza kumhitaji Waziri husika kutoa taarifa zaidi, ikijumuisha—

(a) athari ya kijamii na kimazingira ya mkataba huo katika muda mfupi, muda wa wastani na muda mrefu; na,

(b) aina na ushahidi wa ushirikishwaji wowote wa umma uliofanywa kuhusu mkataba huo.

(4) Ripoti ya Kamati husika kwa Bunge la Taifa itajumuisha—

(a) taarifa ya maoni ya watu kuhusu kuridhiwa kwa mkataba huo inayotokana na ushirikishwaji wa umma uliofanywa na Kamati husika;

(b) matokeo ya Kamati husika kuhusu mkataba huo na taarifa nyingine yoyote ambayo Kamati husika itachukulia kuwa muhimu; na

(c) pendekezo kwamba Bunge la Taifa—

(i) liidhinishe uridhiaji wa mkataba huo, au

(ii) liidhinishe uridhiaji wa mkataba huo bila ridhaa kamili, au

(iii) likatae kuridhia mkataba huo.

(5) Katika kuidhinisha uridhiaji wa mkataba bila ridhaa kamili, Bunge la Taifa litabainisha vipengele na mapendekezo kwa kila kipengele ambacho hakikuridhiwa kikamilifu yanayoweza kujumuisha maelekezo ya muda ambao wajibu mahususi unapaswa kutimizwa kabla ya kutekeleza mkataba huo.

(6) Katika muda usiozidi siku saba kufuatia uamuzi wa Bunge la Taifa kuhusu mkataba, Katibu atamfahamisha waziri husika na Katibu atahifadhi taarifa hiyo katika sajili ya mikataba.

## SEHEMU YA XXII— KAMATI

### Kamati ya Kuratibu Shughuli za Bunge la Taifa

**171.** (1) Kutakuwa na kamati itakayoitwa Kamati ya Kuratibu Shughuli za Bunge la Taifa itakayokuwa na—

(a) Spika ambaye atakuwa Mwenyekiti;

(b) Kiongozi wa Chama cha walio Wengi au mwakilishi wake aliyeteuliwa kimaandishi;

(c) Kiongozi wa Chama cha walio Wachache au mwakilishi wake aliyeteuliwa kimaandishi;

(d) Mratibu wa Chama cha walio Wengi au mwakilishi wake aliyeteuliwa kimaandishi;

(e) Mratibu wa Chama cha walio Wachache au mwakilishi wake aliyeteuliwa kimaandishi; na

(f) Wabunge wengine tisa ambao watateuliwa na Vyama Bunge na kuidhinishwa na Bunge la Taifa mwanzoni mwa kila Kipindi, ikiakisi wingi wa idadi ya Wabunge wa kila Chama Bunge katika Bunge la Taifa na kuzingatia maslahi ya vyama visivyo Vyama Bunge na Wabunge Huru.

(2) Kamati ya Kuratibu Shughuli za Bunge la Taifa itaundwa katika siku zisizozidi saba baada ya Bunge jipya kukutana.

(3) Spika asipokuwepo, Naibu Spika atahudhuria na kuwa mwenyekiti wa mikutano yote ya Kamati ya Kuratibu Shughuli za Bunge la Taifa.

(4) Kamati ya Kuratibu Shughuli za Bunge la Taifa —

(a) itatayarisha, na kila inapohitajika, kubadilisha Kalenda ya Bunge kwa idhini ya Bunge la Taifa;

(b) itafuatilia na kusimamia utekelezaji wa shughuli na mipango ya Bunge la Taifa;

(c) itatekeleza Kanuni za Kudumu zinazohusiana na upangaji au uratibishaji wa shughuli za Bunge na utendakazi wa Kamati za Bunge la Taifa;

(d) itaamua mpangilio ambao ripoti za Kamati zitajadiliwa katika Bunge la Taifa;

(e) itaamua na kutoa maelekezo na miongozo ili kuipa shughuli kipaumbele au kuiahirisha shughuli yoyote ya Bunge la Taifa kwa maafikiano ya Kiongozi wa Chama cha walio Wengi au Kiongozi wa Chama cha walio Wachache, kadri itakavyokuwa; na

(f) itashughulikia masuala yatakayoibuka mara kwa mara kuhusu shughuli za Bunge la Taifa na itakuwa na mamlaka na itatekeleza majukumu iliyokabidhiwa kwa mujibu wa Kanuni hizi au na Bunge la Taifa mara kwa mara.

(5) Akidi ya Kamati ya Kuratibu Shughuli za Bunge la Taifa itakuwa ni Mwenyekiti na angalau thuluthi moja ya Wajumbe wa Kamati hiyo.

(6) Iwapo kwa sababu yoyote, Mjumbe wa Kamati ya Kuratibu Shughuli za Bunge la Taifa hawezi kuhudhuria mikutano, Kiongozi wa Chama katika Bunge la Taifa kilichomteua Mjumbe huyo anaweza kuteua Mbunge mwingine kuhudhuria mikutano kwa kipindi ambacho Mjumbe huyo hataweza kuhudhuria mikutano.

**Kamati ya Kuteua Wajumbe wa Kamati**

**172.** (1) Kutakuwa na kamati itakayoitwa Kamati ya Kuteua Wajumbe wa Kamati itakayokuwa na—

(a) Kiongozi wa Chama cha walio Wengi atakayekuwa Mwenyekiti;

(b) Kiongozi wa Chama cha walio Wachache; na

(c) Wabunge wasiopungua kumi na mmoja na wasiozidi ishirini na mmoja watakaoteuliwa na Vyama Bunge

na kuidhinishwa na Bunge la Taifa kwa kuzingatia maslahi ya vyama visivyo vyama bunge na Wabunge Huru.

(2) Kamati ya Kuteua Wajumbe wa Kamati itateua Wabunge kuhudumu kwa Kamati zote isipokuwa Kamati ya Kuratibu Shughuli za Bunge la Taifa na Kamati ya Uteuzi.

(3) Kamati ya Kuteua Wajumbe wa Kamati itaundwa katika siku zisizozidi kumi baada ya Bunge jipya kukutana.

## Masharti ya kijumla

### Uteuzi wa Wajumbe wa Kamati

**173.** (1) Isipokuwa kama imeelezwa vinginevyo na sheria au Kanuni hizi, Kamati ya Kuteua Wajumbe wa Kamati, kwa kushauriana na Vyama Bunge, itateua Wajumbe watakaohudumu katika Kamati.

(2) Kamati ya Kuteua Wajumbe wa Kamati itazingatia haja ya kuwa na usawa wa kijinsia na kadri iwezekanavyo itahakikisha kwamba idadi isiyozidi thuluthi mbili ya Wajumbe wa Kamati, ikiwemo kamati iliyoundwa kwa uamuzi wa Bunge la Taifa, itakuwa ya jinsia moja.

(3) Nafasi itakayotokea baada ya kujiuzulu au kuondolewa kwa Mjumbe kwenye kamati itajazwa katika muda usiozidi siku kumi na nne tangu nafasi hiyo kuwa wazi.

(4) Mjumbe ambaye aliwahi kutuhumiwa kwenye mapendekezo katika ripoti ya kamati iliyopitishwa na Bunge la Taifa au Seneti hastahili kuteuliwa Mjumbe wa kamati hiyo.

### Uanachama wa Kamati

**173A.** (1) Kila Mbunge ana haki ya kuhudumu angalau katika kamati moja ya Bunge la Taifa.

(2) Mbunge anaweza kukataa kuhudumu katika kamati ya Bunge la Taifa kwa kumwarifu Spika kwa maandishi.

**Vigezo vya uteuzi**

**174.** (1) Katika kuteua Wabunge watakaohudumu kwenye Kamati, Kamati ya Kuteua Wajumbe wa Kamati itahakikisha kwamba—

(a) idadi ya wajumbe katika kila kamati inaakisi wingi wa Wabunge wa kila Chama Bunge katika Bunge la Taifa;

(b) wajumbe wawili wa Kamati ya Kuratibu Shughuli za Bunge la Taifa hawatahudumu katika Kamati moja ya Kiidara;

(c) kadri iwezekanavyo, angalau Mbunge Huru mmoja ameteuliwa kuhudumu katika Kamati ya Hesabu za Hazina Maalum;

(d) wingi wa Wajumbe wa Kamati ya Hesabu za Umma, Kamati ya Uwekezaji wa Umma, Kamati ya Utekelezaji na Kamati ya Hesabu za Hazina Maalum wanateuliwa kutoka kwenye vyama ambavyo sio Vyama Bunge vinavyounda serikali ya taifa; na

(e) kila Mbunge anateuliwa kuhudumu katika angalau kamati moja ya Bunge la Taifa.

(2) Licha ya aya ya (1), Mbunge wa chama kisicho Chama Bunge au Mbunge Huru atateuliwa kuhudumu katika kamati moja na, kadri iwezekanavyo, idadi ya Wabunge katika kila Kamati ina uwiano na idadi ya Wabunge ambao ni wanachama wa vyama hivyo na Wabunge Huru.

(2A) Kadri iwezekanavyo, Spika atahakikisha kwamba Wabunge wa vyama visivyo Vyama Bunge na Wabunge Huru wameteuliwa kuhudumu katika Kamati.

(2B) Spika anaweza kukataa kuidhinisha uwasilishwaji wa orodha ya wajumbe wa kamati unaokiuka Kanuni hii kwa Kamati ya Kuratibu Shughuli za Bunge la Taifa.

(3) Isipokuwa kama Bunge la Taifa litaamua vinginevyo kufuatia pendekezo na sababu zitakazotolewa na Kamati ya kuteua—

(a) hakuna mbunge atakayeteuliwa kuhudumu katika Kamati za kiidara zaidi ya mbili;

(b) Mbunge ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ama Mjumbe wa Tume ya Huduma za Bunge aliyeteuliwa kwa mujibu wa Ibara ya 127(2) (c) ya Katiba atahudumu katika kamati zaidi ya moja.

**Kuidhinisha uteuzi**

**175.** (1) Kamati ya Kuteua Wajumbe wa Kamati itawasilisha katika Bunge la Taifa orodha ya Wabunge watakaohudumu katika Kamati za Bunge katika muda usiozidi siku saba baada ya kuwateua ili uteuzi huo uidhinishwe.

(2) Kila mara Hoja ya kuidhinisha orodha kwa mujibu wa aya ya (1) inapotolewa katika Bunge la Taifa, hakutaruhusiwa pingamizi dhidi ya Mbunge yeyote anayependekezwa kuwa Mjumbe wa Kamati na iwapo pingamizi itakuwapo, pingamizi hiyo itachukuliwa kuwa dhidi ya Wabunge wote wanaopendekezwa.

(3) Mbunge hatakuwa mjumbe wa Kamati ya Bunge la Taifa isipokuwa kama uteuzi wake umeidhinishwa na Bunge la Taifa.

**Kuondolewa kwa Mjumbe kwenye Kamati**

**176.** (1) Chama kinaweza kumwondoa mjumbe kwenye Kamati baada ya kumpa mjumbe huyo fursa ya kusikizwa.

(2) Mratibu wa chama kilichomteua mjumbe kwa Kamati atamwandikia Spika arifa kuhusu nia ya kumwondoa mjumbe yeyote kwenye Kamati.

(3) Spika, katika muda usiozidi siku tatu baada ya kupokea arifa kwa mujibu wa aya ya (2), atamwarifu mjumbe anayehusika kuhusu arifa hiyo.

(4) Spika atamwondoa Mjumbe yeyote anayekiuka Kanuni ya 107A (*Utovu Mkubwa wa Nidhamu*) au anayevunja staha inayompasa Mbunge kutoka kwa Kamati ya Bunge la Taifa inayosimamia mamlaka na haki za Bunge la Taifa na mwenendo wa Wabunge.

**Idadi ya wajumbe wa kamati**

**177.** Kwa kuzingatia sheria yoyote, Kanuni hizi au uamuzi wa Bunge, Kamati itakuwa na idadi witiri ya wajumbe ambayo haitapungua kumi na moja na haitazidi kumi na tano.

**Uteuzi wa Kamati inayosimamia haki na mwenendo wa Wabunge**

**177A.** Katika kuteua wajumbe wa kamati ya Bunge la Taifa inayosimamia mamlaka na haki za Bunge la Taifa na mwenendo wa Wabunge, Kamati ya Kuteua Wajumbe wa Kamati itazingatia—

(a) wadhifa wa awali wa Mbunge katika Bunge la Taifa kama—

(i) Spika;

(ii) Kiongozi wa Chama cha walio Wengi;

(iii) Kiongozi wa Chama cha walio Wachache;

(iv) Naibu Spika; au

(v) mjumbe wa Jopo la Mwenyekiti;

(b) Mbunge aliyehudumu kwa muda mrefu zaidi katika—

(i) Bunge la Taifa;

(ii) Bunge la Taifa, Seneti na Bunge la Afrika Mashariki;

(iii) Seneti; na

(iv) Bunge la Afrika Mashariki;

(c) elimu na weledi katika sheria, uandamizi katika utawala wa umma, upatanisho, usuluhishi, au atakavyobainisha Spika;

(d) tajriba mahususi katika desturi na taratibu za Bunge; na

(e) Ukiukaji wowote wa Kanuni ya 107A (*Utovu Mkubwa wa Nidhamu*) au ukiukaji wa kanuni za maadili yanayomhusu Mbunge katika muhula wa Bunge.

**Uongozi na akidi ya Kamati**

**178.** (1) Kwa kuzingatia aya ya (2) ya Kanuni ya 173 (*Uteuzi wa Wajumbe wa Kamati*), na isipokuwa kama imeelezwa vinginevyo kwenye sheria, Kanuni hizi au uamuzi wa Bunge la Taifa, baada ya kamati kuundwa, itamchagua Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti kutoka miongoni mwa wajumbe wake.

(1A) Mjumbe wa Tume ya Huduma za Bunge aliyeteuliwa kwa mujibu wa Ibara ya 127(2)(c) ya Katiba hastahili kugombea uchaguzi wa Mwenyekiti au Makamu Mwenyekiti wa Kamati.

(2) Wajumbe wa Kamati ya Hesabu za Umma, Kamati ya Uwekezaji wa Umma na Kamati ya Utekelezaji watamchagua Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti miongoni mwa wajumbe wa Kamati wanateuliwa kutoka chama kisicho Chama Bunge ambacho kinaunda serikali ya taifa.

(3) Wajumbe wa Kamati ya Hesabu za Hazina Maalum watamchagua Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti miongoni mwa—

(a) Wabunge huru walioteuliwa kwenye kamati; au

(b) wajumbe wa kamati walioteuliwa kutoka kwenye Chama Bunge kisichounda serikali ya taifa iwapo hakuna wabunge huru.

(4) Isipokuwa kama imeelezwa vinginevyo kwenye sheria, Kanuni hizi au uamuzi wa Bunge la Taifa, akidi ya Kamati itakuwa wajumbe watano.

**Utaratibu wa uchaguzi**

**179.** (1) Katibu atapanga mahali, tarehe na saa ya mkutano wa kwanza wa kamati, katika muda usiozidi siku saba baada ya Bunge la Taifa kuunda kamati hiyo au muda zaidi utakaoidhinishwa na Spika, na mara tu wingi wa wajumbe utakapokuwepo, Katibu ataendesha uchaguzi wa kura ya siri kumchagua Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa kamati.

(2) Nafasi ya Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Kamati inapokuwa wazi, katika muda usiozidi siku saba baada ya nafasi hiyo kutokea, Katibu atapanga mahali na saa ya mkutano wa Kamati ili kumchagua Mwenyekiti au Makamu Mwenyekiti.

(3) Mgombeaji wa nafasi ya Mwenyekiti au Makamu Mwenyekiti wa Kamati atawasilisha kwa Katibu hati ya uteuzi kimaandishi isiwe baada ya saa 11.00 jioni ya siku inayotangulia siku ya uchaguzi.

(4) Hati ya uteuzi ya mgombeaji itakuwa na muundo unaotajwa kwenye Nyongeza ya Tano na itaambatisha jina na saini ya mjumbe anayempendekeza, jina na saini ya mwafiki wake pamoja na tamko la mgombeaji kuridhia kuhudumu nafasi ya Mwenyekiti au Makamu Mwenyekiti.

(5) Mbunge hatapendekeza au kuafiki zaidi ya mgombeaji mmoja kuchaguliwa kama Mwenyekiti au Makamu Mwenyekiti.

(6) Katibu atasambaza orodha kamili ya wagombeaji kwa wajumbe wa kamati bila kukawia baada ya kukamilika kwa shughuli ya uteuzi.

(7) Katibu ataongoza uchaguzi wa Mwenyekiti au Makamu Mwenyekiti na atampa kila mjumbe wa kamati karatasi ya kura.

(8) Mjumbe wa kamati anayetaka kupiga kura ataandika jina la kwanza na la mwisho la mgombeaji anayemchagua kwenye karatasi ya kura na kuitumbukiza kwenye sanduku la kura.

(9) Katibu atahesabu kura na kutangaza matokeo baada ya shughuli ya kupiga kura kukamilika.

(10) Iwapo hamna mgombeaji aliyepata wingi wa kura unaohitajika, Katibu ataongoza awamu nyingine ya upigaji kura bila kumjumuisha mgombeaji aliyepata kura chache zaidi, hadi mshindi atakapopatikana.

(11) Karatasi ya kura itakuwa imeharibika iwapo, kwa maoni ya Katibu karatasi hiyo haibainishi mgombeaji aliyepigiwa kura.

(12) Licha ya masharti ya Sehemu hii, iwapo mgombeaji mmoja ameteuliwa kugombea nafasi ya Mwenyekiti au Makamu Mwenyekiti, mara tu shughuli ya uteuzi inapokamilika, Katibu atamtangaza mgombeaji huyo kuwa amechaguliwa bila ya kura kupigwa.

(13) Katibu atafanya maandalizi yanayohitajika kwa ajili ya uchaguzi wa Mwenyekiti au Makamu Mwenyekiti wa Kamati.

(14) Mwenyekiti wa Kamati ya Kuratibu Shughuli za Kamati, kupitia Taarifa, ataliarifu Bunge la Taifa kuhusu Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Kamati aliyeteuliwa ipasavyo wakati Bunge la Taifa linapofanya kikao kinachofuata uchaguzi huo.

**Majukumu ya Mwenyekiti wa Kamati**

**180.** Kwa kuzingatia masharti ya Kanuni hizi na maelekezo ya Kamati, Mwenyekiti wa Kamati —

(a) ataongoza mikutano ya Kamati;

(b) atatekeleza majukumu na mamlaka ambayo ofisi ya Mwenyekiti imekabidhiwa na Kamati, maamuzi ya Bunge la Taifa au sheria;

(c) atakuwa msemaji wa Kamati.

**Arifa za mikutano**

**181.** (1) Arifa ya mkutano wa Kamati itatolewa na Katibu kwa Wajumbe wote ikionyesha tarehe, saa, mahali na ajenda ya mkutano huo.

(2) Arifa kwa mujibu wa aya ya (1) itachukuliwa kuwa imetolewa pindi inaposambazwa kielektroniki kwa Mbunge kupitia anwani rasmi ya mawasiliano ya Mbunge au nambari yake ya simu, wavuti wa Bunge, kwa kufikishwa kwa ofisi ya Mbunge au kubandikwa kwenye maeneo ya Bunge.

**Vikao vya Kamati**

**182.** Kikao cha Kamati kitafanyika mahali, tarehe na saa itakayoamuliwa na Mwenyekiti au kufuatia ombi lililotolewa na angalau wajumbe saba wa Kamati hiyo lakini hakuna mkutano wa Kamati utakaofanyika nje ya maeneo ya Bunge bila kibali cha Spika.

**Kamati ndogo**

**183.** (1) Kamati inaweza kuunda kamati ndogo kadri itakavyoona ni muhimu kwa utekelezaji bora wa shughuli zake na kuagiza akidi isipungue wajumbe watatu.

(2) Iwapo akidi haitatimia katika muda wa dakika thelathini baada ya saa iliyopangwa, mkutano wa Kamati ndogo utaahirishwa hadi saa au siku nyingine itakayoamuliwa na

Mwenyekiti wa Kamati.

(3) Kazi ya Kamati ndogo itaendeshwa kwa mujibu wa maelekezo ya Kamati na hiyo Kamati ndogo itatoa ripoti mara kwa mara kwa Kamati kuhusu majukumu iliyopewa.

**Mbunge aliyetuhumiwa hatahudhuria mikutano**

**184.** Mbunge ambaye ametuhumiwa kwenye suala linaloshughulikiwa na Kamati hatahudhuria mkutano wowote wa Kamati unaoshughulikia suala hilo lakini anaweza kuhudhuria mwenyewe au kuwakilishwa na wakili kwa ajili ya kutoa ushahidi mbele ya Kamati.

**Ahirisho kutokana na akidi kutotimia**

**185.** Iwapo akidi haitatimia katika muda wa dakika thelathini baada ya saa iliyopangwa kwa ajili ya mkutano wa Kamati, mkutano huo utaahirishwa hadi saa au siku nyingine itakayoamuliwa na Mwenyekiti wa kamati.

**Idadi ya mikutano**

**186.** (1) Isipokuwa kama Bunge la Taifa limeamua vinginevyo, kila Kamati itakutana angalau mara moja katika miezi miwili.

(2) Isipokuwa Kamati ya Kuratibu Shughuli za Bunge la Taifa, Kamati yoyote haitakutana wakati wa kikao cha Bunge la Taifa bila ya ruhusa ya kimaandishi kutoka kwa Spika.

(3) Licha ya aya ya (2), mkutano wa kamati utasitishwa Kengele ya Mgawanyiko au Kengele ya Akidi zinapokirizwa.

(4) Shughuli za mkutano wa Kamati zitakazotekelezwa kinyume na aya ya (2) zitakuwa batili.

**Kutohudhuria mikutano**

**187.** (1) Mjumbe yeyote asipohudhuria mikutano minne ya Kamati mfululizo bila ruhusa kwa maandishi ya Mwenyekiti wa Kamati, au ruhusa ya Spika ikiwa mjumbe huyo ni

Mwenyekiti wa Kamati, Mwenyekiti huyo au Spika, kama hali itakavyokuwa, ataiarifu Kamati kuhusu kutohudhuria huko.

(1A) Arifa kwa mujibu wa aya ya (1) itatolewa kupitia kwa Katibu na kuandikwa katika kumbukumbu za kamati.

(2) Baada ya kuzingatia arifa kwa mujibu wa aya ya (1A), Kamati inaweza kuamua kumsimamisha kwa muda Mjumbe au Mwenyekiti huyo kama hali itakavyokuwa na hatua hiyo itaripotiwa kwa Kamati ya Kuteua Wajumbe wa Kamati.

(3) Baada ya kupokea ripoti kwa mujibu wa aya ya (2), Kamati ya Kuteua Wajumbe wa Kamati itashughulikia suala hilo na kupendekeza Mbunge mwingine ili aidhinishwe na Bunge la Taifa kuchukua nafasi hiyo.

**Kutokuwepo kwa Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti**

**188.** Iwapo Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti hawapo katika mkutano wowote wa Kamati, Wajumbe waliopo watamchagua mmoja wao kuongoza mkutano.

**Orodha ya mahudhurio**

**189.** Majina ya Wajumbe waliohudhuria, wenye udhuru au wasiohudhuria mkutano wa Kamati yataorodheshwa katika kumbukumbu za mkutano huo.

**Kumbukumbu za kamati**

**190.** Kumbukumbu za mikutano ya kamati pamoja na ripoti ya kamati zitawasilishwa kwenye Meza ya Bunge la Taifa na zinaweza kuchapishwa kwa mujibu wa masharti ya Kanuni ya 247 (*Hifadhi ya Majarida na Rekodi za Bunge la Taifa*).

**Mamlaka na haki za kamati**

**191.** (1) Kamati zitakuwa na mamlaka na haki zote ambazo Bunge limepewa na Katiba na sheria, ikijumuisha mamlaka ya —

(a) kumwagiza mtu yeyote kufika mbele ya kamati kwa ajili ya kutoa ushahidi au taarifa;

(b) kuhakikisha mashahidi wanafika mbele ya kamati na kuwahoji kwa kiapo, kukiri kusema ukweli au vinginevyo;

(c) kutoa amri ya kuwasilisha nyaraka;

(d) kuomba na kupokea nyaraka kutoka kwa Serikali na umma; na

(e) kutoa agizo au ombi la kuwahoji mashahidi walioko nje ya nchi.

(2) Kiapo au kukiri kusema ukweli mbele ya Kamati kutafanywa na shahidi aliyefika mbele ya Kamati kwa namna inayoelezwa katika Nyongeza ya Sita.

(3) Hati ya wito itakayotolewa kwa mujibu wa aya ya (1)—

(a) itatolewa na Katibu kwa maelekezo ya Spika au Mwenyekiti wa Kamati kwa kuzingatia uamuzi wa Kamati; na

(b) itakuwa katika muundo unaoelezwa katika Nyongeza ya Saba.

(4) Hati ya wito itawasilishwa na mfanyikazi wa Bunge au ofisa wa polisi aliyeidhinishwa na Katibu kuwasilisha nakala ya Hati ya Wito —

(a) kwa mtu anayetajwa kwenye Hati ya Wito; au

(b) makazi ya kawaida au mahali panapofahamika kuwa makazi ya mwisho ya mtu huyo au eneo lake la kazi au biashara au kumpatia mtu yeyote mwenye umri wa zaidi ya miaka kumi na nane ambaye anaishi au ameajiriwa mahali hapo.

(5) Pale ambapo Hati ya wito imetolewa kwa shirika, hati hiyo inaweza kuwasilishwa —

(a) kwa katibu wa shirika, mkurugenzi au ofisa yeyote aliyeidhinishwa na shirika hilo; au

(b) ikiwa afisa anayewasilisha Hati ya wito ameshindwa kuwapata maofisa wa shirika waliotajwa kwenye aya ya (5)(a)—

(i) ataiacha kwenye ofisi rasmi ya shirika hilo;

(ii) ataituma kama barua iliyosajiliwa au kutuma kwa anwani ya posta ya shirika hilo kupitia kwa tarishi aliyeidhinishwa na mahakama;

(iii) ataiacha mahali ambapo shirika hilo huendesha shughuli zake iwapo hakuna ofisi rasmi wala anwani ya posta iliyosajiliwa; au

(iv) ataituma kama barua iliyosajiliwa, kwa anwani ya mwisho inayofahamika ya shirika hilo.

(6) Hati ya wito inapotolewa kwa namna iliyoelezwa kwenye Kanuni hii, ofisa anayewasilisha hati hiyo ataapa na kuambatisha au kusababisha kuambatishwa kwa hati ya kiapo ya Kupokeza kwenye hati ya wito asilia ikieleza saa na namna hati ya wito ilivyowasilishwa pamoja na jina na anwani ya mtu aliyepokea (iwapo ipo) na aliyeshuhudia kupokewa kwa hati hiyo.

(7) Hati ya kiapo ya Kupokeza itakuwa katika muundo ulioelezwa kwenye Nyongeza ya Nane na inaweza kufanyiwa mabadiliko kadri itakavyohitajika.

(8) Ripoti ya mtu aliyewasilisha hati ya wito kwa mujibu wa Kanuni hii itakuwa ni ushahidi bayana kuwa hati hiyo imewasilishwa.

(9) Mtu yeyote aliyealikwa au kuitwa kufika mbele ya Kamati kwa mujibu wa Kanuni hii atarejeshewa pesa alizotumia kama gharama zake itakavyoidhinishwa na Katibu.

### Utaratibu shahidi asipohudhuria

**191A.** (1) Pale ambapo shahidi atakosa kufika au atafika mbele ya Kamati lakini akatoa ushahidi ambao hauridhishi Bunge la Taifa au Kamati, Bunge la Taifa au Kamati inaweza kumtoza shahidi huyo faini isiyozidi shilingi laki tano ikizingatia hali ya maisha ya shahidi huyo na mambo yoyote yanayohusiana na hali hiyo.

(2) Faini itakayotozwa kwa mujibu wa aya ya (1) italipwa kwa Katibu wa Bunge la Taifa.

(3) Bunge la Taifa au Kamati inaweza kutoa amri ya kukamatwa kwa shahidi atakayekaidi hati ya wito ili kumlazimisha kuhudhuria.

### Mjumbe asipohudhuria kwa muda

**192.** (1) Isipokuwa kama Kanuni hizi zimeeleza vinginevyo, iwapo Mjumbe yeyote wa Kamati hayupo au hawezi kuhudhuria mikutano ya Kamati, mratibu wa chama chake anaweza, kwa ruhusa ya Spika, kumchagua Mbunge mwingine kukaimu nafasi yake katika kipindi ambacho hayupo au ameshindwa kuhudhuria mikutano.

(2) Mjumbe atachukuliwa kuwa hayupo au ameshindwa kuhudhuria mikutano kwa mujibu wa aya ya (1) ikiwa Mjumbe huyo yuko nje ya nchi kwa shughuli rasmi za Bunge au kwa sababu ya kuugua.

### Kura ya kutokuwa na imani na Mwenyekiti au Makamu Mwenyekiti

**193.** (1) Kamati inaweza, kwa uamuzi unaoungwa mkono na wingi wa wajumbe wa Kamati hiyo, kuamua kwamba haina imani na Mwenyekiti au Makamu Mwenyekiti, na Mjumbe atakayeteuliwa na Kamati kwa ajili hiyo atapeleka ripoti hiyo kwa Kamati ya Kuratibu Shughuli za Kamati ambayo, bila kukawia, itamwelekeza Katibu kufanya uchaguzi wa Mwenyekiti au Makamu Mwenyekiti kwa mujibu wa Kanuni ya 179 (*Utaratibu wa Uchaguzi*), kutegemea hali itakavyokuwa.

(2) Wajumbe wanaokusudia kufanya uamuzi kwa mujibu wa aya ya (1) watampa Mwenyekiti au Makamu Mwenyekiti arifa kwa maandishi iliyotiwa saini na wajumbe kupitia kwa Katibu wakibainisha misingi ya kura ya kutokuwa na imani inayokusudiwa na iwapo watatimiza wingi wa wajumbe wa kamati watamwomba Katibu kuitisha mkutano siku tatu baada ya arifa kutolewa.

(2A) Pindi Katibu anapopata arifa kwa maandishi kwa mujibu wa aya ya (2), saini yoyote iliyotiwa kwenye arifa haitaondolewa.

(3) Arifa kutoka kwa wajumbe kwa mujibu wa aya ya (2) itachukuliwa kuwa imetolewa itakapowasilishwa kwa anwani rasmi ya baruapepe ya Mwenyekiti au Makamu Mwenyekiti au ikishawasilishwa kwenye ofisi ya Mwenyekiti au Makamu Mwenyekiti, kutegemea hali itakavyokuwa.

(4) Arifa ya mkutano itakayotolewa na Katibu kwa mujibu wa aya ya (2) itachukuliwa kuwa imetolewa itakapokuwa imesambazwa kwa ofisi za Wabunge na kuwekwa kwenye bao za matangazo zilizo katika maeneo ya Bunge.

**Kura asilia**

**194.** (1) Mwenyekiti wa Kamati isipokuwa Kamati ya Kuratibu Shughuli za Bunge la Taifa atakuwa na kura asilia wala siyo kura ya uamuzi.

(2) Aya ya (1) haitatumika kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kuratibu Shughuli za Bunge la Taifa ambaye hana kura asilia wala kura ya uamuzi.

**Kuhudhuria mikutano ya kamati kwa Wabunge wasio wajumbe wa kamati**

**195.** (1) Mbunge yeyote anaweza kuhudhuria mkutano wa Kamati yoyote ya Bunge la Taifa ambapo yeye si mjumbe, ila Mbunge huyo hatakuwa na haki ya kupiga kura kuamua suala lolote ambalo Kamati inalishughulikia.

(2) Mbunge yeyote anayekusudia kushiriki mkutano wa Kamati ya Bunge la Taifa ambapo yeye si mjumbe atawasilisha ombi kimaandishi kwa Mwenyekiti wa Kamati angalau saa ishirini na nne kabla ya mkutano huo kufanyika au muda mwingine wowote ambao Mwenyekiti anaweza kuruhusu katika hali za kipekee.

(3) Ombi hilo litataja suala lolote ambalo Mbunge huyo anakusudia kulitoa kwenye mkutano huo.

(4) Pale ambapo Mwenyekiti anaidhinisha ombi la Mbunge kushiriki kwenye mkutano wa Kamati kwa mujibu wa aya ya (2), Mbunge huyo anaweza kuhudhuria mkutano na kuwasilisha masuala yoyote aliyotaja kwenye ombi lake.

(5) Mwenyekiti atawapa kipaumbele wajumbe wa Kamati kabla ya kumruhusu Mbunge ambaye si mjumbe wa Kamati kuchangia suala linaloshughulikiwa na Kamati.

(6) Mwenyekiti anaweza kumwamuru Mbunge asiye mjumbe wa Kamati kuondoka kwenye mkutano kwa sababu ya utovu wa nidhamu.

**Utaratibu katika Kamati**

**196.** (1) Isipokuwa na kwa kadri Mwenyekiti atakavyoelekeza kwa lengo la kurahisisha kushughulikia suala lililokabidhiwa Kamati, utaratibu utakaoutumika kwenye Kamati utakuwa kama ule unaotumika katika Kamati ya Bunge Zima kadri itakavyowezekana.

(2) Suala lolote litakalojitokeza kwenye Kamati litaamuliwa kwa kura na uamuzi wowote utakaofikiwa kupitia kura hiyo utakuwa ni uamuzi wa Kamati kuhusu suala hilo.

(3) Kumbukumbu za Kamati zitahifadhiwa kwa namna ambayo Kumbukumbu za Kamati ya Bunge Zima zinahifadhiwa na kwa namna nyingine yoyote kama itakayoelekezwa kwenye Mwongozo wa Kamati za Bunge la Taifa.

(4) Pale ambapo kura ya uamuzi wa suala lolote imegawanyika, majina ya wajumbe wanaounga na wanaopinga suala hilo na wanaopiga kura ya mzio yataorodheshwa kwenye kumbukumbu za Kamati.

(5) Isipokuwa kama Spika ataelekeza vinginevyo, Kamati inaweza kufanya mikutano hata kama Bunge la Taifa limeahirishwa.

**Udhibiti wa wajibu**

**197.** (1) Majadiliano ya Kamati yatajikita kwenye wajibu wa Kamati na nyongeza au mipaka yoyote kwenye wajibu huo kama itakavyoelekezwa na Bunge la Taifa na iwapo ni Kamati inayoshughulikia Mswada, itajikita katika Mswada na marekebisho yanayohusika.

(2) Kamati inapotekeleza majukumu yake haitashughulikia masuala yaliyo nje ya wajibu wa Bunge la Taifa kwa mujibu wa Katiba.

**Mikutano ya Kamati kuwa wazi kwa umma**

**198.** (1) Mikutano yote ya Kamati itakuwa wazi kwa umma isipokuwa pale ambapo katika hali za kipekee, Spika amebaini kuwa kuna sababu za kuridhisha kutoruhusu mkutano kuwa wazi kwa umma.

(2) Kamati inaweza kuahirisha mkutano kwa ajili ya kuomba idhini ya Spika ili kutoruhusu mkutano kuwa wazi kwa umma.

**Ripoti za Kamati**

**199.** (1) Ripoti ya Kamati itaandaliwa na kuhifadhiwa kwa namna ambayo Kumbukumbu za Kamati ya Bunge Zima zinahifadhiwa na kwa namna nyingine yoyote itakayoelekezwa kwenye Mwongozo wa Kamati za Bunge la Taifa.

(2) Ripoti ya Kamati ikisharidhiwa kwa wingi wa wajumbe, itatiwa saini na Mwenyekiti kwa niaba ya Kamati.

(3) Iwapo Mwenyekiti wa Kamati hayupo au hapatikani, Makamu Mwenyekiti atatia saini ripoti kwa mujibu wa aya ya (1), na iwapo Mwenyikiti na Makamu Mwenyekiti hawapo, Kamati itamteua mjumbe mwingine kutia saini ripoti hiyo.

(4) Kamati itaridhia ripoti yake kwenye mkutano utakaohudhuriwa na wingi wa wajumbe wa kamati hiyo.

(5) Ripoti ya Kamati ikishakubaliwa na wingi wa wajumbe, maoni ya walio wachache au maoni tofauti yanaweza kuambatishwa na mjumbe yeyote au wajumbe wowote wa Kamati kwenye ripoti hiyo.

(6) Ripoti ya Kamati ikijumuisha maoni yoyote ya walio wachache, pamoja na kumbukumbu za mikutano na taarifa au rekodi yoyote ya ushahidi uliopokewa na Kamati kadri Kamati itakavyoamua, itawasilishwa kwenye Meza na Mwenyekiti au Makamu Mwenyekiti au mjumbe aliyeidhinishwa na Kamati kuiwasilisha kwa niaba ya Kamati, katika muda usiozidi siku kumi na nne baada ya Kamati kukamilisha shughuli husika.

(7) Katika muda usiozidi saa arobaini na nane baada ya ripoti kuwasilishwa katika Meza, Katibu ataweka ripoti hiyo kwenye wavuti wa Bunge na kusambaza nakala za ripoti hiyo kwa Wabunge.

**Ripoti za utendakazi wa kamati**

**200.** (1) Isipokuwa kama sheria yoyote au Kanuni hizi zimetaja muda maalum, kila Kamati itawasilisha kwa Kamati ya Kuratibu Shughuli za Kamati ripoti ya utendakazi wa kamati kila robo ya mwaka.

(2) Kamati ya Kuratibu Shughuli za Kamati, katika muda usiozidi siku ishirini na moja, itaandaa ripoti inayojumuisha ripoti zilizopokelewa kwa mujibu wa aya ya (1) na kuiwasilisha katika Bunge la Taifa.

**Ripoti za mwisho wa muhula**

**200A.** (1) Mwenyekiti wa Kamati atawasilisha katika Bunge la Taifa ripoti ya mwisho wa muhula wake ikieleza—

(a) kazi na mafanikio yoyote ya Kamati yake katika muhula huo;

(b) suala lolote linaloshughulikiwa na Kamati hiyo pamoja na sababu za kutolikamilisha kabla ya mwisho wa muhula wake.

(2) Ripoti hiyo itakabidhiwa Kamati itakayofuata ambayo inaweza kuizingatia inapoandaa mpangokazi wake.

**Ripoti za maamuzi ya Bunge la Taifa**

**201.** Katika muda usiozidi siku sitini baada ya Bunge la Taifa kupitisha uamuzi au kuiridhia ripoti ya kamati, Waziri anayehusika na utekelezaji wa uamuzi huo ataripoti kwa kamati inayohusika kulingana na Ibara ya 153(4)(b) ya Katiba.

**Mikutano ya Pamoja ya kamati za Bunge la Taifa**

**202.** (1) Kamati mbili za Bunge la Taifa zinazoshughulikia masuala yanayofanana zinaweza kufanya mikutano ya pamoja kwa kibali cha Spika.

(2) Mkutano wa pamoja wa Kamati utaongozwa na mmoja wa Wenyekiti wa kamati hizo na Mwenyekiti atateuliwa kwa kuzingatia muda ambao Mbunge amehudumu kwa mujibu wa mpangilio unaoorodheshwa kwenye aya ya (2) ya Kanuni ya 3 (*Shughuli kwenye kikao cha kwanza cha Bunge jipya la Taifa*) na Mjumbe wa Kamati hiyo nyingine anayefuatia kwa muda wa kuhudumu atakuwa Makamu Mwenyekiti.

(3) Akidi ya mkutano wa pamoja wa kamati mbili au zaidi itakuwa jumla ya idadi ya akidi ya kila Kamati, bila kuwajumuisha Wenyekiti.

(4) Ripoti ya mkutano wa pamoja ya kamati mbili au zaidi haitaridhiwa isipokuwa kwa uamuzi ambao umeungwa mkono na wingi wa wajumbe wote wa kamati hizo.

**Ruhusa ya mikutano ya pamoja na Kamati ya Seneti**

**202A.** (1) Kwa ruhusa ya kimaandishi ya Spika, kamati ya Bunge la Taifa inaweza kufanya mikutano ya pamoja na kamati ya Seneti ili kushughulikia suala linalohusiana na wajibu wa kamati hizo.

(2) Spika atalifahamisha Bunge la Taifa kuhusu ruhusa aliyotoa kwa mujibu wa aya ya (1).

**Kushirikisha wataalamu**

**203.** Kwa ruhusa ya Spika, kamati inaweza kuwashirikisha wataalamu kadri itakavyoona inafaa kwa utekelezaji wa wajibu wake.

**Kamati ya Uteuzi**

**204.** **(**1) Kutakuwa na kamati itakayojulikana kama Kamati ya Uteuzi itakayoteuliwa na Bunge la Taifa na itakuwa na Spika kama Mwenyekiti, Naibu Spika, Kiongozi wa Chama cha walio Wengi, Kiongozi wa Chama cha walio Wachache, Naibu Kiongozi wa Chama cha walio Wengi, Naibu Kiongozi wa Chama cha walio Wachache na Wabunge wengine wasiozidi kumi na watano watakaoteuliwa na Kamati ya Kuratibu Shughuli za Bunge la Taifa kwa kuzingatia nguvu katika wingi wa idadi ya Wabunge katika vyama vilivyowakilishwa katika Bunge la Taifa na maslahi ya Wabunge Huru.

(2) Kamati ya Uteuzi itateuliwa katika muda usiozidi siku saba baada ya kikao cha kwanza cha Bunge jipya na itahudumu kwa muda wa miaka mitatu na kamati itakayoteuliwa baada ya hapo itahudumu kwa muda uliosalia wa muhula wa Bunge la Taifa.

(3) Ikiwa Spika hayupo, Kamati itamteua mjumbe miongoni mwao kuongoza mkutano.

(4) Kamati ya Uteuzi itashughulikia uteuzi uliotajwa katika Ibara ya 152(2) ya Katiba (*Mawaziri*) kwa ajili ya kuidhinishwa na Bunge la Taifa.

(5) Akidi ya Kamati ya Uteuzi itakuwa nusu ya wajumbe wa Kamati lakini Spika hatahesabiwa kwa ajili ya kutimiza akidi na hatapiga kura.

**Kamati ya Hesabu za Umma**

**205.** (1) Kutakuwa na kamati itakayoitwa Kamati ya Hesabu za Umma.

(2) Kamati ya Hesabu za Umma itakuwa na jukumu la kuchunguza hesabu zinazoonyesha matumizi ya fedha yaliyoidhinishwa na Bunge la Taifa kwa ajili ya kukidhi matumizi ya serikali na hesabu nyingine zitakazowasilishwa katika Bunge la Taifa kadri Kamati itakavyoona inafaa.

(3) Kamati ya Hesabu za Umma itakuwa na Mwenyekiti atakayechaguliwa miongoni mwa wajumbe wa Kamati ya vyama visivyounda serikali ya taifa na wajumbe wengine wasiozidi kumi na wanne.

(4) Vyama Bunge visivyounda serikali ya taifa vitakuwa na mjumbe mmoja zaidi ya Vyama Bunge vinavyounda serikali ya taifa kwenye idadi ya wajumbe wa Kamati ya Hesabu za Umma.

(5) Kamati ya Hesabu za Umma itakayoundwa mara tu baada ya Uchaguzi Mkuu itahudumu kwa muda wa miaka mitatu ya kalenda na Kamati itakayoundwa baada yake itahudumu kwa muda uliosalia wa muhula wa Bunge hilo.

**Kamati ya Hesabu za Hazina Maalum**

**205A.** (1) Kutakuwa na kamati itakayoitwa Kamati ya Hesabu za Hazina Maalum.

(2) Kamati hii itakagua ripoti za Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu—

(a) Hazina zinazoundwa kisheria au kupitia sheria ndogo, isipokuwa Hazina kwa mujibu wa Kanuni ya 205B *(Kamati ya Hesabu za Hazina Tengwa)*

(b) Hazina ya Usawazishaji;

(c) Bodi ya Ushauri kwa Hazina ya Usawazishaji; na

(d) Hazina ya Vyama vya Kisiasa.

(3) Kamati hii itakuwa na Mwenyekiti ambaye, kadri iwezekanavyo, atakuwa Mbunge Huru, na wajumbe wengine wasiozidi kumi na wanne.

(4) Vyama, isipokuwa Vyama Bunge vinavyounda serikali ya taifa, vitakuwa na mjumbe mmoja zaidi katika idadi ya wajumbe wa Kamati ya Hesabu za Hazina Maalum.

(5) Kamati ya Hesabu za Hazina Maalum haitakagua masuala ya sera au usimamizi wa kila siku wa hazina hizo maalum.

(6) Mwanzoni mwa kila muhula wa Bunge au wakati mwingine wowote unaofaa, Spika atatoa orodha inayobainisha Hazina zinazohusiana na wajibu wa Kamati hiyo.

(7) Kamati ya Hesabu za Hazina Maalum itakayoundwa mara tu baada ya Uchaguzi Mkuu itahudumu kwa muda wa miaka mitatu ya kalenda na Kamati itakayoundwa baada yake itahudumu kwa muda uliosalia wa muhula wa Bunge hilo.

**Kamati ya Hesabu za Hazina Tengwa**

**205B.** (1) Kutakuwa na kamati itakayoitwa Kamati ya Hesabu za Hazina Tengwa.

(2) Kamati hiyo itawajibika kukagua ripoti za Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali za—

(a) Hazina ya Serikali ya Taifa kwa Maendeleo ya Maeneobunge;

(b) Bodi ya Hazina ya Serikali ya Taifa kwa Maendeleo ya Maeneobunge;

(c) Hazina ya Serikali ya Taifa kwa Hatua Sawazishi; na

(d) Bodi ya Hazina ya Serikali ya Taifa kwa Hatua Sawazishi.

(3) Kamati hii itakuwa na Mwenyekiti atakayechaguliwa miongoni mwa wajumbe wa Kamati ya vyama visivyounda serikali ya taifa na wajumbe wengine wasiozidi kumi na wanne.

(4) Katika uanachama wa Kamati hii, vyama visivyo vyama bunge vinavyounda serikali ya taifa vitakuwa na mjumbe mmoja zaidi.

(5) Kamati ya Hesabu za Hazina Tengwa haitakagua masuala ya sera au usimamizi wa kila siku wa hazina hizo maalum.

(6) Kamati ya Hesabu za Hazina Tengwa itakayoundwa mara tu baada ya Uchaguzi Mkuu itahudumu kwa muda wa miaka mitatu ya kalenda na Kamati itakayoundwa baada yake itahudumu kwa muda uliosalia wa muhula wa Bunge hilo.

**Kamati ya Uwekezaji wa Umma kuhusu Utawala na Elimu**

**206.** (1) Kutakuwa na kamati itakayoitwa Kamati ya Uwekezaji wa Umma kuhusu Utawala na Elimu.

(2) Katika kushughulikia masuala ya sekta za elimu, ulinzi, utawala, haki na uzingatiaji wa sheria, Kamati hii—

(a) itachunguza ripoti na hesabu za uwekezaji wa umma;

(b) itachunguza ripoti, ikiwa zipo, za Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu uwekezaji wa umma; na

(c) itachunguza, kwa kuzingatia uhuru na taratibu bora za uwekezaji wa umma, ili kubaini iwapo masuala

yanayohusu uwekezaji wa umma yanasimamiwa kulingana na kanuni za kifedha au kibiashara pamoja na taratibu zinazofaa za kibiashara.

(3) Licha ya aya ya (2), Kamati hii haitachunguza yafuatayo—

(a) masuala ya sera muhimu ya Serikali ambayo hayahusiani na shughuli za biashara au uwekezaji wa umma;

(b) masuala ya usimamizi wa kila siku; na

(c) masuala ambayo utaratibu wa kuyashughulikia umewekwa katika sheria mahususi iliyoanzisha uwekezaji huo wa umma.

(4) Kamati hii itakuwa na Mwenyekiti atakayechaguliwa miongoni mwa wajumbe wa Kamati ya vyama visivyounda serikali ya taifa na wajumbe wengine wasiozidi kumi na wanne.

(5) Katika uanachama wa Kamati hii, vyama visivyo vyama bunge vinavyounda serikali ya taifa vitakuwa na mjumbe mmoja zaidi.

(6) Mwanzoni mwa kila muhula wa Bunge au wakati mwingine wowote unaofaa, Spika atatoa orodha inayobainisha mashirika ya umma yanayohusiana na wajibu wa Kamati hiyo.

(7) Kamati itakayoundwa mara tu baada ya Uchaguzi Mkuu itahudumu kwa muda wa miaka mitatu ya kalenda na Kamati itakayoundwa baada yake itahudumu kwa muda uliosalia wa muhula wa Bunge hilo.

(8) Kanuni hii itatanguka mwishoni mwa kila muhula wa Bunge la Taifa.

(9) Bunge la Taifa linaweza kuamua kusimamisha kwa muda matumizi ya aya ya (8).

**Kamati ya Uwekezaji wa Umma kuhusu Masuala ya Kibiashara na Kawi**

**206A.** (1) Kutakuwa na kamati itakayoitwa Kamati ya Uwekezaji wa Umma kuhusu Masuala ya Kibiashara na Kawi.

(2) Katika kushughulikia masuala ya sekta za kawi, mazingira, masuala ya jumla ya kiuchumi na kibiashara, Kamati hii—

(a) itachunguza ripoti na hesabu za uwekezaji wa umma;

(b) itachunguza ripoti, ikiwa zipo, za Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu uwekezaji wa umma; na

(c) itachunguza, kwa kuzingatia uhuru na taratibu bora za uwekezaji wa umma, ili kubaini iwapo masuala yanayohusu uwekezaji wa umma yanasimamiwa kulingana na kanuni za kifedha au kibiashara pamoja na taratibu zinazofaa za kibiashara.

(3) Licha ya aya ya (2), Kamati hii haitachunguza yafuatayo—

(a) masuala ya sera muhimu ya Serikali ambayo hayahusiani na shughuli za biashara au uwekezaji wa umma;

(b) masuala ya usimamizi wa kila siku; na,

(c) masuala ambayo utaratibu wa kuyashughulikia umewekwa katika sheria mahususi iliyoanzisha uwekezaji huo wa umma.

(4) Kamati hii itakuwa na Mwenyekiti atakayechaguliwa miongoni mwa wajumbe wa Kamati ya vyama visivyounda serikali ya taifa na wajumbe wengine wasiozidi kumi na wanne.

(5) Katika uanachama wa Kamati hii, vyama visivyo vyama bunge vinavyounda serikali ya taifa vitakuwa na mjumbe mmoja zaidi.

(6) Mwanzoni mwa kila muhula wa Bunge au wakati mwingine wowote unaofaa, Spika atatoa orodha inayobainisha mashirika ya umma yanayohusiana na wajibu wa Kamati hiyo.

(7) Kamati itakayoundwa mara tu baada ya Uchaguzi Mkuu itahudumu kwa muda wa miaka mitatu ya kalenda na Kamati itakayoundwa baada yake itahudumu kwa muda uliosalia wa muhula wa Bunge hilo.

(8) Kanuni hii itatanguka mwishoni mwa kila muhula wa Bunge la Taifa.

(9) Bunge la Taifa linaweza kuamua kusimamisha kwa muda matumizi ya aya ya (8).

**Kamati ya Uwekezaji wa Umma kuhusu Huduma kwa Jamii, Usimamizi na Kilimo**

**206B.** (1) Kutakuwa na kamati itakayoitwa Kamati ya Uwekezaji wa Umma kuhusu Huduma kwa Jamii, Usimamizi na Kilimo.

(2) Katika kushughulikia masuala ya sekta za kilimo, usimamizi wa umma, afya, na maslahi ya kijamii, Kamati hii—

(a) itachunguza ripoti na hesabu za uwekezaji wa umma;

(b) itachunguza ripoti, ikiwa zipo, za Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu uwekezaji wa umma; na

(c) itachunguza, kwa kuzingatia uhuru na taratibu bora za uwekezaji wa umma, ili kubaini iwapo masuala yanayohusu uwekezaji wa umma yanasimamiwa kulingana na kanuni za kifedha au kibiashara pamoja na taratibu zinazofaa za kibiashara.

(3) Licha ya aya ya (2), Kamati hii haitachunguza yafuatayo—

(a) masuala ya sera muhimu ya Serikali ambayo hayahusiani na shughuli za biashara au uwekezaji wa umma;

(b) masuala ya usimamizi wa kila siku; na,

(c) masuala ambayo utaratibu wa kuyashughulikia umewekwa katika sheria mahususi iliyoanzisha uwekezaji huo wa umma.

(4) Kamati hii itakuwa na Mwenyekiti atakayechaguliwa miongoni mwa wajumbe wa Kamati ya vyama visivyounda serikali ya taifa na wajumbe wengine wasiozidi kumi na wanne.

(5) Katika uanachama wa Kamati hii, vyama visivyo vyama bunge vinavyounda serikali ya taifa vitakuwa na mjumbe mmoja zaidi.

(6) Mwanzoni mwa kila muhula wa Bunge au wakati mwingine wowote unaofaa, Spika atatoa orodha inayobainisha mashirika ya umma yanayohusiana na wajibu wa Kamati hiyo.

(7) Kamati itakayoundwa mara tu baada ya Uchaguzi Mkuu itahudumu kwa muda wa miaka mitatu ya kalenda na Kamati itakayoundwa baada yake itahudumu kwa muda uliosalia wa muhula wa Bunge hilo.

(8) Kanuni hii itatanguka mwishoni mwa kila muhula wa Bunge la Taifa.

(9) Bunge la Taifa linaweza kuamua kusimamisha kwa muda matumizi ya aya ya (8).

**Kamati ya Bajeti na Uidhinishaji wa Matumizi**

**207.** (1) Kutakuwa na kamati itakayoitwa Kamati ya Bajeti na Uidhinishaji wa Matumizi.

(2) Kamati itakuwa na Mwenyekiti na wajumbe wengine wasiozidi ishirini na sita.

(3) Majukumu ya Kamati hii yatakuwa—

(a) kupeleleza, kuchunguza na kuripoti kuhusu masuala yote yanayohusiana na ushirikishi, udhibiti na ufuatiliaji wa bajeti ya taifa;

(b) kujadili na kuhakiki makadirio ya bajeti na kutoa mapendekezo kwa Bunge la Taifa;

(c) kutathmini Taarifa ya Sera ya Bajeti iliyowasilishwa kwa Bunge la Taifa;

(d) kutathmini Miswada inayohusiana na bajeti, ikijumuisha Miswada ya Kuidhinisha Matumizi ya Fedha; na

(e) kutathmini makadirio ya kodi, sera za kiuchumi na bajeti na mipango iliyo na athari za moja kwa moja kwenye bajeti.

(4) Kamati ya Bajeti na Uidhinishaji wa Matumizi itakayoundwa na Bunge la Taifa mara baada ya Uchaguzi Mkuu itahudumu kwa muda wa miaka mitatu ya kalenda na kamati itakayoundwa baadaye itahudumu kwa muda uliosalia wa muhula wa Bunge.

(5) Akidi ya Kamati ya Bajeti na Uidhinishaji wa Matumizi itakuwa Mwenyekiti na wajumbe wengine wanane.

(5A) Kamati ya Bajeti na Uidhinishaji wa Matumizi inaweza kuunda kamati ndogo, ikijumuisha kamati ndogo ya kuhakiki masuala yanayohusu utungaji wa sheria, kadri itakavyoona inafaa, kwa uendeshaji bora wa majukumu yake.

(6) Kamati itawaalika Wenyeviti wa kamati zote za kiidara ili watoe mawasilisho ya kamati zao wakati wa kushughulikia bajeti.

**Kamati ya Deni la Umma na Ubinafsishaji**

**207A.** (1) Kutakuwa na kamati itakayoitwa Kamati ya Deni la Umma na Ubinafsishaji.

(2) Kamati hii itawajibikia—

(a) uangalizi wa deni la umma na dhamana kwa mujibu wa Ibara ya 214 ya Katiba;

(b) uchunguzi wa masuala kuhusu dhamana za madeni ya serikali ya taifa;

(c) uangalizi wa huduma zilizogharimiwa na Hazina Kuu isipokuwa hesabu zilizokaguliwa;

(d) uchunguzi wa ripoti za hali ya uchumi kuhusiana na deni la umma;

(e) uangalizi wa miradi inayotokana na Ushirikiano kati ya Umma na Sekta ya Kibinafsi inayotekelezwa na serikali ya taifa kuhusiana na deni la umma; na

(f) uangalizi wa ubinafsishwaji wa rasilimali za taifa.

(3) Kuhusu deni la taifa, Kamati hii—

(a) itazingatia na kukagua masharti ambayo yataongoza ukopaji wa serikali ya taifa ikiwa ni pamoja na upeo wa kukopa;

(b) itachunguza kiasi cha deni la taifa;

(c) itachunguza matumizi yaliyofanywa au yatakayofanywa kutokana na mapato ya mikopo ya taifa na dhamana za Serikali ya Taifa;

(d) itachunguza taratibu zilizowekwa kushughulikia au kulipia mikopo na dhamana za taifa;

(e) itachunguza Mkakati wa Kudhibiti Deni wa kila mwaka kwa muda wastani utakaowasilishwa katika Bunge la Taifa na waziri anayehusika na masuala ya fedha;

(f) itachunguza hatua zilizofikiwa katika ulipaji wa mikopo ya taifa na mikopo iliyodhaminiwa na serikali ya taifa;

(g) itatathmini na kuchunguza mapendekezo ya serikali ya taifa kuhusu mikopo na dhamana kwa serikali ya kaunti kwa mujibu wa Ibara ya 212(a) ya Katiba;

(h) itachunguza ripoti za kila mwaka zilizowasilishwa katika Bunge la Taifa kwa mujibu wa Ibara ya 213(2) ya Katiba kuhusu dhamana zilizotolewa na serikali ya taifa;

(i) itachunguza ripoti za kila robo ya mwaka zilizowasilishwa na Waziri katika Bunge kuhusu mikopo yote kwa serikali ya taifa, asasi za serikali ya taifa na serikali za kaunti kwa mujibu wa Ibara ya 211(2) ya Katiba;

(j) itatathmini sheria na masharti ya serikali ya taifa ya kudhamini mikopo;

(k) itatathmini uzingatiaji wa kanuni ya usawa kati ya vizazi katika ukopaji wa umma;

(l) itatathmini uzingativu wa serikali ya taifa kwa Katiba au sheria zinazohusiana na ukopaji wa umma na dhamana; na

(m) itachunguza ripoti zilizowasilishwa na waziri kuhusu dhamana za mikopo kwa biashara ndogondogo, ndogo na za wastani.

(4) Kamati hii itatoa ripoti na mapendekezo kwa Bunge la Taifa mara kwa mara itakavyowezekana, ikijumuisha mapendekezo ya sheria kwa masuala yanayohusu wajibu wake.

(5) Kamati hii itakuwa na Mwenyekiti atakayechaguliwa miongoni mwa wajumbe wa Kamati ya vyama visivyounda serikali ya taifa na wajumbe wengine wasiozidi kumi na wanne.

(6) Katika uanachama wa Kamati hii, vyama visivyo vyama bunge vinavyounda serikali ya taifa vitakuwa na mjumbe mmoja zaidi.

(7) Kamati ya Deni la Umma na Ubinafsishaji itakayoundwa mara tu baada ya Uchaguzi Mkuu itahudumu kwa muda wa

miaka mitatu ya kalenda na Kamati itakayoundwa baada yake itahudumu kwa muda uliosalia wa muhula wa Bunge hilo.

**Kamati ya Utaratibu na Kanuni za Bunge la Taifa**

**208.** (1) Kutakuwa na kamati itakayoitwa Kamati ya Utaratibu na Kanuni za Bunge la Taifa.

(2) Kamati hii itakuwa na Spika kama Mwenyekiti, Naibu Spika, wajumbe wa Jopo la Mwenyekiti na Wabunge wengine wasiozidi kumi na watatu.

(3) Kamati ya Utaratibu na Kanuni za Bunge la Taifa itashughulikia na kuripoti kuhusu masuala yote yanayohusu Kanuni hizi.

(4) Kamati ya Utaratibu na Kanuni za Bunge la Taifa inaweza kupendekeza marekebisho katika Kanuni hizi na marekebisho hayo yakishaidhinishwa na Bunge la Taifa yataanza kutumika wakati utakaoamuliwa na Bunge la Taifa.

(5) Kamati ya Utaratibu na Kanuni za Bunge la Taifa inaweza kupendekeza masharti yatakayoongoza uendeshaji bora wa shughuli za kamati na masharti hayo yakishaidhinishwa na Bunge la Taifa yataendelea kutumika hadi yatakaporekebishwa au kufutwa na Bunge la Taifa.

(6) Masharti yoyote yatakayoidhinishwa kwa mujibu wa aya ya (5) yataambatishwa kwenye Kanuni hizi na Kamati zitafuata masharti hayo kama ilivyo kwa Kanuni hizi.

(7) Kamati ya Utaratibu na Kanuni za Bunge la Taifa itakayoundwa mara tu baada ya uchaguzi mkuu itahudumu kwa muda wa miaka mitatu ya kalenda na Kamati itakayoundwa baada yake itahudumu kwa muda uliosalia wa muhula wa Bunge hilo.

**Kamati ya Ardhilhali za Umma**

**208A.** (1) Kutakuwa na kamati itakayoitwa Kamati ya Ardhilhali za Umma.

(2) Kamati hii—

(a) itashughulikia ardhilhali zote za umma zilizowasilishwa katika Bunge la Taifa;

(b) itatoa mapendekezo inavyofaa kuhusu maombi ya ardhilhali hizo;

(c) itapendekeza iwapo matokeo yanayotokana na kushughulikia ardhilhali yanafaa kujadiliwa; na

(d) itashauri Bunge la Taifa na kuripoti kuhusu ardhilhali zote za umma ilizokabidhiwa.

(3) Kamati hii itakuwa na Mwenyekiti na wajumbe wengine wasiozidi kumi na wanne.

(4) Kamati itakayoundwa mara tu baada ya uchaguzi mkuu itahudumu kwa muda wa miaka mitatu ya kalenda na Kamati itakayoundwa baada yake itahudumu kwa muda uliosalia wa muhula wa Bunge hilo.

**Kamati ya Masuala ya Ughaibuni na Wafanyakazi Wahamiaji**

**208B.** (1) Kutakuwa na kamati itakayoitwa Kamati ya Masuala ya Ughaibuni na Wafanyakazi Wahamiaji.

(2) Kamati hii—

(a) itashughulikia masuala yote ambayo moja kwa moja yanahusu sera na mipango ya kulinda haki na ustawi wa Wakenya walio ughaibuni, ikijumuisha—

(i) Raia wa Kenya wenye uraia wa nchi mbili;

(ii) Wakenya wahamiaji wanaofanya kazi nje ya nchi pamoja na familia zao ughaibuni; na

(iii) Wakenya wanaosomea ughaibuni;

(b) itatathmini sera na mipango ya serikali ya taifa kuhusu—

(i) kuvutia kwa namna bora, kuleta pamoja na kutumia kwa njia inayofaa rasilimali za Kenya ughaibuni kwa maendeleo ya kiuchumi, kijamii na kitamaduni;

(ii) kuwashirikisha na kuwawezesha Wakenya walio ughaibuni, pamoja na watu wanaostahiki kupata uraia wa nchi mbili; na

(iii) haki ya Wakenya walio ughaibuni kupiga kura.

(3) Kamati hii itakuwa na Mwenyekiti na wajumbe wengine wasiozidi kumi na wanne.

(4) Kamati itakayoundwa mara tu baada ya uchaguzi mkuu itahudumu kwa muda wa miaka mitatu ya kalenda na Kamati itakayoundwa baada yake itahudumu kwa muda uliosalia wa muhula wa Bunge hilo.

**Kamati ya Utekelezaji**

**209.** (1) Kutakuwa na kamati itakayoitwa Kamati ya Utekelezaji.

(2) Kamati itatathmini maamuzi ya Bunge la Taifa (ikijumuisha ripoti za kamati zilizoridhiwa), ardhilhali na ahadi zilizotolewa na Mamlaka Kuu ya Serikali ya Taifa na kutathmini —

(a) iwapo uamuzi na ahadi hizo zimetekelezwa au la, na pale ambapo zimetekelezwa, kiwango cha utekelezaji na iwapo utekelezaji huo umefanywa katika muda mfupi unaohitajika; na

(b) iwapo sheria iliyopitishwa na Bunge la Taifa imetekelezwa au la na kama imetekelezwa, kiwango ambacho utekelezaji wake umefanywa katika muda mfupi unaohitajika.

(3) Kamati inaweza kupendekeza kwa Bunge la Taifa adhabu dhidi ya Waziri atakayeshindwa kutoa ripoti kwa kamati inayohusika kuhusu kiwango cha utekelezaji wa maamuzi ya Bunge la Taifa bila sababu za kuridhisha.

(4) Kamati ya Utekelezaji itakuwa na Mwenyekiti na wajumbe wengine wasiozidi ishirini.

(5) Vyama, isipokuwa Vyama Bunge vinavyounda serikali ya taifa, vitakuwa na mjumbe mmoja zaidi ya Vyama Bunge vinavyounda serikali ya taifa kwenye idadi ya wajumbe wa Kamati ya Utekelezaji.

(6) Kamati ya Utekelezaji itakayoundwa mara tu baada ya uchaguzi mkuu itahudumu kwa muda wa miaka mitatu ya kalenda na Kamati itakayoundwa baada yake itahudumu kwa muda uliosalia wa muhula wa Bunge hilo.

**Kamati ya Sheria Ndogo**

**210.** (1) Kutakuwa na kamati itakayoitwa Kamati ya Sheria Ndogo.

(1A) Kamati hii itakuwa na Mwenyekiti na Wajumbe wengine wasiozidi ishirini.

(2) Kila wakati sheria ndogo inapowasilishwa katika Bunge la Taifa kwa mujibu wa Katiba, sheria yoyote au Kanuni hizi, isipokuwa kama imedhamiriwa vinginevyo kwenye sheria inayohusika, sheria hiyo ndogo itawasilishwa katika Bunge la Taifa na Mwenyekiti wa kamati husika ya kiidara au mjumbe mwingine yeyote wa Kamati hiyo na kisha kukabidhiwa Kamati ya Sheria Ndogo.

(3) Kamati itathmini iwapo sheria ndogo —

(a) imezingatia masharti ya Katiba, Sheria msingi inayotokana nayo au sheria nyingine yoyote;

(b) inakiuka haki na uhuru wa kimsingi wa umma;

(c) ina suala ambalo, kwa maoni ya Kamati, linatakiwa kushughulikiwa kwa mujibu wa sheria;

(d) ina masharti ya kutoza kodi;

(e) inazuia mamlaka ya Mahakama kwa njia ya moja kwa moja au isiyo ya moja kwa moja;

(f) ina masharti ambayo yanakusudia kutumika kwa masuala yaliyofanyika kabla ya kupitishwa kwake kinyume na mamlaka inayopewa na Katiba au Sheria;

(g) inahusisha matumizi kutoka kwenye Hazina Kuu au mapato mengine ya serikali;

(h) ina makosa ya kiuandishi au ya kimuundo au lengo lake linahitaji kufafanuliwa zaidi;

(i) inaelekea kutumia visivyo au kwa namna isiyotarajiwa mamlaka iliyopewa na Katiba au sheria msingi inayotokana nayo;

(j) inaelekea kuchapishwa au kuwasilishwa kwake katika Bunge kumecheleweshwa bila sababu zinazoridhisha;

(k) inategemeza haki, uhuru au wajibu kwa maamuzi yasiyoruhusu kuhakikiwa kisheria;

(l) inategemeza haki, uhuru au wajibu kwa mamlaka ya usimamizi ambayo hayajafafanuliwa kikamilifu;

(m) inakasimisha mamlaka ya kutunga kisheria isivyostahili;

(n) inatoza faini, kifungo au adhabu nyingine pale ambapo sheria msingi haijatoa mamlaka bayana;

(o) inaonekana kwa sababu yoyote kukiuka utawala wa sheria;

(p) inatoa nafasi finyu kwa Bunge kuchunguza utekelezaji wa mamlaka ya kutunga sheria; na

(q) inaashiria sababu nyingine yoyote ambayo Kamati inaona inafaa kuchunguza.

(4) Iwapo Kamati—

(a) itaamua kwamba sheria ndogo ziidhinishwe, Katibu atawasilisha uamuzi huo kwa idara husika au mamlaka iliyotayarisha na kuchapisha sheria ndogo;

(b) imeamua kutoidhinisha sheria ndogo, Kamati inaweza kutoa mapendekezo kwa Bunge la Taifa kwamba sheria ndogo au sehemu yake ibatilishwe na iwapo sheria ndogo —

(i) haijatayarishwa kwa mujibu wa sheria inayohusu serikali za kaunti na uamuzi umepitishwa na Bunge la Taifa katika muda usiozidi siku ishirini Bunge la Taifa litakapofanya kikao baada ya sheria ndogo hiyo kuwasilishwa kwake kwa mujibu wa aya ya (2), kwamba sheria ndogo au sehemu yake ibatilishwe, sheria ndogo au sehemu yake husika itabatilishwa papo hapo; na

(ii) imetayarishwa kwa mujibu wa sheria inayohusu serikali za kaunti, Katibu, katika muda usiozidi ya siku saba baada ya kupitishwa kwa uamuzi huo, atatuma Ujumbe kwa Seneti.

(5) Katibu atawasilisha uamuzi uliopitishwa kwa mujibu wa aya ya (4)(b)(i) kwa idara husika au mamlaka iliyochapisha sheria ndogo hiyo.

(5A) Kamati hii, katika kila robo ya mwaka, itawasilisha ripoti kwa Bunge la Taifa yenye orodha ya sheria ndogo zilizoidhinishwa kwa mujibu wa aya ya (4) (a).

(5B) Pale ambapo Bunge la Taifa linabatilisha sehemu ya sheria ndogo au sheria ndogo yote, mamlaka iliyotunga sheria hiyo itamuarifu Katibu na kuwasilisha ushahidi wa kuchapishwa kwa kubatilishwa huko katika muda usiozidi siku ishirini na moja.

(5C) Katibu atahifadhi taarifa alizopokea kwa mujibu wa aya ya (5B) katika sajili ya sheria ndogo na kuiwasilisha kwa Kamati.

(5D) Kamati ya Sheria Ndogo itakayoundwa mara tu baada ya uchaguzi mkuu itahudumu kwa muda wa miaka mitatu ya kalenda na Kamati itakayoundwa baada yake itahudumu kwa muda uliosalia wa muhula wa Bunge hilo.

(6) Katika Kanuni hii, "sheria ndogo" ina maana ya masharti, amri, utaratibu, maelekezo, fomu, tozo za gharama au ada, idhini maalum, hati ya kutumwa, waranti, kauli ya kisheria, sheria zilizogatuliwa, uamuzi, mwongozo au hati zote za kisheria ambazo zimetungwa au kutolewa kwa ajili ya utekelezaji wa mamlaka yanayokabidhiwa kwa mujibu wa sheria msingi.

**Kuafiki uamuzi wa Seneti kuhusu sheria ndogo**

**211.** (1) Bunge la Taifa linapopokea Ujumbe kutoka Seneti ikiomba maafikiano kuhusu uamuzi wa Seneti, kwamba sheria ndogo au sehemu ya sheria ndogo ibatilishwe, uamuzi wa Seneti utakabidhiwa Kamati ya Sheria Ndogo ambayo itashughulikia uamuzi huo pamoja na sheria ndogo inayohusika na kuripoti katika Bunge la Taifa katika muda usiozidi siku ishirini na moja baada ya kukabidhiwa uamuzi wa Seneti.

(2) Aya ya (3) ya Kanuni ya 210 (*Kamati ya Sheria Ndogo*), kadri itakavyowezekana, itatumika katika kushughulikia uamuzi uliotajwa katika aya ya (1).

(3) Ikiwa Bunge la Taifa—

(a) linakubaliana na uamuzi wa Seneti, Katibu atamjulisha Katibu wa Seneti, kupitia Ujumbe na idara husika au mamlaka iliyochapisha sheria ndogo, kwamba Bunge limebatilisha sheria ndogo au sehemu yake na sheria ndogo au sehemu yake inayohusika imebatilishwa, bila kuathiri uhalali wa jambo lolote lililotendwa

hapo awali kwa mujibu wa sheria ndogo hiyo au kwa utayarishaji wa sheria ndogo yoyote mpya.

(b) halikubaliani na uamuzi wa Seneti, uamuzi huo utakabidhiwa Kamati ya Pamoja ya Bunge, na Kanuni ya 213 (*Uteuzi wa Kamati za Pamoja*) itatumika ikifanyiwa marekebisho yanayofaa.

**Kamati ya Utangamano wa Kikanda**

**212.** (1) Kutakuwa na Kamati itakayoitwa Kamati ya Utangamano wa Kikanda.

(2) Kamati ya Utangamano wa Kikanda—

(a) itaimarisha jukumu na uhusika wa Bunge la Taifa la Taifa katika kuzidisha na kustawisha mchakato wa utangamano katika Jumuiya ya Afrika Mashariki na Afrika nzima;

(b) itatathmini kumbukumbu za mijadala yote inayohusika na maamuzi ya mikutano yote ya Bunge la Afrika Mashariki;

(c) itatathmini Miswada iliyowasilishwa kwenye Bunge la Afrika Mashariki na Sheria za Jumuiya ya Afrika Mashariki;

(d) itatathmini kumbukumbu za mijadala yote inayohusika na maamuzi ya mikutano yote ya Bunge la Afrika, Baraza la Pamoja la Mabunge ya Afrika, Visiwa vya Karibi na Pasifiki-Umoja wa Ulaya na mashirika mengine ya utangamano wa kikanda; na

(e) itachunguza na kutathimini suala lingine lolote linalohusiana na utangamano wa kikanda linalohitajika kushughulikiwa na Bunge la Taifa.

(3) Kamati itakuwa na Mwenyekiti na Wajumbe wengine wasiozidi ishirini.

(4) Kamati ya Utangamano wa Kikanda itakayoundwa mara tu baada ya uchaguzi mkuu itahudumu kwa muda wa miaka mitatu ya kalenda na Kamati itakayoundwa baada yake itahudumu kwa muda uliosalia wa muhula wa Bunge hilo.

**Utaratibu wa kuwasilisha ripoti za Bunge la Afrika Mashariki na Bunge la Afrika**

**212A.** (1) Kamati au Mbunge wa Bunge la Afrika Mashariki au Bunge la Afrika anaweza kuwasilisha ripoti au kushauriana na Kamati ambayo kwa wakati huo inahusika na masuala ya utangamano wa kikanda au kamati nyingine yoyote ya Bunge la Taifa kuhusu suala lolote linalohusiana na kazi za Bunge la Afrika Mashariki au Bunge la Afrika.

(2) Katibu wa Bunge la Taifa anapopokea nakala za kumbukumbu za mijadala ya mikutano ya Bunge la Afrika Mashariki, au nakala za Miswada zilizowasilishwa kwenye Bunge la Afrika Mashariki na sheria za Jumuiya ya Afrika Mashariki, Katibu atazikabidhi kumbukumbu za mijadala, miswada au sheria za Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa Kamati inayohusika.

(3) Kamati itashughulikia ripoti itakayowasilishwa kwa mujibu wa aya ya (1) au kumbukumbu za mijadala, Miswada au Sheria za Jumuiya na kuwasilisha ripoti katika Bunge la Taifa pamoja na mapendekezo yake, ikiwa yapo, katika muda usiozidi siku ishirini na moja.

(4) Bunge la Taifa, katika muda usiozidi siku ishirini na moja, litashughulikia ripoti ya Kamati iliyowasilishwa kwa mujibu wa aya ya (3) na katika muda usiozidi siku saba, Katibu atawasilisha kwa Katibu wa Bunge la Afrika Mashariki uamuzi wa Bunge la Taifa kuhusu ripoti pamoja na nakala za kumbukumbu za mjadala.

**Kamati ya Huduma na Vifaa kwa Wabunge**

**212B.** (1) Kutakuwa na Kamati itakayoitwa Kamati ya Huduma na Vifaa kwa Wabunge.

(2) Majukumu ya Kamati hii yatakuwa—

(a) kupokea na kushughulikia maoni ya Wabunge kuhusu huduma na vifaa wanavyopewa Wabunge kwa manufaa na ustawi wao; na

(b) kushauri na kuripoti kuhusu masuala yote yanayohusiana na huduma na vifaa wanavyopewa Wabunge.

(3) Kamati itakuwa na Mwenyekiti na Wabunge wengine wasiozidi kumi na wanne ambao wataidhinishwa na Bunge la Taifa mwanzoni mwa kila Kipindi.

**Kamati ya Mshikamano wa Kitaifa na Fursa Sawa**

**212C.** (1) Kutakuwa na Kamati itakayoitwa Kamati ya Mshikamano wa Kitaifa na Fursa Sawa.

(2) Kamati itakuwa na Mwenyekiti na Wajumbe wengine wasiozidi ishirini.

(3) Majukumu ya Kamati hii yatakuwa—

(a) kufuatilia na kuimarisha mikakati inayohusiana na sera na mipango ya amani na mshikamano wa kitaifa;

(b) kupeleleza, kuchunguza na kuripoti juu ya masuala yote yanayohusu mshikamano baina ya jamii;

(c) kufuatilia na kuimarisha mikakati iliyobuniwa katika kuongeza fursa sawa na kuboresha usawa wa maisha na hali ya watu wote, ikijumusha watu waliotengwa kwa misingi ya jinsia, umri, ulemavu, hali ya kiafya, kabila, rangi, utamaduni au dini au uhusiano au misingi mingine kama hiyo;

(d) kupeleleza, kuchunguza na kuripoti juu ya masuala yote yanayohusiana na ubaguzi au kutengwa kwa watu kwa misingi iliyotajwa katika aya ya (3)(c);

(e) itatoa mapendekezo katika Bunge ikijumuisha mapendekezo ya miswada kwa ajili ya kulinda, kusawazisha fursa na kuimarisha ustawi wa makundi yaliyotajwa katika aya ya (3)(c); na

(f) itatathmini shughuli na uendeshaji wa idara za serikali na asasi zilizoundwa kwa mujibu wa sheria zote kadri inavyohusiana na haki pamoja na ustawi wa watu waliotengwa kwa misingi iliyotajwa katika aya ya (3)(c).

(4) Kamati ya Mshikamano wa Kitaifa na Fursa Sawa itakayoundwa mara tu baada ya uchaguzi mkuu itahudumu kwa muda wa miaka mitatu ya kalenda na Kamati itakayoundwa baada yake itahudumu kwa muda uliosalia wa muhula wa Bunge hilo.

**Kamati ya Utangazaji wa Shughuli za Bunge na Maktaba**

**212D.** (1) Kutakuwa na Kamati itakayoitwa Kamati ya Utangazaji wa Shughuli za Bunge na Maktaba.

(2) Kamati itakuwa na Mwenyekiti na Wajumbe wengine wasiozidi ishirini.

(3) Majukumu ya Kamati hii yatakuwa—

(a) kushughulikia na kuripoti kuhusu masuala yote yanayohusiana na utangazaji wa shughuli za Bunge la Taifa;

(b) Kulishauri Bunge la Taifa kuhusu masuala yanayohusiana na ushirikishwaji wa umma;

(c) kuandaa ripoti na kutoa mapendekezo kwa Bunge la Taifa ikijumuisha sheria zinazopendekezwa kuhusu masuala yanayohusiana na utangazaji wa shughuli za Bunge la Taifa;

(d) kupendekeza na kushauri Bunge la Taifa kuhusu masuala yanayohusiana na maktaba, machapisho na huduma za utafiti katika Bunge, ikijumuisha kuboresha huduma za maktaba na utafiti; na

(e) kuwasaidia Wabunge katika kutumia huduma za maktaba na huduma za utafiti, ikijumuisha matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano.

(4) Kamati haitashughulikia masuala yanayohusiana na ununuzi wa vifaa au huduma za utangazaji, maktaba au huduma za utafiti, au suala lolote linalohusiana na jukumu la Tume ya Huduma za Bunge.

## Kamati za Pamoja za Bunge

### Uteuzi wa Kamati za Pamoja

**213.** (1) Kamati ambazo masharti ya Kanuni hii yatatumika zitaitwa Kamati za Pamoja za Bunge.

(2) Kamati za Pamoja za Bunge zitakuwa zile ambazo zimeorodheshwa katika Nyongeza ya Nne na zitakuwa na idadi ya Wajumbe kutoka Bunge la Taifa inayolingana na idadi ya Maseneta walioteuliwa au watakaoteuliwa na Seneti ili kuunda Kamati hiyo.

(3) Wabunge watakaohudumu kwenye Kamati ya Pamoja watateuliwa na Kamati ya Kuteua Wajumbe wa Kamati kwa kushauriana na Vyama Bunge, Vyama visivyokuwa Vyama Bunge na Wabunge Huru mwanzoni mwa muhula wa Bunge.

(4) *(imefutwa)*.

(5) Isipokuwa kama Bunge la Taifa litaamua vinginevyo, Mjumbe atakayeteuliwa kuhudumu kwenye Kamati ya Pamoja mwanzoni mwa muhula wa Bunge au wakati mwingine wowote wa muhula wa Bunge atahudumu kwa muhula wa Bunge hilo, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 176 (Kuondolewa kwa mjumbe kwenye Kamati).

(6) Isipokuwa pale ambapo uamuzi kwenye Kamati ya Pamoja umefikiwa kwa makubaliano, kura yoyote itakayopigwa itapigwa kwa kutenganisha wajumbe kutoka Bunge la Taifa na wale wa Seneti.

**214.** (*imefutwa*).

**215.** (*imefutwa*).

## Kamati za Kiidara

### Uteuzi na wajibu wa Kamati za Kiidara

**216.** (1) Kutakuwa na Kamati zitakazoitwa Kamati za Kiidara ambazo wajumbe wake—

(a) watateuliwa na Kamati ya Kuteua Wajumbe wa Kamati ikishauriana na vyama Bunge, Vyama visivyokuwa Vyama Bunge na Wabunge Huru mwanzoni mwa muhula wa kila Bunge; na

(b) hawatazidi wajumbe kumi na watano.

(2) Isipokuwa kama Bunge la Taifa litaamua vinginevyo, Mbunge atakayeteuliwa kwenye Kamati ya Kiidara mwanzoni mwa muhula wa Bunge au wakati mwingine wa muhula atahudumu kwenye Kamati hiyo kwa muhula wa Bunge hilo, ikizingatia Kanuni ya 176 (*Kuondolewa kwa mjumbe kwenye Kamati*).

(3) Isipokuwa kama Bunge la Taifa litaelekeza vinginevyo, Kamati za Kiidara na masuala yaliyokabidhiwa kila Kamati yatakuwa kama inavyobainishwa kwenye Nyongeza ya Pili.

(4) Wajibu wa Kamati za Kiidara kuhusiana na masuala yaliyokabidhiwa kwa mujibu wa Nyongeza ya Pili ya Kanuni hizi utatekelezwa tu kwa kuzingatia mipaka iliyowekwa kwenye Sehemu ya Kwanza ya Nyongeza ya Nne ya Katiba.

(5) Majukumu ya Kamati ya Kiidara yatakuwa—

(a) kupeleleza, kuchunguza na kuripoti masuala yote yanayohusu wajibu, usimamizi, shughuli, utawala, uendeshaji na makadirio ya wizara na idara inazozisimamia;

(b) kudurusu mipango na malengo ya sera za wizara na idara na mafanikio ya utekelezwaji wake;

(ba) kufuatilia na kuripoti utekelezaji wa bajeti ya taifa kuhusu masuala inayoyasimamia, kila robo mwaka;

(c) kudurusu na kuhakiki miswada yote iliyokabidhiwa kwake;

(d) kudurusu, kutathmini na kuchanganua mafanikio ya wizara na idara inazozisimamia yakikadiriwa kwa kuzingatia matokeo yake ikilinganishwa na malengo yaliyowekwa;

(e) kupeleleza na kuchunguza masuala yote yanayohusu wizara na idara inazozisimamia kadri itakavyochukuliwa kuwa muhimu na kama itakavyoelekezwa na Bunge la Taifa;

(f) kutathmini na kutoa ripoti kuhusu uteuzi wote ambao Katiba au sheria yoyote inahitaji Bunge la Taifa kuidhinisha, isipokuwa uteuzi uliotajwa kwa mujibu wa Kanuni ya 204 (*Kamati ya Uteuzi*);

(fa) kutathmini mikataba, makubaliano na maagano;

(g) kutoa ripoti na mapendekezo kwa Bunge la Taifa mara kwa mara kadri itakavyowezekana, ikijumuisha mapendekezo ya sheria;

(h) (*imefutwa*).

(i) kushughulikia ripoti za Tume na Ofisi Huru zilizowasilishwa katika Bunge la Taifa kwa mujibu wa Ibara ya 254 ya Katiba; na

(j) kutathmini masuala yoyote yatakayoibuliwa na Wabunge kuhusu jambo linalohusiana na wajibu wake.

(6) Kiongozi wa Chama cha walio Wengi, kwa kushauriana na Spika, ataamua mpangilio wa Mawaziri kufika mbele ya Kamati ili kujibu maswali yaliyoulizwa kwa mujibu wa aya ya (5)(j).

(7) Kufuatia ombi la Kiongozi wa Chama cha walio Wengi, Spika anaweza kubadilisha mpangilio utakaofuatwa kwenye kamati kwa kushughulikia maswali yaliyoulizwa kwa mujibu wa aya ya (5)(j) au kuahirisha swali lililopangwa kujibiwa.

(8) Endapo Chama cha walio Wachache ndicho kinachounda serikali ya taifa, majukumu kwa mujibu wa aya ya (6) na (7) yatatekelezwa na Kiongozi wa Chama cha walio Wachache.

**Kamati ya Kuratibu Shughuli za Kamati**

**217.** (1) Kutakuwa na kamati itakayoitwa Kamati ya Kuratibu Shughuli za Kamati ambayo itakuwa na Naibu Spika kama Mwenyekiti, Mjumbe wa Kwanza wa Jopo la Mwenyekiti atakayekuwa Makamu Mwenyekiti, na Wenyekiti wa Kamati zote za Bunge la Taifa.

(2) Kamati ya Kuratibu Shughuli za Kamati—

(a) itaongoza na kuratibu uendeshaji, sera na wajibu ya Kamati zote;

(b) itajadili na kutenga bajeti za kila mwaka za uendeshaji wa shughuli za Kamati;

(c) itatathmini mipango ya kamati zote, ikijumuisha mahitaji ya kusafiri na kufanya mikutano nje ya maeneo ya Bunge;

(d) itahakikisha kwamba Kamati zinawasilisha ripoti zinazohitajika kwa mujibu wa Kanuni hizi;

(e) itaamua kamati itakayoshughulikia au zitakazoshughulikia suala lolote kadri itakavyohitajika; na

(f) itatoa ushauri kuhusu kazi na wajibu wa kamati kadri itakavyoona inafaa.

(3) Kamati ya Kuratibu Shughuli za Kamati itatathmini ripoti za kamati ambazo hazijashughulikiwa na Bunge la Taifa na kutoa ripoti katika Bunge la Taifa kuhusu tathmini ya ripoti hizo.

**Kamati kujikita katika Wajibu**

**218.** (1) Isipokuwa kama ilivyoelezwa bayana katika Kanuni hizi, hakuna suala litakalopelekwa kwenye kamati ila kupitia Hoja iliyoidhinishwa baada ya arifa kutolewa.

(2) Bila kuzingatia aya ya (1), Spika, katika hali za kipekee na kufuatia ombi la Mbunge, anaweza kukabidhi suala kwa Kamati.

## SEHEMU YA XXIII- ARDHILHALI ZA UMMA

**Maana ya Ardhilhali**

**219.** Kwa ajili ya sehemu hii isipokuwa Kanuni ya 230 (*Ardhilhali ya kumwondoa mjumbe wa Tume au ofisa wa Ofisi Huru*), ardhilhali ina maana ya ombi rasmi la kimaandishi kwa Bunge la Taifa kwa mujibu wa Ibara ya 37 au ya 119 ya Katiba kutoka kwa mwananchi akiomba Bunge la Taifa kushughulikia suala lililo katika wajibu wa Bunge la Taifa kama ilivyobainishwa kwenye Ibara ya 94 na 95 ya Katiba, ikijumuisha kutunga, kurekebisha au kufuta sheria yoyote.

**Kuwasilishwa kwa Ardhilhali**

**220.** (1) Ardhilhali kwa Bunge la Taifa —

(a) italetwa kwa Katibu na mwenye ardhilhali na kuripotiwa katika Bunge la Taifa na Spika; au

(b) itawasilishwa na Mbunge kwa niaba ya mwenye ardhilhali, kwa ruhusa ya Spika.

(2) Bila kuzingatia aya ya 1 (b), Mbunge hastahili kuwasilisha ardhilhali kwa niaba yake mwenyewe.

(3) Katibu, katika muda usiozidi siku saba baada ya kupokea ardhilhali, ataihakiki kwa ajili ya kuthibitisha iwapo imekidhi vigezo vinavyohitajika kwa mujibu wa Kanuni hizi na sheria.

(4) Pale ambapo Katibu atabaini kuwa ardhilhali haikidhi vigezo kwa mujibu wa aya ya (3), anaweza kutoa maelekezo yanayofaa kwa ajili ya kuhakikisha kwamba ardhilhali hiyo inarekebishwa ili kukidhi masharti ya aya hiyo.

(5) Iwapo Katibu ameridhika kwamba ardhilhali imekidhi vigezo vinavyohitajika kwa mujibu wa aya ya (3), ataituma kwa Spika ili iwasilishwe katika Bunge la Taifa.

(6) Pale ambapo ardhilhali imeletwa katika Bunge la Taifa kuhusu suala ambalo ni wajibu wa Seneti, Katibu ataituma ardhilhali hiyo kwa Katibu wa Seneti.

**Ardhilhali ya Mswada Binafsi**

**221.** Ardhilhali ya Mswada Binafsi itashughulikiwa kwa mujibu wa Sehemu ya XX (*Miswada Binafsi*) ya Kanuni hizi.

**Arifa ya nia ya kuwasilisha Ardhilhali**

**222.** Mbunge atampa Katibu arifa ya siku mbili za vikao kuhusu nia yake ya kuwasilisha Ardhilhali na Katibu atatathmini Ardhilhali hiyo na kuhakikisha kwamba imewasilishwa kwa namna, muundo na maudhui yanayohitajika katika Kanuni hizi.

**Muundo wa Ardhilhali**

**223.** (1) Ardhilhali itakuwa na muundo ulioelezwa katika Nyongeza ya Tatu na—

(a) itaandikwa kwa mkono, kupigwa chapa au taipu;

(b) itaandikwa kwa Kiingereza au Kiswahili na katika lugha ya heshima, ya staha na isiyoudhi;

(c) haitakuwa imefutwafutwa au kuwa na maandishi baina ya mistari katika matini yake;

(d) itaelekezwa kwa Bunge la Taifa;

(e) anwani yake itaandikwa katika kila ukurasa iwapo ina zaidi ya ukurasa mmoja;

(f) itaeleza iwapo juhudi zozote zimefanywa ili suala hilo kushughulikiwa na asasi husika kwa lengo la kulitatua na iwapo asasi hiyo imetoa jibu lolote au kama jibu lililotolewa haliridhishi;

(g) itaeleza iwapo masuala ambayo yamo kwenye Ardhilhali yanasubiri uamuzi wa mahakama au asasi yoyote ya kikatiba au ya kisheria;

(h) itahitimishwa kwa ombi wazi, linalofaa na la heshima linalobainisha dhahiri madhumuni mahususi ya mwenye au wenye Ardhilhali kuhusiana na suala linalohusika;

(i) kwa mujibu wa aya ya (m), itakuwa na majina, anwani au njia nyingine za mawasiliano, nambari za vitambulisho, saini au alama ya kidole gumba cha mwenye Ardhilhali au, kila mwenye Ardhilhali iwapo ni zaidi ya mmoja;

(j) itakuwa na saini au alama za kidole gumba pekee, kadri itakavyokuwa, na anwani na nambari za vitambulisho zilizoandikwa moja kwa moja kwenye Ardhilhali na wala sio za kupachikwa au zilizohamishiwa hapo;

(k) haitaambatishwa barua, hati za viapo au nyaraka nyingine;

(l) pale ambapo ni Ardhilhali inayowasilishwa na Mbunge kwa niaba ya mwenye Ardhilhali, iwe imetiwa saini na Mbunge anayeiwasilisha; na

(m) iwe imetiwa saini na mwenye Ardhilhali au iwapo hawezi kutia saini, iwe imetiwa saini na shahidi mbele ya mwenye Ardhilhali ambaye ataweka alama yake kwenye Ardhilhali.

(2) Licha ya aya ya (1)(k), mwenye Ardhilhali—

(a) ataambatisha ushahidi wa juhudi zilizofanywa ili masuala yanayoibuliwa kwenye Ardhilhali yashughulikiwe na asasi husika kwa ajili ya aya ya (1)(f); na

(b) pale ambapo masuala yangali kortini, ataambatisha ushahidi wa kusikilizwa au uamuzi kwa ajili ya aya ya (1)(g).

**224.** *(imefutwa)*.

**Uwasilishaji wa Ardhilhali**

**225.** (1) Orodha ya Ardhilhali zitakazowasilishwa au kuripotiwa katika kikao cha Bunge la Taifa itaambatishwa kwenye Ratiba ya Shughuli ya siku ikionyesha mpangilio utakaofuatwa wakati wa kuziwasilisha au kuziripoti.

(2) Shughuli ya "Ardhilhali" itakaposomwa, Spika—

(a) atamuagiza Mbunge awasilishe Ardhilhali katika Bunge la Taifa, ikiwa Ardhilhali hiyo iliwasilishwa na Mbunge; au

(b) ataripoti Ardhilhali katika Bunge la Taifa, ikiwa iliwasilishwa kupitia kwa Katibu.

(3) Mbunge anayewasilisha Ardhilhali atasoma Ardhilhali hiyo lakini atajikita kwenye maudhui ya ombi, tuhuma zilizomo na idadi ya saini zilizoambatishwa.

(4) Mbunge aliyewasilisha Ardhilhali, ataiweka Ardhilhali hiyo kwenye Meza bila kulihoji Bunge la Taifa.

(5) Mbunge anayewasilisha Ardhilhali hataongea kwa zaidi ya dakika tano isipokuwa kwa ruhusa ya Spika.

**Maoni kuhusu Ardhilhali**

**226.** Spika anaweza kuruhusu maoni, mapendekezo au ufafanuzi kuhusu Ardhilhali iliyowasilishwa au kuripotiwa na muda utakaotumika kwa ajili hiyo hautazidi dakika thelathini.

**Ardhilhali kukabidhiwa Kamati**

**227.** (1) Kila Ardhilhali itakayowasilishwa au kuripotiwa kwa mujibu wa Sehemu hii itakabidhiwa Kamati ya Ardhilhali za Umma.

(2) Kila mara Kamati ya Ardhilhali za Umma inapokabidhiwa Ardhilhali, itahitajika kumjibu mwenye Ardhilhali katika muda usiozidi siku tisini za kalenda tangu Ardhilhali hiyo kukabidhiwa Kamati kupitia ripoti kwa mwenye au wenye Ardhilhali na kuwekwa kwenye Meza ya Bunge la Taifa.

(2A) Kamati ya Ardhilhali za Umma inaweza kupendekeza kwamba ripoti ya Ardhilhali ijadiliwe kwenye Bunge la Taifa.

(3) Katibu, katika muda usiozidi siku kumi na tano za uamuzi wa Bunge la Taifa, atamuarifu mwenye Ardhilhali kwa maandishi kuhusu uamuzi wa Bunge la Taifa kuhusu Ardhilhali yake.

**Nakala za majibu**

**228.** Katibu atawatumia wenye Ardhilhali nakala za majibu alizopokea kwa mujibu wa Kanuni ya 227 (*Ardhilhali kukabidhiwa Kamati*).

**Sajili ya Ardhilhali**

**229.** (1) Katibu atahifadhi sajili ambamo kutarekodiwa Ardhilhali zote na nyaraka zilizoambatishwa na maamuzi ya Bunge la Taifa.

(2) Sajili ya Ardhilhali kwa mujibu wa aya ya (1) itakuwa wazi kwa umma saa za kazi.

## SEHEMU YA XXIIIA — ARDHILHALI YA KUMWONDOA MJUMBE WA TUME AU OFISI HURU

**Ardhilhali ya kumwondoa Mamlakani Mjumbe wa Tume au ofisa wa Ofisi Huru**

**230.** (1) Pamoja na kufuata masharti ya aya ya (a), (b), (c), (d), (h), (i), (j), (l) na (m) ya Kanuni ya 223 (*Muundo wa Ardhilhali*), Ardhilhali kwa Bunge la Taifa ya kutaka kumwondoa mamlakani mjumbe wa Tume au ofisa wa Ofisi Huru kwa mujibu wa Ibara ya 251 ya Katiba—

(a) italazimika—

(i) kuonyesha sababu zilizoorodheshwa katika Ibara ya 251(1) ya Katiba ambayo mjumbe huyo wa Tume au ofisa wa Ofisi Huru amezikiuka;

(ii) kueleza kwa usahihi vifungu vya Katiba au sheria nyingine yoyote ambayo inadaiwa kukiukwa pale ambapo sababu zilizoorodheshwa katika aya ya 1(a)(i) zinahusiana na ukiukaji wa Katiba au sheria;

(iii) kuonyesha uhusiano wa moja kwa moja baina ya mjumbe au ofisa huyo na madai yaliyotolewa ili kumwondoa mamlakani; na

(b) inaweza kuambatisha hati za viapo au nyaraka nyingine.

(2) Aya ya (1), (3), (4) na (5) ya Kanuni ya 220 (*Kuwasilishwa kwa Ardhilhali*), Kanuni ya 222 (*Arifa ya Nia ya kuwasilisha Ardhilhali*), Kanuni ya 225 (*Uwasilishaji wa Ardhilhali*), na Kanuni ya 226 (*Maoni kwa Ardhilhali*), zitatumika kwa Ardhilhali kwa Bunge la Taifa kumwondoa mamlakani mjumbe wa Tume kwa mujibu wa Ibara ya 251 ya Katiba.

(3) Kila Ardhilhali inayowasilishwa au kuripotiwa kwa mujibu wa Kanuni hii itakabidhiwa Kamati ya Kiidara inayohusika.

(4) Baada ya kupokea Ardhilhali kwa mujibu wa aya ya (3), Kamati ya Kiidara inayohusika itachunguza suala hilo na, katika muda usiozidi siku kumi na nne, itaripoti katika Bunge la Taifa iwapo Ardhilhali inabainisha sababu za kumwondoa mamlakani mjumbe wa Tume au ofisa wa Ofisi Huru kwa mujibu wa Ibara ya 251(a) ya Katiba.

(5) Katika muda usiozidi siku kumi kufuatia kuwasilishwa kwa ripoti ya kamati kwa mujibu wa aya ya (4), Bunge la Taifa litaamua iwapo Ardhilhali inabainisha au haibainishi sababu za kumwondoa mamlakani mjumbe wa Tume au ofisa wa Ofisi Huru kwa mujibu wa Ibara ya 251(a) ya Katiba.

(6) Pale ambapo Bunge la Taifa litaamua kwamba Ardhilhali imebainisha sababu za kumwondoa mamlakani mjumbe wa Tume au ofisa wa Ofisi Huru, Spika, katika muda usiozidi siku saba kufuatia uamuzi huo, atapeleka uamuzi pamoja na Ardhilhali kwa Rais.

(7) Ushughulikiaji wa Ardhilhali kwa mujibu wa Kanuni hii hautatanguka muhula wa Bunge utakapoisha.

## SEHEMU YA XXIV – UTARATIBU WA MASUALA YA FEDHA

### Udhibiti wa masuala mahususi ya kifedha

**231.** (1) Iwapo kwa maoni ya Spika, Hoja inahusu suala lililorejewa katika fasili ya "Mswada unaohusu masuala ya fedha" kwa mujibu wa Ibara ya 114 ya Katiba, suala hilo linaweza kushughulikiwa na Bunge la Taifa kwa kuzingatia mapendekezo ya Kamati ya Bajeti na Uidhinishaji wa Matumizi kwa kutilia maanani maoni ya Waziri anayehusika na masuala ya fedha.

(2) "Mswada unaohusu masuala ya fedha" kama ilivyoelezwa katika Ibara ya 114 ya Katiba ina maana ya Mswada, isipokuwa Mswada wa Kugawa Mapato au Mswada wa Kutenga Mapato

kwa Kaunti ambayo imetajwa katika Ibara ya 218 ya Katiba, wenye vipengele vinavyohusu—

(a) kodi;

(b) kutoza ada kwenye fedha za umma au kubadilisha au kufuta ada hizo;

(c) kutumia, kupokea, kuhifadhi, kuwekeza au kutoa pesa za umma;

(d) kuchukua au kudhamini mkopo wowote au ulipaji wa mkopo; au

(e) masuala mengine yanayotokana na masuala hayo.

(3) Katika aya ya (2), "kodi", "pesa za umma", na "mkopo", hazijumuishi kodi, pesa za umma au mkopo unaochukuliwa na serikali za kaunti.

**Kuwasilishwa kwa Taarifa ya Sera ya Bajeti**

**232.** (1) Kila mwaka na isiwe baada ya tarehe 15 Februari Waziri anayehusika na masuala ya fedha atawasilisha katika Bunge la Taifa Taarifa ya Sera ya Bajeti na itachukuliwa kuwa imewasilishwa kwenye Meza.

(2) Taarifa ya Sera ya Bajeti itajumuisha—

(a) tathmini ya hali ya uchumi kwa wakati huo na mwelekeo wa hali ya kifedha kwa kipindi cha muda wastani ikijumuisha makisio ya hali pana ya uchumi;

(b) mwelekeo wa hali ya kifedha kuhusu mapato ya Serikali, matumizi na ukopaji kwa mwaka wa fedha unaofuata na katika kipindi cha muda wastani;

(c) mapendekezo ya ukomo wa matumizi kwa serikali ya taifa, ikijumuisha matumizi ya Bunge na Mahakama na hawilisho kwa serikali za kaunti;

(d) kanuni za uwajibikaji wa kifedha na malengo ya kifedha katika kipindi cha muda wastani ikijumuisha ukomo wa deni la jumla la mwaka;

(e) jumla ya rasilimali zitakazotengwa kwa ajili ya kila mpango na mradi ndani ya sekta, Wizara au idara katika kipindi kilichotajwa kwenye aya ndogo ya (a) ikibainisha matokeo yanayotarajiwa kutoka kwa kila mpango au mradi katika kipindi hicho;

(f) orodha ya miradi inayopendekezwa katika kipindi kilichotajwa kwenye aya ya (2)(a) ikitaja ukomo wa matumizi yake ambao unawiana na jumla ya ukomo uliopendekezwa kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

(3) Taarifa ya Sera ya Bajeti itaeleza vigezo vitakavyotumika kutenga au kugawa rasilimali za umma zilizopo kwa mipango na miradi mbalimbali.

(4) *(imefutwa)*.

(5) Baada ya Taarifa ya Sera ya Bajeti kuwasilishwa kwenye Meza, taarifa hiyo itakabidhiwa kila Kamati ya Kiidara kwa ajili ya kuishughulikia na kutoa mapendekezo kwa Kamati ya Bajeti na Uidhinishaji wa Matumizi, katika muda usiozidi siku saba baada ya kupokea taarifa hiyo.

(6) *(imefutwa)*.

(7) Katika muda usiozidi siku kumi na nne baada ya kuwasilishwa kwa Taarifa ya Sera ya Bajeti katika Bunge la Taifa, Kamati ya Bajeti na Uidhinishaji wa Matumizi itawasilisha ripoti kwenye Meza ili ishughulikiwe kwa mujibu wa masharti ya kifungu cha 25(7) cha Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma.

(8) Pamoja na mapendekezo ya kamati, ripoti itakayowasilishwa kwa mujibu wa aya ya (7) itakuwa na—

(a) jedwali linaloonyesha mgao wima wa rasilimali kati ya serikali ya taifa na serikali za kaunti;

(b) ukomo wa jumla wa rasilimali ambao umependekezewa kwa ajili ya serikali ya taifa, Mahakama na Bunge;

(c) *(imefutwa)*.

(9) Idhini ya Bunge la Taifa kwa hoja kuhusu ripoti ya Kamati ya Bajeti na Uidhinishaji wa Matumizi kwenye Taarifa ya Sera ya Bajeti itakuwa ndio Uamuzi wa Bunge la Taifa utakaoorodhesha jumla ya makisio ya mapato na ukopaji, mgao wima wa rasilimali kati ya serikali ya taifa na serikali za kaunti, ukomo uliopendekezewa serikali ya taifa, Mahakama na Bunge na itaonyesha jumla ya mgao kwa kila Fungu na migao kwa kila mpango katika mwaka wa fedha unaohusika.

(10) Uamuzi wa Bunge la Taifa kuhusu Taarifa ya Sera ya Bajeti utatumika kama msingi wa mapendekezo ya makadirio ya matumizi kwa mwaka wa fedha unaofuata na kipindi cha muda wastani.

**Kuwasilishwa kwa Mkakati wa Kudhibiti Deni**

**232A.** (1) Kila mwaka na isiwe baada ya tarehe 15 Februari Waziri anayehusika na masuala ya fedha atawasilisha katika Bunge la Taifa Mkakati wa Kudhibiti Deni na itachukuliwa kuwa umewasilishwa kwenye Meza.

(2) Mkakati wa Kudhibiti Deni utajumuisha—

(a) jumla ya deni lote kufikia tarehe ya kuwasilisha Mkakati;

(b) vyanzo vya mikopo iliyotolewa kwa serikali ya taifa na aina ya dhamana zilizotolewa na serikali ya taifa;

(c) hatari kuu zinazohusiana na mikopo hiyo na dhamana zake;

(d) chukulizi zilizo msingi wa Mkakati wa Kudhibiti Deni; na

(e) uchanganuzi wa uhimilivu wa kiwango cha deni, ikiwemo deni halisi na linalotarajiwa.

(3) Baada ya Mkakati wa Kudhibiti Deni kuwasilishwa kwenye Meza, Mkakati huo utakabidhiwa Kamati ya Deni la Umma na Ubinafsishwaji.

(4) Katika muda usiozidi siku kumi baada ya kuwasilishwa kwa Mkakati wa Kudhibiti Deni, Kamati ya Deni la Umma na Ubinafsishwaji itawasilisha ripoti kwenye Meza ili ishughulikiwe.

(5) Ripoti ya Kamati ya Deni la Umma na Ubinafsishwaji kwa mujibu wa aya ya (4) itajumuisha—

(a) jedwali linaloonyesha deni la ndani na la nje ya nchi ikiwemo dhamana, kufikia tarehe ya Mkakati;

(b) tathmini ya hatari kuu zinazohusishwa na mikopo na dhamana zilizopo.

(c) tathmini ya uhimilivu wa kiwango cha deni, ikiwemo deni halisi na linalotarajiwa.

(d) pendekezo la Mkakati wa Kudhibiti Deni kwa mwaka wa fedha unaofuata na kipindi cha muda wastani; na

(e) pendekezo la ukomo mwafaka kuhusu mapendekezo ya mikopo ya ndani na ya nje ya nchi kwa mwaka wa fedha unaofuata na miaka miwili ya fedha inayofuata.

(6) Bunge la Taifa litashughulikia ripoti ya Kamati ya Deni la Umma na Ubinafsishwaji kuhusu Mkakati wa Kudhibiti Deni kabla ya kushughulikia ripoti ya Kamati ya Bajeti na Uidhinishaji wa Matumizi kuhusu Taarifa ya Sera ya Bajeti.

(7) Uamuzi wa Bunge la Taifa kwa ripoti ya Kamati ya Deni la Umma na Ubinafsishwaji kuhusu Mkakati wa Kudhibiti Deni utakuwa Uamuzi wa Bunge la Taifa kuhusu ukomo mwafaka kwa mapendekezo ya mikopo ya ndani ya nchi na ya nje ya nchi kwa mwaka wa fedha unaofuata.

(8) Uamuzi wa Bunge la Taifa kuhusu Mkakati wa Kudhibiti Deni—

(a) utakuwa ukomo mwafaka kwa mapendekezo ya mikopo ya ndani ya nchi na ya nje ya nchi kwa mwaka wa fedha unaofuata; na

(b) utakuwa msingi wa kuidhinishwa kwa Ripoti ya Kamati ya Bajeti na Uidhinishaji wa Matumizi kuhusu Taarifa ya Sera ya Bajeti.

**Kushughulikia Mswada wa Kugawa Mapato**

**233.** (1) Kila mwaka, isiwe baada ya tarehe 10 Machi, Mswada wa Kugawa Mapato utawasilishwa katika Bunge la Taifa na utagawa mapato yaliyokusanywa na serikali ya taifa kati ya serikali ya taifa na serikali za kaunti kwa mujibu wa Katiba.

(2) Mswada unaohitajika kwa mujibu wa aya ya (1) utaambatishwa maelezo yatakayobainisha—

(a) ufafanuzi kuhusu mgao wa mapato kama ilivyopendekezwa na Mswada;

(b) tathmini ya Mswada kuhusiana na vigezo vilivyotajwa katika Ibara ya 203(1) ya Katiba; na

(c) muhtasari wa kiwango cha kutozingatia mapendekezo ya Tume ya Ugavi wa Mapato pamoja na maelezo ya kila hali ya kutozingatiwa huko.

(3) Bunge la Taifa litashughulikia Mswada wa Kugawa Mapato katika muda usiozidi siku kumi za vikao baada ya kukabidhiwa Mswada huo kwa ajili ya kuupitisha ukiwa na marekebisho au bila marekebisho.

(3A) Katika kushughulikia Mswada wa Kugawa Mapato, Bunge la Taifa litazingatia mapendekezo yoyote yaliyowasilishwa kwa Tume ya Ugavi wa Mapato, kwa mujibu wa Ibara ya 205 ya Katiba.

(4) Mswada wa Kugawa Mapato, ukishapitishwa na Bunge la Taifa, utapelekewa Seneti kwa mujibu wa Kanuni ya 142 (*Maafikiano na Seneti*).

**Kushughulikia Mswada wa Kutenga Mapato kwa Kaunti**

**234.** (1) Kila wakati Mswada wa Kutenga Mapato kwa Kaunti unapowasilishwa katika Bunge la Taifa, Bunge la Taifa litaushugulikia Mswada huo katika muda usiozidi siku kumi na masharti ya Ibara ya 111 ya Katiba yatatumika.

(2) Katika kushughulikia Mswada wa Kutenga Mapato kwa Kaunti, Bunge la Taifa litazingatia mapendekezo yaliyowasilishwa na Tume ya Ugavi wa Mapato kwa mujibu wa Ibara ya 205 ya Katiba.

**Uwasilishaji wa Makadirio ya Bajeti na Kukabidhiwa Kamati**

**235.** (1) Waziri anayehusika na masuala ya Fedha, Ofisa Masuuli wa Tume ya Huduma za Bunge na Msajili Mkuu wa Mahakama watawasilisha katika Bunge la Taifa Makadirio ya Bajeti na hati nyingine zinazohitajika kisheria zinazohusiana na serikali ya taifa, Mahakama na Bunge isiwe baada ya tarehe 30 Aprili.

(2) Makadirio ya bajeti yanayotajwa katika aya ya (1) yatajumuisha makadirio ya matumizi kutoka kwenye Hazina ya Usawazishaji kwa mujibu wa Ibara ya 221(2) ya Katiba.

(3) Makadirio ya Bajeti na nyaraka zinazohusu makadirio hayo zilizowasilishwa kwa mujibu wa aya ya (1) na (2) yatawasilishwa kwenye Meza katika muda usiozidi siku tatu baada ya kuwasilishwa kwake.

(4) Baada ya kuwasilishwa kwenye Meza —

(a) Makadirio ya Bajeti kwa mujibu wa aya ya (1) yatakabidhiwa kila Kamati ya Kiidara kwa ajili ya kuyashughulikia na kutoa mapendekezo kwa Kamati ya Bajeti na Uidhinishaji wa Matumizi, katika muda usiozidi ya siku ishirini na moja baada ya kupokea Makadirio hayo;

(b) Makadirio kwa mujibu wa aya ya (2) yatakabidhiwa Kamati ya Bajeti na Uidhinishaji wa Matumizi kwa

ajili ya kuyashughulikia na kutoa mapendekezo katika Bunge la Taifa pamoja na ripoti ya Kamati kwenye Makadirio ya Bajeti.

(5) Kamati ya Bajeti na Uidhinishaji wa Matumizi itajadili na kuhakiki Makadirio ya Bajeti na Makadirio ya Matumizi kutoka kwa Hazina ya Usawazishaji na kutoa mapendekezo katika Bunge la Taifa, ikizingatia mapendekezo ya Kamati za Kiidara, maoni ya Waziri anayehusika na masuala ya fedha pamoja na maoni ya umma.

(6) Pale ambapo Kamati inapendekeza mabadiliko yoyote au ugawaji upya katika Makadirio, Kamati ya Bajeti na Uidhinishaji wa Matumizi itajumuisha katika mapendekezo yake kwa mujibu wa aya ya (5) jedwali linaloonyesha mabadiliko au ugawaji upya unaopendekezwa kwa kila Fungu, Fungu Dogo, Mpango, Mradi, Matokeo Tarajiwa au Lengo.

**Kamati ya Ugavi wa Fedha**

**236.** Kamati ya Ugavi wa Fedha itakuwa ni Kamati ya Bunge Zima.

**Fasili ya siku**

**237.** Kwa ajili ya matumizi ya Sehemu hii, siku itachukuliwa kujumuisha kipindi chochote kisichozidi saa tatu kabla ya saa 7.00 mchana au muda usiozidi saa tatu kati ya saa 8.30 alasiri na saa 1.30 jioni au muda usiozidi saa tatu baada ya saa 1.30 jioni.

**238.** *(imefutwa)*.

**Kuingia katika hatua ya Kamati ya Ugavi wa Fedha**

**239.** Shughuli ya Kamati ya Ugavi wa Fedha inaposomwa, Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti na Uidhinishaji wa Matumizi au Mjumbe aliyeteuliwa na Kamati atatoa Hoja ***"Kwamba Bunge la Taifa liidhinishe Ripoti ya Kamati ya Bajeti na Uidhinishaji wa Matumizi kuhusu Makadirio ya Bajeti kwa***

***mwaka wa fedha wa …. na Makadiro ya Matumizi kutoka kwa Hazina ya Usawazishaji na migao kwa mafungu yanayohusika na mipango iliyoorodheshwa kwenye Nyongeza"*** kwa kufanyiwa mabadiliko kadri itakavyohitajika.

**Kushughulikia Makadirio kwenye Kamati ya Ugavi wa Fedha**

**240.** (1) Ripoti ya Kamati ya Bajeti na Uidhinishaji wa Matumizi kwa Makadirio ya Bajeti na Makadirio ya Matumizi kutoka kwa Hazina ya Usawazishaji itashughulikiwa kwenye Kamati ya Ugavi wa Fedha baada ya Hoja kutolewa ***"Kwamba Bunge la Taifa liidhinishe ripoti ya Kamati ya Bajeti na Uidhinishaji wa Matumizi kuhusu Makadirio ya Bajeti kwa mwaka wa fedha …. na Makadiro ya Matumizi kutoka kwa Hazina ya Usawazishaji na migao kwa mafungu yanayohusika na mipango iliyoorodheshwa kwenye Nyongeza"*** kwa kufanyiwa mabadiliko kadri itakavyohitajika.

(2) Mwenyekiti atapendekeza Hoja ili iamuliwe kwa kila Fungu au mpango.

(3) Katika kushughulikia Makadirio, Bunge la Taifa litazingatia maamuzi yake kwenye Taarifa ya Sera ya Bajeti na kuhakikisha kwamba—

(a) ongezeko la matumizi kwenye mgao uliopendekezwa limesawazishwa kwa kupunguza matumizi kwenye mgao mwingine uliopendekezwa; au

(b) punguzo lililopendekezwa kwenye matumizi linatumika kupunguza nakisi katika Bajeti.

(4) Rekebisho kwa Fungu lolote kwa ajili ya kuongeza au kupunguza fedha zilizotengwa kwenye mpango wowote au fungu hilo linaweza kuwasilishwa tu kwa kuzingatia mapendekezo ya Kamati ya Bajeti na Uidhinishaji wa Matumizi.

(5) Rekebisho kwenye Kamati ya Ugavi wa Fedha linaweza kuwa kwa muundo wa Hoja ***"Kwamba Fungu …. liongezwe/***

***lipunguzwe kwa Shilingi …. (kuhusu mpango….)"*** au kwa namna itakayoidhinishwa na Spika.

(6) Rekebisho la kuondoa Fungu halitaruhusiwa na halitawekwa kwenye Ratiba ya Shughuli na badala yake, Mbunge anayekusudia kulitoa anaweza kupinga idhinisho la Fungu hilo.

(7) Pale ambapo Arifa ya marekebisho mawili au zaidi imetolewa ili kupunguza kipengele, kifungu kidogo au Fungu hilo hilo, marekebisho hayo yatawekwa kwenye Ratiba ya Shughuli na yatashughulikiwa kwa kuzingatia kiasi cha punguzo kilichopendekezwa, ambapo rekebisho linalopendekeza punguzo kubwa zaidi litapewa kipaumbele kwa kila hali na kiasi cha fedha kilichopunguzwa kuhusiana na Fungu lolote kinaweza kuhamishwa kwenda Fungu lingine ilimradi Fungu hilo liwe halijashughulikiwa.

(8) Mjadala kwa kila rekebisho utajikita katika kipengele, kifungu kidogo au Fungu linalohusika na baada ya rekebisho kwenye kipengele, kifungu kidogo au Fungu kukamilika, hakuna rekebisho au mjadala utakaoruhusiwa kuhusu kipengele au kifungu kidogo ambacho kimeshashughulikiwa katika Fungu hilo.

(9) Siku ya mwisho ya Siku Tengwa, ambayo itakuwa kabla ya tarehe 26 Juni, saa moja kabla ya muda wa kusitisha shughuli, Mwenyekiti atatoa Hoja ili mjadala wa kuidhinisha Fungu linaloshughulikiwa, na mara moja atatoa Hoja ziamuliwe kwa kila Fungu ambalo halijaidhinishwa na iwapo wakati huo Bunge la Taifa haliko kwenye Kamati ya Bunge Zima, Bunge la Taifa litaingia kwenye hatua ya kamati mara moja bila Hoja kutolewa, kwa ajili hiyo.

(10) Siku yoyote ambayo Mwenyekiti ameelekezwa na kanuni hii kutoa Hoja yoyote iamuliwe, ushughulikiaji wa shughuli ya Ugavi wa Fedha hautawahishwa kupitia Hoja ya kuahirisha Bunge la Taifa na Hoja ya kuahirisha mjadala unaohusiana na

shughuli hiyo haitatolewa, na shughuli hiyo haitasitishwa kwa mujibu wa Kanuni yoyote.

(11) Wakati ambapo marekebisho kuhusu Mafungu yameshughulikiwa, Mwenyekiti atapendekeza Hoja ***"Kwamba Bunge la Taifa liidhinishe Ripoti ya Kamati ya Bajeti na Uidhinishaji wa Matumizi kuhusu Makadirio ya Bajeti kwa mwaka wa fedha…. na Makadiro ya Matumizi kutoka kwa Hazina ya Usawazishaji na mgao kwa kila Fungu na mipango iliyoorodheshwa kwenye Nyongeza"*** kwa kufanyiwa mabadiliko kadri itakavyohitajika.

(12) Mjadala unapohitimishwa, Mwenyekiti atatoa Hoja iamuliwe na kamati iliyotajwa kwenye aya ya (11) na kuripoti kwa Bunge la Taifa mara moja.

**Kushughulikia Maamuzi ya Ugavi wa Fedha**

**240A.** (1) Ripoti au uamuzi wowote wa Kamati ya Matumizi utashughulikiwa kufuatia Hoja, ***"Kwamba, Bunge la Taifa likubaliane na uamuzi wa Kamati."***

(2) Hoja itakayotolewa kwa mujibu wa aya ya (1) itaamuliwa mara moja bila kuruhusu rekebisho, ahirisho au mjadala, isipokuwa kama Mbunge yeyote atakusudia kurekebisha au kuongeza kwenye uamuzi anaweza kupendekeza kuongeza mwishoni mwa Hoja maneno ***"kwa sharti kwamba uamuzi (kuhusu Fungu au mpango mahususi) lirejeshwe tena kwenye Kamati ya Ugavi wa Fedha."***

(3) Iwapo Hoja imekubalika pamoja na marekebisho ya Mbunge, uamuzi utarejeshwa kwenye Kamati ya Ugavi wa Fedha na Bunge la Taifa litarejea kwenye Kamati ya Ugavi wa Fedha mara moja au siku ambayo Spika ataamua ili kushughulikia uamuzi uliorejeshwa.

(4) Pale ambapo uamuzi wowote umerejeshwa kwenye Kamati ya Ugavi wa Fedha, Kamati itashughulikia

masuala yaliyorejeshwa pekee na suala lolote ambalo linaathiriwa moja kwa moja na masuala yaliyorejeshwa kwenye Kamati.

(5) Isipokuwa kwa mujibu wa aya ya (4) ya Kanuni hii, masharti ya aya ya (2) na (3) ya Kanuni hii yatatumika kuhusu uamuzi uliorejeshwa kwenye Kamati.

**Mswada wa Kuidhinisha Matumizi ya Fedha na Mswada wa Kuidhinisha Matumizi ya Fedha ya Hazina ya Usawazishaji**

**240B.** (1) Uamuzi wa Bunge la Taifa kwenye Makadirio ya Bajeti na Makadirio ya Matumizi kutoka kwa Hazina ya Usawazishaji utatumika kama msingi wa kuandaa Mswada wa Kuidhinisha Matumizi ya Fedha na Mswada wa Kuidhinisha Matumizi ya Fedha ya Hazina ya Usawazishaji.

(2) Baada ya makadirio ya bajeti kuidhinishwa, Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti na Uidhinishaji wa Matumizi atawasilisha katika Bunge la Taifa Mswada wa Kuidhinisha Matumizi ya Fedha na, iwapo itahitajika, Mswada wa Kuidhinisha Matumizi ya Fedha ya Hazina ya Usawazishaji.

(3) Bunge la Taifa litashughulikia marekebisho yoyote yatakayopendekezwa kwenye Mswada uliotajwa kwenye aya ya (1) kwa kuzingatia mapendekezo ya Kamati ya Bajeti na Uidhinishaji wa Matumizi baada ya kushauriana na kamati za kiidara zinazohusika.

(4) Bunge la Taifa litashughulikia na kupitisha Mswada wa Kuidhinisha Matumizi Fedha na isiwe baada ya tarehe 26 Juni kila mwaka.

(5) Baada ya kupitishwa kwa Mswada wa Kuidhinisha Matumizi ya Fedha, haraka iwezekanavyo, Katibu atathibitisha kwa maandishi marekebisho yoyote yaliyofanywa kwa Fungu au Mpango na ataonyesha ugawaji upya, nyongeza au mapunguzo yaliyofanywa na Bunge la Taifa kwa Fungu, Fungu Dogo, Mpango, Mradi, Matokeo Tarajiwa au Lengo

kumwezesha Waziri anayehusika na masuala ya fedha kuchapisha Makadirio ya mwisho yaliyoidhinishwa.

(6) Kufuatia kupitishwa kwa Sheria ya Kuidhinisha Matumizi ya Fedha, Kamati ya Bajeti na Uidhinishaji wa Matumizi itahakikisha kwamba ugawaji upya wowote, nyongeza au mapunguzo yaliyofanywa na Bunge la Taifa katika Makadirio kwa kila Fungu, Fungu Dogo, Mpango, Mradi, Matokeo Tarajiwa au Lengo yanajumuishwa kwenye vitabu vya bajeti vya mwisho ambavyo vitachapishwa tena.

**241.** *(imefutwa)*.

**Idhini ya kutoa Fedha**

**242.** (1) Kufuatia kuidhinishwa kwa Makadirio ya Bajeti na kabla ya Mswada wa Kuidhinisha Matumizi ya Fedha kupata kibali cha Rais, Bunge la Taifa linaweza kuidhinisha fedha zitolewe kwenye Hazina Kuu kulingana na Ibara ya 222 ya Katiba na, katika muda usiozidi siku saba baada ya idhini hiyo kutolewa, Spika wa Bunge la Taifa atawasilisha idhini hiyo kwa Waziri anayehusika na masuala ya fedha.

(2) Hoja ya kuomba idhini ya kutoa fedha kwenye Hazina Kuu kwa mujibu wa aya ya (1) itaitwa Idhini ya Kutoa Fedha na itatolewa siku yoyote kabla ya tarehe 30 Juni.

**Utaratibu wa Makadirio ya Ziada**

**243.** (1) Serikali ya taifa itawasilisha Bajeti ya Ziada kwa Bunge la Taifa kwa ajili ya kuidhinisha bajeti ya ziada ili kuhalalisha fedha ambazo zimetumika kwa mujibu wa Ibara ya 223 ya Katiba.

(2) Bajeti ya Ziada itajumuisha—

(a) taarifa inayoonyesha jinsi matumizi ya ziada yanavyohusiana na kanuni za uwajibikaji wa kifedha na malengo ya kifedha;

(b) nyongeza inayoonyesha orodha ya mipango au miradi inayoathiriwa na Bajeti ya ziada iliyopendekezwa;

(c) sababu na stakabadhi za kifedha kama ushahidi wa pesa zilizotumiwa;

(d) nyongeza tofauti kwa matumizi yaliyofanywa kwa mujibu wa Ibara ya 223 ya Katiba na ugawaji upya wowote uliofanywa katika Fungu lolote;

(e) nyongeza inayoonyesha pesa zilizotumiwa na sababu ya pesa hizo kutumiwa katika kila Fungu, Mpango au Mradi; na

(f) tarehe ambapo pesa hizo zilitolewa kwa mara ya kwanza.

(3) Utaratibu wa kuidhinisha Makadirio ya Bajeti kwa mujibu wa Kanuni ya 240 (*Kushughulikia Makadirio kwenye Kamati ya Ugavi wa Fedha*) na Kanuni ya 240A (*Kushughulikia Maamuzi ya Ugavi wa Fedha*) ukifanyiwa marekebisho kama itakavyohitajika, utatumika kuidhinisha Bajeti ya Ziada.

(3A) Ripoti ya Kamati ya Bajeti na Uidhinishaji wa Matumizi kwa Bunge la Taifa kuhusu Makadirio ya Ziada—

(a) itajumuisha tathmini ya uzingativu wa mapendekezo ya Makadirio ya Ziada kwa—

(i) masharti yaliyoorodheshwa katika Ibara ya 223 ya Katiba na sheria nyingine yoyote; na

(ii) kanuni na maadili ya fedha za umma kwa mujibu wa Ibara ya 201 ya Katiba;

(b) itakuwa na vipengele pekee vya pesa ambazo tayari zimetolewa na kutumiwa na Serikali ya Kitaifa kwa mujibu wa Ibara ya 223 ya Katiba; na

(c) itakuwa na nyongeza tofauti ya matumizi yaliyofanywa kwa mujibu wa Ibara ya 223 ya Katiba na ugawaji upya wowote wa kawaida uliofanywa katika fungu lolote na nyongeza ya fedha au maamuzi ya sera.

(3B) Aya ya (3A) itatumika kwa Kamati ya Kiidara inayotathmini Makadirio ya Ziada na kutoa mapendekezo kwa Kamati ya Bajeti na Uidhinishaji wa Matumizi kwa mujibu wa Kanuni ya 243(3).

(3C) Katibu atahifadhi sajili mahususi ya kurekodi maombi yoyote ya idhini yanayofanywa na Waziri anayehusika na fedha kwa mujibu wa Ibara ya 223 ya Katiba na atahakikisha maombi hayo yanawasilishwa katika Bunge la Taifa kwa muda unaofaa.

(4) Siku yoyote ambapo shughuli ya hatua ya Kamati ya Ugavi wa Fedha imewekwa kwenye Ratiba ya Shughuli, shughuli hiyo ianze na isiwe ni baada ya saa tatu kabla ya wakati wa kuahirisha kikao.

**244.** *(imefutwa)*.

**Kuidhinisha matumizi yanayozidi asilimia kumi**

**244A.** (1) Kwa kuzingatia masharti ya Ibara ya 223(5) ya Katiba, kufuatia ombi la Wizara inayohusika na Hazina ya Taifa na pendekezo la Kamati ya Bajeti na Uidhinishaji wa Matumizi, Bunge la Taifa linaweza kupitisha uamuzi kwa ajili ya kuidhinisha matumizi ya fedha yanayozidi asilimia kumi zaidi ya kiasi kilichoidhinishwa kwenye Sheria ya Kuidhinisha Matumizi ya Fedha kwa mwaka huo wa fedha.

(2) Kamati ya Bajeti na Uidhinishaji wa Matumizi itajiridhisha kwamba matumizi yanayopendekezwa kwa mujibu ya aya ya (1) yanahusu hali za kipekee.

**Mswada wa Kuidhinisha Matumizi ya Ziada ya Fedha**

**244B.** (1) Uamuzi wa Bunge la Taifa kuhusu Makadirio ya Nyongeza litakuwa msingi wa kuandaa Mswada wa Kuidhinisha Matumizi ya Ziada ya Fedha.

(2) Makadirio ya Ziada yanapoidhinishwa, Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti na Uidhinishaji wa Matumizi atawasilisha

katika Bunge la Taifa Mswada wa Kuidhinisha Matumizi ya Ziada ya Fedha ili ushughulikiwe.

(3) Utaratibu wa kuidhinisha Mswada wa Kuidhinisha Matumizi ya Fedha kwa mujibu wa Kanuni ya 240B (*Mswada wa Kuidhinisha Matumizi ya Fedha na Mswada wa Kuidhinisha Matumizi ya Fedha ya Hazina ya Usawazishaji*) ukifanyiwa marekebisho kadri itakavyowezekana, utatumika kuidhinisha Mswada wa Kuidhinisha Matumizi ya Ziada ya Fedha.

(4) Mswada wa Kuidhinisha Matumizi ya Ziada ya Fedha utakuwa na nyongeza itakayoonyesha–

(a) kiasi cha fedha kilichopangwa kutumika katika Sheria ya Matumizi ya Fedha; na

(b) kiasi halisi cha mabadiliko kinachopendekezwa kutokana na Makadirio ya Ziada yaliyoidhinishwa kwa mujibu wa Kanuni ya 243 (*Utaratibu wa Makadirio ya Ziada*) na Kanuni ya 244A (*Kuidhinisha matumizi yanayozidi asilimia kumi*).

**Kutangazwa kwa vidokezo vya Bajeti na mikakati ya Ukusanyaji mapato**

**244C.** (1) Waziri anayehusika na masuala ya Fedha atasoma vidokezo vya sera ya bajeti na mikakati ya ukusanyaji wa mapato kwa ajili ya serikali ya taifa kulingana na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma.

(2) Spika anaweza kutenga sehemu maalum katika Ukumbi kwa ajili ya kumruhusu Waziri anayehusika na masuala ya fedha kusoma vidokezo vya sera ya bajeti na mikakati ya ukusanyaji wa mapato.

(3) Waziri anaposoma vidokezo vya sera ya bajeti kwa mujibu wa aya ya (1) atasikilizwa bila kuulizwa swali au kuhitajika kutoa ufafanuzi.

(4) Siku ambayo vidokezo vya sera ya bajeti na mikakati ya ukusanyaji mapato itasomwa katika Bunge la Taifa, Waziri atawasilisha kwa Bunge la Taifa pendekezo la Mswada linaloonyesha mikakati ya ukusanyaji wa mapato ya serikali ya taifa pamoja na taarifa ya sera inayofafanua mikakati hiyo.

(5) Masharti ya Sheria ya Mamlaka na Haki ya Bunge yatatumika kwa Waziri aliyeruhusiwa katika Ukumbi kwa mujibu wa Sehemu hii.

**Kushughulikia Mswada wa Fedha**

**245.** (1) Baada ya Waziri kuwasilisha pendekezo la Mswada kwa Bunge la Taifa kwa mujibu wa Kanuni ya 244C (*Kutangazwa kwa vidokezo vya Bajeti na mikakati ya Ukusanyaji mapato*), Kamati ya Kiidara kuhusu Fedha na Mipango ya Taifa itawasilisha Mswada wa Fedha katika Bunge la Taifa kwa muundo wa pendekezo la Mswada lililowasilishwa na Waziri anayehusika na masuala ya fedha, pamoja na ripoti ya Kamati kuhusu Mswada huo.

(2) Mapendekezo yoyote yaliyofanywa na Kamati au kupitishwa na Bunge la Taifa kuhusu mapato—

(a) yatahakikisha kwamba jumla ya mapato yaliyokusanywa yanalingana na mfumo wa fedha ulioidhinishwa pamoja na Sheria ya Kugawa Mapato;

(b) yatazingatia kanuni ya usawa, uhakika na wepesi wa ukusanyaji wa mapato;

(c) yatazingatia athari ya marekebisho yanayopendekezwa kwenye vijenzi vya mapato yanayotokana na kodi za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja;

(d) yatazingatia mienendo ya mifumo ya kodi za ndani ya nchi, kikanda na kimataifa;

(e) yatazingatia athari kwa maendeleo, uwekezaji, ajira na ukuaji wa uchumi;

(f) yatazingatia mapendekezo ya Waziri kwa mujibu wa Ibara ya 114 ya Katiba; na

(g) yatazingatia makubaliano na majukumu ambayo yameridhiwa na Kenya kuhusu masuala ya kodi na tozo mbalimbali ikijumuisha makubaliano ya masuala ya kodi na tozo kwa mujibu wa Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

(3) Mapendekezo yatakayotolewa na Waziri katika aya ya (2)(f) yatajumuishwa kwenye ripoti na kuwasilishwa kwenye Meza ya Bunge la Taifa.

(4) Bunge la Taifa litashughulikia na kupitisha Mswada wa Fedha ukiwa na marekebisho au bila marekebisho kabla ya tarehe 30 Juni kila mwaka.

**Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Bajeti**

**245A.** (1) Katika kutathimini utekelezaji wa bajeti ya serikali ya taifa, Kamati ya Bajeti na Uidhinishaji wa Matumizi—

(a) itahakiki ripoti za kila robo mwaka zinazowasilishwa na Waziri anayehusika na masuala ya fedha kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma;

(b) itahakiki ripoti zinazowasilishwa na Msimamizi wa Bajeti ambazo zinahusu utekelezaji wa Bajeti kuhusiana na Bunge na Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali;

(c) itatathmini na kuripoti kuhusu matumizi na utendakazi usio wa kifedha wa Bajeti ya Bunge na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali;

(d) itatathmini utimilifu wa mchakato wa utekelezaji kwa misingi ya kanuni na maadili ya fedha za umma kama inavyoelezwa na Ibara ya 201 ya Katiba; na

(e) itahakikisha iwapo rasilimali zozote mpya zinazotoka kwa mapato ya kodi na ruzuku zilizokusanywa na Serikali ya Taifa katika mwaka zinatumiwa kupunguza nakisi ya fedha.

(2) Kwa mujibu wa Kanuni ya 216(5) (ba), kila Kamati ya Kiidara—

(a) itatathmini ripoti za kila robo mwaka zilizowasilishwa na Waziri anayehusika na masuala ya fedha kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma;

(b) itachanganua ripoti zilizowasilishwa na Msimamizi wa Bajeti ambazo zinahusu masuala ya utekelezaji wa Bajeti kuhusiana na serikali ya taifa;

(c) itatathmini na kuripoti kuhusu matumizi na utendakazi usio wa kifedha wa bajeti ya serikali ya taifa; na

(d) itatathmini utimilifu wa mchakato wa utekelezaji kwa misingi ya kanuni na maadili ya fedha za umma kama inavyoelezwa na Ibara ya 201 ya Katiba.

## SEHEMU YA XXV–MAJARIDA, REKODI NA UPEPERUSHAJI WA MATANGAZO YA VIKAO

**Majarida ya Bunge la Taifa**

**246.** Kumbukumbu za vikao vya Bunge la Taifa zitaandaliwa na Katibu na zitakuwa sehemu ya Majarida ya Bunge la Taifa.

**Hifadhi ya Majarida na Rekodi za Bunge la Taifa**

**247.** (1) Hifadhi ya Majarida na Rekodi za Bunge la Taifa, iwe za sauti, kielektroniki au za namna nyingine yoyote, ikijumuisha kila nyaraka na taarifa zote zilizowasilishwa kwa namna yoyote ile au zinazomilikiwa na Bunge la Taifa, itakuwa ni wajibu wa Katibu ambaye, isipokuwa kama amekatazwa na sheria yoyote, ataruhusu ziwekwe wazi kwa umma.

(2) Katibu atachapisha Kumbukumbu za vikao vya Bunge la Taifa katika muda usiozidi saa arobaini na nane za kikao chochote kuahirishwa.

(3) Spika anaweza kuweka masharti ya namna umma unavyoweza kupata Majarida na Rekodi za Bunge la Taifa zinazotajwa kwenye aya ya (1).

**Taarifa Rasmi**

**248.** (1) Taarifa ya neno kwa neno ya vikao vya Bunge la Taifa itachapishwa katika muda usiozidi saa arobaini na nane isipokuwa pale ambapo Spika ameridhika kwamba haiwezekani kutokana na tukio la dharura.

(1A) Taarifa ya neno kwa neno ya vikao vya Kamati za Bunge la Taifa pale ambapo ushahidi unatolewa itachapishwa katika muda usiozidi saa sabini na mbili isipokuwa pale ambapo Spika ameridhika kwamba haiwezekani kwa sababu ya tukio la dharura.

(2) Kila Mbunge atakuwa na fursa ya kurekebisha sehemu ya mchango wake kwenye rasimu ya taarifa ya neno kwa neno ilimradi isiwe kwa ajili ya kubadilisha maudhui ya kile alichokisema.

(3) Pale ambapo patatokea shaka kuhusiana na yaliyomo kwenye taarifa ya neno kwa neno ya vikao vya Bunge la Taifa, Spika atatoa uamuzi.

**Masuala ya siri au ya kibinafsi**

**249.** Spika anaweza kuagiza kuondolewa kwenye Majarida ya Bunge la Taifa na Taarifa Rasmi ya Bunge la Taifa na Kamati zake suala lolote ambalo kwa maoni yake ni la siri au la kibinafsi na kuagiza liwekwe kwenye Taarifa Rasmi tofauti ambayo itahifadhiwa na Katibu na kuwekwa wazi kwa Wabunge pekee.

**Upeperushaji wa matangazo ya shughuli za Bunge la Taifa**

**250.** (1) Shughuli za Bunge la Taifa na Kamati zake zinaweza kupeperushwa.

(2) Upeperushaji wa matangazo ya shughuli za Bunge la Taifa na Kamati zake utazingatia masharti yaliyowekwa katika Nyongeza ya Kwanza ya Kanuni hizi.

**251.** *(imefutwa).*

## SEHEMU YA XXVII - BUNGE LA TAIFA NA KAMATI ZAKE KUWA WAZI KWA UMMA

### Masharti ya jumla ya kuingia kwenye Bunge la Taifa

**252.** (1) Isipokuwa kama mashati yanaeleza vinginevyo, kila mtu anaruhusiwa kuingia kwenye Bunge la Taifa na kamati zake.

(2) Bunge la Taifa au Kamati haliwezi kumkataza mtu yeyote au chombo chochote cha habari kuingia kwenye vikao na mikutano yake isipokuwa pale ambapo, kwa hali za kipekee, Spika amebaini kuwa kuna sababu za kuridhisha kutoruhusu kikao au mkutano kuwa wazi kwa umma.

(2A) Mtu anayehitajika kujiwasilisha mbele ya Kamati ya Bunge la Taifa anaweza kuomba kwa maandishi kwamba umma usiruhusiwe kuingia katika kikao atakachojiwasilisha angalau saa ishirini na nne kabla ya kujiwasilisha.

(2B) Kamati italifikiria ombi lililotolewa kwa mujibu wa aya ya (2A) kwa kuzingatia mahitaji ya Ibara ya 118 ya Katiba ya kuruhusu umma kuingia katika Bunge na maslahi ya umma, na kila mara Kamati inapokubali ombi kama hilo italiarifu Bunge la Taifa na kutoa sababu za kulikubali.

(3) Mara kwa mara, Spika anaweza kuweka masharti ya namna umma unavyoweza kuingia kwenye vikao vya Bunge la Taifa au mikutano ya kamati.

### Udhibiti wa kuingia katika Ukumbi

**253.** (1) Mtu yeyote asiye Mbunge hataruhusiwa kuingia katika sehemu yoyote ya Ukumbi iliyotengewa Wabunge wakati wa kikao cha Bunge la Taifa au Kamati ya Bunge Zima.

(2) Aya ya (1) haitatumika kwa Katibu au maofisa wengine wa Bunge wakati wa kutekeleza majukumu ya uendeshaji wa kikao cha Bunge la Taifa.

**Kuondolewa bungeni au kwenye Kamati**

**254.** (1) Wakati wowote, Mbunge anaweza kusimama na kudai kwamba umma au mtu fulani, kwa sababu atakazozitaja, aondolewe bungeni au kwenye Kamati, na ikiwa Spika au Mwenyekiti ana maoni kwamba kuna sababu za kuridhisha za kuondolewa huko, anaweza kuagiza kwamba umma au mtu huyo aondoke katika Bunge la Taifa au kwenye kamati.

(2) Pale ambapo Spika au Mwenyekiti ameamua kuwa mtu yeyote aondolewe kwenye kikao cha Bunge la Taifa au Kamati, Spika au Mwenyekiti ataliarifu Bunge la Taifa au Kamati sababu za kuondolewa kwa mtu huyo.

(3) Uamuzi wa Spika au Mwenyekiti kwa mujibu wa aya ya (2) hautatolewa maoni wala kujadiliwa.

(4) Katibu atahakikisha kuwa amri ya kuondolewa kwa umma au mtu inatekelezwa.

**Wanahabari wanapokiuka Kanuni hizi au Kanuni za Spika**

**255.** Chombo chochote cha habari ambacho mwanahabari wake atakiuka masharti ya Kanuni hizi au masharti yoyote kwenye Kanuni za Spika kuhusu ruhusa ya umma kuingia katika Bunge la Taifa au kwenye Kamati, au kuendelea kuripoti visivyo habari za Bunge la Taifa, kupuuza au kukataa amri ya Spika ya kurekebisha taarifa yoyote yenye makosa kuhusiana na shughuli za Bunge la Taifa, kinaweza kunyimwa nafasi ya kuwakilishwa kwenye dungu la wanahabari kwa muda ambao Spika ataamua.

## SEHEMU YA XXVIII — JUMLA

### Kutengua Kanuni

**256.** (1) Kwa kuzingatia aya ya (2) na (3), kwa idhini ya Spika, Hoja inaweza kuwasilishwa na Mjumbe yeyote, ama baada ya kutoa arifa au bila ya arifa kwamba masharti ya Sehemu ya VI (*Kalenda, kikao na Maahirisho ya Bunge la Taifa*), Sehemu ya VIII (*Mpangilio wa Shughuli*), Sehemu ya XVII (*Kudhibiti Mjadala*), Sehemu ya XIX (*Miswada ya Umma*), Sehemu ya XX (*Miswada Binafsi*), Sehemu ya XXI (*Kamati ya Bunge Zima*) Sehemu ya XXIV (*Utaratibu wa Masula ya Fedha*), Sehemu ya XXII (*Kamati*), Sehemu ya XXIII (*Ardhilhali za Umma*) na Sehemu ya XXVII (*Bunge la Taifa na Kamati zake kuwa wazi kwa Umma*) yatenguliwe kuhusiana na shughuli iliyotajwa.

(2) Hoja ya kutengua Kanuni haitatolewa kuhusiana na shughuli yoyote katika Sehemu ya XIII (*Hoja maalum*), Sehemu ya XIV (*Utaratibu wa Kumwondoa Ofisa wa Serikali Mamlakani*), Kanuni ya 120 (*Uchapishaji wa miswada*) au Kanuni ya 231 (*Udhibiti wa masuala mahususi ya kifedha*).

(3) Hoja zaidi ya moja ya kutengua Kanuni haitatolewa kwenye kikao kimoja, isipokuwa kwa idhini ya Bunge la Taifa.

(4) Hoja kwa mujibu wa Kanuni hii itaeleza madhumuni au sababu za pendekezo la kutengua Kanuni na —

(a) inaweza kutolewa wakati wowote na shughuli yoyote itakayokuwa ikiendelea inaweza kusitishwa mara moja;

(b) haiwezi kurekebishwa bila ruhusa ya Mtoahoja.

### Kuongeza muda uliotengewa shughuli

**256A.** (1) Licha ya masharti ya Kanuni hizi yanayotaja muda ambao Bunge la Taifa au Kamati inafaa kuchukua hatua yoyote, Bunge la Taifa, kupitia hoja, linaweza kuamua kuongeza muda huo.

(2) Mamlaka ya Bunge la Taifa kwa mujibu wa aya ya (1), yanaweza kutumika tu katika hali za kipekee zitakazoruhusiwa na Spika.

(3) Pale ambapo ombi la kuongeza muda kwa mujibu wa Kanuni hii limekubaliwa, muda wa utendaji wa shughuli zitakazoibuka utachukuliwa kuwa umeongezwa.

**Hati ya Wito**

**256B.** (1) Mbunge anaweza kutoa arifa ya siku tatu ya Hoja inayohitaji Bunge la Taifa kumwita mtu yeyote afike mbele ya Bunge la Taifa kwa mujibu wa masharti ya Ibara ya 125 (1) ya Katiba.

(2) Spika atakataa arifa hiyo iwapo ana maoni kwamba Hoja hiyo haina maana, inakera au inahujumu shughuli za Bunge la Taifa au ni jaribio la kutwaa suala linaloshughulikiwa na Kamati kwa namna isiyofaa.

(3) Arifa iliyotolewa kwa mujibu wa aya ya (1) itabainisha—

(a) mtu au watu watakaoitwa.

(b) sababu ya kuitwa.

(c) ushahidi au nyaraka zitakazotolewa mbele ya Bunge la Taifa, kama zipo; na

(d) saa na mahali pa kufika mbele ya Bunge la Taifa.

(4) Baada ya uamuzi wa Bunge la Taifa kuhusu Hoja iliyotolewa kwa mujibu wa aya ya (1), Katibu, na isiwe baada ya siku tatu kuanzia tarehe ya uamuzi huo, atatoa Hati ya Wito kwa watu waliotajwa katika Hoja ikimtaka mtu huyo kufika mbele ya Bunge la Taifa ikionyesha tarehe, saa na mahali palipotajwa kwenye Hoja.

(5) Mtu ataitwa kufika mbele ya Bunge la Taifa kwa mujibu wa Kanuni hii ikiwa tu—

(a) madhumuni ya kuitwa sio kwa ajili ya kushughulikia suala ambalo tayari linashughulikiwa na Kamati; au

(b) mtu huyo amewahi kuitwa kufika mbele ya Kamati lakini akashindwa au akakataa kufika bila sababu zinazokubalika kisheria.

**Kufika mbele ya Seneti**

**257.** (1) Ombi la Seneti la kumhitaji Mbunge, Katibu, au ofisa wa Bunge la Taifa afike mbele ya Seneti kwa ajili ya kuhojiwa au kufika mbele ya kamati yoyote ya Seneti litatolewa kupitia Ujumbe kutoka Seneti ukiomba Bunge la Taifa kutoa idhini ili Mbunge, Katibu au ofisa huyo afike mbele yake.

(2) Iwapo Bunge la Taifa litatoa idhini kwa mujibu wa aya ya (1)—

(a) Katibu au ofisa atafika mbele ya Seneti au kamati ya Seneti;

(b) Mbunge, pale ambapo anaona ni vyema kufanya hivyo, anaweza kufika mbele ya Seneti au Kamati ya Seneti.

(3) Mbunge, Katibu au ofisa hatafika yeye mwenyewe au kuwakilishwa na wakili mbele ya Seneti au Kamati ya Seneti kufuatia Hati ya Wito au mwaliko wa Seneti au kutuma jibu kimaandishi kwa hati au mwaliko huo, isipokuwa kwa idhini iliyotolewa kwa mujibu wa aya ya (2).

**Ruhusa ya kutohudhuria vikao**

**257A.** (1) Mbunge anayekusudia kutofika kwenye kikao cha Bunge la Taifa atamwomba Spika ruhusa kimaandishi kwa namna ambayo Spika ataamua, akitaja muda ambao hatafika, sababu za kutofika na taarifa nyingine yoyote inayofaa.

(2) Katibu atahifadhi maombi ya ruhusa na anaweza kutoa habari hiyo kwa idhini iliyotolewa na Spika kimaandishi.

**Kutohudhuria vikao**

**258.** (1) Iwapo, katika Kipindi chochote, Mbunge hatahudhuria vikao vinane vya Bunge la Taifa bila ruhusa ya Spika iliyotolewa kwa maandishi, Spika ataripoti suala hilo kwa Bunge la Taifa na litakabidhiwa Kamati ya Mamlaka na Haki ya Bunge la Taifa kwa ajili ya kusikizwa na kuamuliwa.

(2) Kamati ya Mamlaka na Haki ya Bunge la Taifa itachunguza suala ambalo imekabidhiwa kwa mujibu wa aya ya (1) katika muda usiozidi siku kumi na nne baada ya kukabidhiwa suala hilo na kuwasilisha Ripoti katika Bunge la Taifa.

(3) Ikiwa ripoti ya Kamati itabaini kuwa Mbunge ametoa maelezo ya kuridhisha ya kutohudhuria vikao vinane vya Bunge la Taifa bila ruhusa ya kimaandishi kutoka kwa Spika, suala hilo halitashughulikiwa zaidi katika Bunge la Taifa.

(4) Ikiwa ripoti ya Kamati itabaini kuwa Mbunge hajatoa maelezo ya kuridhisha ya kutohudhuria vikao vinane vya Bunge la Taifa kwa mujibu wa aya ya (1), Mwenyekiti wa Kamati au mjumbe aliyeteuliwa na Kamati kwa ajili hiyo baada ya kuwasilisha ripoti ya kamati, atatoa arifa ya hoja ya siku tatu ***"Kwamba Bunge la Taifa litambue Ripoti ya Kamati ya Mamlaka na Haki za Bunge iliyowekwa kwenye Meza ya Bunge mnamo ... kuhusu ......"*** na ikifanyiwa marekebisho kadri itakavyofaa.

(5) Hoja itakayotolewa kwa mujibu wa aya ya (4) itajadiliwa kwa namna ya kawaida ya kujadili Hoja, isipokuwa—

(a) hakuna rekebisho litakaloruhusiwa kwenye Hoja.

(b) mjadala wa Hoja hautawahishwa kwa Hoja ya kuahirisha Bunge la Taifa, na hakuna Hoja ya kuahirisha shughuli itakayotolewa kuhusiana na shughuli hiyo na shughuli haitasitishwa kwa mujibu wa Kanuni hizi.

(6) Mjadala kwa hoja iliyotolewa kwa mujibu wa aya ya (4) ukihitimishwa, Spika hatahitajika kulihoji Bunge la Taifa bali, kwa mujibu wa Ibara ya 103(1)(b) ya Katiba, atatangaza kwamba nafasi ya Mbunge huyo iko wazi.

**Utaratibu wa kuketi katika Ukumbi**

**259.** (1) Kutakuwa na viti vilivyotengwa katika Ukumbi wa Bunge la Taifa kwa ajili ya wafuatao—

(a) Naibu Spika;

(b) Kiongozi wa Chama cha walio Wengi;

(c) Kiongozi wa Chama cha walio Wachache;

(d) Wabunge wenye ulemavu.

(1A) Spika anaweza kutenga viti katika Ukumbi kwa ajili ya wajumbe wa Jopo la Mwenyekiti, Naibu Kiongozi wa Chama cha walio Wengi na Naibu Kiongozi wa Chama cha walio Wachache, Wenyekiti wa Kamati, Mratibu wa Chama cha walio Wengi na Mratibu wa Chama cha walio Wachache.

(2) Viti vingine vyote katika Ukumbi vitatumiwa na Mbunge yeyote.

(3) Kwa kuzingatia Kanuni hii na amri nyingine yoyote ya Bunge la Taifa, suala lolote linalohusiana na kuketi katika Ukumbi litaamuliwa na Spika.

**Kutambuliwa kwa Kikundi cha Wabunge**

**259A.** (1) Kufuatia ombi lililowasilishwa kimaandishi na angalau Wabunge kumi, Spika anaweza kutambua kikundi cha wabunge kilichoundwa kwa ajili ya kuendeleza lengo sawa linalohusu utungaji wa sheria.

(2) Ombi kwa Spika kwa mujibu wa Kanuni hii—

(a) litaonyesha jina la kikundi;

(b) litataja lengo linalohusu utungaji wa sheria ya kikundi hicho; na

(c) litakuwa na majina na saini za Wajumbe wa kikundi hicho.

(3) Kikundi cha wabunge hakitakuwa na mamlaka na haki sawa na kamati ya Bunge la Taifa.

**Kikundi cha Wabunge Huru**

**259B.** (1) Kufuatia ombi la kimaandishi la angalau Wabunge Huru kumi, Spika anaweza kutambua kikundi cha Wabunge Huru kilichoundwa kwa minajili ya kuwawezesha Wabunge Huru kutekeleza majukumu yao katika Bunge la Taifa.

(2) Ombi kwa Spika kwa mujibu wa Kanuni hii litakuwa na majina na saini za Wabunge wa kikundi hicho.

(3) Kwa mujibu wa Kanuni hii, Spika atatambua kikundi kimoja pekee.

**Kamati za Muda**

**259C.** (1) Baada ya kupata idhini kutoka kwa Kamati ya Kuratibu Shughuli za Bunge la Taifa, Mbunge anaweza kutoa hoja inayopendekeza kuundwa kwa Kamati ya Muda kuhusu suala maalum na la kipekee ambalo kwa wakati huo halishughulikiwi na Kamati ya Bunge la Taifa.

(2) Hoja kwa mujibu wa Kanuni hii—

(a) itataja jina linalopendekezwa kuwa la kamati hiyo;

(b) itaeleza wajibu unaopendekezwa na upekee wa suala litakaloshughulikiwa na Kamati hiyo; na

(c) itafafanua uanachama na uongozi unaopendekezwa wa Kamati hiyo.

(3) Mtoahoja anayetoa hoja kwa mujibu wa Kanuni hii atahakikisha kwamba—

(a) uanachama wa Kamati hiyo unaopendekezwa unaakisi wingi wa Wabunge wa kila Chama Bunge katika Bunge la Taifa na unazingatia maslahi ya vyama ambavyo sio Vyama Bunge na Wabunge Huru; na

(b) uanachama unaopendekezwa kwa Kamati hiyo hauna zaidi ya thuluthi mbili ya wajumbe wa jinsia moja.

(4) Isipokuwa Bunge la Taifa liamue vyinginevyo, Kamati ya Muda itashughulikia suala inalowajibikia na kutoa ripoti yake katika muda usiozidi siku tisini.

**Risala za Bunge la Taifa**

**259D.** (1) Spika ataripoti kwa Bunge la Taifa kifo cha mtu ambaye, kwa maoni ya Spika, ni muhimu Bunge la Taifa kuarifiwa na risala za Bunge la Taifa zinaweza kutolewa kupitia kwa hoja ya kipekee.

(2) Kwa idhini ya Spika, Mbunge anaweza—

(a) kuripoti kifo cha Mbunge wa zamani; au

(b) kuarifu Bunge la Taifa kuhusu mafanikio ya kipekee ya Mkenya katika ngazi ya kitaifa, kikanda au kimataifa.

(3) Spika anaweza kuwaruhusu Wabunge kutoa maoni kwa ufupi baada ya ripoti au arifa kutolewa kwa mujibu wa Kanuni hii.

(4) Katibu atawasilisha nakala iliyothibitishwa ya Taarifa Rasmi kwa familia ya mtu ambaye Bunge la Taifa limemtolea risala.

**Bunge la Taifa kupendekeza au kuteua maafisa kwa Ofisi za Umma**

**259E.** Pale ambapo sheria au sheria ndogo inahitaji Bunge la Taifa kumpendekeza mtu kuteuliwa au kuteua mtu katika ofisi ya umma, Spika anaweza, ikiwa hakuna mwongozo, kutoa mwongozo wa jinsi uteuzi huo utafanywa.

## Wasifu na Sajili ya Wabunge

**259F.** (1) Mwanzoni mwa kila Bunge au baada ya uchaguzi mdogo, Mbunge atawasilisha kwa Katibu wasifu wake kwa njia inayoelekezwa kwenye Nyongeza ya Kumi kwa minajili ya kumwezesha Mbunge huyo katika masuala ya Bunge la Taifa na kuufahamisha umma.

(2) Wakati wowote katika muhula wa Bunge, Mbunge anaweza kusasisha taarifa aliyotoa kwa mujibu wa aya ya (1).

(3) Katibu atahifadhi wasifu wa Wabunge na mara kwa mara kusasisha taarifa hiyo kila wakati Mbunge anapowasilisha taarifa na anaweza kuchapisha taarifa hizo kwenye wavuti wa Bunge.

(4) Mbunge atawajibikia usahihi wa taarifa anayotoa kwa mujibu wa Kanuni hii.

(5) Angalau mwezi mmoja kabla ya muhula wa Bunge kumalizika, Katibu atachapisha kwenye *Gazeti Rasmi la Serikali*, sajili ya Wabunge waliohudumu kwenye Bunge hilo kwa kufuata mpangilio wa kialfabeti.

## Utambuzi wa Wabunge wenye Hadhi

**259G.** (1) Mara kwa mara, Spika anaweza kumtambua na kumtaja Mbunge wa Bunge la Taifa kuwa Mbunge mwenye Hadhi.

(2) Katika kumteua Mbunge mwenye Hadhi, Spika—

(a) atazingatia—

(i) huduma ya awali ya Mbunge huyo katika Bunge la Taifa kama Spika, Naibu Spika, Kiongozi wa Chama cha Walio Wengi, au Kiongozi wa Chama cha Walio Wachache; na

(ii) jumla ya muda ambao Mbunge huyo alihudumu katika Bunge la Taifa; na

(b) atamwarifu Mbunge huyo na Bunge la Taifa kuhusu haki zinazoambatana na uteuzi huo.

**Wabunge wanaosafiri nje ya Kenya**

**260.** (1) Mbunge anayekusudia kusafiri nje ya Kenya kwa shughuli rasmi au shughuli binafsi atampa Spika arifa ya kimaandishi, ikionyesha—

(a) mahali anapokusudia kusafiri;

(b) tarehe aliyopanga kusafiri na muda ambao atakuwa nje ya Kenya; na

(c) baruapepe, namba ya simu, anwani ya posta au anwani ya makazi ya Mbunge kwa muda atakaokuwa nje ya Kenya.

(2) Habari zote zitakazotolewa kwa mujibu wa Kanuni hii zitawekwa kwenye sajili ambayo itahifadhiwa na Katibu kwa ajili hiyo na haitawekwa wazi kwa mtu yeyote isipokuwa kwa ruhusa ya Spika.

**Gharama za mashahidi**

**261.** Mtu yeyote aliyeitwa kutoa ushahidi au kuwasilisha nyaraka mbele ya Bunge la Taifa au Kamati anaweza kurejeshewa gharama kiasi kinachofaa cha pesa alizotumia, zikijumuisha gharama za usafiri kama Katibu atakavyoamua mara kwa mara, ama kijumla au kwa kila gharama.

## SEHEMU YA XXIX — MAREKEBISHO YA KANUNI

**Mapendekezo ya kurekebisha Kanuni kutoka kwenye Kamati ya Utaratibu na Kanuni za Bunge la Taifa**

**262.** Kamati ya Utaratibu na Kanuni za Bunge la Taifa inaweza kupendekeza marekebisho kwenye Kanuni hizi wakati wowote.

**Rekebisho linalotokana na Mbunge**

**263.** (1) Mbunge, kwa kuungwa mkono na angalau Wabunge wasiopungua hamsini, anaweza kuiomba Kamati ya Utaratibu na Kanuni za Bunge la Taifa kushughulikia rekebisho kwenye Kanuni hizi.

(2) Ombi kwa mujibu wa aya ya (1) litakuwa kwa maandishi na—

(a) litakuwa na matini ya marekebisho yanayopendekezwa pamoja na sababu zake;

(b) litakuwa na majina na saini za Wabunge wanaoliunga mkono;

(c) litapelekwa kwa Spika.

(3) Spika akiridhika kuwa ombi hilo limekidhi mahitaji ya aya ya (1) na ya (2), atalipeleka kwenye Kamati ya Utaratibu na Kanuni za Bunge la Taifa.

(4) Kamati ya Utaratibu na Kanuni za Bunge la Taifa, katika muda usiozidi siku ishirini na moja baada ya kupokea ombi kwa mujibu wa aya ya (3), italishughulikia ombi hilo na kuwasilisha ripoti katika Bunge la Taifa ikiwa na marekebisho yaliyopendekezwa katika ombi na mapendekezo ya Kamati kwa kila pendekezo.

(5) Bunge la Taifa litashughulikia marekebisho yanayopendekezwa kwa Kanuni za Kudumu kama ilivyoripotiwa na Kamati ya Utaratibu na Kanuni za Bunge la Taifa kupitia Hoja ***"Kwamba, ripoti ya Kamati ya Utaratibu na Kanuni za Bunge la Taifa iidhinishwe."***

(6) Kanuni ya 136 (*Utaratibu kwa Miswada inayoripotiwa kutoka kwa Kamati ya Bunge Zima*) itatumika kwa Hoja ya kuidhinisha ripoti ya Kamati ya Utaratibu na Kanuni za Bunge la Taifa kuhusu marekebisho yaliyopendekezwa kwenye Kanuni za Kudumu.

**Udurusu wa mara kwa mara wa Kanuni za Kudumu**

**264.** Kamati ya Utaratibu na Kanuni za Bunge la Taifa itadurusu Kanuni za Kudumu za Bunge la Taifa na kutoa ripoti katika Bunge la Taifa ikipendekeza marekebisho ya Kanuni za Kudumu, kama yapo, angalau mara moja katika kila Muhula wa Bunge.

**Kushughulikia ripoti za Kamati ya Utaratibu na Kanuni za Bunge la Taifa**

**265.** (1) Ripoti ya Kamati ya Utaratibu na Kanuni za Bunge la Taifa inapowasilishwa katika Bunge la Taifa kwa mujibu wa Kanuni za 263 (*Rekebisho linalotokana na Mbunge*) na 264 (*Udurusu wa mara kwa mara ya Kanuni za Kudumu*), utaratibu uliowekwa kwenye aya ya (5) na ya (6) ya Kanuni ya 263 (*Rekebisho linalotokana na Mbunge*) itatumika kadri itakavyohitajika.

(2) Marekebisho ya Kanuni za Kudumu yanayopendekezwa kwa mujibu wa Sehemu hii, yakishaidhinishwa na Bunge la Taifa, yataanza kutumika wakati utakaoamuliwa na Bunge la Taifa.

## SEHEMU YA XXIXA— UENDESHAJI VIKAO KATIKA HALI ZA KIPEKEE

**Matumizi**

**265A.** (1) Sehemu hii itatumika kuendesha vikao vya Bunge la Taifa na Kamati zake katika hali ya kipekee.

(2) Masharti ya Kanuni za Kudumu yanayotangulia Sehemu hii yataendelea kutumika isipokuwa kama yatakavyorekebishwa katika Sehemu hii.

(3) Pale ambapo sharti lolote la Sehemu hii linakinzana au haliwiani na sharti la kanuni yoyote iliyotangulia ama kwa sehemu au kwa jumla, masharti ya Sehemu hii yatatumika.

(4) Katika Sehemu hii, "hali ya kipekee" ina maana ya tukio linalotangazwa kihalali kwa mujibu wa sheria yoyote linalozuia Bunge la Taifa kufanya vikao vya ana kwa ana na inajumuisha tangazo la maradhi kumbakumba, maradhi tandavu, janga la kimaumbile lililokithiri, ndwele inayoua au ambo ama tendo la ugaidi.

**Mipangilio mbadala ya Vikao**

**265B.** (1) Spika atatumia masharti ya Sehemu hii na kuruhusu Bunge la Taifa na Kamati zake kuendesha vikao ama –

(a) ana kwa ana na kimtandao, pale ambapo Bunge la Taifa limezuiliwa kwa kiasi fulani kufanya kikao ana kwa ana kutokana na hali ya kipekee; au

(b) kimtandao, pale ambapo Bunge la Taifa limezuiliwa kabisa kufanya kikao cha ana kwa ana kutokana na hali ya kipekee.

(2) Spika akishatumia masharti ya aya ya (1) kutokana na pendekezo la Kamati ya Utaratibu na Kanuni za Bunge la Taifa, atatoa miongozo itakayoelekeza—

(a) utaratibu wa kuendesha shughuli za Bunge la Taifa;

(b) namna ya kupiga kura, namna ya kuendesha kura ya mgawanyiko na thibitisho la kura katika shughuli hizo;

(c) mwenendo wa Wabunge wakati wa shughuli za Bunge la Taifa;

(d) ufikiwaji wa shughuli za Bunge la Taifa kwa umma na vyombo vya habari;

(e) ushirikishwaji na uhusishwaji wa umma;

(f) staha; na

(g) suala lingine lolote linalohusu uendeshaji wa shughuli za Bunge la Taifa.

(3) Miongozo iliyoagizwa katika aya ya (2) itakoma kutumika pindi itakapobatilishwa na Spika au hali ya kipekee kwisha, kutegemea hali itakayotangulia.

**Mipango mingine**

**265C.** Wakati wa ya hali ya kipekee—

(a) Bunge la Taifa linaweza, kwa kupitia uamuzi, kubadilisha idadi ya vikao vyake vya kawaida kutegemea hali;

(b) Kamati ya Kuratibu Shughuli za Bunge la Taifa itaamua na kuyapa kipaumbele masuala muhimu yatakayoshughulikiwa na Bunge la Taifa; na

(c) Spika anaweza—

(i) kutenga mahali nje ya Ukumbi lakini ndani ya Maeneo ya Bunge ambapo Wabunge watashiriki shughuli za Bunge la Taifa;

(ii) kuelekeza idadi ya Wabunge wanaoweza kushiriki shughuli katika Ukumbi au mahali popote palipotengwa nje ya Ukumbi;

(iii) Kumruhusu Mbunge au mtu mwingine yeyote anayehitajika kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu au sheria yoyote kusajili, kuwasilisha au kuleta waraka wowote kwenye Meza ya Bunge la Taifa afanye hivyo kielektroniki;

(iv) pale ambapo Bunge la Taifa limezuiwa kabisa kuendesha kikao cha ana kwa ana, kuchukulia waraka kuwa umewasilishwa, ikijumuisha waraka uliotumwa kielektroniki, kwamba umewasilishwa kwenye Meza ya Bunge la Taifa, kwa kuzingatia ukubalifu wake; na

(v) kuzuia umma kuhudhuria vikao vya Bunge la Taifa na mikutano ya Kamati kwa mujibu wa Kanuni ya 252(1) *(Masharti ya jumla ya kuingia kwenye Bunge la Taifa*).

**Matumizi ya teknolojia**

**265D.** (1) Spika, akizingatia masharti ya Ibara ya 126(1) ya Katiba, anaweza kuelekeza mfumo wa teknolojia ya habari na mawasiliano unaofaa kuendeshea vikao vya kimtandao kwa mujibu wa Sehemu hii.

(2) Mfumo utakaoelekezwa kwa mujibu wa aya ya (1)—

(a) utajumuisha video na sauti au matini;

(b) utawezesha Wabunge kushiriki katika vikao mubashara na upeperushaji wa shughuli za Bunge la Taifa;

(c) utawezesha shughuli kurekodiwa na kunakiliwa kwa mujibu wa Kanuni ya 248*(Taarifa Rasmi)*; na,

(d) utajumuisha mfumo unaowezesha Wabunge kupiga kura pale ambapo Bunge la Taifa linazuiwa kabisa kufanya vikao vya ana kwa ana.

(3) Mfumo wa kupiga kura utakaotumika kwa mujibu wa aya ya (2) (d) utakuwa rahisi kutumia, sahihi, unaothibitishika, salama, unaoelezeka, wazi na unaowezesha utangazaji wa haraka wa matokeo ya kila kura iliyopigwa.

(4) Katibu atawawezesha Wabunge kushiriki vikao va kimtandao kwa kutumia vyombo vya kielektroniki vya viwango vilivyokubalika na vilivyosanidiwa maalum kwa shughuli za Bunge la Taifa

## SEHEMU YA XXX—MASHARTI YA MPITO

**Uamuzi wa Bunge la Taifa kuhusu Kanuni za Kudumu**

**266.** Katika kutekeleza mamlaka kwa mujibu wa Ibara ya 124 ya Katiba ya Jamhuri ya Kenya, Bunge la Taifa, kupitia uamuzi uliofanywa mnamo tarehe 9 Januari 2013, liliridhia hizi Kanuni za Kudumu pamoja na Masharti ya Vikao vya Pamoja vya Bunge.

**Kubatilisha Kanuni za Kudumu za awali**

**267.** Kanuni za Kudumu zilizoridhiwa na Bunge la Taifa mnamo tarehe 10 Desemba 2008 kwenye Kipindi cha Pili cha Bunge la Kumi sasa zimebatilishwa

**Kuanza kutumika**

**267A.** Kwa kuzingatia uamuzi wa Bunge la Taifa uliofanywa mnamo tarehe 7 Juni 2022—

(a) marekebisho yaliyofanywa na Bunge la Taifa kwa Kanuni hizi tarehe 7 Juni 2022 yataanza kutumika baada ya muhula wa Bunge la Kumi na Mbili kumalizika;

(b) licha ya aya ya (a), Kanuni ya 259F (5) itaanza kutumika mara moja.

## NYONGEZA YA KWANZA

## MASHARTI YA UPEPERUSHAJI WA MATANGAZO YA SHUGHULI ZA BUNGE

**[Kanuni ya 250]**

**Kitengo cha Utangazaji cha Bunge**

**1.** (1) Kutakuwa na Kitengo cha Utangazaji cha Bunge ambacho kitasimamia upeperushaji wa matangazo ya shughuli za Bunge.

(2) Isipokuwa kama Bunge la Taifa litaelekeza vinginevyo, Kitengo cha Utangazaji cha Bunge kinaweza kupeperusha matangazo ya shughuli za Bunge na kuruhusu upatikanaji wa habari za Bunge.

**Haki za Bunge**

**2.** Sauti na video za kidijitali za shughuli za Bunge zitalindwa na sheria zinazohusiana na haki za Bunge na zitahifadhiwa na Katibu wa Bunge la Taifa kama sehemu ya rekodi za Bunge la Taifa.

**Upeperushaji wa matangazo kupitia kwa runinga**

**3.** Wakati wa kupeperusha matangazo ya shughuli za Bunge la Taifa kupitia kwa runinga, mwongozo ufuatao utazingatiwa—

(a) kamera itaelekezwa kwa Mbunge aliyepewa fursa na kiongozi wa kikao hadi Mbunge huyo atakapomaliza kuzungumza;

(b) picha za makundi na visehemu vya picha vinaweza kunaswa kwa minajili ya kuonyesha jinsi kundi fulani la Wabunge lilivyopokea suala lililotolewa katika Ukumbi;

(c) Unasaji wa picha zenye upeo mpana zinazoonyesha Ukumbi utafanyika wakati wa kupiga kura au wakati

wa Kura ya Mgawanyiko na hakuna picha itanaswa kuonyesha namna Mbunge fulani alivyopiga kura katika kura yoyote ya siri;

(d) maofisa wa Bunge la Taifa wanaohusika moja kwa moja na shughuli za Bunge katika Ukumbi wanaweza kuonyeshwa;

(e) anayeongoza kikao anaweza kuonyeshwa anapoingia au kutoka kwenye Kiti na wakati wowote anaposimama;

(f) madungu ya wanahabari na umma hayataonyeshwa isipokuwa wakati wa kunasa picha za Ukumbi wote na katika shughuli muhimu kadri itakavyoamuliwa na Kamati ya Upeperushaji wa Matangazo ya Bunge;

(g) picha za karibu za karatasi za Wabunge au nyaraka za marejeleo hazitaonyeshwa.

**Upeperushaji wa Matangazo ya Bunge kupitia kwa redio**

**4.** Katika kupeperusha matangazo ya shughuli za Bunge la Taifa kupitia kwa redio, mwongozo ufuatao utatumika—

(a) sauti zitakazorekodiwa zitajikita katika shughuli za Bunge la Taifa au Kamati pekee;

(b) maelezo wakati wa matangazo mbashara yatajikita katika kutoa utangulizi wa suala linalojadiliwa na utambulisho wa Mbunge anayetoa mchango.

**Kulinda hadhi ya Bunge la Taifa**

**5.** (1) Maofisa wa Kitengo cha Utangazaji cha Bunge watatekeleza majukumu yao kwa weledi na bila upendeleo wowote kwa kutoa matangazo sahihi na ya haki kuhusu shughuli za Bunge.

(2) Picha zinazonaswa kwa nia ya kuwadhalilisha Wabunge bila wenyewe kujua hazitaonyeshwa.

(3) Sauti na video za shughuli za Bunge hazitatumiwa kwa matangazo ya vyama vya kisiasa, kejeli, udhamini wa kibiashara au kwa namna nyingine yoyote inayoathiri hadhi ya Bunge.

**Vyombo vingine vya Habari**

**6.** (1) Katika Masharti haya, "Chombo kingine cha habari" ni shirika lingine la habari isipokuwa Kitengo cha Utangazaji cha Bunge.

(2) Hakuna chombo kingine cha habari au mtu yeyote atakayeruhusiwa kutangaza shughuli za Bunge la Taifa isipokuwa kama yalivyopokelewa kutoka kwa Kitengo cha Utangazaji cha Bunge au kwa kibali cha Spika.

(3) Chombo cha habari kitakachopokea habari kutoka Kitengo cha Utangazaji cha Bunge kitazitangaza bila kubadili au kupotosha maudhui yake.

(4) Kamera au vifaa vingine vya matangazo havitaruhusiwa ndani ya Ukumbi wa Bunge la Taifa bila idhini.

(5) Wanahabari walioidhinishwa wataruhusiwa kuketi katika maeneo waliyotengewa kwa ajili ya kufuatilia shughuli za Bunge na kuchukua habari na mwanahabari yeyote aliyeruhusiwa atazingatia Kanuni za Kudumu na masharti haya.

**Ukiukaji wa Masharti ya utangazaji**

**7.** (1) Mtu yeyote anayekiuka Masharti haya atakuwa amefanya kosa na ataadhibiwa na Bunge la Taifa kwa namna litakavyoona inafaa kufuatia mapendekezo ya Kamati ya Upeperushaji wa Matangazo ya Bunge.

(2) Kamati ya Upeperushaji wa Matangazo ya Bunge itatayarisha taratibu za kuhakikisha kwamba Masharti haya yanatekelezwa.

**Matumizi**

**8.** Masharti haya yatatumika kwenye upeperushaji wa shughuli katika Bunge la Taifa, kwenye Kamati na kadri itakavyofaa, katika shughuli na matukio mengine ya Bunge.

## NYONGEZA YA PILI

## KAMATI ZA KIIDARA

**[Kanuni ya 216]**

| **Kamati** | **Masuala** |
|---|---|
| **Utawala na Usalama wa taifa** | Masuala ya ndani, usalama wa ndani—ikiwemo huduma za polisi na huduma za kikosi cha ulinzi wa fukwe, utawala wa umma, uhamiaji na uraia. |
| **Kilimo na Mifugo** | Kilimo, mifugo, uzalishaji wa chakula na mauzo. |
| **Uchumimaji, Maji na Unyunyiziaji Maji** | Matumizi na udhibiti wa rasilimali za maji, unyunyizaji maji, ustawishaji na maendeleo ya shughuli za uvuvi ikiwemo kilimo cha mimea ya majini, ufugaji wa samaki, uvuvi wa baharini, matumizi endelevu ya rasilimali za majini kwa minajili ya ukuaji wa uchumi na ustawi wa jamii, isipokuwa bandari na usafiri wa majini. |
| **Mawasiliano, Habari na Uvumbuzi** | Mawasiliano, habari, vyombo vya habari na utangazaji (isipokuwa upeperushaji wa shughuli za Bunge), teknolojia ya habari, teknolojia ya mawasiliano, ikiwemo ustawi na uboreshaji wa teknolojia, ulinzi na usiri wa data, mtandao na usalama wa kimtandao, akiliunde, teknolojia ya msururu wa muundo wa data kwa njia salama (block-chain), na teknolojia nyingine zinazoibuka. |

| Kamati | Masuala |
|---|---|
| **Ulinzi, Ujasusi na Mahusiano ya Kigeni** | Ulinzi, ujasusi, mahusiano ya kigeni, huduma za kidiplomasia na kibalozi, mipaka ya kimataifa, ikiwemo mipaka ya majini na mahusiano ya kimataifa na masuala ya wanajeshi wastaafu. |
| **Elimu** | Elimu, mafunzo, uundaji wa mtaala, na utafiti. |
| **Kawi** | Uchunguzi wa Mafuta ya visukuku, uendelezaji, uzalishaji, udumishaji na usambazaji, kawi ya nyuklia, kawi safi na udhibiti wa kawi. |
| **Mazingira, Misitu na Uchimbaji Madini** | Mabadiliko ya tabianchi, usimamizi na uhifadhi wa mazingira, misitu, uchimbaji madini na mali asili, uchafuzi wa mazingira na udhibiti wa taka. |
| **Fedha na Mipango ya Taifa** | Hazina ya umma, sera za ukaguzi wa hesabu za umma, sera za kifedha, asasi za kifedha (isipokuwa zile za soko la hisa), uchumi, sera za uwekezaji, ushindani, shughuli za benki, bima, takwimu za kitaifa, idadi ya watu, sera za mapato ikiwemo kodi, mipango na maendeleo ya taifa na hazina za kidijitali ikiwemo sarafu za kidijitali. |
| **Afya** | Afya, huduma za matibabu na bima ya afya ikiwemo bima ya afya kwa wote. |
| **Makazi, Mipango ya Miji na Ujenzi wa Miradi ya Umma** | Makazi, ujenzi wa miradi ya umma, mipango ya miji, masuala ya miji, uendelezaji wa makazi na maeneo yaliyojengwa. |

| Kamati | Masuala |
| --- | --- |
| **Masuala ya Haki na Sheria** | Idara ya Mahakama, mahakama maalum, upatikanaji wa haki, mashtaka ya umma, maadili, uadilifu na kupambana na ufisadi, huduma za kurekebisha tabia, kifungo cha nje na usalama wa mashahidi, masuala ya kikatiba, kinga dhidi ya mashtaka inayotokana na mamlaka, uchaguzi pamoja na kura za maoni, haki za kibinadamu, vyama vya kisiasa, Ofisi ya Sheria ya Nchi ikiwemo ufilisi, mageuzi ya sheria, udhamini wa mali ya umma, ndoa na elimu ya sheria. |
| **Leba** | Leba ikiwemo masuala ya wafanyakazi wahamiaji, usimamizi wa wafanyakazi na mishahara, mahusiano ya vyama vya wafanyakazi na huduma kwa umma. |
| **Ardhi** | Masuala yanayohusu ardhi na makao ikiwemo sera ya ardhi, shughuli za ardhi, usoroveya na ramani, upimaji wa ardhi, makao, usajili wa ardhi, ukadiriaji wa thamani ya ardhi, usimamizi wa ardhi ya jamii na ya umma, na mfumo wa usimamizi na taarifa za ardhi. |
| **Ustawi wa Kikanda** | Ustawi wa kikanda, ikiwemo asasi za ustawi wa kikanda; masuala ya wakimbizi; ugatuzi; ustawi wa pamoja; maeneo kame; usimamizi wa hatari ya majanga; ukame, njaa na kupambana na majanga; ahueni na ufufufuaji baada ya majanga. |

| **Kamati** | **Masuala** |
|---|---|
| **Ulinzi wa Jamii** | Maslahi na usalama wa jamii, malipo ya uzeeni, masuala ya jinsia, usawa na juhudi za kuleta usawa, masuala ya watoto, vijana, watu wanaoishi na ulemavu na wazee. |
| **Michezo na Utamaduni** | Michezo, utamaduni, lugha, uchumisanaa ikiwemo ukuzaji wa muziki, sanaa, ukuzaji na ustawi wa filamu, turathi za kitaifa, na michezo ya kamari na bahati nasibu. |
| **Utalii na Wanyamapori** | Utalii, ukuzaji na usimamizi wa utalii, utafiti wa utalii na usimamizi wa wanyamapori. |
| **Biashara, Viwanda na Vyama vya Ushirika** | Biashara, ikiwemo soko la hisa, kulinda haki za watumiaji, sera za udhibiti wa bei, biashara, ustawi wa viwanda, ikiwemo maeneo maalum ya kiuchumi), ukuzaji wa biashara (ikiwemo biashara ndogondogo, biashara ndogo na biashara za wastani (MSMEs), na biashara ndogo na za wastani (SMEs), haki miliki, viwango vya ubora wa bidhaa, sera za kupambana na bidhaa ghushi na maendeleo ya vyama vya ushirika. |
| **Uchukuzi na Miundomsingi** | Uchukuzi, ikiwemo uchukuzi wa vyombo visivyotumia injini, ujenzi na ukarabati wa barabara, reli, uchukuzi wa angani na majini, bandari na sera na mipango ya miundomsingi ya kitaifa na usalama wa uchukuzi. |

## NYONGEZA YA TATU

## MUUNDO WA JUMLA WA ARDHILHALI

**[Kanuni ya 223]**

**Mimi/ Sisi tuliotia saini,**

(Hapa, tambulisha kwa jumla mwasilishaji ardhilhali, kwa mfano, wananchi wa Kenya, wakazi wa Kaunti au eneo, wafanyakazi wa kiwanda, nk)

**NINALIFAHAMISHA/TUNALIFAHAMISHA Bunge la Taifa**

**yafuatayo:**

(Hapa, eleza kwa ufupi sababu za msingi za kutaka Bunge la Taifa liingilie kati kwa kubainisha malalamiko au matatizo kwa muhtasari wa masuala ambayo mwenye ardhilhali au wenye ardhilhali wanataka Bunge la Taifa kuzingatia.)

**KWAMBA,**

(Hapa thibitisha kwamba juhudi zimefanywa kuhakikisha kuwa jambo limeshughulikiwa na idara husika na imeshindwa kutoa majibu ya kuridhisha mwenye ardhilhali.)

**KWAMBA,**

(Hapa thibitisha kwamba masuala yaliyomo kwenye ardhilhali hayapo mbele ya mahakama yoyote au asasi ya kikatiba au kisheria.)

**KWA HIVYO, mimi/sisi mwenye/wenye ardhilhali kwa unyenyekevu ninaliomba/tunaliomba Bunge—**

(Hapa, eleza kwa muhtasari ombi kwa kutaja hatua ambazo wenye ardhilhali wanaomba Bunge kuchukua au kutochukua.)

| Jina la mwenye Ardhihali | Anwani kamili | Nambari ya kitambulisho/ Nambari ya Pasipoti | Saini/ Alama ya kidole |
|---|---|---|---|
| .................. | ............ | ............... | ............ |
| .................. | ............ | ............... | ............ |
| .................. | ............ | ............... | ............ |
| .................. | ............ | ............... | ............ |

(Hapa, rudia muhtasari ulio katika ukurasa wa kwanza)

| Jina la mwenye Ardhihali | Saini/ Alama ya kidole |
|---|---|
| .............................. | .............................. |
| .............................. | .............................. |
| .............................. | .............................. |
| .............................. | .............................. |

(Kurasa zinazofuata)

*Fomu hii inaweza kubadilika kulingana na hali itakavyohitaji

# NYONGEZA YA NNE

## MASHARTI YA VIKAO VYA PAMOJA

## MASHARTI YA VIKAO VYA PAMOJA VYA BUNGE

**[Kanuni ya 24(3) na 213]**

**Jina**

**1.** Masharti haya yataitwa Masharti ya Vikao vya Pamoja vya Bunge.

**Ufafanuzi**

**2.** Katika Masharti haya, isipokuwa kama muktadha utaeleza vinginevyo, — "Mabunge" ina maana ya Bunge la Taifa na Seneti; "Kikao cha Pamoja" ina maana ya kikao cha pamoja cha Bunge;

"Mbunge" ina maana ya Mbunge au Seneta;

"Makatibu" ina maana ya Katibu wa Seneti na Katibu wa Bunge la Taifa na inajumuisha mtu yeyote anayeshughulika na majukumu ya Katibu wa Seneti au wa Bunge la Taifa.

**Wito kwa Wabunge**

**3.** Pale ambapo kuna kikao cha pamoja, Makatibu watamtumia kila Mbunge wito unaobainisha saa na mahali ambapo kikao cha pamoja kitafanyika.

**Saa za vikao**

**4.** Spika wa Bunge la Taifa na wa Seneti ataamua saa ambayo kikao cha pamoja kitaahirishwa na wataamua siku na saa au sehemu ya siku hiyo ambapo kikao kinachofuata kitafanyika.

**Kuongoza vikao vya pamoja**

**5.** (1) Wakati wa kikao cha pamoja, Spika wa Bunge la Taifa ataongoza kikao cha pamoja cha Bunge akisaidiwa na Spika wa Seneti.

(2) Iwapo Spika mmoja hatakuwepo, Spika atakayekuwepo ataongoza kikao cha pamoja akisaidiwa na Naibu wa Spika asiyekuwepo.

**Akidi**

**6.** Akidi ya kikao cha pamoja itakuwa Maseneta kumi na watano na Wabunge hamsini wa Bunge la Taifa.

**Utaratibu katika kikao cha pamoja**

**7.** Katika kikao cha pamoja, utaratibu wa Bunge la Taifa utatumika kadri Spika wa Bunge la Taifa au kiongozi wa kikao atakavyoona inafaa.

**Ripoti ya mikutano ya vikao vya pamoja**

**8.** Makatibu wataandaa ripoti kamili ya kila kikao cha pamoja na kuichapisha haraka iwezekenavyo katika umbo na mtindo utakaoelekezwa na Spika kwa pamoja mara kwa mara.

**Kamati za Pamoja za Bunge**

**9.** (1) *(imefutwa).*

(2) Kila uamuzi wa Bunge la Taifa au Seneti wa kuunda kamati ya pamoja ambayo haijabainishwa katika Kanuni za Kudumu utakuwa kwa kupitia Ujumbe kwa Bunge la Taifa au Seneti ukitaja lengo la kamati na idadi ya wabunge watakaoteuliwa katika kamati.

(3) Kamati ya pamoja itakayoundwa kwa mujibu wa Masharti haya itakuwa na angalau wabunge watano wa Bunge la Taifa na angalau watano wa Seneti.

(4) Kabla ya shughuli yoyote kuanza, kila kamati ya pamoja itamchagua mmoja wa Wajumbe wake kuwa Mwenyekiti wa kamati na mmoja wa Wajumbe kuwa makamu Mwenyekiti wa kamati.

(5) Iwapo Mwenyekiti au Makamu Mwenyekiti hawatakuwepo katika mkutano wa kamati, Wajumbe waliopo watamchagua mmoja wao kuongoza mkutano.

(6) Isipokuwa kama uamuzi utafikiwa kwa maafikiano, kura yoyote itakayopigwa itapigwa kwa kutenganisha wajumbe kutoka Bunge la Taifa na wale wa Seneti.

(7) Ripoti ya Kamati ya Pamoja itawasilishwa katika Bunge la Taifa na katika Seneti kwa ajili ya kushughulikiwa.

(8) Bila kudhibiti matumizi ya Masharti haya, Kanuni za Kudumu za Seneti na za Bunge la Taifa kuhusu kamati zitatumika, lakini Spika wa Bunge la Taifa na wa Seneti wanaweza kutoa maelekezo kwa pamoja endapo Kanuni za Bunge la Taifa na za Seneti zinakinzana.

**Makatibu wa Vikao vya Pamoja**

**10.** Katibu wa Bunge la Taifa na Katibu wa Seneti watakuwa makatibu wa vikao vya pamoja na yeyote kati yao anaweza kutimiza majukumu yanayohitajika kutekelezwa na Katibu.

**Marekebisho kwa Masharti ya Pamoja**

**11.** (1) Rekebisho kwa Masharti haya linaweza kupendekezwa na Kamati ya Pamoja.

(2) Ripoti ya Kamati ya Pamoja kwa mujibu wa aya ya (1) inayopendekeza marekebisho kwa Masharti haya itawasilishwa katika Bunge la Taifa na katika Seneti.

**Marekebisho kwa Kanuni za Kudumu zinazoathiri Bunge la Taifa na Seneti**

**12.** (1) Wakati ambapo Spika wa Seneti au Spika wa Bunge la Taifa atakuwa na maoni kwamba rekebisho kwa Kanuni za Kudumu za Bunge la Taifa au za Seneti linaweza kuathiri kwa kiasi kikubwa uendeshaji bora wa shughuli kati ya Seneti na Bunge la Taifa, Spika wa Bunge la Taifa na Spika wa Seneti kwa pamoja wataelekeza kamati zinazohusika na masuala yanayohusiana na Kanuni za Kudumu ili kwa pamoja zishughulikie marekebisho hayo na kupendekeza nakala ya marekebisho yanayokubalika na Bunge la Taifa na kwa Seneti na kuripoti kwa Bunge la Taifa au kwa Seneti.

(2) Aya ya (6) ya kifungu cha 9 (*Kamati za Pamoja za Bunge*) ya Masharti haya itatumika katika kura kwenye vikao vya pamoja vya kamati.

(3) Kamati zilizotajwa katika aya ya (3) zitawasilisha ripoti kwa Bunge la Taifa au kwa Seneti.

## NYONGEZA YA TANO

## MUUNDO WA HATI YA UTEUZI

**[Kanuni ya 179(4)]**

**Uchaguzi wa Mwenyekiti/ Makamu Mwenyekiti wa________Kamati ya Bunge la Taifa utakuwa siku ya_________Mwezi wa_________ Mwaka wa____________.**

Sisi, kama Wabunge tulioteuliwa kama wajumbe kuhudumu katika Kamati ya_____________ya Bunge la Taifa tunamteua mtu anayetajwa hapa chini kugombea kuwa Mwenyekiti/Makamu Mwenyekiti wa Kamati katika uchaguzi huo.

(1) Maelezo kumhusu mgombeaji

| | |
|---|---|
| Jina Kamili | |
| Kitambulisho cha Taifa/ Namba ya Pasipoti | |
| Jinsia | |
| Anwani | |
| Chama cha Kisiasa | |
| Namba ya Simu | |

(2) Maelezo kumhusu anayependekeza

| | |
|---|---|
| Jina Kamili | |
| Kitambulisho cha Taifa/Namba ya Pasipoti | |
| Jinsia | |
| Anwani | |
| Chama cha Kisiasa | |
| Namba ya Simu | |
| Saini | |

(3) Maelezo kumhusu anayeunga mkono

| | |
|---|---|
| Jina Kamili | |
| Kitambulisho cha Taifa/Namba ya Pasipoti | |
| Jinsia | |
| Anwani | |
| Chama cha Kisiasa | |
| Namba ya Simu | |

Na Mimi,________________ ninakubali kuteuliwa kuwa mgombeaji wa uchaguzi wa Mwenyekiti/Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya___________________ya Bunge la Taifa.

___________________________

Saini ya Mgombeaji.

Tarehe___________ Mwezi wa________ Mwaka wa__________.

## NYONGEZA YA SITA

## MUUNDO WA KIAPO/KUKIRI KUWAJIBIKA KWA SHAHIDI ALIYEFIKA MBELE YA KAMATI YA BUNGE LA TAIFA

## [Kanuni ya 191]

Mimi_________________naapa/ nakiri ya kwamba ushahidi nitakaoutoa mbele ya kamati hii kuhusu masuala yanayoshughulikiwa na Kamati utakuwa ukweli, ukweli kamili na hakuna kingine ila ukweli. (Iwapo ni kiapo—Ewe Mwenyezi Mungu nisaidie.)

## NYONGEZA YA SABA

## WITO KWA MASHAHIDI

**[Kanuni ya 191]**

Kwa_______________________________

Unahitajika kufika mbele ya Kamati ya _______________ya Bunge la Taifa kwa ajili ya___________________ (taja suala), na unahitajika (wewe mwenyewe) kufika mbele ya kikao cha Bunge la Taifa/ Kamati ya_________________siku ya____________, 20___________, saa _______________kabla ya saa sita mchana na ulete_________________ (taja habari au stakabadhi zinazohitajika kuwasilishwa).

Utarejeshewa gharama zako za usafiri na masurufu ya siku moja baada ya kutoa ithibati ya kuridhisha ya matumizi hayo. Ikiwa hautatii amri hii bila sababu halali, utaadhibiwa kulingana na masharti ya Kanuni ya 191.

Nimetia saini mnamo tarehe…………

mwezi…………..20……………..

…………………………….

**Katibu wa Bunge la Taifa**

**ILANI:** Ikiwa umeitwa kutoa stakabadhi tu na si kutoa ushahidi, utachukuliwa kuwa umetii mwaliko huu ikiwa utatuma stakabadhi husika kwa Katibu kabla ya siku na saa iliyotajwa.

## NYONGEZA YA NANE

## HATI YA KIAPO YA KUPOKEZA HATI YA WITO

**[Kanuni ya 191]**

Mimi ........................wa……………………ofisa wa Tume ya Huduma za Bunge/ofisa wa polisi ninaapa na kueleza ifuatavyo:

1. Mnamo tarehe..............20......saa................(saa) nilimkabidhi ……….hati ya wito kuhusu suala hili tarehe …………………… katika………… (mahali) kwa kutoa nakala kwake na kuhitaji saini kwenye hati asilia. Ametia saini/amekataa kutia saini kwenye hati ya wito. Ninamfahamu mimi mwenyewe /alitambulishwa kwangu na..................... na alikubali kuwa shahidi.

2. Baada ya kushindwa kumpata ....................shahidi mnamo tarehe ....................20........... saa................(saa) nilimkabidhi Hati ya Wito …………………………(jina) ambaye ni mtu mzima wa familia ya shahidi na anayeishi naye.

3. Baada ya kushindwa kumpata ..................................shahidi au mtu yeyote ambaye alifaa kukabidhiwa hati ya wito, mnamo tarehe ................................ 20...... saa ........... (saa), nilibandika nakala ya hati ya wito kwenye mlango wa nje wa......................................... . ambayo ni nyumba anamoishi/kufanya biashara/anamofanya kazi kwa ajili ya kujikimu. Nilikuwa nimeandamana na……………….. ambaye alinionyesha nyumba hiyo.

4.……………………………… (vinginevyo, bainisha jinsi ambavyo hati ya wito ilikabadhiwa).

KIAPO kimetolewa na…………………..

mnamo.......... mwezi........., 20......

**Mbele yangu**

**Kamishna wa Viapo/Hakimu**

# NYONGEZA YA TISA

# MUUNDO WA HATI YA UTEUZI

**[Kanuni ya 5(3A)]**

**HATI YA UTEUZI KWA UCHAGUZI KATIKA OFISI YA SPIKA WA BUNGE LA TAIFA**

**1. MGOMBEAJI:**

(a) Jina la Ukoo .....................................

(b) Majina Mengine................................

(c) Nambari ya Kitambulisho au Pasipoti......

(d) Jinsia ...............................................

(e) Tarehe ya kuzaliwa ...........................

(f) Anwani ya Posta ................................

(g) Anwani ya Makazi ............................

(h) Anwani ya Baruapepe ........................

(i) Nambari ya simu ya rununu ..............…

(j) Nambari nyingine za simu ……………..

(k) Kazi ..............................................

## 2. RIDHAA YA MGOMBEAJI YA KUTEULIWA

Mimi, ……………… naridhia uteuzi wangu kama mgombeaji katika uchaguzi wa Spika wa Bunge la Taifa na nimeambatisha—

(a) barua kutoka kwa Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka kama ushahidi kwamba nimehitimu kuchaguliwa kama Mbunge kwa mujibu wa Ibara ya 99 ya Katiba na kwamba mimi sio Mbunge;

(b) wasifukazi wangu; na

(c) nakala za vyeti vyangu na stakabadhi nyingine zinazohitajika.

Saini ya Mgombeaji …………………………

Tarehe……………………………………………

## 3. WAPENDEKEZAJI:

Sisi ambao tumetia saini hapa chini, ambao tumechaguliwa kuwa Wabunge katika Bunge la Taifa, tunakiri kwamba kulingana na tunavyojua, mgombeaji aliyetajwa hapo juu sio Mbunge, amehitimu kuchaguliwa kama Mbunge kwa mujibu wa Ibara ya 99 ya Katiba na amekubali kuhudumu kama Spika wa Bunge la Taifa na hivyo basi tunampendekeza kuchaguliwa awe Spika wa Bunge la Taifa—

| NA. | JINA LA MBUNGE: (Andika jina la ukoo na majina mengine) | ENEOBUNGE | NAMBARI YA KITAMBULISHO/ PASIPOTI | SAINI |
|---|---|---|---|---|
| 1 | | | | |
| 2 | | | | |
| 3 | | | | |
| 4 | | | | |
| 5 | | | | |
| 6 | | | | |
| 7 | | | | |
| 8 | | | | |
| 9 | | | | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 10 | | | | |
| 11 | | | | |
| 12 | | | | |
| 13 | | | | |
| 14 | | | | |
| 15 | | | | |
| 16 | | | | |
| 17 | | | | |
| 18 | | | | |
| 19 | | | | |
| 20 | | | | |

## 4. CHETI CHA KATIBU WA BUNGE LA TAIFA

Ninathibitisha kwamba hati hii ya uteuzi iliwasilishwa kwangu katika ofisi yangu na ………………… mwenye Nambari ya Kitambulisho/ Pasipoti ……………… saa……………………..asubuhi/alasiri/ jioni/usiku* tarehe…………………mwezi wa…………….Mwaka wa…………………………

Saini ya Katibu ………………………………

(Muhuri Rasmi)

Katibu wa Bunge la Taifa

Maelekezo:

**Hati ya uteuzi lazima iwasilishwe ikiwa imejazwa na mgombeaji kwa Katibu wa Bunge la Taifa katika Ofisi ya Katibu angalau saa arobaini na nane (48) kabla ya kikao ambacho kimeratibiwa kumchagua Spika.*

## NYONGEZA YA KUMI

## FOMU YA WASIFU

**[Kanuni ya 259F]**

**FOMU YA WASIFU WA MBUNGE**

Tafadhali jaza fomu hii kwa makini. Taarifa zitakazokusanywa zitatumika katika tovuti ya Bunge na kwa matumizi mengine rasmi.

1. Anwani: Bw./Bi./Prof./Dkt./Mengine ______ (Chagua au ubainishe moja)
2. Jina la ukoo:___________ Majina mengine: _____
3. Eneobunge/Kaunti unayowakilisha: ___________
4. Chama cha kisiasa __________/Mbunge Huru
5. Tarehe ya kuzaliwa: Siku____ Mwezi______ Mwaka_____
6. Jinsia: _____________________
7. Anwani ya Posta: _____________
8. Simu ya ofisini: __________Nambari ya kuunganisha: ________
9. Anwani ya/za Baruapepe: ___________
10. Nambari ya/za simu ya rununu: ___________
11. Dini: ________________________________

12. Elimu (Kuanzia kiwango cha juu zaidi):

| Kuanzia | Hadi | Taasisi | Cheti |
|---|---|---|---|
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |

13. Ajira ya Awali/Historia ya Huduma:

| Kuanzia | Hadi | Mwajiri | Nafasi uliyohudumu |
|---|---|---|---|
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |

14. Uanachama wa Kamati katika mabunge ya awali, kwa mfano: Bunge la Kumi na Mbili, la Kumi na Moja, la Kumi, la Tisa na kadhalika:

| Kuanzia | Hadi | Kamati | Nafasi uliyohudumu |
|---|---|---|---|
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |

15. Uanachama wa Kitaaluma:

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

16. Taji/Tuzo:

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

17. Stadi za Kipekee:

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

18. Mambo yanayokuvutia:

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

19. Je, unaishi na ulemavu?

Ndio ☐ La ☐

Ikiwa jibu lako ni "Ndio", tafadhali eleza hali ya ulemavu huo na mahitaji yoyote maalum:

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

MUHIMU: Mbunge atawajibikia usahihi wa habari alizotoa katika fomu hii.

Saini __________Tarehe__________

Zimechapishwa na
Katibu wa Bunge la Taifa
Majengo ya Bunge
Nairobi